

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Saba – Tarehe 7 Februari, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae, Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha (Mapitio ya Nusu mwaka 2017/2018) [Monetary Policy Statement (The Mid – Year Review 2017/2018)].

MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

MHE. DANIEL E. MTUKA – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

MWENYEKITI: Asante sana, Katibu tuendelee.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 84

Kuimarisha Huduma za Kijamii maeneo ya Vijiji

MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y MHE. UPENDO F. PENEZA)
aliuliza:-

Je, Serikali imeweka mikakati gani kuimarisha huduma za umeme, maji, afya na elimu katika maeneo ya vijijini ili kuongeza uzalishaji katika maeneo hayo na kuzuia wimbi la watu kukimbilia mijini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza uzalishaji katika maeneo ya vijijini kwa kuimarisha huduma za umeme, maji, afya na elimu kwa lengo la kuzuia wimbi la watu kukimbilia mijini Serikali inatekeleza mikakati ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kuendelea kuboresha miundombinu ya shule za msingi na sekondari kwa kujenga na kukarabati madarasa, vyoo, maabara, mabweni, nyumba

za walimu, mabwalo, maktaba kwa kuzingatia mahitaji ya shule husika. Pia kujenga shule mpya katika maeneo ambayo shule za msingi na sekondari ziko mbali. aidha, mkakati wa madawati kwa kila shule, mkakati wa kujenga maabara kwa shule za sekondari na ajira mpya kwa walimu wapya wa michepuo ya sayansi ni miongoni mwa mikakati mahususi ya kuboresha sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, kuendelea kuboresha miundombinu kwenye sekta ya afya ambapo kwa mwaka huu wa fedha pekee Serikali inajenga na kukarabati vituo vya afya 183 kwa gharama ya shilingi bilioni 81 vitakavyokamilika ifikapo tarehe 30/4/2018; ambapo shilingi bilioni 35.7 zimetolewa kwa ajili ya vifaa tiba. Ili kuongeza upatikanaji wa dawa Serikali imeongeza bajeti ya dawa kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016 hadi shilingi bilioni 260 mwaka huu wa fedha 2017/2018 ambazo zimesaidia sana kuongeza upatikanaji wa dawa mijini na vijiji. Pia kipaumbele maalum kimewekwa kuhusu kuongeza watumishi wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya nishati vijiji 7,873 katи ya vijiji 12,545 vya Tanzania Bara vitapatiwa umeme kuanzia mwaka huu wa fedha 2017/2018 hadi 2021. Umeme utasambazwa hadi kwenye maeneo yote ya shule, zahanati, vituo vya zfya, hospitali, mitambo ya maji, viwanda vidogo vidogo, viwanda vya katи na viwanda vikubwa.

Aidha, huduma za maji zitaboreshwazaidi kuitia utekelezaji wa awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Serikali pia itaendelea kuimarisahabarabavijijini ili kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji hasa wa mazao kwenda kwenye soko.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecil Mwambe maswali ya nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nitakuwa nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Serikali imejipanga kuhakikisha wanafikisha umeme pamoja na maji hasa zaidi kwenye shule pamoja na sehemu zingine za kutolea huduma za kijamii, lakini ningependa kwa uhakika kabisa aseme kwamba ni lini Serikali itatimiza suala hili kwa sababu ni muda mrefu wamekuwa wakiliongea kila mara bila kuwa na tarehe ya uhakika kwamba itakapofika wakati fulani tutakuwa kwa kweli tumetekeleza, bado shule nydingi pamoja na vituo vya afya vinakosa huduma ya umeme pamoja na maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna vijiji vingi sana, kama anavyosema kwamba Serikali imeazimia kupeleka umeme kwenye vijiji vyote zaidi ya 7,000, lakini ukipita Jimbo la Ndanda kwa mfano Vijiji vya Nangoo, Liputo, Ndolo pamoja na Mdenga vinapitila na umeme wa msongo wa megawati 33. Sasa Waziri angetusaidia kutueleza ni lini kwa hakika Serikali sasa wako tayari kushusha umeme ule kwa ajili ya matumizi ya watu wale walioko chini ya hizi waya ambazo kwao ni hatari kwa maisha?Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maswali yake mawili ya nyongeza aliyouliiza Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge wa Ndanda ye ye mwenyewe ni shahidi anafahamu kwa sababu ameshiriki kuitisha bajeti hapa anajua mipango ya Serikali ilivyo. Sina shaka kwamba anatambua kwamba ahadi iliyoko kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano inaendelea kutekelezwa vizuri na tuna uhakika vijiji vyote nilivyovitaja kwenye jibu la msingi vitapata umeme pamoja na vitongoji vyake kama ambavyo Wizara ya Nishati imeahidi, na mikakati iko wazi na ye ye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge ni shahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la maji, Mheshimiwa Waziri wa Maji ametoa ahadi hapa Bungeni

kuhusu kutekeleza awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, na hii itaongezeka kasi zaidi pale ambapo tutaanza kutekeleza miradi ya maji vijiji kuititia ile Wakala wa Maji Vijiji ambao utafanya kazi sawasawa na REA inavyofanya kazi. Kwa hiyo, ndugu yangu Mwambe ondoa shaka katika swali lako la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, huu umeme ambaao umepita kwenye vijiji alivyovitaja na msongo anaujua ameutaja, mimi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati namuhidi kwamba mikakati ya Serikali itatekelezwa na wanavijiji aliovatata hao watapata umeme.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika mipango yote ya kujenga shule za sekondari, shule za msingi, zahanati, vituo vyatya tunasahau sana huduma za maji, umeme pamoja na afya. Sasa nataka niulize swali kwa Mheshimiwa Waziri na bahati nzuri sana Mheshimiwa Jafo, Waziri wa TAMISEMI Mpwapwa anaifahamu vizuri sana. Katika bajeti ya mwaka 2018/2019; je, Serikali itakuwa tayari kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vituo vyatya, zahanati, shule za msingi, sekondari zote Jimbo la Mpwapwa zinapata huduma ya maji, umeme na afya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOANA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri wangu kwa majibu mazuri sana aliyoyatoto hapo awali. Pia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lubeleje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ukiangalia hali halisi ya Jimbo la Mpwapwa changamoto hizo alizozungumza

Mheshimiwa Mbunge ni kweli, lakini hata hivyo tunachokifanya ni kuhakikisha kwamba tunawapatia huduma ya maji. Nafahamu kwamba Jimbo la Mpwapwa, Wilaya ya Mpwapwa ina changamoto kubwa. Tumeweza kuhakikisha kwamba; kwa mfano ile miradi sita na Mzee Lubeleje anafahamu tulivyokuwa kule Mima pamoja katika ujenzi wa Kituo cha Afya, mtandao wa maji ambaeo kwa muda mrefu wakandarasi walikuwa mradi huo walikuwa hawaajaanza sasa wakandarasi wote sita wako site.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu letu kubwa ni kwamba maji yale yatakapotoka katika jamii kuna *water points* tutazipeleka katika taasisi hizi za Umma kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vituo hivyo vinapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa *REA* mnafahamu kwamba Wizara ya Nishati imezungumza wazi katika mpango wa *REA* Awamu ya Tatu kwamba itahakikisha katika sehemu zote za umma hasa vituo vya afya, shule pamoja na taasisi za dini zote zitapatiwa umeme kuititia katika mpango wa *REA* III. Isipokuwa katika hili niwaombe Waheshimiwa Wabunge katika ajenda hiyo lazima tuanze maandalizi ya awali ya kuweka *wiring* katika maeneo hayo, kwa sababu umeme ukishafika hapo ni lazima taasisi yenye we iwe imeshafanya *wiring* ili kuhakikisha kwamba huduma hiyo inapatikana vizuri. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Ally Seif Ungando Mbunge wa Kibiti sasa aulize swalii lake.

Na. 85

Mipango Miji

MHE. ALLY S. UNGANDO aliuliza:-

Maeneo ya Kibiti, Bungu, Jaribu Mpakani na Nyamisati katika Jimbo la Kibiti yanakuwa kwa haraka sana na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupanga mipango miji?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka mitandao na kuchonga barabara za mitaa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti kwa mujibu wa Sheria Namba 8 ya Mipango Miji ya mwaka 2007 imeandaa Mpango Kabambe (*Master Plan*) wa Mji Mdogo wa Kibiti ili kuwa dira ya upangaji na uendelezaji wa mji huo ambao ni Makao Makuu ya Wilaya ya Kibiti. Kazi hiyo imepangwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Februari, 2018 na kuwasilishwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kuidhinishwa na kusajiliwa. Michoro hiyo itakuwa na jumla ya viwanja 360 ambapo kati ya hivyo, viwanja vya matumizi ya makazi ni 205, makazi na biashara 82, viwanja vya matumizi ya umma 25, makazi maalum (*housing estate*) nane , viwanda vidogo 20 na maeneo ya wazi 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa miundombinu zikiwemo barabara ndani ya Mji Mdogo wa Kibiti utaanza kutekelezwa baada ya kuidhinishwa kwa michoro ya mipango miji na Wizara yenye dhamana na Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ungando swalii la nyongeza.

MHE. ALLY S. UNGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza; Serikali ina mpango gani wa kuajiri watumishi wa sekta ya ardhi ikiwemo Kibiti ambako kuna watumishi wachache?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia vifaa vya upimaji katika Wilaya mpya ya Kibiti kwa sababu mapato yake ya ndani yamekuwa madogo sana?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchache wa watumishi wa ardhi, naomba nimsihi Mheshimiwa Mbunge na ninaamini kabisa ana nia njema na amekuwa akipigania wananchi wa jumbo lake; katika ikama ambayo itakuwa imewekwa na halmashauri yake ni vizuri wakaonesha uhitaji wake na halafu utaratibu wa kuwaajiri watumishi wa ardhi kama ambavyo ilikuwa kwa watumishi wengine ikafuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, uwezo wa Halmashauri ni mdogo kwa hiyo wanaomba vifaa vya kupimia ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi ambayo ndiyo Wizara yenye dhamana kwa kujua iko haja kubwa ya kuhakikisha kwamba ardhi inapimwa katika maeneo yote na Wilaya zote, juzi juzi Serikali kwa kupitia Wizara ya Ardhi wameweka katika mpango wa kuhakikisha kwamba Wilaya zote zinanunuliwa vipima ardhi ili iweze kurahisisha suala hili. Naamini na wao watakuwa wanufaika.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Fatma Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo lililopo katika jumbo la Kibiti linafanana na baadhi ya maeneo katika mji wa Dodoma, kwamba baadhi ya

mitaa mfano Nkuhungu, Ilazo, Makole barabara zake za mitaa zipo katika hali duni sana. Je, Serikali itarekebisha lini barabara hizi ukizingatia kwamba sasa hivi Dodoma ni Makao Makuu? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu wazi hoja anayozungumza Mheshimiwa Fatma Toufiq kwamba ni kweli ni hoja halisia. Hii ni kwa sababu mji wetu wa Dodoma sasa hivi kwa maamuzi sahihi yaliyofanywa Serikali ni Makao Makuu yetu. Hata hivyo kuptitia miradi yetu ambayo tunaendelea nayo hapa Dodoma, sawasawa na miradi ambayo tunaendelea nayo katika miji saba katika ile *Strategic City Project*; kazi hii inaendelea awamu kwa awamu. Wabunge nadhani mnakuwa ni mashahidi. Wabunge waliofika mwaka 2010 hapa Dodoma wakifanya ulinganifu na hali ilivyo hivi sasa ni tofauti sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tutaendelea kujenga miundombinu hii. Sasa hivi kuna *ring road* karibuni zitakuwa tatu. Kuna hii ambayo hata ukifika kule inakatisha, vilevile tuna barabara zetu za mitaa na wataalam wetu wanaendelea na kazi hiyo. Lengo letu ni kwamba tukifika mwaka 2020 Jiji la Dodoma litakuwa ni tofauti sana kwa sababu mpango wetu huo ambaou unaenda mpaka mwaka 2020 utahakikisha mji wa Dodoma wote mitaa yake yote itakuwa na kiwango cha barabara za lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo si lami peke yake isipokuwa tutapeleka na mataa pamoja na mifereji yote ya kuondoa maji kuhakikisha jiji hili linakuwa jiji la mfano ambaou ndio mpango hasa wa Serikali yetu ilivyoamua.

MWENYEKITI: Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe sasa aulize swali lake.

Na. 86

Malimbikizo ya Madai ya Walimu nchini

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA aliuliza:-

Wilaya ya Karagwe ina walimu ambao bado wanadai malimbikizo ya mishahara, walimu hawa hupandishwa madaraja bila ya kurekebishiwa mishahara yao kitu ambacho kimekuwa ni kero kubwa kwa walimu wa Karagwe na maeneo mengine nchini.

(a) Je, Serikali inawaambia nini walimu hawa na imefikia wapi kutatua kero zao?

(b) Je, Serikali imefikia wapi katika kuhakikisha *Teachers Service Commission (TSC)* inapata rasillimali watu na fedha ili iweze kutetea maslahi ya walimu nchini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikilipa madeni ya malimbikizo ya mishahara ya walimu kila mwezi kupitia akaunti zao za benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30/6/2017 Serikali imelipa kiasi cha shilingi bilioni 14.236 kwa walimu 18,865 katи ya shilingi bilioni 69.461 ilizokuwa ikidaiwa hadi kipindi cha 2015/2016 ambapo walimu 12,284 ni wa shule za msingi na 6,581 ni wa shule za sekondari wakiwemo walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe 105 waliolipwa jumla ya shilingi 110,555,836.70. Serikali itaendelea kuongeza kiasi inacholipa kwa mwezi ili kumaliza kabisa deni hili kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TSC*, Serikali imeendelea kuimarisha Tume ya Utumishi wa Walimu (*TSC*) kwa kuipatia Ofisi za Makao Makuu, Ofisi za Wilaya pamoja na kuipatia samani na watumishi katika ofisi hizo. Kwa mfano, Ofisi ya *TSC* Wilaya ya Karagwe yupo Katibu wa Wilaya na Maofisa wawili. Katika mwaka huu 2017/2018 *TSC* imepewa kibali cha nafasi za ajira mpya 26 na mwaka ujao 2018/2019 nafasi 43 endapo Bunge litaridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kukamilisha ikama iliyoidhinishwa inayohitaji watumishi wasiopungua sita na wasiozidi nane kwa kila Wilaya. Hadi Desemba, 2017 *TSC* imepewa shilingi bilioni 1.247 za matumizi mengine ukiacha mishahara kati ya shilingi bilioni 4.622 zilizotengwa mwaka huu 2017/2018. Bajeti ya mishahara ikijumlishwa na hiyo Bajeti ya Matumizi Mengineyp (*OC*), *TSC* kwa mwaka 2017/2018 imetengewa jumla ya shillingi 12,422,291,495.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bashungwa swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza, lakini kabla ya kuuliza maswali haya, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais na Serikali kwa utaratibu uliowekwa sasa wa kuhakikisha hakuna mwalimu anahama mpaka stahiki zake zinalipwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu mawili ni kama ifuatavyo; naishukuru Serikali imeongeza *annual increment* kwa walimu lakini ni lini Serikali itawapandishia mishahara? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa nini walimu wanachukua muda mrefu kupandishwa madaraja? Kuna walimu tangu mwaka 2012 mapaka hivi sasa walitakiwa wawe wamepandishwa zaidi ya mara tatu lakini mpaka sasa walimu hawa hajapandishwa daraja hata mara moja.

Je, ni nini majibu ya Serikali? Nashukuru. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa kazi anazozifanya ikiwemo ushauri wa mara kwa mara anaoutoa kwa Serikali na sisi tunaupokea na pongezi alizotoa kwa Mheshimiwa Rais, tutamfikishia.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, ameshukuru kuhusu *annual increment*, sasa ameuliza ni lini Serikali itapandisha mishahara. Utaratibu huu ambao ulikuwa umesimama kwa kipindi kifupi cha miaka kama miwili hivi kupisha uhakiki wa watumishi, zoezi ambalo limefanywa kwa umahiri na weledi mkubwa, baada ya kuwa tumelikamilisha sasa tutaingia kwenye awamu ambayo tutaboresha maslahi ya watumishi ikiwemo mishahara yao.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kuhusu walimu ambao hawajapandishwa daraja kwa muda mrefu. Mimi napenda nikiri kwamba Serikali haijapandisha daraja kuanzia kipindi cha mwaka 2016 hadi 2017, lakini kuanzia mwaka huu wa fedha, matayarisho yanaendelea huko mengi kwa ajili ya kuwapandisha madaraja ikiwemo kuwapandisha wale ambao walistahili kupandishwa tarehe 01 Julai, 2016 na wale ambao walistahili kupandishwa moja mwezi wa saba mwaka 2017 watapandishwa kwa pamoja kwa mserereko. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zacharia Issaay, halafu Mheshimiwa Gekul.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyezekiti, nashukuru sana. Pamoja na changamoto nyingi zilizokuwa zinakabiri kundi hili la walimu, moja ya changamoto kubwa inayokabili kundi la walimu ni mazingira magumu ya kufanya kazi. Na kwa kuwa hivi sasa Serikali yetu inatekeleza mpango kabambe wa vituo vyaa afya kwa nchi nzima, je ni kwa nini

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Serikali ione umuhimu sasa wa kushirikiana na jamii, Halmashauri na Serikali Kuu ili kuona ni namna gani kwa kila Halmashauri katika mwaka wa fedha tunajenga nyumba kadhaa za walimu hasa mazingira yale ya vijiji ili walimu waweze kufanya kazi zao katika mazingira mazuri. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Zacharia Issaay kwa swali lake zuri na ninaomba sasa kumjibu kwamba Serikali inakubaliana kwamba kuna maeneo ambayo kweli yana mazingira magumu hasa maeneo ambayo yapo mbali na Makao Makuu ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo yanahitaji mkakati maalum, na kama tulivoyeleza katika mipango mingi ya Serikali, ni kwamba tunaomba sana ushiriki wa jamii katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na miundombinu ambayo inavutia walimu waendelee kukaa katika maeneo hayo na miundombinu hiyo ni pamoja na nyumba za walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili natoa wito kwamba halmashauri zote ziweke kipaumbele kwenye maeneo ambayo yapo mbali zaidi na halmashauri kwa kutenga kwanza fedha/mapato ya ndani kabla hatujapeleka sisi kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kukamilisha maboma. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa...

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, umenitaja Mheshimiwa Gekul.

MWENYEKITI: Aaaa, Mheshimiwa Gekul anza, halafu Mheshimiwa Masoud na baadae Mheshimiwa Mhagama

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa madaraka ya Wakuu wa Mikoa ambayo ipo kisheria si kushusha vyeo walimu ambao wamekuwa wakifundisha watoto wetu katika mazingira magumu. Hata hivyo hili limekuwa likijitokeza sasa baadhi ya Wakuu wa Mikoa akiwemo Mkuu wangu wa Mkoa wa Manyara kuwashusha vyeo walimu kwa kisingizo cha kwamba eti wamefelisha wakati watoto wanafeli kwa sababu ya mazingira magumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifahamu nini tamko la Serikali juu ya Wakuu hao wa Mikoa akiwemo wa Mkoa wa Manyara ambaye ameshusha Simanjiro, Kiteto na Babati Vijiji na anaendelea na ziara kuendelea kuwashusha walimu vyeo, nini kauli ya Serikali? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo inaeleweka ni kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ndio wasimamizi wakuu wa shughuli zote za Serikali katika Wilaya na Mikoa yao. Kwa hiyo, kama inatokea masuala yanayohusu uzembe au utoro wanayo mamlaka ya kutoa maelekezo kwa mamlaka za nidhamu ambazo ni *TSC*. Mamlaka ya nidhamu *TSC* inaanzia katika eneo la shule, shulenii pale Mwalimu Mkuu mwenyewe ni mwakilishi wa *TSC*. Kwa hiyo, kama ye ye mwenye ndio anakuwa anaongoza katika kuonyesha uzembe labda na utoro, hiyo lazima hatua ziweze kuchukuliwa. Lakini mambo mengine ambayo pengine yanaonesha kwamba labda kuna mambo ambayo yamevuka mpaka, tutayafanyia uchunguzi maalumu, ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na tatizo la malimbikizo ya mishahara ya walimu na kupandishwa madaraja bila kurekebishiwa mishahara yao kuna tatizo kubwa la walimu la muda mrefu ambalo ni ahadi ya Serikali karibu miaka sita sasa kwamba walimu wangepewa posho ya kufundishia yaani *teaching allowance*. Ni mara kadhaa Serikali imekua na kigugumizi hapa Bungeni na imekuwa haina jibu. Madaraja hayo au *teaching allowance* hiyo wamekuwa wakipewa Wakuu wa Shule na Waratibu wa Elimu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiuliza, je, Serikali ina mkakati gani wa ziada kuhakikisha kwamba ahadi waliyoiweka mwaka 2012 kwamba watawapatia walimu posho ya kufundishia (*teaching allowance*) sasa itakuwa imepatiwa ufumbuzi wa kudumu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajipanga kwa mambo mengi na ahadi zetu ni nyingi ambazo bado tunaendelea kuzitekeleza na hii ahadi ambayo anaisema Mheshimiwa Mbunge, nayo tutaitekeleza mara tutakapokuwa vizuri kifedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kizito Mhagama.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu wa shule zote za Wilaya ya Songea walismamishwa wakati Wilaya zingine wamepandiswa madaraja na maslahi yao yameongezeka, walimu wa Songea Vijijini hawakufanyiwa hivyo kwa sababu taarifa kutoka kwa Mkurugenzi zilichelewa kuifikia Wizara. Suala hili limefuatiliwa kwa miaka miwili sasa na walimu hawa hawajapata stahiki zao mpaka sasa.

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa walimu waliopo Songea, kwa maana ya Songea Vijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Madaba kuhusu madai na malalamiko yao? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Jafo majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna kesi za aina mbalimbali, na hata jana nilipata kesi inayofanana na hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Kanyasu. Nimewaelekeza wataalam wetu wafanye tathmini maeneo mbalimbali yenye changamoto, nikifahamu kwamba lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba watumishi wetu wanafaya kazi kwa amani. Maeneo mengine wamefanya vizuri, maeneo mengine bado hawajafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimewaelekeza wataalam wangu waweze kufanya kufanya tathmini maeneo mbalimbali yenye changamoto ili tuwasaidie watumishi wote ambao wana changamoto mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuweze kubaini utendaji wa kazi wa baadhi ya watu tulio wapa mamlaka. Wale wataonekana kwamba wamekuwa ni kikwazo basi ni vyema tukaweza tukawachukulia hatua za kinidhamu kwa sababu katika njia moja au nyingine wanaweza wakasababisha Serikali ikalaumiwa kumbe kutokana na uzembe wa watu wachache.

Kwa hiyo jambo hili tumelichukua na toka jana timu yangu inafanya kazi jambo hilo kwa sababu lilitoka vile vile katika Mkoa wa Geita. Maeneo mbalimbali kuna kesi kama hiso, kwa hiyo Serikali tunaichukulia yote kwa ujumla wake na kuyafanya kazi. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunamalizia na Mheshimiwa Shaaban Shekilindi.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ilihamisha walimu 210 kwa wakati mmoja, lakini mpaka sasa hivi walimu wale hawajalipwa stahili zao.

Je, ni lini walimu wale wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto watalipwa pesa zao za uhamisho?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri Jafo majibu kwa ufupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza tulichukue hilo tujue kwa nini kwa sababu kuna fedha maalum tulizitoa kwa *EPforR* kwa ajili ya kuhakikisha walimu wanahamishwa katika maeneo mbalimbali na stahili zao zinapatikana. Kesi kama hiyo tumeshaanza kuishughulikia katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ambako nadhani kuna maeneo mbalimbali imejitokeza kesi kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaangalia *nature* ya uamisho huo ulikuwaje na kwa nini watu walikuwa hawajalipwa, na kama walikuwa hawajalipwa ikiwa tayari Serikali ilishatoa pesa kwa *EPforR* tutaangalia nini tufanye.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Shekilindi naomba tulichukue hilo kama Serikali kwa *concern* ya eneo la Lushoto pamoja na maeneo mbalimbali ambayo yatakuwa na kesi kama hiyo. Tutaweza kuratibu vizuri jinsi gani ya kuondoa tatizo hili ambalo hatimaye kama nilivyo sema awali tunataka walimu waweze kuhama kwenye maeneo ya kazi wakiwa wamefanya kazi kwa amani kama inavyokusudiwa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na utalii, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo sasa aulize swalii lake.

Na. 87

Mgogoro wa Mpika Katika Pori la Hifadhi ya *North Ugala*

MHE. MARGARET S. SITTA aliuliza:-

Kumekuwa na mgogoro wa mipaka katika Pori la Hifadhi ya *North Ugala*, Wilayani Urambo, Kata ya Nsenda, Kijiji cha Kangome, Kitongoji cha Lunyeta. Mgogoro huo umesababishwa na mipaka mipya iliyowekwa na hivyo kusababisha upungufu wa eneo la shughuli za kilimo na ufugaji.

(a) Je, Serikali inafahamu kuwepo wa mipaka ya zamani ambayo haikuzingatiwa wakati wa kuweka mipaka mipya?

(b) Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro wa mipaka ili wananchi wapate eneo la kutosha kwa ajili ya kilimo na ufugaji?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msitu wa Hifadhi ya *North Ugala* unapatikana katika Wilaya za Urambo na Kaliua. Msitu huu unaomilikiwa na Serikali Kuu chini ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania na una ukubwa wa hekta 163,482.39 na ulianzishwa rasmi 1956 na kuchorewa ramani ya JB Namba 307 ya tarehe 22/10/1956.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msitu wa *North Ugala* umehifadhiwa kutokana na umuhimu wake hasa katika kuhifadhi vyanzo vya maji, mapito (shoroba) za wanyamapori hasa wanapohama kutoka katika Mapori ya Akiba ya Kigosi,

Ugala na Rungwa kuelekea Pori la Akiba la Rukwa, Lukwati hadi Hifadhi ya Taifa ya Katavi iliyopo Mkoani Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hifadhi hii inatumika katika uzalishaji na uvunaji wa mazao ya misitu ikiwemo asali, nta, mbao na mkaa. Serikali iliagiza kuweka vizingi kwenye mipaka yote ya Hifadhi za Taifa, misitu, mapori ya akiba na tengefu. Katika hifadhi ya misitu wa *North Ugala*, vizingi viliwekwa na baadae kuwaondoa wananchi wote waliokuwa wamevamia hifadhi hiyo. Baada ya kupitia na kuweka vizingi katika mpaka, ilionekana kwamba mpaka umenyooka kutoka kigingi namba 5 hadi 6 na kupitia katika mpaka wa vijiji vya Izengabatogilwe, Isongwa, Azimio, Mtakuja, Ifuta, Utenge, Tumaini, Kamalendi, Igombe, Zugimlole na Uyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mpaka mpya uliowekwa bali vizingi viliwekwa kwa mujibu wa *GN* iliyounda hifadhi hiyo. Ili kumaliza migogoro kati ya hifadhi na wananchi wanaopakana na hifadhi ya misitu; Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa misitu, ushirikishwaji wa wananchi katika uhifadhi, kuimarisha mipaka kwa kuweka vizingi na mabango ya tahadhari, kupanda miti mipakani, kushirikiana na sekta nyingine katika kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi na kuhamasisha ufugaji na kilimo cha kisasa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Margaret Sitta swali la nyongeza.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba amejibu swali ambalo yeye mwenyewe alifika Urambo na kujionea kwamba mpaka uliowekwa na Serikali upo, *beacon* zilizowekwa na Serikali zipo, lakini cha kushangaza ni kwamba wananchi waliondolewa kwenye eneo ambalo lina mpaka halali wa

Serikali. Kwa hiyo, kuwaondoa wananchi kwangu mimi naona ni kwamba hawakutendewa haki kwa sababu waliiidhinishwa na mpaka wa Serikali uliokuwepo. Kwa hiyo, kuwaondoa ni kwamba kumewapunguzia eneo lao la kilimo na la ufugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ulijiona wewe mwenyewe, je, upo tayari kurudi tena na mimi tukakae na wale wananchi tuondoe huu mgogoro ili wananchi waendelee kutumia maeneo yao waliyoyazoea ambayo sasa hivi tunawapa umaskini kutokana na kuwapunguzia eneo la kulima? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Pori la Hifadhi ya *North Ugala* lina maeneo mengi ya migogoro ya aina hiyo hiyo kutokana na kubadilishiwa mpaka wa awali na kuwawekea wa pili ambao umesababisha upungufu. Sasa swali langu, je, upo tayari kutenga muda wa kutosha tukakae mimi na wewe muda mrefu hasa Urambo umalize migogoro yote katika mpaka huo wa msitu? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana mheshimiwa Mbunge Margaret Simwanza Sitta kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akifanya katika kuwatetea wananchi wake wa Urambo. Kwa kweli anafanya kazi nzuri sana na ni mwanamke wa Jimbo ambaye kwa kweli anaonyesha mfano wa kuigwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilishawahidi kutembelea katika hili eneo na nilijiona hali yenye na tulikaa na wananchi tukatoa elimu tukaelimishana vizuri kabisa na niombe kusema kwamba nipo tayari kurudi tena kwenye eneo lile ili twende pamoja, tuambatane na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi na ambao ndio wenye

dhamana ya kuthibitisha mipaka. Tukakae na Wizara ya Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii na wananchi ili tuitie hatua kwa hatua kuweza kumaliza migogoro ambayo ipo katika eneo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swalii la pili, nipo tayari pia kutenga muda wa kutosha kabisa kuhakikisha tunapitia miogoro yote ambayo ipo katika Jimbo hilo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Devotha Ninja na Mheshimiwa Juma Nkamia.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwanza nianze kuwapa pole wananchi wa Kilolo ambao wameunguliwa na shule ya wazazi kule Ukumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niulize swalii langu moja, kwa kuwa wananchi wa Kilolo moja ya zao kubwa wanadolitegemea ni misitu, tumehamasisha na inasaidia kutunza mazingira. Pia kwa njia ya misitu wanapata mbao ambazo zimesaidia kwa kiwango kikubwa sana kujenga majengo ambayo yamesababisha ofisi nyingi kuhamia Dodoma haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ambalo lipo sasa ni kwamba wale wananchi wameanza kunyanyasika kusafirisha mbao, watu wa *TFS* (Wakala wa Misitu) wanawasumbua, *TRA* wanawasumbua kiasi kwamba wananchi sasa wako tayari kuacha kupasua mbao. Je, Mheshimiwa Waziri utakuwa tayari kwenda kukaa na watu wa *TRA* kule ili tatizo hili liishe na wananchi wa Kilolo waendelee kufanya biashara zao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa zao la misitu ni la muhimu sana

na limekuwa likitoa mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu, na wananchi wa Kilolo ni mojawapo ambao wmaekuwa wakijishughulisha sana na hili zao, kwa kweli hongera sana kwa kuhamasisha jinsi wanavyojishughulisha na hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumeweka utaratibu kwamba mwananchi yeote mwenye misitu ambaye anataka kujishughulisha na hili zao lazima apate kibali kutoka kwa Wakala wa Misitu Tanzania (*TFS*) pamoja na *TRA* ili ahakikisha kwamba anasafirisha kwa kufuata utaratibu. Na niombe tu kusema kwamba niko tayari kwenda kukaa na *TRA* pamoja na *TFS* kuhakikisha kwamba utaratibu mzima unafuatwa pale ambapo wananchi wa Kilolo wanataka kusafirisha mbazo zao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Devotha Minja, halafu Mheshimiwa Juma Nkamia.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kukosekana kwa mipaka limeendelea kuleta migogoro na kuwaumiza wananchi wengi hapa nchini. Tatizo hilo limeendelea kuwaumiza wananchi wa Mtaa wa CCT Mkundi pale Manispaa ya Morogoro ambao wamevunjiwa nyumba zao, takribani miaka miwili imepita baada ya kuambiwa kwamba wamejenga kwenye Hifadhi ya Misitu wa Kundu. Hata hivyo wananchi wale walikuwa na vibali halali na walipewa ramani zote na mji kujenga nyumba zao. Je, Serikali ipo tayari kuwalipa fidia wananchi hawa wa Mtaa wa CCT Mkundi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kulikuwa na matatizo katika msitu wetu ule wa Mkundi ambapo wananchi wengi walikuwa wameondolewa kwa sababu walikuwa wamevamia katika

maeneo haya. Kama nilivyokuwa nimesema, hata jana ambapo tumekuwa tukitoa maelezo kwa muda mrefu, kwamba yapo maeneo ambayo yalikuwa yamepimwa katika hifadhi za Taifa, maeneo ni mengi, na jana nilisema kwamba vijiji takribani 366 vimepimwa kwenye hifadhi za misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili eneo pia wananchi hawa kweli walikuwa wamepewa katika hayo maeneo lakini tulipogundua kwamba wamepewa kimakosa ndiyo maana jitihada zikafanyika katika kuwaondoa.

Kuhusu fidia, kwa sababu taratibu zilikuwa zimekiukwa, kwa kweli Wizara tutaangalia kama kweli wanaweza waka-*qualify* kupata fidia, lakini tunaamini kabisa kwamba kama walivamia na kama Serikali hawakupewa kihalali kwa kupitia, kwa sababu ule ni msitu, basi fidia inaweza isitolewe, lakini kama tutakuta kwamba waliondolewa kimakosa basi tutalitafakari na kuona namna bora ambavyo tunaweza tukalitatua hilo tatizo la wananchi wake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Juma Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nipate kuuliza swali dogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliahidi ndani ya Bunge kwamba ingeweza kumaliza migogoro ya wananchi na mapori ya hifadhi mwezi Desemba mwaka jana. Moja kati ya maeneo ambayo yanakabiliwa na mgogoro mkubwa sana ni pamoja na eneo la Swagaswaga katika Wilaya ya Chemba ambako wananchi wamekuwa wakifukuzana na askari wanyamaporii kila siku.

Ningeomba kauli ya Serikali, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri anajiaandaa kwenda Urambo, hapa Chemba ni karibu sana, yuko tayari kwenda Chemba pale kabla ya kwenda Urambo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyeekiti, ni kweli kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu katika Pori letu la Swagaswaga na ninaomba nimjibu tu kwamba hivi sasa ninavyoongea, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii leo hii ameenda kutembelea hilo pori pamoja na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ajili ya kuangalia huo mgogoro ili waweze kulitatua hili tatizo ambalo limedumu kwa muda mrefu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyeekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kuna mgogoro wa misitu na wananchi wa Jimbo la Ukonga Kata ya Vingiziwa, Chanika, Buyuni na Pugu tangu mwaka 1998, mgogoro huu Mheshimiwa Waziri Mkuu anaufahamu, wameshaunda timu huko nyuma.

Ninaomba nipate kauli ya Serikali leo; mgogoro huu unafikia lini mwisho ili wananchi wale wajue kwamba wanaendelea kuishi kwa kufanya maendeleo au wanaondoka na wanakwenda wapi? Naomba nipate majibu hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyeekiti, ni kweli kumekuwepo na mgogoro wa muda mrefu katika msitu ule na mimi mwenyewe katika kipindi cha hivi karibuni nimetoka kule nimetembelea mipaka ile na kuangalia, lakini naomba nilitaarifu Bunge lako tukufu kwamba hatua zilichukuliwa na Serikali katika kuwaondoa wananchi wote waliokuwa wamevamia katika yale maeneo

na mipaka rasmi imechorwa pamoja na kuweka barabara pembezoni ya mpaka. Kwa hiyo, wananchi wale wote ambao wako ndani wameshaondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yapo maeneo machache ambayo yamebaki ambayo sasa Mheshimiwa Waitara alisema kwamba bado inabidi tukae nao chini na mimi nakubali kwamba baada ya Bunge hili leo hii ntaomba tukutane ili tukae pamoja ili tuweze kutoa tamko la mwisho juu ya wale watu ambao wako katika haya maeneo yaliyobaki.

MWENYEKITI: Haya, naomba maswali mafupi sana Mheshimiwa Aida na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo cha migogoro hii pia kinatokana na hifadhi ambazo zinatolewa bila utaratibu, tunajua mpaka eneo litangazwe kuwa hifadhi kuna utaratibu ambao unatakiwa kufuatwa. Hivi karibuni kumekuwa na utaratibu wa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kushirikiana na halmashauri kuwaondoa wananchi na kusema maeneo fulani ni hifadhi na wakijua kabisa maeneo hayo hayajatangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Nini tamko la Serikali juu ya Halmashauri ambazo zinaondoa wananchi hao na ikiangalia kabisa hawajafuata taratibu na sheria za nchi yetu? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi kabisa.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hifadhi za misitu kuna misitu ambayo inasimamiwa na Serikali Kuu, kuna misitu inayosimamiwa na TAMISEMI na kuna misitu inayosimamiwa na Serikali za Vijiji. Kwa hiyo, kama vijiji vimetenga kwamba maeneo hayo ni ya hifadhi basi mamlaka zinazohusika zina wajibu wa

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kuhakikisha kwamba wananchi hawavamii katika hayo maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi, mimi naamini kabisa Wakuu wa Wilaya wamechukua hatua kutokana na maamuzi yaliyokuwa yamefanywa na Halmashauri zinazohusika. Kama kuna maeneo ambayo wananchi wameondolewa bila kufuata taratibu basi ntaomba Mheshimiwa Mbunge anipe hayo maeneo ili tuone na tutafakari ni hatua zippi zilistahili kuchukuliwa. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, tunamalizia na Mheshimiwa Hawa.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la ardhi katika Wilaya ya Sikunge, Mkoa wa Tabora, eneo kubwa ni eneo la hifadhi kuliko eneo ambalo wanaishi binadamu na inabidi wale wanadamu wafanye kazi kwenye eneo la hifadhi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza eneo la hifadhi na kuwapa wananchi ili waweze kufanya shughuli zao za kibinadamu kuliko ilivyo hivi sasa ambapo wananyanyasika, wanadhalilika na kuteseka? Nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli na mimi naomba niungane naye kusema kwamba Mkoa wa Tabora ni mojawapo ya mikoa ambayo ina sehemu kubwa sana ya Hifadhi ya Taifa, kwa kweli hilo Serikali tunakubali na tumeona kabisa juhudimbalimbali ambazo zimefanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nchi yetu kama tulivyokuwa tunasema kila siku na tumekuwa tukisema, ardhi

haiongezeki, idadi ya watu inazidi kuongezeka, shughuli za kibinadamu zimezidi kuongezeka, mambo mengi yamezidi kuongezeka. Kwa kweli mpango wa kupunguza maeneo ya hifadhi hautatusaidia kutatua matatizo, tatizo linaweza kutatuliwa kwa kuwa na mipango bora ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na mipango mizuri ya kutumia ardhi iliyopo hiyo itatusaidia kuliko kupunguza hifadhi. Leo hii tutapunguza kesho idadi ya watu itaongezeka zaidi, je tutazidi kupunguza? Mwisho hifadhi zote zitaisha.

Kwa hiyo hatuna mpango wa kuweza kupunguza bali ni kuwashauri wananchi watumie muda wao vizuri wapangilie vizuri ardhi yao ili ile ambayo ipo kwa ajili ya shughuli za kilimo na makazi itumike kama ambavyo imekusudiwa. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano; swalii la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Stephen, Mbunge wa Longido.

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kipekee kwa kunipa nafasi hii, naomba pia nilishukuru Bunge hili kwa jinsi walivyonyopokea nilipojiunga nalo mwanzoni mwa wiki iliyopita. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru wananchi wa Longido na chama changu kwa kunichagua kwa asilimia 99.1 niweze kuwawakilisha katika Bunge hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Catherine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, naomba swalii lake namba 88 lipewe majibu. (*Makof*)

Na. 88

Ujenzi wa Barabara ya Mto wa Mbu – Loliondo kwa Lami

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA (K.n.y. MHE. CATHERINE V. MAGIGE) aliliza:-

Serikali ilishatoa ahadi ya kujenga barabara ya Mto wa Mbu hadi Loliondo kwa kiwango cha lami.

Je, mchakato wa mradi huo umefikia hatua gani na ujenzi wake utanza lini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J.KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Stephen kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge na ninamtakia kila la heri katika kuwatumikia wananchi wa Longido. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa barabara ya Mto wa Mbu – Longido kwa kiwango cha lami na imeshaanza kutekeleza ujenzi wa barabara hiyo kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Mkataba wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hii unaohusisha kilometra 49 kutoka Loliondo (Waso) hadi Njiapanda ya Sale tayari umesainiwa na utekelezaji ulianza tarehe 18, Oktoba, 2017. Ujenzi wa sehemu hii ya barabara unaotekelzw na mhandisi aitwaye *Ms China Wu Yi Co. Ltd.* kwa gharama ya shilingi 87,126,445,712.35 unasimamiwa na *TECU (TANROADS Engineering Consulting Unit)*. Mradi huu unaoghamiwa na

Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 unatarajija kukamilika baada ya miezi 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa Wizara yangu itaendelea kutekeleza ahadi ya Serikali na miradi iliyowekwa katika llani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Dkt. Stephen swalii la nyongeza.

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ziara yake Wilayani Ngorongoro mwaka jana aliahidi nyongeza ya kilometra 50 kwenye ujenzi wa barabara unaoendelea. Je, ahadi hii itatekelezwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili; kwa kuwa llani ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 imeanisha ujenzi wa barabara ya lami yenye urefu wa kilometra 65 kutoka Sanya Juu hadi Longido; ni lini ujenzi wa barabara hii utaanza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze sana Wabunge wa Chama cha Mapinduzi waliopo Mkoa wa Arusha, ninatambua juhudii nyingi wanazozifanya ili kuhakikisha miundombinu ya barabara katika mkoa inaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Mheshimiwa Olenasha kwa sababu amefuatilia barabara hii ya Loliondo – Mto wa Mbu, na mimi niseme tu kwamba tutaendelea kuhakikisha kwamba barabara zinajengwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea Loliondo na aliahidi ujenzi wa barabara ya nyongeza kwa kilometra 50, kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili tunalishughulikia na tunaangalia kadri itakavyowezekana katika bajeti hii inayokuja nyongeza ya hii barabara tutaendelea kujenga. Kwa sababu barabara hii inayo urefu wa kilometra 218 kwa hiyo karibu asilimia 25 sasa barabara hii inajengwa, sasa tukiendelea kuongeza tutapata asilimia 50 na hatimaye barabara hii itakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, barabara hii ya Sanya Juu hadi Longido imetamkwa katika llai ya Uchaguzi, na niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu kwamba tunaendelea kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi na tuna kipindi cha miaka mitano nah ii barabara tutaitazama katika bajeti zinzaokuja ili tuhakikishe ahadi za Chama cha Mapinduzi na tuna kipindi cha miaka mitano nah ii barabara tutaitazama katika bajeti zinazokuja ili tuhakikishe ahadi za Chama cha Mapinduzi zinatekelezwa kikamilifu. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zainab Mndolwa, Mheshimiwa Hongoli, Mheshimiwa Shangazi, naomba maswali yawe mafupi ili wengi mpate.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu ya Tanzania kuna baadhi ya barabara za lami zimejengwa chini ya kiwango, kwa mfano barabara ya Chalinze hadi Mlandizi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuzikarabati barabara hizi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu nawe kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J.KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu barabara hii imekuwa ni barabara ya siku nydingi, barabara hii ilijengwa kwa kiwango kizuri, lakini kwa sababu haikudumu kwa muda mrefu na matumizi ya barabara yameongezeka kwa maana ya kupitisha magari mengi na mizigo, kwa hiyo barabara imechakaa. Serikali inao mpango wa kuifanya matengenezo makubwa barabara hii ili iweze kuwa imara zaidi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hongoli na Mheshimiwa Shangazi niliwataja.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kibena – Lupembe – Madeke, kilometra 126 ni barabara pekee ambayo inaunganisha Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Morogoro kupitia Mlimba. Barabara hii mwaka wa fedha 2016/2017 ilitengewa fedha, mwaka 2017/2018 ilitengewa fedha lakini mpaka leo hii haijaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Nataka kupata kauli ya Serikali, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuweza kuokoa uchumi unaopotea kule Lupembe na Mkoa mzima wa Njombe kwa ujumla?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J.KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Hongoli kwa sababu amekuwa akiifuatilia sana hii barabara, na hii barabara ni muhimu sana inapita sehemu ambazo zina uzalishaji mkubwa lakini pia ni kiungo kikubwa cha wananchi wa Njombe na wananchi wa Morogoro, na tumezungumza juu ya ujenzi wa hiyo barabara, barabara hii imeshasanifiwa. Kwa hiyo niseme ujenzi wa kiwango cha lami umeshaanza

kwa sababu baada ya usanifu wa barabara hizo ndiyo harakati za kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge, kwa vile barabara hii ilikuwa imetengewa fedha na Serikali ilikuwa inaendelea kupata fedha mara tu fedha zikipatikana ujenzi wa barabara hii utaanza mara moja. Naomba tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Njombe wawe na matumaini, wawe na imani na Serikali, inatafuta fedha na itaendelea kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niliambie tu Bunge lako Tukufu kwamba kila mwezi tunatumia fedah nydingi sana kulipa *certificates* zinazotoka, takribani bilioni 80 zinalipwa kila mwezi, kwa hiyo hii ni ushuhuda kwamba Serikali inafanya kazi kubwa kuhakikisha kila wakati, kila siku barabara tunaendelea kuziboresha na kuzijenga. Ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shangazi halafu Mheshimiwa Haonga atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Lushoto kwenda Mlalo, lakini pia kutoka Mlalo kwenda Bombo Mtoni hadi Maramba ni ya muda mrefu sana na inakuwa inajengwa kwa kiwango cha kilometa mbili mbili kila mwaka. Je, ni lini sasa Serikali itaweka nguvu ili barabara hii ya kutoka Lushoto - Mlalo na kutoka Mlalo kwenda mpaka Maramba ijengwe kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J.KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Shangazi amekuwa akifuatilia sana barabara pamoja na maendeleo

mbalimbali katika Jimbo la Lushoto. Ninatambua mahitaji ya barabara katika maeneo haya ambayo ameyataja maeneo ya kiunganishi cha Lushoto - Mlalo na ile barabara ya Mlalo kupita Maramba kwenda Mkinga na Mheshimiwa Kitandula amekuwa akifuatilia hii.

Kwa hiyo, kama nilivyojibu pale awali kwamba tunaendelea kutafuta fedha kama Serikali inavyokusanya fedha vizuri tutaendelea kujenga barabara mbalimbali. Kwa hiyo, niwaombe tu wananchi wa Mlalo, Maramba Mkinga na wananchi wa Lushoto kwa ujumla na watanzania wote kwamba waendelee kuvuta subira tu kadri fedha zinavyopatikana tutaendelea kuboresha barabara zote nchini ili ziweze kutoa mchango mkubwa katika ujenzi wa uchumi wa nchi yetu.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Haonga halafu Mheshimiwa Stephen Ngonyani.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wilaya ya Mbozi ambayo ni Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe inapakana na Wilaya ya Songwe lakini Wilaya hizi mbili hazijaunganishwa kwa barabara na hivyo wananchi wa Wilaya ya Songwe hulazimika kupita Mkoa mwingine wa Mbeya kuitia njia ya Mbalizi kwenda Makao Makuu ya Mkoa ambayo yako Mbozi.

Naomba sasa kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini Wilaya ya bozi na Wilaya ya Songwe zitaunganishwa kwa barabara ili kuwasaidia wananchi wa maeneo haya yote mawili kuweza kurahisisha mawasiliano?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J.KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Mbunge nikupongeze tu kwa kufuatilia na unajua umuhimu wa barabara ina mchango mkubwa sana kwenye maendeleo. Kwa vile

sijapata fursa ya kutembelea wa Mbeya mimi napenda tu nilichukue hili ni jambo la kufanya kazi na mimi nitatembelea Mbeya ili niweze kufika maeneo haya ili tuweze kushauriana vizuri na Mheshimiwa Mbunge wakati Serikali inafanya harakati za kufanya makusanyo na kuboresha barabara nchini. (*Makof!*)

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza niipongeze Serikali kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Mto wa Mbu lina linalingana kabisa na tatizo la Mji wa Mombo. Mji wa Mombo toka Awamu ya Nne ulihaidiwa na Serikali kwamba utajengwa kiwango cha lami kilometra moja na nusu, na wataalam walienda pale wakapima na wakachukua *sample* ya udongo, lakini cha kushangaza mpaka leo hii barabara hile ya Mji Mdogo wa Mombo haijafanyiwa utafiti wala haijafanyiwa chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini tamko la Serikali kuhusiana na Mji Mdogo wa Mombo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J.KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi kwamba amekuwa akilifuatilia suala hili na tumezungumza naye. Nitumie tu nafasi hii nimuelekeze Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga ili aweze kuharakisha zoezi la kusanifu eneo hili ili sasa tuweze kujenga na kuboresha kama ilivyo kwenye ahadi, ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, muda wetu wa maswali unazidi kwenda na sasa tunaingia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Philipo Augustino Mulugo Mbunge wa Songwe sasa aulize swalı lake.

Na. 89

Kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Polisi Mpona - Songwe

MHE. PHILLIPO A. MULUGO aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Songwe kwa michango yao wenyewe wamejenga jengo kubwa kwa ajili ya Kituo cha Polisi katika Kata ya Mpona tangu mwaka 2014 ili kupambana na majambazi wanaovamia wananchi hasa wakati wa mavuno ya zao la ufuta.

Je, ni lini Serikali itasaidia kuamlizia jengo hilo na kupeleka askari polisi ili kituo hicho kianze kutoa huduma?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo kwa uhakika, Mbunge wa Songwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Songwe ni kati ya mikoa mipyaa iliyoanzishwa hivi karibuni ambayo ina changamoto nyingi ya vituo vyaa polisi, ofisi pamoja na nyumba za askari kama ilivyo katika maeneo mengine ya nchini. Aidha, katika mkoa mpyaa wa Songwe hakuna Ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa na Wakuu wa Polisi wa Wilaya mbili mpyaa za Momba na Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada alizofanya yeeye na kushirikiana na wananchi wa Kata ya Mpona za kujenga Kituo cha Polisi katika eneo hilo. Aidha, kwa sasa kipaumbele ni ujenzi wa Ofisi ya Kamanda wa Mkoa pamoja na Wilaya mpyaa. Hata hivyo Serikali inafanya jitihada ili kukamilisha kituo hicho kulingana na upatikanaji rasilimali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Philipo Augustino swalilanyongeza kama unalo.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo itakuwa ni mara ya pili nipende tu kusikitika kwamba swalihili tena halijajibwa na Bunge lililopita mwezi Novemba, swalilangu nalo halikujibwa vizuri sasa sijui nina mkosi gani. Kwa sababu swalila msingi haliendani kabisa na majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na swalilangu la kwanza liwe hivi. Naomba Serikali iniambie inatumia mfumo gani wa kuwajibu maswali Wabunge humu ndani, kwa sababu Wabunge wengi wamekuwa wakilalamika maswali hayohayajibwi vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalila pili, bado niseme namuomba Waziri tena Waziri mwenye dhamana aje Jimbo la Songwe afanye ziara aangalie jinsi ambavyo vijiji vyangu na kata vilivyo *scattered* ili aone umbali wa kutoka kijiji kimoja kwenda kijiji kingine, karibuni kilometra 20 hapa, ndipo wanaweza kujenga vituo vya polisi. Lakini kunijibu kwamba kipaumbele ni *RPC* na *OCD* wala haviingi akilini naomba Mheshimiwa Waziri mwenyewe anijibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya ndani majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mulugo; ni kweli anaafuatilia sana masuala ya Jimbo lake na hasa haya yanayohusu askari kufuatana na aina ya Wilaya yake na aina ya Jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwa sababu la msingi na ushauri alioutoa ni kufika kule, nimuahidi baada ya Bunge hili kabla ya Bunge la Bajeti nitazungukia Wilaya yake kule ili nijionee mwenyewe haya anayoyasemea ili tuweze kutengeneza utaratibusi ulio mzuri wa kushughulika na jambo hilo aliloliezea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Fakharia Shomari, Mheshimiwa Badwel na Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Kwa kuwa kituo cha polisi Ziwani Zanzibar kuna baadhi ya majengo yamechakaa na yanahitaji ukarabati. Je, Mheshimiwa Waziri anawajulisha nini askari hao polisi wa Ziwani kuhusu ukarabati wa majengo yao?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi kama lilivyo swalii.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Makao Makuu ya Polisi Ziwani kuna changamoto ya miundombinu ikiwemo uchakavu wa majengo. Serikali tunalitambua hilo na tupo katika mbalimbali za kuhakikisha kwamba tunafanya marekebisho hayo kadri ya hali ya upatikanaji fedha itakaporuhusu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Badwel.

MHE. OMARY A BADWELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wa Tarafa ya Chipanga wameitikia wito wa kujenga kituo cha polisi miaka 13 iliyopita, kituo kikubwa kizuri na cha kisasa na wakati huo kilighalimu 40,000,000. Hata hivyo tangu nikiwa diwani mpaka nimekuwa Mbunge kipindi cha miaka 13 nimehangai na Wizara ya Mambo ya Ndani wafungue wapokee na wafungue kituo kile cha polisi hawajafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kumpeleka Mheshimiwa Shamsa Vuai Nahodha akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani akaagiza kifunguliwe hakikufunguliwa; nikampeleka Mheshimiwa Silima akaagiza kifunguliwe na

akawahaidi wananchi wa pale ndani ya miezi sita kwamba kituo kile kitakuwa kimefunguliwa mpaka leo hakijafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swalilangu, je, Serikali inajua kwamba miezi sita waliohaidi wananchi wa Kata ya Chipanga na Tarafa ya Chipanga kwamba imekwisha na hawajapokea kituo hicho cha polisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama leo sikupata majibu ya uhakika ya kwamba wanakipokea na kuja kukifungua kituo kile cha polisi nawaambia Jumamosi ijayo nakwenda kuwakabidhi wananchi kituo chao cha polisi ili wafanyie shughuli zingine ikiwemo kukaa watumishi kama nyumba ambaa na wenyewe wana matatizo makubwa. Ahsante.

MWNYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hii si mara ya kwanza Mheshimiwa Badwel kuuliza swalihili Bungeni na binafsi nilipata fursa ya kuzungumza naye kuhusianana mchakato wa ufunguzi wa kituo hiki na nilikuwa nimemwambia kabisa niko tayari kwenda kufungua wakati wowote. Lakini Mheshimiwa Badwel tulikubaliana kwamba tuchukue hatua kwanza kuhakikisha kwamba *RPC* wa Mkoa wa Dodoma anakwenda kulikagua ili kuona maandalizi yote kabla ya ufunguzi yamekamilika. Makubaliano hayo baina yangu mimi na Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo nashangaa sana leo Mheshimiwa Badwel hazungumzii zile hatua ambazo tumepiga mimi na yeye binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu ambacho kilikwamisha ufunguzi ni changamoto ambayo imetokana na wananchi wenyewe pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa eneo lile. Tulichokubaliana na Mheshimiwa Badwel ni kwamba kutokana na hali ya kituo ilivyo inahitaji kiweze kuwekwa sawa vizuri. Nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake kwa kazi kubwa waliyoifanya

kwa muda mrefu. Hiyo hiyo hatuwezi kuwa wezi wa fadhila tusipompongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa hali ya bajeti ilivyo mwaka huu wa fedha tumepanga takribani shilingi milioni 150 ambazo tutatoa kipaumbele katika kukamilisha vituo ambavyo vimefikia katika hatua kama ambavyo kituo hiki ambacho kiko katika Jimbo la Mheshimiwa Badwel kilipofikia.

Lakini kipindi hiki ambapo bado fedha hazijapatikana, ikiwa kuna uwezekano wa kuendelea kukamilisha yale marekebisho madogo madogo ili kiweze kufikia viwango yya kuweza kufunguliwa rasmi waweze kufanya hivyo, vinginevyo tusubiri bajeti itakapokuwa imekamilika ili tuweze kukamilisha na kuweza kukizindua. Wakati wowote hayo yatakapofanyika nitakuwa tayari kwenda kukizindua ili wananchi waweze kukturumia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko, tutamalizia na Mheshimiwa Musukuma.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ingawa kwa kweli majibu ya Waziri, Naibu Waziri yanakatisha tamaa maana tumekuwa tukisikia siku zote kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa raia na mali zao ni muhimu sana katika nchi yetu. Kwenye Jimbo la Tarime Mjini katika Kata zote name tuna kituo cha poilisi kwenye Kata ya Bomani tu, na Kata zingine ambazo za pembezoni wananchi wamejitolea kujenga vituo vya polisi. Tunataka kujua mkakati thabiti wa Serikali katika *ku-support* zile juhudhi za wananchi hasa Kata ya Nyandoto, Kenyamanyoli, Nkende na Kitale ambazo ni mbali na mji, na kuna gari moja tu ambayo inafanya *patrol*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini mkakati wa Serikali maanake mnakusanya mapato mengi, muweze kuelekeza kwenye kumalizia vituo vya poilisi ili tuweze kuimarisha ulinzi wa raia na mali zao?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nieleze tu kwa ufupi, ni kwamba changamoto ya vituo vya polisi haipo tu katika vituo vya polisi vya ngazi ya kata na tarafa, tuna Mikoa ya kipolisi takribani 34 nchi nzima. Kati ya hiyo majengo ambayo ya makamanda wa mikoa yaliyopo nchini ni 19. Kwa hiyo takribani mikoa 15 haina Ofisi ya Makamanda wa Mikoa. Mikoa miwili Manyara na Mara ndiyo ambapo ujenzi wa Ofisi mpya za makanda unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mtaona changamoto hii ni pana sana, na ndiyo maana wakati wote tumeendelea kuwashawishi wadau werevu ikiwemo ninyi Waheshimiwa Wabunge ambao wengi wenu mmekuwa mkijitolewa na sisi tumekuwa tukichukua jithada mbalimbali kuhamasisha wananchi kujitolea kuchangia ujenzi wa vituo hivyo vya polisi ili kabiliana na changamoto hii; wakati ambapo Serikali kila mwaka imekuwa ikitenga bajeti kwa ajili ya ujenzi pamoja na ukarabati wa vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hii haiwezi kumalizika kwa wakati mmoja. Naamini wewe Mheshimiwa Mbunge ni Mbunge wa Jimbo na una fedha za Mfuko wa Jimbo. Unaweza ukatumia hizo vilevile kusaldia jithada hizi za Serikali katika kuhakikisha kwamba ina punguza changamoto ya upungufu wa vituo vya polisi nchi nzima kuanzia ngazi ya Wilaya, Kata na Tarafa. Serikali kama ambavyo tunasema pale fedha zitakapopatikana tutapunguza tatizo hili hatua kwa hatua, hatuwezi tukamaliza kwa wakati mmoja.

MWENYEKITI: Tunamalizia na Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yaliyoko Songwe yanafanana kabiasa na matatizo yaliyoko kwenye Jimbo la

Geita Vijijini. Jimbo la Geita Vijijini lina wakazi kama 650,000, na tuna vituo viwili vikubwa ambavyo wasimamizi wao ni askari wenye nyota mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelalamika muda mrefu sana kwa ngazi ya Mkoa wetu naona sasa tutafute msada huku kwa Waziri. Jimbo zima na vituo hivi vikubwa havina askari wa kike, kwa hiyo askari wa kiume wanawapekua wanawake.

Sasa pengine kwa kuwa sisi ni vijijini hakuna haki za binadamu, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri, ni lini utatuletea askari wa kike kwenye vituo vile vikubwa ili wake zetu wakapekuliwe na askari wa kike na si askari wa kiume? (*Makof*).

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake ni ya msingi tutaifanya kazi.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini Mbunge wa Rombo sasa aulize swalii lake.

Na. 90

Serikali Kumaliza Ujenzi wa Vituo vya Polisi - Rombo

MHE. JOSEPH R. SELASINI aliuliza:-

Wananchi wa Kata za Mahinda, Ngoyoni, Mengwe na Kirongo – Samanga walifanya uamuzi wa kujenga vituo vya polisi kwa nguvu zao na vituo hivyo vimefikia hatua mbalimbali za ujenzi, lakini kutokana na kuwepo na shughuli nyingine zinazohitaji michango ya wananchi kama vile ujenzi wa vituo vya afya, zahanati na maabara wameshindwa kumalizia vituo hivyo.

Je, Serikali iko tayari kuchukua hatua za kumalizia ujenzi wa vituo hivyo njia ya kuwatia moyo wananchi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kupongeza sana juhudii za wananchi wa Mahida, Ngoyoni, Mengwe na Korongo kwa uamuzi wao wa kujenga vituo vya polisi kwa nguvu zao wenye. Kutokana na ujenzi wa vituo hivyo kuwa katika hatua mbalimbali. Serikali kupitia jeshi la polisi itafanya ukaguzi wa vituo hivyo ili kupata tathmini ya gharama zitakazohitajika katika kukamilisha ujenzi huo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini swalii la nyongeza kama unalo.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukisubiri sungura mdogo huyu wa Serikali kugawanywa nchi nzima sisi watu wa Rombo tumeamua kujiongeza, na tumejenga Kituo cha Polisi Useri kimeshaanza kufanya kazi, Kituo cha Ngoyoni kiko kwenye *rooffing*, kituo cha Kirongo Samanga pamoja na nyumba ya polisi karibu inafika kwenye linta na kituo cha Mahida kiko kwenye msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa jibu la hakika ili wananchi wa Rombo waamasike kuchangia zaidi ujenzi wa hivi vituo. Ni lini mtakuja kufanya hiyo tathimini ili kuwatia moyo wananchi wakamilishe hivi vituo kwa sababu kazi ya kuchangia vituo vya polisi ni ngumu kuliko hata kuchangia zahanati na shule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa sababu ya urefu wa mpaka wa Rombo na Kenya na njia za panya kuwa nyingi, Jeshi la Polisi Rombo lina magari ya zamani sana na chakavu.

Je, Serikali iko tayari kuweka katika bajeti ijayo gari kwa ajili ya kusaidia shughuli za polisi katika Wilaya ya Rombo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue furusa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, na hii ndiyo aina ya Wabunge wakutolewa mfano. Kazi waliyoifanya ni kubwa ya kushirikiana na kuhamasisha wananchi wake kujenga vituo vitatu hivi kituo cha Ngoyoni, Mahida na Kirongo si kazi ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishie mbele ya Bunge hili Tukufu kwamba jitihada za aina kama hii za Mbunge Selasini na Wabunge wengine wengi tu wamo katika Bunge hili wanafahamu wamefanya kazi nzuri kama hii. Serikali itaziunga mkono na mimi nimuhakikishie kwamba nitahakikisha tathimini hii imekamilika haraka na natarajia kufanya ziara hiyo karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda kushuhudia hii kazi mimi mwenyewe na ndiyo maana nazungumza kwa kujiamini sana. Nilikwenda nilifanya ziara Rombo na nikaona kazi hii inafanyika vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa hiyo basi namuhakikishia kwamba nitakuja tena Rombo karibuni ili tushirikiane kwa pamoja. Kuna mambo mawili ambayo tutafanya; la kwanza tutatoa kipaumbele katika bajeti ambayo inakuja ili kuhakikisha vituo hivi vinakamilika; lakini la pili nitashirikiana na Mheshimiwa Mbunge ili kuendelea kuhamasisha wadau zaidi ili tumalize vituo hivi ili viweze kutumika.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kulingana na kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Mbunge anaifanya nina uhakika kabisa tutaangalia uzito wa changamoto ya gari katika Mkoa wa Rombo ili tuone katika gari ambazo tunatarajia kuzipokea wakati wowote tuweze kupeleka huko zisaidie kupunguza changamoto za askari.

MWENYEKITI: Ahsante sana, muda wetu unakwenda nitawapa watu wawili tu, Mheshimiwa Gimbi Masaba na Mheshimiwa Omari Kigua.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naomba niulize swali la nyongeza.

Wilaya ya Itilima iliyoko Mkoani Simiyu ni miongoni mwa Wilaya zilizoanzishwa mwaka wa fedha 2012/2013, lakini ninavyozungumza hivi Wilaya hiyo haina Kituo cha Polisi. Ni lini mkakati wa Serikali kuhakikisha Wilaya hiyo mpya inapata Kituo cha Polisi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua Wilaya ya Itilima ina changamoto hiyo, lakini kama ambavyo tunatambua maeneo mengine vilevile na tuna mikakati ya kukabiliana na tatizo hilo, kama nilivyozungumza katika majibu yangu ya msingi na hili nalo tunalichukua, tunalijua na tutalifanyia kazi. Pale ambapo hali itakaporuhusu kituo kitajengwa katika Wilaya hiyo

MWENYEKITI: Mheshimiwa Omari Kigua.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilindi ina takribani miaka 20 toka imeanzishwa lakini hali ya kusikitisha ni kwamba kituo kinachotumika ni kama *post* wakati ikiwa ni

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Wilaya ya Handeni zamani. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri yuko tayari kutembelea Jimbo la Kilindi ili kujionea hali halisi ya jinsi ambavyo hata *OCDanakaa guest house* mpaka leo? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Shekilindi, Mbunge wa Kilindi kuwa....

Samahani Mheshimiwa Kigua, Mbunge wa Kilindi kuwa tutakuja Kilindi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli sasa aulize swali lake.

Na. 91

Kufuta Hati za Mashamba 25 Wilaya ya Monduli

MHE. JULIUS K. LAZIER aliuliza:-

Hivi karibuni Serikali ilitoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa kusimamia urejeshwaji wa mashamba makubwa ambao hayakuendelea yakiwemo ya Wilaya ya Monduli.

Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa kufuta mashamba 25 katika Wilaya ya Monduli ambayo mchakato wake kwa ngazi ya Halmashauri umekamilika?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba kujibu swalii

Ia Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer Mbunge wa Monduli kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia maelekezo ya Serikali kwa mikoa kusimamia urejeshwaji wa mashamba yasiyoendelezwa nchini, Wizara yangu imekuwa ikipokea mapendekezo ya kubatilisha miliki za mashamba na viwanja ambavyo wamiliki wake wakiuka masharti ya kumiliki ardhi kwa kutoendeleza, kutelekeza au kuendeleza kinyume na masharti au kutolipa kodi ya pango la ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015 Halmashauri ya Wilaya ya Monduli ilifanya ukaguzi kwa mashamba 25 ambayo yalikuwa hayajaendelezwa. Katika ukaguzi huo ilibainika kuwa kati ya mashamba yaliyokaguliwa, mashamba 12 hayakuwa na nyaraka kamili za umiliki, kwa maana ya barua ya toleo au hati na hivyo kutokuwa halali kwa kubatilishwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri iliwasilisha mapendekezo ya kufutwa mashamba 13 tu na Wizara yangu imekamilisha utaratibu wa kubatilisha miliki za mashamba hayo yote 13 yaliyopo katika maeneo ya Mswakini Juu, Lolkisale na Maserani yenye ukubwa wa jumla ya ekari 131,873.35 Mashamba haya yamerejeshwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli chini ya usimamizi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa ajili ya kuandaliwa mpango wa matumzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nichukue fursa hii kuwakumbusha Halmashauri kuwa maeneo yanayorejeshwa kwao wakumbuke kuwa na mpango mzuri wa matumizi ikiwepo kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji pamoja na matumizi mengine ya wananchi. Hata hivyo hadi leo Wilaya na Mkoa hawajaleta mapendekezo rasmi ya kutumia ardhi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inaendelea kupokea na kushughulikia mapendekezo ya kubatilisha miliki za mashamba mengine kutoka Halmashauri mbalimbali nchini baada ya wamiliki kupewa ilani kwa mujibu wa sheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Julius Kalanga swalii la nyongeza.

MHE. JULIUS K. LAZIER: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaauliza swalii la nyongeza naomba nikiri kwamba kwa kweli naipongeza Wizara hii kwa jitihada kubwa ambazo imefanya katika kusaidia wananchi wa Wilaya ya Monduli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla pia sijaauliza swalii la nyongeza, naomba nimwambie tu Waziri kwamba waliokuandalia majibu wamekudanganya. Kwanza kwa mujibu wa taarifa tu ekari zilizofutwa Monduli ni ekari 13,000 na si 131,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, mashamba tunayoyazungumzia ni mashamba ambayo Mheshimiwa Waziri wa Ardhi alivyokuja katika Jimbo la Monduli mwaka 2016 mwezi Machi, alizuiliwa na wananchi njiani na akatoa maelekezo kwamba Halmashauri ifanye mchakato wa mashamba yale ambayo yalikuwa na mashamba pori na wananchi wale walikuwa wanasumbuliwa na wale ambao waliyatelekeza mashamba na kuchukua mikopo kwa hati ya mashamba yale. Waziri akatoa maelekezo ambayo ndiyo ambayo mchakato wake ukafanyika na tarehe 09 Januari, 2018 tuka-*submit* taarifa ya Wilaya kwa kamishina wa ardhi wa kanda ambae taarifa yake haionekani hapa, kwa hiyo mchakato wa Halmashauri tulishamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri, nataka njue tu kwamba, kwa kuwa jambo hili Waziri wa Ardhi alishatoa maelekezo na kwa kuwa Halmashauri ilishafanya mchakato wa kuyafuta mashamba haya 25, je, ni lini Serikali itamalizia huu mchakato wa ufutaji wa mashamba haya 25 ambayo tumeanza mchakato upya kama ulivyoeleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kwa kuwa Waziri alitoa pia maelekezo kwamba mapendekezo ya matumizi ya mashamba yale 13 yaletwe na kwa kuwa Halmashauri na wananchi tumeshamaliza mchakato wa kutenga maeneo kwa ajili yauwekezaji, maeneo ya akiba ya ardhi na maeneo

mengine ya wananchi na kwa kuwa huu ni msimu wa kilimo na mchakato huo bado haujakkamilika japo Halmashauri imeshakamilisha na taarifa yote iko Kanda; ni lini Serikali itaagiza Mkoa na Kanda walete mapendekezo ya wananchi ya matumizi ya mashamba hayo 13? Nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO

YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anataka kujua ni lini mchakato utakamilika. Mchakato wa kukamilika unategemea na wao wenyewe kwa sababu si kazi ya Wizara kufuatilia na kuweza kujua ni jinsi gani mchakato unakwenda mbele; kwa hiyo wao wameshaona hawajaendelezwa na sheria zipo. Ibara ya 45 mpaka ya 47 kuna maonyo ambayo yanaweza kutolewa kwa muhusika kama hajaendeleza; na Ibara ya 48 unabatilisha kwa maana ya kumpelekea ilani kwa ajili ya ubatilisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wao wenyewe ndio wanatakiwa wakamilishe na wakileta kwa Waziri haina tatizo. Kwa hiyo si jukumu la Wizara kuona ni lini itakamilishwa ni mchakato ambao unatakiwa umalizwe na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili anauliza kwamba ni lini Wizara itaagiza Mkoa ili waweze kutimiza. Kila Mkoa unataratibu zake katika mipango yake, kwa hiyo kama mlileta maombi mahitaji ambayo mnataka kutumia yale maeneo ni jukumu lenu pia kuona kwamba maeneo hayo yanatakiwa yafanyiwe kazi ile iliyokusudiwa. Kwa sababu unapoleta kubatilisha tayari umeshaona kuna hitaji na tayari una mpango.

Mhe shimiwa Mwenyekiti, kwenye jibu langu la msingi nimesema kwamba hawaajaleta mpango wowote kwa hiyo sisi hatuwezi kuwasukuma mfanye nini pengine hamjahitaji kwa maana hiyo. Kwa hiyo, ni jukumu la Mkoa kuhakikisha taratibu zote zinakamilika na Wizara inaweza ukafanya pale ambapo itakuwa imeletewa ofisini.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea na Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed, Mbunge wa Muheza sasa aulize swalii lake.

Samahani Mheshimiwa Waziri wa Ardhi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mweyekiti, nampongeza sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini kwa sababu Mheshimiwa Mbunge anasema kazi zote ziko kwenye kanda na watumishi wa kanda ni wa Wizara sisi tutafuatilia kule kwenye kanda tuone yale yaliyokwama yaje haraka Wizarani ili niweze kuyaona. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa majibu ya Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed.

Na. 92

NHC Kujenga Nyumba za Bei Nafuu-Muheza

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB aliuliza:-

Wilaya ya Muheza imetenga eneo sehemu ya Chatur kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za *NHC* za bei nafuu na baadae kuuziwa wananchi na *NHC* walishalipia eneo hilo.

Je, ni lini ujenzi huo utaanza?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Balozi Adadi, Mbunge wa Muheza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba la Taifa linatambua kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kuna mahitaji makubwa ya nyumba. Utekelezaji wa mradi wa

nyumba Muheza unakwenda sambamba na mpango wa Shirika wa kujenga nyumba za bei nafuu katika Wilaya mbalimbali hapa nchini. Kwa sasa Shirika la nyumba tayari limeingia makubaliano na Halmashauri ya Muheza ili kujenga nyumba 10 katika makubaliano yaliyofanyika tarehe 29 Septemba, 2017 baada ya Halmashauri kuridhia rasmi rramani ya nyumba ambazo zilipendekezwa. Aidha, Halmashauri imeshalipa malipo ya awali kiasi cha shilingi milioni 100 ikiwa ni sehemu ya malipo ya nyumba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba lina eneo lenye ukubwa wa ekari 83 katika eneo la Chatur. Kwa sasa watalaam wa Shirika la Nyumba wako katika eneo la mradi wakiandaa mpango wa kina kwa matumizi ya viwanja (*site plan*). Baada ya kukamilisha kwaundaa mpango wa kina wa matumizi ya ardhi, Shirika la Nyumba litajenga nyumba 20 kwa gharama nafuu ambapo nyumba 10 ni kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na nyumba nyingine 10 zitauzwa kwa wananchi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa halmashauri nyingine kuiga mfano wa Halmashauri ya Muheza pamoja na halmashauri zingine ambazo tayari zimekwisha faidika na huduma hiyo zikiwemo Halmashauri ya Busokelo, Uyui, Momba, Geita na kwingineko ambaao kwa kiasi kikubwa wamepunguza tatizo la makazi kwa wafanyakazi wao. Kwa Halmashauri ambazo zilijengewa nyumba lakini hawajanunua nyumba hizo kwa sasa soko liko wazi kwa mwananchi yejote kununua nyumba hizo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Balozi kama una swali la nyongeza.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuwa na mambo mawili. Kwanza ni swali na pili ni ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekii, ni kweli kabisa watalaam walikuja Muheza na walikwenda wakaangalia hiyo sehemu

na Wana Muheza waliamasika sana baada ya kuwaona watalaan hao. Hata hivyo tangu watalaan hao wamendoka naifikiri mwezi mmoja au miwili iliyopita bado hawajarudi. Sasa nilitaka kujua, ni lini watalaan hao watarudi tena na ujenzi wa hizi nyumba utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ambalo naona kama ni ushauri; ni kwamba eneo ambalo linajengwa ni eneo la Chatur sehemu ya Kibanda, Kata ya Kilulu na lina ekari 83. Sasa nyumba ambazo zimeshawekeana saini ni nyumba 20, kwa hiyo ina maana kwamba kuna eneo kubwa ambalo litabaki. Ni ushauri tu kwamba ni kwa nini sasa hivi Shirika la Nyumba lisianze *marketing* kushawishi wana Muheza waanze kulipia kwenye hizo nyumba ambazo zitajengwa ili eneo lote la ekari 83 liweze kutumika ipasavyo? Pamoja na hayo, ni vizuri wakati *marketing* hiyo inafanyika basi na watu wa benki wanakuwepo ili kuweza kutoa mikopo kwa wananchi wa Muheza. Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anauliza ni lini watalaan hawa watarudi tena na ujenzi uanze kuanza. Naomba nimwambie tu kwamba tatizo ambalo limefanya wasianze mapema ni kwa sababu mpango wa matumizi ya eneo lile awali watu wa Muheza walipanga kama eneo la matumizi ya umma, kwa maana walikuwa wamekusudia kuweka *stand pale*. Sasa unapobadilisha kupeleka kwenye kujenga makazi inabidi mchakato wa kubadili matumizi ya eneo lile ufanyike. Kinachofanyika sasa ni kubatilisha ili litoke kwenye matumizi ya umma na liende kwenye eneo la makazi, wakikamilisha wataanza kazi hiyo.

Swali la pili, anasema *marketing* ianze kufanyika kwa ajili ya zile nyumba 10 ziweze kununuliwa. Napenda nimhakikishie tu Mheshimiwa Balozi Adadi kwamba tayari wanunuzi wameshaanza kujitekeza, wanachosubiri ni kuona

nini kinafanyika pale. Kwa wazo lake la kusema mabenki wasogee nadhani hilo tunalichukua na ni kawaida ya *National Housing* wanafanyakazi sambamba na mabenki katika zoezi zima la uendelezaji miliki.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 93

Kufufua Kiwanda cha SONAMCU-Songea Mjini

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua Kiwanda cha *SONAMCU* kilichopo Songea Mjini?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuwaongezea gawio la uzalishaji wa tumbaku wananchi wa Wilaya ya Namtumbo?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ambayo ni msimamizi wa vyama vya Ushirika Tanzania imewezesha kukamilisha mkataba katika mnunuzi mwagine wa Tumbaku Kamouni ya *Premium Active Tanzania Limited* na Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya za Songea na Namtumbo (*SONAMCU Ltd.*) wa miaka saba na mkataba huu umeboreshwa zaidi kwa kuweka kipengele cha tumbaku yote inayozalishwa Songea lazima isindikwe katika Kiwanda cha Tumbaku kilichopo Songea Mjini. Mkataba huu tayari umeshasainiwa

na umeshaanza msimu huu wa mwaka 2018/2019 ambao utadumu kwa miaka saba hadi mwaka 2025/2026. Vyama vyote vya msingi vimeingia mkataba na Chama Kikuu cha Ushirika (*SONAMCU*) ili kudhibiti tumbaku yote itakayozalishwa Songea na Namtumbo kusindikwa katika kiwanda cha tumbaku kilichopo Songea Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi huu wa Februari, kampuni hii itawaleta wahandisi wawili kutoka nchi ya Italia ambao watafika Songea na kushirikiana na Mkoa ili kuandaa gharama halisi za ukarabati na mtambo mwingine utakaoagizwa Italia ili tumbaku yote itakayozalishwa kuanzia msimu huu wa 2018/2019 isindikwe katika Kiwanda cha Songea Mjini. Serikali ina matumaini kuwa kiwanda hiki kitafunguliwa na kuanza upya kazi ya usindikaji wa tumbaku ifikapo mwezi Julai, 2018 hivyo kuwezesha kutoa ajira kwa wananchi zilizembelewa za kudumu na za msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa ununuzi wa tumbaku uliopo sasa katika *SUNAMCU* na *Premium Active Tanzania Limited* umeanza kuongeza uzalishaji wa tumbaku kwa wananchi wa Wilaya ya Namtumbo kutoka kilo 250,000 za mwaka 2017/2018 hali kufikia kilo milioni moja kwa mwaka 2018/2019. Aidha, mkataba unaonesha kila mwaka kutakuwa na ongezeko la uzalishaji wa tumbaku kutoka kwa mnunuzi aliyeingia mkataba kufuatana na ubora na mahitaji ya soko la nje ya nchi.

Hata hivyo, Serikali inaendelea kuboresha mazingira na fursa ya wanunuzi wengine watakaojitokeza wenye mahitaji ya tumbaku. Ikumbukwe kuwa ongezeko hutokeea endapo tu kuna mwenendo mzuri wa biashara katika soko na ongezeko la uzaishaji. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Jacqueline swalifupi la nyongeza.

MHE. JAQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza yenye seheu (a) na (b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubora wa tumbaku unategemea sana upatikanaji wa mbegu, mbolea, madawa kwa wakati muafaka. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati unaotakiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni nini faida na hasara ya kumruhusu mnunuzi kupeleka mbolea kwa wakulima?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA

UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kama inavyofahamika kwamba zao hili la tumbaku limekuwa na mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi yetu. Kwa misingi hiyo, Serikali imekuwa ikijitahidi kuhakikisha kwamba pembejeo zinapatikana na zinawafikia walengwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nini tatizo la kumfanya mnunuzi aweze yeye kupeleka mbolea. Mnunuzi mzuri anapopeleka mbolea kwa tija ili mwananchi huyu apate hiyo mbolea kwa tija huwa hakuna tatizo lakini kuna wanunuzi ambaao ni wanyonyaji ambaao wanapeleka mbolea na kumwambia mwananchi kwamba ukishapata hii mbolea yangu na mazao yako yote lazima uniuzie mimi kwa bei anayoitaka yeye, huo ni unyonyaji na mnunuzi wa aina hiyo huwa tunakuwa hatumtaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndio maana sasa hivi kupitia maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa, katika mazao makuu matano ya nchi hii yanawekewa utaratibu maalum ili kuhakikisha kwamba vyama vyaya ushirika viwe na nguvu na kusaidia kuwawezesha wananchi ili wasiendelee kunyonywa.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 94

Tanzania Kuagiza Mafuta ya Kula Nje ya Nchi

MHE. KHADIJA NASSIR ALI aliuliza:-

Kila mwaka Tanzania inaagiza tani laki nne za mafuta ya kula wakati tuna malighafi za kutosha kama vile alizeti, ufuta na kadhalika kwa ajili ya kuzalisha mafuta hayo.

Je, Serikali haioni haja ya kuchukua hatua za makusudi za kutumia malighafi hizo ipasavyo na kuokoa fedha za kigeni zinazopotea nchini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Khadija kuwa nchi yetu imebarikiwa kuwa na mazao ya aina nyingi ambayo ni vyanzo vya mafuta ya kula. Ni kweli kuwa kama Taifa, Tanzania tunaagiza zaidi ya tani laki nne za mafuta hali inayotugharimu fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua fursa ya kuwa na malighafi pamoja na soko la bidhaa zitokanazo na mazao hayo. Katika uhamasishaji wa ujenzi wa viwanda, tuna mkakati wa uhamasishaji wa kilimo na ujenzi wa viwanda vinavyosindika alizeti ili kupata mafuta ya kula. Mkakati wa pamba mpaka mavazi utekelezaji wake utatuwezesha kupata mafuta ya kula yatokanayo na mbegu

za pamba. Pia kupitia Shirika la NDC, mradi wa mfano unaandaliwa Mkoani Pwani ambako shamba la mchikichi litaanzishwa tukilenga kuzalisha tani 60,000 za mafuta ghafi ya mawese kila mwaka. Ni maoni yetu kuwa sekta binafsi itaazima uzoefu wa Mkao wa Pwani na kuanzisha mashamba kama hayo katika mikoa ya Mbeya, Kigoma na Kagera kwa kutaja tu baadhi ya maeneo yanayostawisha michikichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuomba Mikoa, Wilaya na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinapohamasisha suala la ujenzi wa viwanda sekta ya mafuta ya kula pia ipewe kipaumbele. Vilevile wananchi wahimizwe kuongeza uzalishaji wa malighafi kama alizeti, mawese na pamba kadri zinavyopatikana kwenye maeneo yao.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khadija Nassir, kama una swali la nyongeza.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kila Wilaya nchi nzima vijana wametenga maeneo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi. Je, Serikali lini itaona umuhimu wa kutumia maeneo haya kwa ajili ya uzalishaji wa malighafi hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, tumekuwa tukiona Serikali ikihamasisha wakulima wetu kulima mazao mbalimbali ya kibiashara bila ya kuwa na mikakati mizuri ya masoko na matumizi. Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya hili? Ahsante. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli Serikali imesisitiza na imeendelea kutenga maeneo kwa ajili ya vijana pamoja na wajasiriamali wengine. Serikali katika

kusaidia hilo, kwa mfano katika bajeti ya mwaka 2017/2018 tayari kuititia *SIDO* imetenga shilingi bilioni saba kwa ajili ya kujenga *sheds* yaani sehemu za kufanya kazi ikiwa ni pamoja na kuweka viwanda. Maeneo hayo yapo katika Mikoa ya Kagera, Geita, Simiyu, Mtwara, Manyara na Katavi, hiyo ni kwa kuanzia. Kwa hiyo, niseme tu kwamba itakapotokea *sheds* hizo zimekamilika, tutawahamasisha vijana pia kutumia fursa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa masoko, tumekuwa tukiendelea kuhakikisha kwamba tunalinda wazalishaji wa mafuta walioko nchini lakini vilevile kwa kushirikiana na nchi zinazotuzunguka kuona kwamba mazingira ya biashara ya mafuta ya kula ushindani wake ni ule ambao hauithiri nchi yetu. Kwa misingi hiyo, kwa kuangalia mafuta ya kula ambayo yanaagizwa kutoka nje na uhallsia wa kodi ambazo zinatolewa tayari kuna timu inafanya utafiti ili kuhakikisha kwamba masoko yanakuwa ya uhakika na watu wanazalisha kwa faida.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalı lake.

Na. 95

Maendeleo ya Zao la Karafuu Tanzania Bara

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga viwanda kwa ajili ya malighafi ya karafuu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kujenga viwanda hivyo hapa nchini itapunguza kusafirisha karafuu nje ya nchi kinyume na utaratibu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swalı hilo.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, kwama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la karafuu huzalishwa kwa wingi Zanzibar kwa wastani wa tani 5,500 kwa mwaka na Tanzania Bara kwa Mikoa ya Morogoro na Tanga kwa wastani wa tani 364.4 kwa mwaka. Sehemu kubwa ya zao hili huuzwa nje ya nchi hasa nchini India, Singapore, Indonesia, Umoja wa Nchi za Kiarabu na Ulaya. Kwa sasa kuna kiwanda kimoja cha kuzalisha mafuta ya makonyo kwa kutumia malighafi zitokanazo na karafuu ambacho kipo Kisiwani Pemba. Kwa mwaka 2016/2017 kiwanda hicho killiweza kuzalisha mafuta ya makonyo jumla ya tani 974.714 yenye thamani ya shilingi milioni 974.714 yaliyouzwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa viwanda ni jukumu la sekta binafsi Serikali inabaki na jukumu la uhamasishaji na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji. Kutokana na fursa iliyopo kwenye zao la karafuu katika ujenzi wa uchumi wa viwanda tutaongeza jitihada ya kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya kuongeza thamani zao la karafuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Angelina Malembeka kuwa kwa kujenga viwanda nchini kutapunguza kusafirisha karafuu nje ya nchi kinyume na taratibu. Pia ujenzi wa viwanda nchini utatengeneza ajira kwa wananchi wetu na kuongeza thamani ya karafuu hali itakayowezesha wazalishaji kupata bei nzuri na kutokana na kuwa shuguli hizi zinafanyika kwa utaratibu rasmi tutaongeza wigo wa walipa kodi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Malembeka, swali la nyongeza.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, yenye *data* na yamenifurahisha. Pamoja na majibu hayo mazuri nina swali moja la nyongeza na ombi moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais juu ya kujenga viwanda ili kutoa ajira, kujenga uchumi na kutumia malighafi za eneo husika lilizungumzwa bila ubaguzi wowote na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake amesema jukumu la Serikali ni kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri ya uwezesehaji na ujenzi ni jukumu la sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi nimekuwa nikisikia Wizara hiyo ikitiwa hapa na kupiga debe kuhusu ngozi, pamba, matunda, sukari, ndizi, mihogo hadi pilipili sijasikia hata siku moja Wizara hiyo ikizungumza kuhusu mchakato wa karafuu. Ni lini sasa Mheshimiwa Waziri ataanza kuweka hamasa ya kasi ili Zanzibar tupate kiwanda cha kuchakata karafuu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu sasa, kwa kuwa suala la viwanda ni la nchi nzima bila kujali suala la Muungano na kuna vitu ambavyo vimefanyika Zanzibar bila kujali suala la Muungano nikitolea mfano wa barabara iliyojengwa *round aboutya* Amani hadi Mtoni ambayo ilijengwa kwa fedha ya Muungano na kupewa jina la *Mkapa Road*, kwa nafasi hii kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja naomba tujengewe kiwanda cha karafuu Zanzibar ili vijana wetu wapate ajira. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya suala hilo, kwa ufupi.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lile la kwanza ambalo litajibu na namba mbili, kuhamasisha uchumi wa viwanda nchi nzima ni jukumu la Wizara yangu na nitashirikiana na Mheshimiwa Mbunge

twende Zanzibar niweze kuhamasisha kwa nguvu ileile ambapo nimeanzia sehemu nyingine. Katika utaratibu huo nitawahasisha wawekezaji ambao najua wapo kusudi tu-*take advantage* ya karafuu, mwani na michaichai kusudi tu-*take advantage* ya viungo hivi na manukato. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu hauruhusu maswali ya nyongeza tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Daniel Nikodemous Nsanzugwako swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Kamala.

Na. 96

Ushirikiano katika Nchi za Afrika Mashariki

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA (K.n.y. MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO) aliuliza:-

Ibara ya 89 hadi 101 ya Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki inazitaka nchi wanachama wa Afrika Mashariki kubadilishana uzoefu (*exchange of information on technological development and research findings*).

(a) Je, ni taarifa zipi kiutafiti ambazo nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeshirikiana?

(b) Je, ni taarifa zipi za sekta ya kilimo na mifugo ambazo nchi zimeshirikiana?

(c) Je, ni watumishi wangapi waandamizi kutoka Tanzania ambao wamepata ajira katika Jumuiya ya Afrika Mashariki?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, karibu kwa majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO
WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzungwanko, Mbunge wa Kasulu, lenye vipengele (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo mafupi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 89 hadi ya 101 ya Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki inazitaka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kubadilishana uzoefu na kushirikiana katika uendelezaji wa sekta ya uchukuzi kwa maana ya barabara, reli, bandari, usafiri wa anga na majini, taratibu za usafirishaji wa shehena, huduma za posta na simu, mawasiliano, hali ya hewa na nishati. Aidha, Ibara ya 103 ya Mkataba huo imeweeka misingi ya ushirikiano kwenye sayansi na teknolojia ikiwemo kubadilishana taarifa za utafiti wa kisayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya mafupi, naomba kujibu swali sasa la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsazungwanko, Mbunge wa Kasulu, lenye vipengele (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinashirikiana katika kuandaa taarifa za kitafiti hususani katika hatua za upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya kikanda inayotekelizwa kwa pamoja mionganoni mwao kama vile Mpango wa Uendelezaji wa Mtandao wa Barabara na Reli wa Afrika Mashariki.

Aidha, nchi wanachama zinashirikiana kwenye tafiti za kuandaa sera, mikakati, sheria za Jumuiya ili kupata matokeo tarajiwa. Vilevile nchi wanachama zimeanzisha Kamisheni ya Pamoja ijulikanayo kama Kamisheni ya Afrika Mashariki ya Sayansi na Teknolojia ambapo makao yake makuu yapo Jijini Kigali, Rwanda. Uwepo wa Kamisheni hii utaiwezesha nchi wanachama kufanya utafiti kwa pamoja,

kubadilishana uzoefu na hata kunufaika pamoja kutokana na matokeo ya tafiti hizo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 105 ya Mkataba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inazitaka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kushirikiana katika sekta ya kilimo na mifugo. Katika eneo hili nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeendelea kushirikiana katika masuala yanayohusu mbegu, madawa ya mimea na mifugo, usalama wa chakula na udhibiti wa magonjwa ya wanyama na mimea.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na muundo wa utumishi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ina nafasi tano za Maafisa Waandamizi Wateule ambapo Tanzania inashikilia nafasi mbili ambazo ni Naibu Katibu Mkuu anayeshughullikia Masuala ya Mipango na Miundombinu na Mwakilishi wa Majeshi. Kwa upande wa nafasi zinazojazwa kupitia ushindani ambazo ni Wakuu wa Taasisi za Jumuiya katika nafasi saba Tanzania ina nafasi mbili ambazo ni Mtendaji Mkuu wa Kamisheni ya Utafiti wa Afya na Naibu Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uvuvi wa Ziwa Victoria. Kwa upande wa nafasi za Wakurugenzi, katika nafasi 12 katika Jumuiya Tanzania ina nafasi nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo tuna jumla ya Watanzania nane wanaoshikilia nafasi ya watumishi waandamizi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na taasisi zake.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kamala kama una swali la nyongeza.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa wakuu wa nchi za Afrika Mashariki katika kushirikiana katika masuala ya chakula na mifugo, waliipitisha mpango kazi wa

usalama wa chakula, je, utekelezaji wa mpango huo umefikia wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wakuu wa nchi pia katika kikao chao walitoa mapendekezo ya kuanzisha ufugaji wa kisasa katika nchi za Afrika Mashariki, je, utekelezaji wake umefikia wapi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi kabisa.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango kazi wa chakula na utekelezaji wa usalama wa chakula katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao ulijadiliwa na wakuu wa nchi, kwa sasa hivi ni kwamba kwa utaratibu wa sheria na kanuni za Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi husika zinachukua uzoefu na makubaliano waliokuwa wamefikia wakuu wa nchi ili kutekeleza lile waliokubaliana nalo. Nafikiri katika suala hili Wizara ya Kilimo ambayo ndiyo Wizara ya kisekta inaweza kuwa na jibu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la ufugaji wa kisasa zimechukuliwa jithada za makusudi za kuhamasisha wakulima na wafugaji hasa wa kuku ili kuweza kujifunza kutoka kwenye nchi hizi za Jumuiya kuweza kupata uzoefu wenzao wanafanya je ili kuweza kuendeleza *area* hii ya ufugaji wa kisasa. Wafugaji hawa ni wafanyabiashara wanaweza kuwa wakubwa na wadogo na wameweza kuwa wamejifunza katika mikutano ile ya wafanyabiashara ambayo huwa inaitwa katika *East African Council* katika jumuiya ili kuweza kupeana uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kutokana na mikutano hii wanaweza kujadili jinsi wenzao kwenye nchi zinazotoka kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki wanavyofanya basi na wao wanaweza kujifunza. Ninachowea kusema kwamba Tanzania kama Tanzania wanafanya vizuri katika *area* hii ya ufugaji wa kisasa na hasa kuku.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Uhustiano wa Afrika Mashariki. Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, sasa aulize swali lake.

Na. 97

Miradi ya Umwagiliaji Liwale

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA aliuliza:-

Wilaya ya Liwale ina miradi mikubwa miwili ya umwagiliaji, Mradi wa Ngongowele na Mtawango lakini Mradi wa Ngongowele umesimama kwa muda mrefu sasa.

(a) Je, ni nini hatma ya mradi huu wa Ngongowele kwa sasa?

(b) Je, Serikali iko tayari kumpeleka Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ili kukagua mradi huu ambao unaonekana kuhujumiwa kwa muda mrefu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza wa Mradi wa Ngongowele ilianza kutekelezwa mwaka 2009 kwa kujenga banio na miundombinu yake kwa gharama ya shilingi milioni 346.1 kupitia Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Taifa. Awamu ya pili wa mradi ilitekelezwa mwaka 2010 kwa gharama ya shilingi milioni 400. Kazi zilizofanyika ni kuchimba na kusakafia mfereji mkuu mita 2,500; kujenga

vigawa maji sita; kujenga makalvati matano; kujenga kujenga kivusha maji chenye urefu wa mita 80 na kuchimba mfereji wa kutoa maji mita 200. Awamu hii ya utekelezaji ilikumbwa na changamoto ya mafuriko makubwa yaliyotokea katika maeneo hayo na kuharibu miundombinu. Hali hiyo ilipelekea mkandarasi kuongezewa muda wa kukabidhi kazi kutoka tarehe 01.10.2011 hadi tarehe 30.10.2011. Baada ya kushindwa kukabidhi kazi kwa tarehe hiyo, Halmashauri ilianza kumkata *liquidated damage* ya asilimia 0.15 ya thamani ya mkataba wa siku kwa muda wa siku 100 hadi tarehe 15.02.2012 na baadaye ilivunja mkataba kutokana na mkandarasi huyo kushindwa kukabidhi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa mradi huo kwa wananchi wa Ngongowe na Taifa kwa ujumla, Serikali kuitia mradi wa kuendeleza skimu ndogo za wakulima itatenga fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi huu ili ufanye kazi. Aidha, Serikali itafuatilia utekelezaji wa Mradi wa Ngongowe na endapo itabainika kuna hujuma katika utekelezaji wa mradi huo hatua stahiki zitachukuliwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuchauka kama una swalilala nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utangulizi tu nipende kusema kwamba jibu ni jibu hata kama halikutosha kwa muuliza swalilala ni jibu. Hii bla bla yote iliyoolewa kwenye aya ya pili mimi sioni kama ni jibu linalijitosheleza kwa sababu mradi huu umehujumiwa kwa kiwango kikubwa sana. Kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kwenye Jimbo langu, mimi na Mkuu wetu wa Wilaya na Mkurugenzi wetu wa Halmashauri tulipanga ziara Mheshimiwa Waziri Mkuu akakague aone nini kimefanyika kwenye mradi ule. Hata hivyo, hao watu wa Kanda wa Umwagiliaji wakishirikiana na Mkuu wa Mkoa wa Lindi waliifuta hiyo ziara katika

mazingira yasiyofahamika na ni kwa sababu tu huu mradi umehujumiwa kwa kiwango kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, je, Serikali iko tayari sasa kama hii awamu wanayotaka kuisema awamu ya tatu, kutukabidhi Halmashauri mradi huu tuutekeleze badala ya kuwaachia hawa watu wa Kanda ambao wamekuwa wakiuhujumu mradi huu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kutembelea mradi huu ili aangalie pesa hizi shilingi milioni 746 za Serikali ambavyo zimepotea bila sababu zozote zile za msingi? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa ufupi.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na la mwisho, tuko tayari kuongozana na wewe kwenda kuangalia ule mradi. Kwanza nishukuru kwamba umekubali kwamba ule mradi tumetekeleza lakini mafuriko yalitokea, sasa kama tulivyojibu katika swalii la msingi tutaunda timu ya wataalam tuipeleke kule iende ikachunguze na huo ndiyo utaratibu wa kisheria wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimuombe Mheshimiwa Mbunge tu kwamba Halmashauri ni taasisi ya Serikali, umwagiliaji ni taasisi ya Serikali, hawa wote wanafanya kwa niaba ya Serikali. Kwa sababu wote ni wa Serikali hakuna kitu chochote kwamba pengine Mkuu wa Mkoa alifuta ratiba ya Waziri Mkuu ili asije kuangalia mradi ule, tusiletie mgongano kati ya Halmashauri na Idara ya Umwagiliaji iliyo chini ya Wizara ya Maji, zote ni Serikali.

Suala la msingi ni kwamba changamoto ipo, tushirikiane na Mheshimiwa Mbunge tutume timu ikaangalie na kama tulivyojibu kama kuna hujuma yoyote imetokea basi waliofanya hivyo watawajibishwa kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Tunamalizia swalii letu la mwisho, Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swalii lake.

Na. 98

Bwawa katika Kijiji cha Mbwasa, Tarafa ya Kintinku

MHE. DANIEL E. MTUKA aliuliza:-

Bwawa linalotarajiwa kuchimbwa katika Kijiji cha Mbwasa, Tarafa ya Kitinku ni la kimkakati kwa wakazi wa Tarafa nzima ya Kintinku.

Je, ni lini Serikali itaanza rasmi ujenzi wa bwawa hilo baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Halmashauri ya Manyoni ilipanga kujenga Bwawa la Mbwasa kwa kupitia Mto wa Msimu wa Liula ikiwa ni hitaji la wananchi wa Kijiji cha Mbwasa kwa ajili ya shughuli za kilimo, mifugo na matumizi ya nyumbani. Ujenzi wa Bwawa la Mbwasa ulikusudiwa kunufaisha pia wananchi wa vijiji jirani vya Mwiboo, Mtuwe na Chikuyu, lengo kuu likiwa na kuimarishe kilimo cha umwagiliaji wa zao la mpunga. Hali hii inatokana na maeneo hayo kutokuwa na uhakika wa mvua za kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013 upembuzi yakinifu na usanifu wa Bwawa la Mbwasa ulifanyika kupitia Ofisi ya Umwagiliaji wa Kanda ya Dodoma. Aidha, matokeo ya upembuzi huo yalibaini kuwa

jumlah ya shilingi bilioni 2.5 zingehitajika kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo.

Mheshimiwa Mwenyiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilianza kufanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 kwa kutambua umuhimu wa ujenzi wa mabwawa kama hatua ya kimkakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Katika kuwezesha kilimo cha uhakika katika maeneo kame, Bwawa la Mbwasa litapewa kipaumbele katika bajeti ijayo ya mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtuka, kama una swali la nyongeza.

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niipongeze tu Serikali kwa jibu zuri lenye matumaini hasa kwa wananchi wa Manyoni wanaoishi katika Bonde la Ufa katika maeneo ya Unyambwa, Unyangwila na Mgunduko. Hata hivyo, nina swali dogo la nyongeza pamoja naombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na ombi, naomba katika bajeti hii inayofuata ya 2018/2019 nione bajeti ya uchimbaji wa bwawa hili imetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza ni kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni imebainisha maeneo katika vijiji vitatu kwa ajili ya kuchimba mabwawa madogo. Vijiji hivi ni Makutupora, Winamila pamoja na Igwamadete. Je, Serikali itakuwa tayari kutuuunga mkono kama Halmashauri?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze

Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya kuwatetea wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa napenda nimueleze Mheshimiwa Mbunge, sisi ni Wizara ya Maji na jukumu letu ni kuhakikisha wananchi wanapata maji. Nimhakikishie katika Bwawa lile la Mbwasa tutawaweka katika bajeti 2018/2019 ili kuhakikisha wananchi wake wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa lingine pamoja na jitihada ya kuainisha maeneo kwa ajili ya mabwawa, nataka nimhakikishie Serikali na Wizara yetu pamoja na wadau wa maendeleo tumekuwa tukishirikiana katika kuhakikisha tunachimba mabwawa maeneo yenye ukame. Sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo, tuko tayari kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge katika kuhakikisha maeneo yenye uhitaji wa mabwawa wanapata mabwabwa ili waondokane na ukame kwa kupata maji. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Maswali yetu kwa siku ya leo yameishia hapo, nina matangazo hapa sasa. Kwanza ni wageni ambaao wako Bungeni asubuhi hii.

Kuna wageni 12 wa Mheshimiwa Dkt. Angeline S. L. Mabula, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambayo ni viongozi wa CCM , Kata, Mitaa na wapiga kura wake kutoka llemtela, Mkoa wa Mwanza. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Mabula. (*Makofii*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Hassan Elias Masala ambaao ni Wakurugenzi wa Redio Mashujaa ya Mkoani Dodoma, karibuni sana katika Bunge letu. (*Makofii*)

Vilevile kuna wageni 18 wa Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha ambaao ni vijana wa Kanisa la *Free Pentecostal Church Tanzania* kutoka Chang'ombe, Mkoani Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Daudi Msaghaa. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wengine ni wageni sita wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambao ni wanachuo wa Chuo Kikuu cha Dodoma na wavuvi kutoka Mkoa wa Dodoma na Geita. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tuna wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, hawa ni wanafunzi 100 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma kilichopo Mkoani Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu katika Bunge letu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hapa pia nina matangazo matatu, kwanza ni tangazo la semina. Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge ananiomba niwatangazie au niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo Jumatano tarehe 7 Februari, 2018 kutakuwa na semina kuhusu masuala ya afya ya moyo ambayo itaanza saa 7.30 mchana katika ukumbi wa Msekwa. Semina hii itatolewa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na kwa ujumla wake italenga kutoa elimu kuhusu dalili na tiba ya magonjwa ya shinikizo la damu, kiharusi, tezi dume *pre-menopause* *menopause*. Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria semina hiyo muhimu sana.

Pia kuna tangazo lingine kwa Waheshimiwa Wabunge Wakristo wa Katoliki, leo Jumatano tarehe 7 Februari 2018 kutakuwa na Ibada ya Misa Takatifu itakayotanguliwa na Ibada Maalum ya Upatanisho (*Special Rites of Reconciliation*) katika kanisa dogo lililopo ghorofa ya pili, Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kuahirishwa Bunge leo saa 7.00 mchana. Waheshimiwa Wabunge Wakatoliki wote mnakaribishwa kushiriki.

Tangazo la mwisho, Waheshimiwa Wabunge Wanafaraja mnakumbushwa kuchangia Mfuko wa Faraja kwa mwaka 2017/2018. Mwisho wa michango ni Machi 2018, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama ndiye anatoa tangazo hilo.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya dharura.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Mwalimu Bilago na Mheshimiwa Gekul. Tunaanza na Mheshimiwa Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Natumia Kanuni ya 47, sina sababu ya kuisoma kuomba Bunge hili kama litaridhia na nitaomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono kujadili jambo la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Mji wa Nzega lakini na Halmashauri nyingi katika nchi hii zimekuwa zikikatiwa umeme katika chanzo cha maji na Shirika la Umeme kwa sababu ya madeni ya miaka mingi ambayo yamekuwa yakidaiwa yaliyotokana na *central government* kutokupeleka fedha za *utility* katika Halmashauri kwa muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni siku ya kumi wananchi wa Mji wa Nzega hawana maji, lakini hawadaiwi ankara za maji zinazodaiwa ni taasisi za Serikali na tulikubaliana katika Kamati ya Bajeti kwamba Wizara ya Fedha itayachukua madeni yale ya nyuma ambayo yameshathibitika ili kuititia Hazina waweze kuyalipa. Leo ninavyoongea akina mama wajawazito katika Hospitali ya Wilaya ya Nzega hawawezi kupata huduma, tumeweka magari kuwapeleka Nkingi, leo Mji wa Nzega hauna maji, wananchi wa Nzega hawadaiwi hata shilingi moja ya ankara za maji. Pamoja na kwamba maji tunayapata kwa mgao lakini maji hayo hayo hatudaiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge hili liniunge mkono tujadili jambo hili kwa sababu tulishalfanya maamuzi

kwenye bajeti, Serikali hajachukua hatua wala ku-take responsibility, wananchi wanateseka bila sababu yoyote. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono na wewe ikikuridhia jambo hili tuweze kulijadili ndani ya Bunge hili, tulifanyie maamuzi, Serikali ikatekeleze. Kabla hatujaondoka katika Bunge hili hatua madhubuti juu ya tatizo hili ziwe zimechukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba Wabunge waniunge mkono.

MBUNGE FULANI: Toa hoja.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja. (*Makofii*)

(Hapa baadhi ya Wabunge Wallisimama kuunga mkono Hoja ya Mhe. Hussein M. Bashe)

MBUNGE FULANI: Hawa hawajasimama hawana shida ya maji.

MWENYEKITI: Tunaendelea na mwingine, Mheshimiwa Mwalimu Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7), naomba nisiliome, naomba kuzungumzia jambo ambalo linatokea mara kwa mara humu Bungeni na kwa kweli naomba tuitendee haki hii *Order Paper*. *Order Paper* inakuja na maswali na mambo mbalimbali lakini maswali haya ya mwisho mwisho hayatendewi haki yaani tuna-dilute *Order Paperyetu*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani ukishaona kama una swali liko mwishoni kwenye *Order Paper* yako unaanza kuhesabu maumivu kwamba leo swali langu halitakuwa na maswali ya nyongeza. Huu siyo utendaji bora wa Kibunge. Tuione *Order Paper* kama ina thamani kubwa kuanzia swali la kwanza mpaka swali la mwisho. Nikiombe Kiti mjaribu ku-balance muone namna bora ambayo wenye maswali ya

mwishoni huku nao watatendewa haki, tunakaa tunabaki na maswali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mwongozo wako na hili limekuwa kama mazoea ya kawaida kila anyekaa hapo yakifika maswali matano ya mwisho akiangalia ile saa, muda hautoshi, hautoshi kwa nini, tunakimbia kwenda wapi? Hebu mtusaidie tumalize *Order Paper* yetu na maswali yote yatendewe haki. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwamba hii tabia sasa itaisha, ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nipate mwongozo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nauliza swalii la nyongeza leo asubuhi kuhusu hi halisi inayoendelea katika Mikoa yetu kwa Wakuu wa Mikoa kukiuka sheria na taratibu ambazo Bunge hili tumetunga, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI aliona kama ni sawa na nilizungumza kuhusu Wakuu wa Shule na Waratibu kushushwa vyeo vyao kwa kisingizio cha kwamba shule zao zimefelisha ilhali tuna sheria inayooongoza Wakuu wa Mikoa ya mwaka 1997 ikionyesha majukumu yao ni yapi na Wakuu wa Mikoa hawahusiki moja kwa moja kuwajibisha walimu na waratibu kwa sababu tuna Wakurugenzi ambao ndiyo mamlaka za uteuzi na kuna Tume ya Walimu kama walimu wameharibu au wame-misbehave chochote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, Bunge linatunga sheria, tunategemea Serikali ndiyo wasimamie hiyo sheria, lakini majibu ya Serikali ni kwamba wanabariki Wakuu wa Mikoa wafanye kazi za Wakurugenzi, jambo ambalo *it is very wrong*.

Naomba Mwongozo wako ni kwa nini Serikali isituletee kauli hapa Bungeni tufahamu ni nani anaingilia

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

mwenzie katika majukumu kwa sababu Wakuu hawa wa Mikoa sasa wanafanya kazi za Wakurugenzi ambazo siyo zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul ahsante. Mheshimiwa Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 46; nilitaka kutoa maelezo kidogo kuhusu swali la 96 la Mambo ya Nchi za Nje la Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma swali hilo (a), ni taarifa zipo za kiutafiti ambazo nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeshirikiana, jawabu tunaambiwa na *feasibility study*. *Feasibility study* haijawahi kuwa utafiti, ni utaratibu wa kujenga barabara.

Kwa hiyo, nataka umuombe Mheshimiwa Waziri aje alijibu tena swali hili (a) na (b) kwa sababu hajajibu, ameulizwa utafiti, yeye anaelezea ujenzi wa barabara, ni kitu gani hiki? (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba angalieni jibu hii lilitojibwa kwenye swali la 96, (a) na (b) hakuna jawabu. Ameulizwa tafiti anasema upembuzi yakinifu wa barabara. Upembuzi yakinifu wa barabara haujawahi kuwa utafiti, ni process ya kujenga barabara. Swali lilitolizwa hapa ni tafiti zipo na naamini tafiti zipo lakini walikuwa wanajibu swali hawakuhangaika kuzitafuta hizo tafiti ili waziweke hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba. Nina miongozo minne ambayo nimeipokea. Wa kwanza ni

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

kutoka kwa Mheshimiwa Bashe ambaye ana Mwongozo wa kutaka kujadili jambo la dharura katika Jimbo lake la Halmashauri ya Nzega kuhusiana na kukatiwa maji na wananchi wake siku kumi sasa hivi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa suala hili haliko Nzega peke yake ingawa hiyo dharura iko kwake kwa muda huu sasa hivi, mimi sioni hoja ya kujadili isipokuwa sasa hivi naiagiza Serikali kushirikiana na Mbunge kuweza kuona tatizo hilo linatatuliwa haraka iwezekanavyo. Huo ndiyo Mwongozo wangu kuhusiana na suala hilo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tukija kwa suala la Mwalimu Bilago kuhusiana na maswali ambayo yapo kwenye *Order Paper*, ni kweli na hilo linatokana na Wabunge wenyewe kutouliza maswali ya Kibunge. Pia hata mkiuliza ya Kibunge muda ambao tunapewa kwa maswali ikiwa ni dakika 90 ama ni saa moja, ikiwa tutaweza kuwapa watu wawili tu waulize maswali ya nyongeza basi muda wote utakwisha na ziada juu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nini Mwongozo wangu? Mwongozo wangu ni kwamba Wabunge tujifunze vizuri na tujirekebishe. Tuulize maswali mafupi ya nyongeza ili kila mmoja na swali lake liweze kupata maswali ya nyongeza.

Aidha, Waheshimiwa Mawaziri nao majibu yao yawe ya kuridhisha na mafupi. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kupata nafasi ya kuuliza maswali yetu yote ambayo yapo kwenye *Order Paper*. Huo ndiyo Mwongozo wangu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, suala la Mheshimiwa Gekul kuhusu Wakuu wa Shule kushushwa vyeo pia na suala la Mheshimiwa Serukamba, haya nitayatolea maamuzi baadaye. Katibu tunaendelea. (*Makofi*)

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

**Hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na
Maendeleo ya Jamii Kuhusu Shughuli za Kamati kwa
Mwaka 2017**

na

**Hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya
UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017**

MWENYEKITI: Hoja za Kamati, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Serukamba karibu. (*Makofii*)

MHE. PETER J. SERUKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGESA YA HUDAUMA NA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya mwaka kuhusu majukumu na shughuli zinazotekelizwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii katika kipindi cha 2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) za Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2016.

Mheshimiwa Mwenyekti, muundo wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 113 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 na imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ni utangulizi unaofafanua muundo na majukumu pamoja na maelezo ya jumla. (*Makofii*)

Sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati; sehemu ya tatu Kamati inabainisha maoni na mapendeleko na sehemu ya mwisho ni kuhitimisha taarifa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba uniruhusu nisisome sehemu ya kwanza na ya pili, nitaanza kusoma sehemu ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla, bajeti; maendeleo yoyote yanategemea uwepo wa rasilimali ikiwemo rasilimali watu, muda pamoja na rasilimali fedha. Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zimeonesha uwepo wa changamoto ya kuchelewa kwa fedha zilizotengwa kwenye bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara zote tatu zinazosimamiwa na Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hiyo imesababisha shughuli nyingi kushindwa kutekelezaka kwa wakati, hadi wakati Bunge linapitisha bajeti ya mwaka wa fedha wa 2017/2018 Wizara zote chini ya Kamati hii hazikuwa zimepokea fedha zaidi ya asilimia 50 ya bajeti zao kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Aliyekuwa Rais wa Marekani Barrack Obama aliwahi kusema, naomba kunukuu; "*A budget is more than a series of numbers on a page, it is an embodiment of our values.*" Kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba bajeti ni zaidi ya mfululizo wa namba katika ukurasa bali ni utambuzi wa thamani yetu. Hivyo basi, Serikali itambue kwamba, taswira na ubora wa nchi yetu inaonekana pia kupitia upangaji na utekelezaji wa bajeti yake. Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu unachangia kuzorota kwa utekelezaji wa majukumu mbalimbali ikiwemo miradi ya maendeleo kwa ajili ya kuwashudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali kuna fedha maalum ambazo zimekuwa zikitengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wizara zilizo chini ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua baadhi ya miradi ukiwemo mradi wa mabweni ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mradi wa ujenzi wa

maktaba kubwa na ya kisasa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati ilibaini kuwa miradi hiyo ilitekelezwa vizuri na Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya vizuri katika miradi hiyo iliyotajwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati kwamba utekelezaji wa miradi hiyo umesaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili Chuo Kikuu cha Dar es salam hasa katika suala la mahali pa kulala wanafunzi wa chuo hicho. Serikali ihakikishe inapeleka fedha pia katika miradi ya maendeleo mingine kama ilivyopangwa ili nayo iweze kutekelezwa kwa wakati kama ambavyo imefanyika katika mradi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Katika Wizara hii Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bohari Kuu ya Dawa imekuwa ikifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuhakikisha inasambaza dawa muhimu kwa wananchi licha ya changamoto inazokumbana nazo na kuendelea kuzitafutia ufumbuzi. Upatikanaji wa dawa katika maeneo mengi ya kutolea huduma za afya imeendelea kuwa changamoto siku hadi siku, Kamati inaendelea kusisitiza kutekeleza mipango mikakati ambayo itatatua changamoto za Bohari Kuu ya Dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*). Bima ya afya ni sehemu ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambao unamhakikishia mwananchi kwamba yupo salama wakati afya yake itakapotetereka. Kamati inasikitishwa sana na suala la Bima ya Afya kubaki kwa wananchi wachache ambao wana uhakika na kipato na kuwaacha kando wale ambao hawana uhakika na kipato, hawajui kesho yao na ndiko ambako wananchi wengi wako katika hali hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeomba mara nyingi kufahamu mchakato wa Bima ya Afya kwa Wote

(Universal Coverage) lakini mrejesho ambao Kamati imekuwa ikipata kutoka Serikalini kuititia Wizara ya Afya kuhusu hatua ambayo Serikali imefikia ni kuwa bado ipo kwenye mchakato wa Bima ya Afya kwa Wote. Kamati inajuliza lini mchakato huu utakamilika, kwa nini Serikali isiende kujifunza kutoka kwa jirani ambao wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika suala hili. Je, hakuna cha kujifunza kutoka kwao, nini kauli ya Serikali kuhusu suala la bima ya afya kwa wananchi wote? Ikumbukwe kwamba maendeleo ya nchi huletwa na wananchi wenyewe afya bora na afya bora inapatikana kwa wananchi kuwa na bima ya afya ambayo inaweza kupatikana wakati wowote na mahali popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uzazi salama; kumekuwa na changamoto ya masuala ya uzazi salama katika nchi yetu hasa kwa watoto walioko katika umri wa shule. Hali inavyoonesha kwamba wananchi ambao watoto wao wanakumbana na changamoto ya kupata mimba shulenii wameanza kuchukuliwa hatua watoto wenyewe pamoja na wazazi wao. Hali ambayo inaonesha kwamba kumekuwa na ongezeko na ongezeko hilo linasababishwa na wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha katika masuala ya uzazi. Kamati inasisitiza Serikali iweke mkakati wa kuanza kutoa elimu kwa wananchi wake na ikibidi iingizwe katika mtaala wa shule ili watoto waanze kupatiwa mafunzo hayo wakiwa shulenii ili kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *sanitary pads*; mtoto wa kike anapitia changamoto nyingi katika kuhakikisha anapata elimu bora kwa maendeleo ya yake na Taifa kwa ujumla. Changamoto hiyo ikiwemo kupoteza siku zisizopungua tano katika mwezi akiwa anaiingia katika siku zake. Ili kupunguza changamoto hiyo Kamati inashauri, tauko safi kwa watoto wa kike zitolewe bure au ziondolewe kodi kwa nia ya kumkomboa mtoto wa kike kwani watoto wa kike wengi wamekuwa wakishindwa kwenda shule wakiwa kwenye hedhi kutokana na ukosefu wa *sanitary pads*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya maendeleo ya wanawake. Serikali imekuwa ikitenga

fedha kwa ajili ya kuwasaidia akina mama kujikwamua kiuchumi kwa maendeleo yao kwa njia ya mikopo yenye riba nafuu kupitia Fungu 53, Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Kamati inashauri kwamba, Serikali ihakikishe fedha zinazotengwa kwa ajili ya akina mama zinatolewa kwa kuwa wanawake wengi wanaishi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utambuzi wa wazee na kupewa vitambulisho rasmi; katika kikao cha Kamati na Wizara, Waziri aliahidi kutoa vitambulisho vya wazee lakini mpaka sasa havijatolewa hii inasikitisha sana. Pamoja na kuwa na Sera ya Wazee iliyopitishwa mwaka 2003 na ikatarajiwa Muswada wa Sheria hiyo ya Wazee kwa ajili ya kuwasimamia lakini mpaka sasa Muswada huu bado haujaletwa Bungeni. Kamati inajiliza, je, hakuna wazee au wazee wa nchi hii thamani yao imepotea? Ikumbukwe kwamba kijana wa leo ni mzee wa kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa wodi ya wajawazito. Wizara ya Afya imepata ufadhili wa kujenga wodi kwa ajili ya wajawazito kwa viwango vinavyohitajika kuitwa wodi ya wajawazito kwa maana ya chumba cha kujifungulia, chumba cha upasuaji, chumba cha kutunza damu salama na nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chumba cha kuhifadhia miili kwa maeneo ambayo hayana huduma hiyo. Upatikanaji wa fedha hizi ni juhudi binafsi za Waziri kuzitafuta kutoka kwa wafadhili. Kamati inaipongeza Wizara ya Afya kwa juhudhi hizo na ni maoni ya Kamati kuwa, fedha hizo zisimamiwe na Wizara ya Afya yenye kama ambavyo Wizara ya Elimu inafanya na kupata mafanikio makubwa katika Mradi wa EPforR.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa ugatuaji wa madaraka. Katika taarifa ya Kamati ya mwaka 2017 ilitoa maoni na mapendekemo kuhusu mfumo wa ugatuaji wa madaraka (*D by D*) ambao umekuwa ukisababisha Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati kukosa mamlaka ya

kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kutokana na masuala yanayohusu Wizara hizo kugawanyika katika Wizara mama na TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona ni vyema mfumo huu ukafanyiwa tathmini na kuona kama bado unatufaa kwa ajili ya kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara husika hasa Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya. Ni vyema masuala ya elimu na afya yakawa chini ya msimamizi mmoja badala ya kugawanywa katika Wizara zaidi ya moja. Aidha, kuna umuhimu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na Kamati ya Serikali za Mitaa kufanya vikao vya Kamati pamoja pale inapotokea hitaji la kujadili masuala ya afya na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa wataalam wa afya nchini. Nchi yetu imekuwa ikikumbwa na changamoto ya wataalam wa afya wakiwemo madaktari bingwa katika maeneo mengi hapa nchini hali inayopelekea wagonjwa wengi kuteseka kwa kusubiri matibabu kwa muda mrefu na wengine hata kupoteza maisha yao, hili limekuwa ni hitaji la kila Mbunge humu ndani. Kamati inaona kwamba changamoto hii si kwa sababu ya wataalam hakuna, lakini ni Serikali haijaamua kutoa nafasi za ajira za kutosha kwa ajili ya kukidhi mahitaji haya. Kamati inashauri kuwa ni vyema Serikali itoe ajira nyingi kwa wataalam hawa wakiwemo madakatari bingwa muhimu kwa afya na maisha ya Watanzania kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ongezeko la ukatili wa kijinsia katika jamii zetu hapa nchini ikiwemo kwa watoto, wanawake na wanaume pia ingawa taarifa zimekuwa zikipatikana kwa wanawake na watoto pekee. Ukatili wa wanawake na watoto umekuwa ukiongezeka siku hadi siku. Kamati inashauri Serikali kuja na mkakati madhubuti wa kutatua tatizo hili ikiwemo utoaji wa elimu ya ukatili wa kijinsia, kuongeza madawati ya jinsia katika vituo vya polisi ili kuweza kusaidia kutatua matatizo mengi yakiwemo magonjwa ya akili yatokanayo na ukatili wa kijinsia

ikiwemo kubakwa, unyanyasaji, kunyimwa haki ya ndoa na mengine mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa taasisi mbalimbali; Wizara ya Afya imekuwa ikitekeleza majukumu yake ikisaidiana na taasisi mbalimbali inazozisimamia pamoja na changamoto zote inazokabiliana nazo. Kamati inazipongeza baadhi ya taasisi kwa kufanya kazi vizuri zikiwemo Mamlaka ya Chakula na Dawa (*TFDA*), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Bohari ya Dawa (MSD) na Taasisi ya Mifupa (MOI). Kipekee JKCI imekuwa na ubunifu mkubwa na wenye tija kwa Taifa kwa namna inavyotekeleza majukumu yake. Serikali haina budi kuunga mkono juhudhi hizo kwa kuiwezesha kifedha ili ifike mahali wagonjwa kutoka nje ya Tanzania waje kutibiwa hapa nchini na waweze kuitangaza hospitali yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, ni maoni ya Kamati kuwa kwa utendaji huu bora wa Hospitali ya Muhimbili, Serikali itaendelea kuisimamia hospitali hii ili iweze kuendeleza na kuongeza viwango vyake bora zaidi vya utoaji wa huduma ya afya kwa wananchi. Ni imani ya Kamati kuwa Chuo Kikuu cha Tiba cha Muhimbili kitaendelea kuitumia Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kuwa hospitali yake ya kufundishia kama ilivyokuwa kwa kipindi chote tangu chuo hicho kilipoanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma ambayo ipo chini ya Chuo Kikuu cha Dodoma imejengwa kwa ubora mkubwa na kuwekwa vifaa vya kutosha na vya kisasa. Hospitali hii inakabiliwa na changamoto ya watumishi ambao wangeweza kutoa huduma kwa wananchi. Ni maoni ya Kamati kuwa hospitali hii haitumiki ipasavyo (*under-utilized*) ikilinganishwa na ubora wake kwa maana ya miundombinu, vifaa na vifaa tiba. Kamati inaishauri Serikali, ipeleke watumishi wa kutosha katika Hospitali ya Benjamin Mkapa ili iweze kuhudumia wakazi wa Dodoma na hata nje ya Dodoma ili iweze kupunguza msongamano mkubwa uliopo katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma ifahamikayo kama *General Hospital*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Chakula na Lishe; Kamati inaona ni wakati sasa Serikali itambue lishe ni kinga na tiba tosha kwa magonjwa mengi hasa yasiyo ya kuambukiza (*Non Communicable Diseases*). Hivyo, Idara hii ipewe bajeti ya kutosha ili kutoa elimu ya umuhimu wa lishe bora katika kukabiliana na magonjwa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na taasisi zake zinakumbana na changamoto mbalimbali ambazo Kamati inapenda kuzitolea maoni, ushauri na mapendelekezo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Utangazaji la Taifa (*TBC*); Kamati inaishauri Serikali kufanya mapinduzi ya mikakati ya namna ya kuweza kuliboresha shirika hili ili liweze kufanya kazi yenye tija kwa shirika lenyewe na Taifa kwa ujumla katika kutoa habari zenyne uhakika. Ni wakati sasa Shirika hili kujifunza kutoka katika makampuni binafsi ya utangazaji kama vile Azam Tv na mengineyo kwa ajili ya kufanya uboreshaji wa Shirika hilo. Serikali ikiona inapendeza itangaze zabuni ili kampuni binafsi waweze kusaidia uboreshaji huo kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA); Baraza hili liliundwa kwa ajili ya kuboresha na kusimamia kazi za wasanii hapa nchini kwa kuwapa miongozo mbalimbali ya namna ya kuweza kufanikisha kazi zao. BASATA badala ya kuwa mwelekezaji kwa wateja wake imegeuka kuwa mahakama ya kuhukumu wasanii pale wanapokesea tu lakin wanapofanya vizuri Baraza hili halisikiki kuwapa motisha au kuwapongeza wasanii hao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na mwenendo wa kuwafungia wasanii wanaokiuka yanayoitwa maadili ya Mtanzania kwa mujibu wa BASATA, lakin hakuna katika matamko hayo kwamba tulikaa na msanii huyo kumuelekeza misingi na utaratibu wa kuwa msanii. Katika taarifa za Baraza hakuna mahali panapoonesha kuwa kuna vikao vilivyowahi kufanyika na wasanii chipukizi, wakongwe kwa maana ya kuwaelekeza namna ya kuenenda kama

msanii wa Kitanzania. Kamati inaona kuna changamoto ya mawasiliano kati ya Baraza na wasanii wa Kitanzania ambao ni wateja wake. Hivyo, Serikali kupitia BASATA liweke mikakati maalumu ya kuhakikisha inakuwa na mahusiano mazuri kati ya wasanii na Baraza ili wasanii waone Baraza ni sehemu ya kukimbilia na siyo sehemu ya kuikimbia. Kamati inaishauri Serikali kuliwezesha Baraza hili liweze kutimiza majukumu yake kiuweledi kwa kufanya kazi kimizania badala ya kugeuka kuwa mahakama ya kuhukumu msanii aliyefanya vibaya pasipo na miongozo kwa msanii huyo kabla hajakosea. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA); Kamati inaishauri Serikali kutengeneza mpango mkakati ambao utasaidia kukuza lugha yetu ya kiswahili ndani na nje ya nchi kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa utamaduni na sanaa; nchi yoyote ile inatambulishwa na kazi ya utamaduni na sanaa yake na ni kazi kama kazi nyingine hapa nchini na duniani kote na inalipa kodi kubwa kwa Serikali husika. Utamaduni na sanaa ukiendeshwa vizuri utakuwa ni sehemu ya utalii na kuweza kuzuia vizazi vyetu kuiga utamaduni wa nje ambao unakwenda kinyume na maadili ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha wasanii wote nchini wanasa jiliwa na kupewa utambulisho maalum kwa ajili ya kusaidia kulipa kodi ya mapato lakini pia kuboresha maisha yao kama wasanii ikiwemo kuwaweka katika mfumo wa Bima ya Afya na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ili kuendelea kulinda hadhi yao katika jamii badala ya kudhalilika wapatapo majanga kama vile ugonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa tasnia ya filamu Tanzania; tasnia ya filamu duniani kote imekuwa ni sehemu ya utangazaji wa vitu mbalimbali vya nchi husika ikiwemo mila, desturi na utamaduni wa nchi, vivutio vya kitalii, lugha husika na hata uwekezaji katika nchi hiyo ambayo inaongeza tija katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Korea ya Kusini katika miaka 1990 iliweka mkakati wa kuwekeza katika kutangaza utamaduni wa nchi hiyo kupitia filamu, muziki na burudani ujulikanayo kama *Korean Wave* ambapo kwa kufanya hivyo mwaka 2004 iliingizia nchi hiyo pato la Taifa kiasi cha dola bilioni 1.8 ambaao ni sawa na asilimia 1.2 kwa uchumi wa Korea Kusini na mwaka 2014 iliingizia tena pato la nchi hiyo kiasi cha dola bilioni 11.6. Kwa mfano huo wa Korea ya Kusini ni maoni ya Kamati kwa Serikali kupitia Wizara kuiboresha tasnia hiyo kwa kuiga mfano wa Korea Kusini ambayo imefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Aidha, uboreshaji huo unaweza kufanyika kwa njia mbalimbali ikiwemo kupunguza urasimu wa kupata vibali vyta kupata mandhari halisi kwa ajili ya kurekodi filamu hizo kama maeneo ya polisi, bandari, mbuga za wanyama, Mlima Kilimanjaro na kwingineko. Hii itasaidia kutangaza utalii badala ya kuwa na filamu ambazo nusu saa nzima inaonesha mtu yupo kwa mganga wa kienyeji au kuonesha utapeli unavyofanyika. Kamati inaona ni wakati sasa wa kufanya mageuzi makubwa ya ukuzaji wa tasnia hii ili kuendeleza uibuaji na ukuzaji wa viwanda ikiwemo viwanda vya filamu nchini na kuiingizia pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Wizara hii pamoja na taasisi zake inakumbana na changamoto mbalimbali ambazo Kamati inapenda kuzitolea maoni, ushauri na mapendekezo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı Stadi (*VETA*); Kamati inasisitiza kuvifanyia tathmini vyuo vyote vya *VETA* nchini ili kubaini kama vinatekeleza malengo ya kuanzishwa kwake au la na kama kuna haja ya kuhakikisha kila Wilaya inakuwa na Chuo cha Ufundı Stadi kwa ajili ya kuzalisha taaluma mbalimbali kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Huria (*Open University of Tanzania*) kilianzishwa kwa malengo ya kuwawezesha wale ambaao hawakuweza kuendelea na

utafutaji wa elimu kwa mfumo ambao umezoleka na hasa kwa wale ambao wako makazini. Kwa msingi huo, chuo kiliwekewa utaratibu kwamba kwa mtu ambaye hakuwa na sifa za kuendelea na masono ya ngazi ya juu alitakiwa kuanza na kozi ya msingi (*foundation course*) ili aweze kupata sifa za kuendelea na masomo ya elimu ya juu. Utaratibu huu ulianza kuigwa na vyuo vingine ambavyo havikuwa kwa malengo ya mfumo huu na kuonekana kupoka majukumu ya Chuo Kikuu Huria na hata kusababisha kufanya kozi ya msingi chini ya muda ule ambao ni utaratibu kwa mujibu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inahoji, je, Chuo Kikuu Huria kinafutwa na kuwa katika utaratibu wa vyuo vingine au la? Kama lengo la Serikali chuo hicho kiendelee, hivyo Kamati inaomba kulitaarifu Bunge ili liweze kuishauri Serikali kuhakikisha inarejesha majukumu ya chuo hicho kama ilivyokuwa hapo awali na kuweza kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mloganzila; hospitali ya kisasa kabisa iliyojengwa kwa weledi mkubwa imekamilika na nchi nzima ilishuhudia uzinduzi wake. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kukamilisha mradi huo ulijengwa kwa viwango vikubwa na kwa wakati mfupi ikilinganishwa na miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mapendekezo ya Kamati kwa Serikali kwamba ili kuendeleza ubora ule wa majengo, ihakikishe inapeleke watumishi wa kutosha wakiwemo wakufunzi na wafanyakazi wa kada nyingine mbalimbali wenye weledi na wapewe motisha kulingana na utendaji wao wa kazi ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi. Ikifanyika hivyo hospitali ya Mloganzila inaweza ikawa ni hospitali bingwa katika utoaji wa huduma bora ya afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima; Kamati inashauri kwamba taasisi hiyo ivunjwe kwani hakuna majukumu ya kutekeleza badala yake imegeuka kuwa kijiwe cha kupumzikia endapo mtumishi ataonekana

hatoshi katika kitengo chake cha awali ndani ya Wizara ya Elimu. Kwa kufanya hivyo basi kutakuwa kumeipunguzia mzigo Serikali na watumishi hao wapangiwe majukumu mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya wahadhiri na walimu nchini; Kamati iliishauri Serikali kuititia TAMISEMII kwa kushirikiana na Chama cha Walimu kufanya uhakiki wa madeni haya ya walimu ili waweze kulipwa stahiki zao. Kwa masikitiko makubwa mpaka leo hii hakuna taarifa yoyote iliyofika mbele ya Kamati au Bunge ya utekelezaji wa ushauri huu na kueleza ni kwa kiasi gani walimu wamelipwa au la. Naliomba Bunge lako, lichukue hoja hii na kuiagiza Serikali kutekeleza uhakiki huo na kuwalipa madeni walimu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitabu vyenye makosa kuondolewa shulen; wakati Bunge lako Tukufu likijadili Bajeti ya Serikali ya mwaka 2017/2018 iliibuka hoja ya suala la uchapisha na usambazaji wa vitabu vilivyo na makosa mengi ya kimaudhui pamoja na mantiki yake hali iliyopelekea Kamishna wa Elimu na baadhi ya watendaji waliohusika katika jukumu hilo ndani ya Wizara ya Elimu kusimamishwa kazi na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaviondoa vitabu hivyo mapema iwezekanavyo katika shule zote na kuviharibu. Aidha, Serikali isambaze vitabu vipya visivyo na makosa kwa ajili ya kuendeleza ufundishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mwenendo wa ufaulu katika elimu ya sekondari; nchi yetu imeweka utaratibu wa ufaulu katika elimu ya sekondari kwa viwango vya madaraja kwa maana daraja la kwanza mpaka daraja la nne (*division one* mpaka *division four*). Kwa utaratibu huo, mwenendo wa ufaulu katika elimu ya sekondari haujawa wa kuridhisha kwani ufaulu huo kwa daraja la kwanza hadi la tatu haujawahi kuuvuka asilimia 80 ya idadi ya watoto waliofanya mtihani katika mwaka husika katika shule za Serikali na shule binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa matokeo hayo, kama ilivyooneshwa katika jedwali, ni dhahiri kuwa asilimia 70 ya watoto walipata daraja la nne na daraja sifuri. Kamati inahoji ni Taifa gani ambalo tunajaribu kulitengeneza na ikumbukwe kwamba elimu ndiyo msingi wa maisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali hufanya tathmini ya ufaulu wa watoto kila mwaka, Kamati ina maoni kuwa taarifa hizo hazifanyiwi kazi kwa ajili ya kutatua changamoto zinazoikabili Wizara ya Elimu ili kuhakikisha inaboresha kiwango cha ufaulu wake wa mwaka uliopita na kuweza kuboresha ufaulu na matokeo yasijirudie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali pamoja na uboreshaji wa masuala mengine ya msingi ikiwemo uongezaji wa walimu pamoja na uboreshaji wa miundombinu, ifanyile kazi maoni na mapendekezo ya taarifa ya tathmini inayofanywa kila mwaka ili iweze kuboresha ufaulu wa watoto katika ngazi za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo Katika Elimu (Education Program for Results – EPforR). Wizara ya Elimu imekuwa ikitekeleza mradi unaojulikana kama Lipa Kulingana na Matokeo (EPforR) ambao unafadhiliwa na wafadhili. Kamati ilipata fursa ya kutembelea moja ya shule ambazo zipo katika mradi huo katika Shule ya Msingi Ihumwa iliyoko Mkoani Dodoma. Kamati illridhishwa na utekelezaji huo. Ni maoni ya Kamati kwamba mradi huo kwa usimamizi bora ambao umefanywa na Wizara yenye we na siyo TAMISEMI, utakuwa na mafanikio makubwa sana. Kamati inashauri Serikali kuwa Wizara ya Elimu iendelee na usimamizi wa mradi huu uliopata matokeo yanakusudiwa katika kuboresha shule hizo. Aidha, Kamati inashauri Serikali kupitia Mradi wa (EPforR) jenje shule za mfano (model school) katika kila Halmashauri ambayo ina viwango vya kuitwa shule ya msingi ambayo imekamilika. [Maneno haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufadhili wa elimu ya juu kwa watoto wanaofanya vizuri katika masomo; katika Taarifa za

Kamati ambazo ziliwahi kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu, Kamati ilitoa mapendekezo kwamba katika matokeo ya Kidato cha Sita kumekuwa na watoto wanaofanya vizuri sana katika masomo yao yaani kupata daraja la kwanza alama tatu (*division 1.3*). Watoto hao wanakuwa wamefanya juhudii kubwa sana kwa kufaulu kwa kiwango hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kamati tena Serikali iwave motisha watoto hawa kwa kuweka kiwango cha idadi ya wanafunzi angalau 100 tu ambaa watapata ufadhili wa moja kwa moja wa Serikali katika vyuo vikuu vinavyotambulika duniani na ufadhili huo usiingiliane na hali ya kipato cha mzazi wa mtoto. Kwa kufanya hivyo kutawapa watoto sababu nydingine ya kufanya vizuri zaidi katika masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya mwisho ni hitimisho; napenda tena kukushukuru kwa kunipa fursa hii kuwasilisha taarifa ya shughuli za Kamati.

Napenda kuwashukuru Mawaziri wote, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Waziri Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Juliana Shonza, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Naibu wake Mheshimiwa William T. Olenasha na Makatibu Wakuu na watendaji wa Wizara hiso. Kipekee zaidi namshukuru Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa ushirikiano wake. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini na ushirikiano wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai, watendaji Ndugu Athuman B. Hussein, Ndugu Dickson Bisile, Makatibu wa Kamati Ndugu Pamela Pallangyo, Ndugu Agnes Nkwera pamoa na wasaidizi Gaitana Chima na Ndugu Waziri Kizingiti kwa kazi kubwa wanayoifanya na kuisaidia Kamati ikiwemo kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuelezea shughuli zilizoteklezwa, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo mbele ya Bunge lako Tukufu, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofii)

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA SHUGHULI ZA
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA
MAENDELEO YA JAMII KWA MWAKA 2017/2018 KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Mwaka kuhusu majukumu na shughuli zilizoteklezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii katika kipindi cha 2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Spika, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 113 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kwa kugawanyika katika sehemu kuu tatu (3). Sehemu ya kwanza ni utangulizi unaofafanua, muundo wa majukumu pamoja na maelezo ya jumla. Sehemu ya pili inahusu Uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Katika sehemu ya tatu Kamati imebainisha Maoni na Mapendekezo na kuhitimisha Taarifa katika sehemu ya mwisho.

1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5(5) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 kimeipa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii jukumu la kusimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

- a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;
- b) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na
- c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kusimamia majukumu ya Wizara hizo, Kamati hii ambayo ni moja kati ya Kamati tisa (9) za Kudumu za Bunge za Kisekta zilizopewa majukumu manne kwa mujibu wa kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, majukumu hayo ni;

- a) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazosimamia;
- b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazosimamia;
- c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo na;
- d) Kufuatilia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hizo.

1.2 Shughuli zilizotekelizwa na Kamati

Mheshimiwa Spika, Wakati wa kutekeleza majukumu yake Kamati kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018, Kamati ilikuwa na shughuli zifuatazo:-

- i) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi zilizoko katika Wizara hizo;

- ii) Kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- iii) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Bajeti za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- iv) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;
- v) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Utendaji wa Wizara kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2017);
- vi) Kuchambua Miswada Miwili (2) iliyowasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa; na
- vii) Kupokea Semina na mafunzo mbalimballi yaliyotolewa kwa ajili ya kuboresha ushauri katika sekta ya Elimu, Afya na Habari.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii inaeleza kwa kina kuhusu utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018.

2.1 Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

2.2 Kupokea Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali

Mheshimiwa Spika, Katika nyakati tofauti kuanzia Machi 2017 hadi Januari 2018, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa za

Utendaji wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo kama ifuatavyo:-

a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Mheshimiwa Spika, Baada ya Bunge kupitisha Bajeti ya Serikali ikiwemo ya Wizara hii, Kamati iliendelea kufanya kazi na wizara kwa kupokea taarifa ya Wizara na Taasisi zake ikiwemo Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Hospitali ya Benjamin Mkapa na Hospitali ya Magonjwa ya akili Mirembe zilizoko Mkoani Dodoma, ili kupata taarifa za utendaji wa Wizara kupitia Taasisi zake. Utendaji wake ni kama ifuatavyo;

i) Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA)

Mheshimiwa Spika, Katika kikao cha Kamati kilichofanyika tarehe 29 Agosti, 2017, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ambayo ndio mamlaka iliyopewa jukumu la udhibiti wa usalama na ubora wa chakula nchini, dawa, vipodozi, pamoja na vifaa tiba na vitendanishi. Taarifa ya TFDA ilionesha kuwepo kwa ongezeko la ukusanyaji wa maduhuli kutoka kiasi cha shilingi 34,735,783,943/= kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 hadi kiasi cha shilingi 38,879,986.47/= kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017. Ongezeko hili linatokana na kuimarika kwa mifumo ya makusanyo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imefanikiwa kuongeza usajili wa bidhaa mbalimbali baada ya kuzifanyia tathmini, kwa mfano, bidhaa za vipodozi zilizosajiliwa katika Mwaka **2016/2017** ni **1413** ambazo ni aina tofauti ikilinganishwa na **1213** za **2015/2016** sawa na ongezeko la bidhaa **200 sawa na asililimia 16.5**. Sanjari na hili, Mamlaka imefanikiwa kuongeza ukaguzi wa maeneo mbalimbali kutoka **6,839** kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 hadi kufikia **17,250** sawa na ongezeko la **asilimia 60** kwa Mwaka wa Fedha **2016/2017** ambapo **asilimia 75** ya maeneo yaliyokaguliwa kwa mwaka **2016/2017** yalikidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, Ni matarajio ya Kamati kwamba Taasisi hii itaendelea kupata mafanikio zaidi kwa kuendelea kuboresha utendaji wake wa kazi ili kudhibiti ubora wa chakula na Dawa pamoja na vitendanishi. Aidha, itaimarisha mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa maduhuli katika taasisi hiyo kama ambavyo imeonekana kuimarike katika mwaka wa fedha 2015/2016 na 2017/2018.

ii) Hospitali ya Afya ya Akili, Mirembe - Dodoma

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utendaji wa Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe ambayo ilionesha kuwa ni moja kati ya Hospitali kongwe nchini. Hospitali ilianza kujengwa mnamo mwaka 1925 na Serikali ya Mkoloni Mwingereza mkoani Dodoma. Hospitali inahudumia wagonjwa wa akili raia (*Civill mental patients*) wakati Taasisi yake ya Isanga inatoa huduma kwa wagonjwa wa Akili wahalifu (*Criminal Mental Patient*). Aidha, kwa wastani wagonjwa kati ya 7-10 wa akili hulazwa kila siku hivyo kuwa na wastani wa wagonjwa 317 wodini kila siku. Kwa upande wa wagonjwa wa nje (*Out Patient Department*), Hospitali inahudumia wastani wa wagonjwa wa akili 43 kwa siku ambapo wapya ni kati ya 7-10. Mbali na wagonjwa wa akili, Hospitali inatoa huduma kwa magonjwa mengine mbalimbali ambapo kwa siku inahudumia wastani wa wagonjwa 119.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Hospitali hii hasa ikizingatiwa kuwa ndiyo Hospitali kubwa ya Afya ya Akili nchini, lakini hali ya Hospitali hii hairidhishi na haiendani na hadhi ya Mkoa wa Dodoma kama Makao Makuu ya Nchi. Kamati ilishuhudia uwepo wa majengo chakavu, majengo ambayo yalijengwa na mkoloni miaka 92 iliyopita pamoja na upungufu wa watumishi 375 sawa na **asilimia 60** ikillinganishwa na mahitaji ya watumishi 616.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwama hospitali hii ipo katika mji ambao kwa sasa ndiyo makao makuu ya nchi na hivyo kufanya mji kuwa na ongezeko kubwa la watu ambapo ni wazi kwamba hata uwezekano wa kuongezeka kwa

wagonjwa wa akili upo, hivyo basi Kamati inashauri Serikali ifanye mkakati maalumu kwa kusaidia na Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI ili kuweza kufanya maboresho makubwa kwa ajili ya kuhakikisha huduma kwa wagonjwa wa akili inaimarishwa na kutolewa kwa wananchi.

b) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Mheshimiwa Spika, Katika vikao vyatubu vya Kamati vilivyofanyika mwezi Agosti, 2017 mjini Dodoma, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Kamatoi ilipokea taarifa ya utendaji wa Wizara katika Taasisi ya COSTECH, Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam (DIT) na Chuo Kikuu cha Nelson Mandela kilichopo Arusha. Utekelezaji wa Taasisi hizo ni kama ifuatavyo;

i) Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utendaji wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) mnamo tarehe 6 Septemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu ya DIT kumekuwepo na upanuzi wa miundombinu ya Taasisi hiyo ambapo Kamati ililitembelea wakati wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kutoridhika na utekelezaji wa mradi huo. Aidha katika ziara hiyo Kamati iliomba ipate taarifa ya utekelezaji wa mradi wakati wa vikao vingine vyatubu vya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Mpaka wakati Kamati inakaa kikao cha tarehe 9 Septemba, 2017 mkandarasi wa jengo hilo alikuwa hajamaliza kazi yake kwa asilimia 100. Kamati ilihoji kwanini jengo halijakamilika ili liweze kuanza kutumika na changamoto yake kubwa ilikuwa ni fedha kwa ajili ya kumalizia.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaomba Serikali ifanye ukaguzi wa kimahesabu katika Taasisi hiyo kuhusu mradi huo kwani ni mradi ambao umechukua muda mrefu kuliko ambavyo

ilikuwa imetarajiwa na taarifa hiyo ifike mbele ya Kamati yako na kama itaonekana inafaa basi ifike katika kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa ajili ya kujadili.

c) **Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Spika**, Katika kuendelea na utekelezaji wa majukumu ya Bunge, kamati ilipokea taarifa ya Wizara ya Habari kuhusu baraza la michezo Tanzania (BMT) na Shirika la Uchapishaji Magazeti ya Serikali (TSN)). Kamati ilipokea na kujadili Taarifa za Utendaji wa Taasisi mbalimbali zikiwemo:-

i) **Baraza la Michezo Tanzania (BMT)**

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha kamati na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kilichofanyika tarehe 4 Septemba, 2017 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utendaji wa Baraza la Michezo Tanzania. Katika kikao hicho Kamati ilielezwa kuwa Baraza kwa kushirikiana na Vyama vya Michezo limeendelea kuwezesha timu na wachezaji wa Tanzania kushiriki katika mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa. Aidha, Baraza liimeendelea kusimamia uanzishwaji wa Michezo mingi mipyka kama Baseball, Woodball, Football freestyle, Rolliball na Martial Arts.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilielezwa kuwa Baraza limekuwa likikumbana na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na:-

- Baadhi ya vipengele vya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa ya Mwaka 1967 kuwa na mapungufu yanafanya utendaji kazi wa Baraza kuwa mgumu;
- Gharama kubwa za vifaa vya michezo inayotokana na kodi inayotozwa hasa kwa vifaa kutoka nje ya nchi na vile vinavyotolewa na Mashirikisho ya Kimataifa kama msaada;
- Uvamizi na kubadilishwa kwa matumizi ya viwanja vya michezo na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya burudani.

ii) Shirika la Uchapishaji Magazeti ya Serikali (TSN)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Uchapishaji Magazeti ya Serikali (TSN) linaendeshwa kwa Sheria ya Makampuni ya Mwaka 1961 kwa hisa za **asilimia 99** zinazomilikiwa na Serikali na **asilimia 1** inamiliikiwa na Mhariri Mtendaji kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Kampuni huchapisha magazeti mbalimbali ya lugha ya Kiswahili na Kingereza ambayo ni Habari Leo, Spotileo, **Daily News na Sunday News**. Lakini pia Kampuni hutoa vijarida mbalimbali vinavyolenga makundi maalum kwa lugha ya Kiswahili na Kingereza

Mheshimiwa Spika, shirika la uchapichaji Magazeti pamoja na mafanikio katika kutekeleza majukumu yake, linakumbana na changamoto mbalimbali za utendaji na kifedha pia zikiwemo;

- Uzorotaji wa biashara ya matangazo;
- Ucheleweshwaji wa kulipwa madeni ya matangazo kiasi cha shilingi Bilioni 7.2 ambako kunakwamisha utendaji wa Taasisi na madeni mengi ya kiwa ni ya Serikali na
- Gharama kubwa za usambazaji wa magazeti ikiwemo ukosefu wa usafiri wa uhakika;

2.3 **Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 97 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ukaguzi wa Miradi mbalimbali iliyo chini ya usimamizi wa Wizara inazozisimamia ambayo ilitengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea jumla ya Miradi kumi na moja (11) ambayo ilitengewa fedha katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

- i) Mradi wa Upanuzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA);
- ii) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam;
- iii) Mradi wa Usikivu TBC;
- iv) Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo;
- v) Mradi wa Upanuzi wa Hospitali na Uwekaji wa Mashine za CT; Scan na LINAC katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* (ORCI);
- vi) Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Kufundishia na kutoa Huduma Mloganzila;
- vii) Mradi wa Ujenzi wa DIT-Teaching Tower;
- viii) Mradi wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH;
- ix) Mradi wa Ununuzi wa Vifaa Tiba wa Hospitali ya Taifa Muhimbili;
- x) Mradi wa Ununuzi wa Mitambo na Vifaa Tiba katika Taasisi ya Mifupa (MOI);
- xi) Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya kuzalisha dawa Asili wa Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR).

Mheshimiwa Spika, Taarifa za ukaguzi wa Miradi hii zilishawasilishwa katika Taarifa za Uchambuzi wa Bajeti zilizowasilishwa mwezi Mei 2017 na hali ya upatikanaji wa fedha kwa miradi mingi siyo ya kuridhisha kwani katika tathmini ya Kamati ilibaini kuwa kati ya Miradi 11 iliyokaguliwa yenye thamani ya shilingi **63,939,654,851** kiasi kilichotolewa kwa miradi yote ni shilingi **14,172,609,934** sawa na **asilimia 22** tu ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi hiyo ya maendeleo.

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HEDDUMA MA MAENDELEO YA JAMII, HALI YA UPATIKANAJI WA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ZA WIZARA INAZOSIMAMIA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017						
WIZARA	NAMBA YA MRADI	FUNGU	JINA LA MRADI	KILICHOIDHINISHWA	KILICHOOTELEWA	%
WIZARA YA AFYA NA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO	5412	52	Mradi wa Upuzi Hospitali na Uwekaji wa Mashine za CT scan na LINAC Taasisi ya Saratani Ocean Road	5,000,000,000/=	5,000,000,000/=	100
	5491		Mradi wa Ununuzi wa Vifaa liba katika Hospitali ya Taifa Muhimibili	4,000,000,000/=	0	0
			Mradi wa Ununuzi wa Mitambo na Vifaa liba katika Taasisi ya Mifupa (MOI)	4,800,000,000/=	0	0
	2208		Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya kuzalisha dawa asilia wa Taasisi ya Utaliti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)	8,000,000,000/=	0	0
WIZARA YA HABARI, UTAMADU NI, SANAA NA MICHEZO	4279	46	Mradi wa Usikuri TBC	1,000,000,000/=	0	0
	4353		Mradi wa Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo	300,000,000/=	100,000,000	33.3
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOGIA	6361	96	Mradi wa Upuzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokine-SUA	4,000,000,000/=	0	0
	6350		Mradi wa Upuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Dar Es Salaam	9,443,256,575/=	0	0
	6364		Mradi wa Hospitali ya Kufundisha na kutoa huduma - Mloqanzila	14,549,727,933 /=	0	0
	4384		Mradi wa Ujenzi wa Dif - Teaching Tower	5,000,000,000/=	5,000,000,000	100
	6345		Mradi wa Mfuko wa Utaliti na Maendeleo wa COSTECH	12,846,670,343/=	4,072,609,934	31.7
JUMLA				63,939,654,851	14,172,609,934	22.2

2.4 Kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 na mchakato wa Bajeti za Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ilikutana na Wizara inazozisimamia kwa lengo la kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kuwasilisha Taarifa zake Bungeni kwa nyakati tofauti mnamo mwezi Februari, 2017.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Bajeti imekuwa ni chagamoto kwani Wizara karibu zote zimekuwa hazipewi fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge kama ifuatavyo;-

a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee wa Watoto

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na Utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Utekelezaji wa Ushauri na maoni ya kamati haukutekelezwu vile ipasavyo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa fedha za kutosha na kwa wakati. Changamoto hizi zimeipelekea Wizara kukwama katika kutekeleza majukumu yake kiufanisi kama ilivyokuwa inatarajiwa na wengi. Kamati imekuwa ikielezwa nia na mipango mikakati mbalimbali ya Wizara pasipokuwa na utoaji wa taarifa kutoka wizarani wa nini kimefanyika hasa katika mawanda ya maeneo halisi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Kamati ilichambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 na kutoa maoni na mapendekezo yake kwa Serikali ambayo yaliwasilishwa Bungeni tarehe **03 Mei, 2017** ambapo Wizara kuititia Fungu 52 ilitengewa kiasi cha **shilingi Triliioni 1.077** ikiwa ni ongezeko la takribani **asilimia 25.9** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa Fedha wa 2016/2017. **Kamati inasisitiza Serikali kwa ongezeko hilo**

la fedha lipelekwe kadiri ilivyopangwa badala ya kuongeza fedha katika karatasi bali Serikali iifanye kwa vitendo.

b) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa mwaka 2016/2017 wa Kamati ulikuwa wa kuridhisha kwa kiasi chake. Utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii hayakuwa ya kuridhisha kutokana na changamoto ya kutopatiwa fedha kwa wakati ambao ulitarajiwa. Aidha, Kamati ilionna kwamba katika Wizara ambayo haipewi kipaumbele cha kupewa fedha za utekelezaji, Wizara ya Habari imekuwa katika orodha hiyo ambapo Kamati inaona si sawa, kwani Wizara hii hakuna siku ambayo haijatumika kwa ajili ya kuwasiliana na umma katika matukio mbalimbali kwa maana ya upashanaji wa habari.

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote ambayo haina tasnia ya habari bora nchi hiyo ipo kisiwani kwani haitahabarishwa nini kinaendelea ndani na hata nje ya nchi, **hivyo Kamati inaendelea kusiistiza kuipa kipaumbele Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ili iendelee kutekeleza majukumu yake kama ambavyo inatarajiwa.**

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2017 wakati wa ukaguzi wa miradi Wizara ilikuwa haijapokea hata shilingi moja ya fedha iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, kwa kutopeleka fedha hizo za maendeleo katika Wizara utekelezaji wa majukumu mengine na Taasisi zake kama vile TaSuBa haukufanya ikiwa ni pamoja na ujenzi wa uzio wa chuo hicho cha Bagamoyo ambapo ilisabaisha uzio huo kutojengwa kama ilivyokuwa imepangwa.

c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Mheshimiwa Spika, Katika vikao vya Kamati vilivyopita na upitishaji wa Bajeti ya mwaka 2017/2018 Kamati ilitoa Ushauri na Mapendekezo kwa Wizara kwa ajili ya kuyafanyia kazi ya Mwaka wa Fedha wa 2016/2017. Katika utekelezaji wa maoni

hayo Wizara ilifanikiwa kutekeleza maoni hayo kwa asilimia kubwa na Kamati inaipongeza Wizara kwa utekelezaji huo. Pamoja utekelezaji huo bado kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini kwenda Wizarani ingawa kila mwaka inaonekana Bajeti ya Wizara inaongezeka licha ya upatikanaji wa Fedha kuwa hafifu tofauti na inavyotarajiwa.

Kamati pia ilipokea Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara Mwaka kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kamati ilibaini kuwa hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka yaani Machi 2017, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **316,402,868,828/=** sawa na **asilimia 61.8** tu. Aidha, kuhusu Bajeti ya Maendeleo, Kamati ilibaini kuwa katika robo tatu ya Mwaka wa Fedha, Wizara imepokea jumla ya shilingi **Bilion 360.922** sawa na **asilimia 61.9** ya fedha iliyoidhinishwa **Bilion 582.670**. Kamati imebaini kuwa kiasi **hiki cha fedha kisichokidhi mahitaji ni moja ya sababu ya kutotekelzwa kwa Miradi ya Maendeleo ipasavyo.**

2.5 Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha Nusu Mwaka (Julai – Disemba 2017)

Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikisha Kamati inafuutilia kwa ukaribu utendaji wa Wizara, Kamati imojiwekea utaratibu wa kupokea Taarifa za Utekelezaji na Mpango wa Bajeti wa Wizara inazozisimamia kwa kipindi cha Nusu Mwaka. Hivyo basi, katika vikao vyake vya mwezi Januari 2018, Kamati ilipokea Taarifa hizo kwa kipindi cha Julai – Disemba 2017 kama ifuatavyo:-

a) Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto

Mheshimiwa Spika, katika vikao vya Kamati vilivyofanyika mwezi Januari 2018, Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 kwa kipindi cha nusu Mwaka kuanzia Julai hadi Desemba, 2017. Wizara

ya Afya inatekeleza majukumu yake kuititia mafungu mawili yaani **Fungu 52** –Idara Kuu Afya na **Fungu 53** – Idara Kuu Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Katika Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati mnamo tarehe **23 Januari, 2017**, Wizara hii ilionesa kuwa hadi kufikia mwezi Desemba 2017 ilikuwa imekusanya kiasi cha shillingi **Bilioni 118.848** sawa na **asilimia 52.8** ya shillingi **Bilioni 225.038** ya lengo lilokutwa limekadiriwa kukusanya kwa Mwaka mzima wa fedha wa Mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Katika **Fungu 52 Idara Kuu Afya**, ilikuwa imepokea fedha kiasi cha shillingi **Bilioni 224.816** sawa na **asilimia 41.7** ya kiasi cha **shillingi 538.869** ya fedha zilizopaswa kuwa zimepokelewa kwa kipindi hicho cha Nusu mwaka wa fedha. Aidha, ni **asilimia 20.8** tu ya fedha iliyoidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa mwaka mzima ndizo zilizokuwa zimepokelewa.

Mheshimiwa Spika, Ni tathmini ya Kamati kwamba fedha zilizotolewa na Serikali kwenda Wizarani ni kidogo sana kwani ni **asilimia 20** tu ikilinganishwa na matarajio kwa mujibu wa bajeti ambayo Bunge pia huwa inahusika katika kuichambua na kuipitisha. Hali hii inasikitisha sana kwani Kamati inaona ni kiasi kidogo sana cha fedha kilichotolewa ambacho kisingeweza kusukuma gurudumu la maendeleo ya sekta ya Afya ipasavyo. **Kamati inahoji je, kwa kipindi hiki cha miezi sita iliyobaki, Serikali itaweza kukamilisha asilimia 80 za fedha zilizobaki na kama ni ndiyo lini majukumu hayo yatakelezwa kwa kuwa mwaka mwingine wa bajeti utakuwa umeanza?**

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Fungu 53 Idara Kuu Maendeleo ya Jamii**, Kamati ilipokea taarifa ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara ambayo ilionesa hadi kufikia Mwezi Desemba 2017, makusanyo yalikuwa kiasi cha **shillingi Bilioni 1.223** sawa na **asilimia 58.2** ya lengo ambalo Wizara ilijiwekea kukusanya ambacho ni kiasi cha shillingi **Bilioni 2.101** kwa mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweka mifumo madhubuti ya ukusanyaji wa maduhuli hayo ndani ya Wizara ikiwemo mfumo wa ulipaji wa huduma kwa njia ya benki, udhibiti wa makusanyo mbalimbali, uboreshwaji wa huduma za bima na njia nyingine kwa mafungu yote mawili kwa maana ya Idara Kuu Afya Fungu 52 na Idara Kuu Maendelo ya Jamii Fungu 53 na kuweza kufikia zaidi ya lengo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilitoa taarifa kuhusu changamoto mbalimbali zinazoikabili katika utendaji kazi wake, ikiwemo changamoto ya upungufu wa rasilimali fedha na rasilimali watu kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Afya kulingana na mipango na mikakati ili kuweza kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kufuata mahitaji halisi. Aidha, baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya kutowasilisha mahitaji ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa wakati, wigo mdogo wa wananchi wanaohudumiwa kwa mfumo wa bima ya afya, ongezeko la watu wenye magonjwa yasiyo ya kuambukiza na Serikali kutopeleka fedha kwa ajili ya shughuli husika na ambazo hazitolewi kwa wakati ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kuboresha huduma za afya.

b) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2017 ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi **Milioni 449.514** sawa na **asilimia 29** ya kiasi ambacho kilikuwa kimekadiriwa kukusanywa na Wizara. Aidha, kwa kipindi hicho Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi **Bilioni 12.261** ambayo ni sawa na **asilimia 53.1** ya bajeti nzima ya Wizara ya mwaka mzima tu ya bajeti nzima iliyotengewa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo Wizara ilipokea kiasi cha shilingi **Bilioni 3.0** ambayo ni sawa na **asilimia 47.4** ya fedha zote zilizopangwa kutumika katika miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kupeleka fedha**

katika Wizara kwa zaidi ya asilimia 50 kwa kipindi cha Nusu mwaka.

c) **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utendaji wa Wizara hii ilionesa kuwa hadi kufikia mwezi Disemba 2017, Wizara ilikuwa imekusanya maduhuli ya kiasi cha **shilingi Bilioni 215.580** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya Wizara ambayo ni sawa na **asilimia 59** ya malengo ambayo Wizara ilikuwa imejivekea katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018. Aidha, katika ukusanyaji huo kuna baadhi ya Taasisi zilizokusanya maduhuli kwa kuvuka lengo na taasisi nyingine zilikusanya chini ya **asilimia 1** ya lengo walilojiwekea Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hiyo, hadi Desemba, 2017 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi Bilioni 711.595** sawa na **asilimia 53** ya bajeti nzima ya mwaka ya Wizara kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, katika fedha za maendeleo Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **shilingi Bilioni 373.756** kati ya hizo kiasi cha shilingi **Bilioni 290.492** sawa na **asilimia 77.7** ni fedha za ndani na kutoka kwa wahisani ni **shilingi Bilioni 83.263** sawa na **asilimia 32.3**. Fedha hizi ndizo zilizopokelewa kwa kipindi cha nusu mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, fedha za maendeleo zilizopokelewa na Wizara kwa ujumla wake ni sawa na **asilimia 40.7** tu ya fedha zote zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Ikumbukwe kwamba fedha za bodi ya mikopo zinajumuishwa katika fedha za maendeleo ya Wizara ambapo kiasi cha shilingi **Bilioni 253.984** sawa na **asilimia 67.9** ya fedha za maendeleo ya Wizra zilizopokelewa katika kipindi cha Nusu Mwaka zilitumika na Bodi ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na ndicho kinachofanya kiasi cha fedha za maendeleo ya Wizara hiyo kuonekana ni kikubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio mengi yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii, Kamati ilielezwa changamoto mbalimbali ikiwemo

ukosefu wa walimu wa kutosha kwa ajili ya elimu msingi kwa maana ya shule ya msingi na sekondari, uchakavu na kutotosheleza kwa miundombinu ya shule ikilwemo maabara, madarasa, upungufu wa wahadhiri wa vyuo vikuu katika ngazi ya PhD, ukosekanaji wa elimu ya ufundi stadi, uhaba wa vifaa vya maabara kama vile kemikali na hakuna **changamoto ya fedha licha ya bajeti ya fedha za miradi ya maendeleo** kuegamia katika upande wa bodi ya mikopo tu kwa asilimia 67.9 katika fedha zilizokuwa zimepokelewa katika Wizara ya Elimu na kuacha **miradi ya maendeleo mingine.**

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Wizara ilieleza changamoto ambazo yenye na Taasisi zake imekuwa ikikumbana nazo kama kutopata kwa wakati fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo, madeni ya walimu, uhaba wa wahadhiri wenye sifa hasa ikizingatiwa wahadhiri wengi wenye elimu nzuri wanastaafu katika umri wa miaka 60 wakati ndipo wanapohitajika, miundombinu chakavu na isiyokidhi mahitaji katika vyuo vikuu, na ongezeko la wanafunzi pamoja na mahitaji yao.

2.6 Uchambuzi wa Miswada mbalimbali ya Serikali

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane (7) (b) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati katika kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018, iliweza kuchambua upya Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalam wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016 (*The Medical, Dental and Allied Professionals Bill, 2016*). Itakumbukwa kuwa Muswada huu uliwhali kujadiliwa katika vikao vya Mwezi Februari lakini haukuweza kuingizwa Bungeni kutokana na marekebisho ambayo Serikali ilienda kuyafanya. Baada ya Serikali kuzingatia hoja za wadau mbalimbali iliuleta Muswada huu tena katika vikao vya Mwezi Agosti 2017 na Taarifa yake kuingizwa Bungeni **tarehe 11 Septemba, 2017**.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni kati ya Miswada iliyoweza kujadiliwa na kuitishwa na Bunge lako Tukufu

katika vikao vya Bunge vilivyofanyika mwezi Septemba, 2017 na kupelekwa kwa ajili ya kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuwa Sheria kamili na tayari kwa matumizi.

Aidha, Kamati ilichambua na kujadili muswada wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma wa Mwaka 2017 (*The Public Service Social Security Fund, 2017*), ambayo taarifa yake iliwasishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na kupitishwa katika Mkutano huu wa Bunge.

2.7 Semina kwa Wajumbe wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Katika kuhakikiha Wajumbe wa Kamati wanajengewa uwezo katika maeneo mbalimbali lakini pia wanashirkina ana wadau katika kubadilishana mawazo na uzoefu, Kamati ilipewa semina kutoka katika Taasisi mbalimbali kama ifuatavyo:-

a) Semina ya tiba ya msaada (*Palliative Care Service*)

Semina hii iliendeshwa na Shirika lisilo la kiserikali ambalo linatoa msaada kwa watu wanaougu magonjwa mbalimbali yakiwemo ya kusendeka kama vile saratani, shinikizo la damu, watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na mengineyo. Semina hii iliwapa uelewa wa kwamba kuna umuhimu wa Serikali kutayarisha wataalamu wa kutoa huduma ya tiba ya msaada ikiwemo ushauri nasaha lakini pia kuhakikisha vifaa kama vile dawa za kupunguza maumivu makali zinapatikana ili kuwapa huduma wananchi kwa urahisi. Semina hii ilitolewa katika Ofisi za Bunge mjini Dodoma mwezi Julai, 2017.

b) Semina ya Masuala ya Afya ya Uzazi

Semina hii ilitolewa kwa wajumbe wa Kamati na shirika lisilo la kiserikali ifahamikalo kwa jina la Utepe Mweupe (*White Ribbon*) kwa ajili ya kukuza uelewa kwa wajumbe wa umuhimu wa kuhakikisha Serikali inatenga fedha za kutosha

kwa ajili ya masuala ya afya ya uzazi kwa wote kwa maana ya wanawake na wanaume.

c) Semina ya Masuala ya uchambuzi wa Bajeti

Semina hii iliendeshwa na Mradi ufahamikao kama *Legislative Support Project* unaosimamiwa na Ofisi ya Bunge kwa ajili ya kuwaongezea ujuzi wajumbe wa namna ya kuchambua bajeti (*Budget Scrutiny*) mbalimbali za Afya, Elimu na nyingine kwa kuweza kuoanisha na malengo makuu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals*). Semina hii iliwapa uelewa zaidi wa namna gani bajeti inaweza ikachambuliwa kwa manufaa ya nchi.

d) Semina ya Masuala ya Elimu

Semina hii illendeshwa na Shirika linalotambulika kama Tanzania *Youth Association* – TAYOA kwa ajili ya kuangalia changamoto zinazowakabili vijana hasa katika masuala ya Elimu na Afya. Semina hii ilifanyika mara mbili kwa ajili ya kufanya pia ufuatilaji na kuona ni namna gani vijana wanapata fursa ya kuweza kutatua changamoto zao wenyewe. Aidha, waandaaji hao walifahamisha kamati kwamba changamoto za vijana ni nyingi ingawa hazipewi kipaumbele na zinatatuliwa kwa ujumla wake tu badala ya kuzitatau kwa kuzingatia uwingu wao na hata idadi ya changamoto na jinsia. Mfano katika suala la Elimu, upatikanaji wa elimu kwa kijana wa kike, masuala ya uzazi kwa kijana wa kike na kiume na mambo mengineyo. Semina hii ilitolewa katika viwanja vyta Bunge, mjini Dodoma.

e) Semina ya masuala ya Uzazi wa Mpango

Semina ilitolewa kwa wajumbe na shirika lisilo la kiserikali la *Tanzania Communication Development Centre* -TCDC kwa ajili ya kuwapa uelewa wa umuhimu wa uzazi wa mapango nakwa ajili ya maendeleo ya Taifa kwa ujumla wake. Aidha, uzazi w mpango haumaanishi ni kuwa na idadi ndogo ya watoto bali kuwa na idadi ya watoto ambao wazazi

wataweza kuwatimimizia mahitaji ya msingi na wakati huo huo afya ya mama ikibaki imeimarika. Semina hii ilitolewa hapa mjini Dodoma katika ukumbi ulioko Hoteli ya Morena.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kutoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kama ifuatavyo:-

3.1 Maoni ya Jumla 3.1.1 Bajeti

Mheshimiwa Spika, Maendeleo yoyote yanategemea uwepo wa rasilimali ikiwemo rasilimali watu, muda pamoja na rasilimali fedha. Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zimeonesha uwepo wa changamoto ya kuchelewa kwa fedha zilizotengwa kwenye Bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara zote tatu (3) zinazosimamiwa na Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, Changamoto hiyo imesababisha shughuli nyingi kushindwa kutekelezeka kwa wakati, hadi wakati Bunge linapitisha bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2017/2018, Wizara zote chini ya Kamati hii hazikuwa zimepokea fedha zaidi ya **asilimia 50** ya Bajeti zao kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Aliyekuwa Rais wa Marekani Barrack Obama aliwahi kusema, naomba kunukuu, "*A budget is more than a series of numbers on a page, it is an embodiment of our values*" kwa tafsiri isyo rasmi ni kwamba bajeti ni zaidi ya mfululizo wa namba katika ukurasa bali ni utambuzi wa thamani yetu. Hivyo basi, Serikali itambue kwamba, taswira na ubora wa chi yetu inaonekana pia kupitia upangaji na utekelezaji wa bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa, mwenendo huu unachangia kuzorota kwa utekelezaji wa majukumu mbalimbali ikiwemo miradi ya maendeleo kwa ajili ya kuwashudumia wananchi.

3.1.2 Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/ 2017

Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa bajeti ya serikali kuna fedha maalumu ambazo zimekuwa zikitengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wizara zilizo chini ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua baadhi ya miradi ukiwemo mradi wa mabweni ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam na mradi wa ujenzi wa maktaba kubwa na ya kisasa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa miradi hiyo ilitekelezwa vizuri na Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya vizuri katika miradi hiyo iliyotajwa. Ni maoni ya Kamati kwamba utekelezaji wa miradi hiyo umesaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili Chuo Kikuu cha Dar es salaam hasa katika suala la mahali pa kulala wanafunzi wa chuo hicho. **Serikali ihakikishe inapeleka fedha pia** katika **miradi ya maendeleo mingine kama ilivyopangwa ili nayo iweze kutekelezwa kwa wakati kama ambavyo imefanyika katika mradi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**

3.1.3 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Mheshimiwa Spika, katika Wizara hii Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo:-

a) Bohari Kuu ya Dawa (*Medical Store Department*)

Mheshimiwa Spika, bohari ya Dawa imekuwa ikifanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuhakikisha inasambaza dawa muhumu kwa wananchi licha ya changamoto inazokumbana nazo na kuendelea kuzitafutia ufumbuzi. Kamati ina maoni kuwa, Serikali lendelee kuipa nguvu Bohari Kuu ya Dawa ili iweze kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuitengeta fedha za kutosha kutasaidia kuiwezesha taasisi hiyo kuwa na mchango wa kutosha katika huduma

ya tiba, kwani tumaini la mgonjwa ye yote ni kupata dawa itakayomtibu maradhi yake katika kituo anachopata huduma ya afya na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa dawa katika maeneo mengi ya kutolea huduma za afya imeendelea kuwa changamoto siku hadi siku, **Kamati inaendelea kusitiza kutekeleza mipango mikakati ambayo itatatua changamo za Bohari Kuu ya Dawa.**

b) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

Mheshimiwa Spika, Bima ya afya ni sehemu ya mfuko wa hifadhi ya jamii ambao unamhakikishia mwananchi kwamba yupo salama wakati afya yake itakapotetereka. Kamati inasikitishwa sana na suala la Bima ya afya kubaki kwa wananchi wachache ambao wana uhakika na kipato na kuwaacha kando wale ambao hawana uhakika na kipato, hawajui kesho yao na ndiko ambako wananchi wengi wako katika hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeomba mara nyingi kufahamu mchakato wa Bima ya afya kwa wote (*Universal Coverage*) lakini mrejesho ambao Kamati umekuwa ikipata kutoka Serikalini kuititia Wizara ya Afya kuhusu hatua ambayo Serikali imefikia ni kuwa bado ipo kwenye mchakato wa bima ya afya kwa wote. **Kamati inajiliza lini mchakato huu utakamilika, kwanini Serikali isiende kujifunza kutoka kwa jirani na rafiki zetu nchini Rwanda ambao wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika suala hili. Je, hakuna cha kujifunza kutoka kwao, nini kauli ya Serikali kuhusu suala la Bima ya Afya kwa wananchi wote?**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kutoa msisitizo wa Bima ya Afya yenye uhakika isiyokuwa na ubaguzi wa aina ye yote ikiwemo vigezo vya kipato, kuchagua aina ya magonjwa aina za vituo vya kutolea huduma za afya na sababu nyingine mbalimbali. **Ikumbukwe kwamba maendeleo ya nchi huletw na wananchi wenye afya bora na afya bora inapatikana kwa wananchi kuwa na Bima ya**

afya ambayo inaweza kupatikana wakati wowote na mahali popote.

c) Mafunzo kuhusu Uzazi salama

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto ya masuala ya uzazi katika jamii zetu hasa kwa watoto walioko katika umri wa shule. Na hali inavyoonesha ni kwamba wananchi ambao watoto wao wanakumbana na changamoto ya kupata mimba shulen i wameanza kuchukuliwa hatua watoto wenye pamoa na wazazi wao. Hali ambayo inaonesha kwamba kumekuwa na ongezeko. Na ongezeko hilo linasababishwa na wananchi kutokuwa na uelewa wa kutosha katika masuala ya uzazi. **Kamati inasisitiza Serikali iweke mkakati wa kuanza kutoa elimu kwa wananchi wake na ikibidi iingizwe katika mtaala wa shule ili watoto waanze kupatiwa mafunzo hayo wakiwa shulen ili kupunguza tatizo hili.**

d) Utolewaji wa Taulo safi (*Sanitary Pads*) kwa watoto wa kike

Mheshimiwa Spika, Mtoto wa kike anapitia changamoto nyingi katika kuhakikisha anapata elimu bora kwa maendeleo ya yake na taifa kwa ujumla. Changamoto hiyo ikiwemo kupoteza siku zisizopungua 5 (ambazo ni siku 60 kwa mwaka) katika mwezi akiwa analiingia katika siku zake za hedhi (*Menstrual Period*) ambayo inamlazimu kukaa nyumbani siku hizo na kumfanya akose haki yake ya masomo. Aidha, kutokana na changamoto hii kumepelekea watoto wengine kuacha kabisa masomo.

Mheshimiwa Spika, Ili kupunguza changamoto hiyo Kamati inashauri, taulo safi (*Sanitary pads*) kwa watoto wa kike zitolewe bure au ziondolewe kodi kama kwa nia ya kumkomboa mtoto wa kike kwani watoto wa kike wengi wamekuwa wakishindwa kwenda shule wakiwa kwenye hedhi kutokana na ukosefu wa *Sanitary pads*.

e) **Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya maendeleo ya wanawake**

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia akina mama kujikwamua kiuchumi kwa maendeleo yao kwa njia ya mikopo yenye riba nafuu kupitia Fungu 53 Idara ya maendedeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. **Kamati inashauri kwamba**, Serikali ihakikishe fedha zinazotengwa kwaajili ya akina Mama zinatolewa kwa kuwa wanawake wengi wanaishi katika mazingira magumu.

f) **Utambuzi wa wazee na kupewa vitambulisho rasmi Mheshimiwa Spika**, katika kikao cha Kamati na Wizara, Waziri aliahidi kutoa vitambulisho vya Wazee lakini mpaka sasa havijatolewa hii inasikitisha sana. Pamoja na kuwa na Sera ya Wazee iliyopitishwa Mwaka 2003 na ikatarajiwा Muswada wa Sheria hiyo ya Wazee kwaajili ya kuwasimamla lakini mpaka sasa Muswada huu bado haujaletwa Bungeni. Kamati inajuliza je hakuna wazee au wazee wan chi hii thamani yao imepotea? Ikumbukwe kwamba kijana wa leo ni mzee wa kesho.

Mheshimiwa Spika, Kamati ni maoni ya Kamati kuwa, ni jambo jema kwa Serikali kuuleta Muswada huu ili kuwalinda wazee na matendo maovu dhidi yao kama vile kuuwawa kwa imani za kishirikina na hata kutelekezwa pasipo msaada wowote ule.

Aidha kamati inashauri, Serikali iboresha Makazi ya Wazee kwani yana hali mbaya sana, Serikali itoe vitambulisho kwa wazee wote nchini wakiwemo waliowahi kushika nyadhfa kubwa hapa nchini, Serikali isogeze huduma za afya, maji na hata chakula kwani wanateseka kufuata huduma hizi, na ikibidi iweke utaratibu wa wananchi kujivekea akiba ya izeeni kama ambavyo nchi za wenzetu zinafanya.

g) **Uhaba wa wataalamu wa afya nchini**

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ikikumbwa na changamoto ya wataalamu wa afya wakiwemo madaktari

bingwa katika maeneo mengi hapa nchini hali inayopelekea wagonjwa wengi kuteseka kwa kusubiri matibabu kwa muda mrefu na wengine hata kupoteza maisha yao. Na hili limekuwa ni hitaji la kila mbunge humu ndani. Kamati inaona kwamba changamoto hii si kwa sababu ya wataalamu hakuna lakini ni Serikali haijaamua kutoa nafasi za ajiri za kutosha kwa ajili ya kukidhi mahitaji haya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa ni vyema Serikali itoe ajira nydingi kwa wataalam hawa wakiwemo madakatari bingwa muhimu kwa afya na maisha ya Watanzania kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

h) Ongezeko la Ukatili wa Kijinsia

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ongezeko la ukatili wa kijinsia katika jamii zetu hapa nchini ikiwemo kwa watoto, wanawake na wanaume pia ingawa taarifa zimekuwa zikipatikana kwa wanawake na watoto pekee. Ukatili wa wanawake na Watoto umekuwa ukiongezeka siku hadi siku. Kamati inashauri Serikali kuja na Mkakati madhubuti wa kutatua tatizo hili ikiwemo utoaji wa elimu ya ukatili wa kijinsia, kuongeza madawati ya jinsia katika vituo vya polisi ili kuweza kusaidia kutatua matatizo mengi yakiwemo magonjwa ya akili yatokanayo na ukatili wa kijinsia ikiwemo kubakwa, unyanyasaji, kunyimwa haki ya ndoa na mengine mengi.

i) Pongezi kwa Taasisi mbalimbali

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya imekuwa ikitekeleza majukumu yake ikisaidiana na Taasisi mbalimbali inazozisimamia pamoja na changamoto zote inazokabiliana nazo kuna baadhi ya Taasisi zimekuwa zikifanya vizuri sana. Kamati haina budi kuzipongeza pale zinapofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, Kamati inazipongeza baadhi ya Taasisi kwa kufanya kazi vizuri zikiwemo Mamlaka ya chakula na Dawa (TFDA), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Bohari ya Dawa (MSD), na Taasisi ya Mifupa (MOI). Kipekee

JKCJ imekuwa na ubunifu mkubwa na wenyе tija kwa taifa wa namna ya kutekeleza majukumu yake, Serikali haina budi kuunga mkono juhudи hiso kwa kuiwezesha kifedha ili ifike mahali wagonjwa kutoka nje ya Tanzania waje kutibiwa hapa nchini na waweze kuitangaza hospitali hiyo.

j) Hospitali ya Taifa ya Muhimbili

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ndiyo Hospitali pekee kubwa ya Serikali hapa nchini ambayo wagonjwa wote wakishindikana katika hospitali nyngine za mikoani wanapelekwa Muhimbili kwa Matibabu. Hospitali hii imekuwa ikifanya vizuri sana katika maeneo mbalimbali ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli ambao licha ya kuwa na mzigo mkubwa wa wagonjwa na ikizingatiwa kwamba wagonjwa wote sasa wanatibiwa hapa nchini na siyo nje ya nchi lakini bado imeendelea kufanya vizuri katika utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa kwa utendaji huu bora wa Hospitali ya Muhimbili, Serikali itaendelea kuisimamia Hospitali hii ili iweze kuendeleza na kuongeza viwango vyake bora zaidi vya utoaji wa huduma ya afya kwa wananchi na ni imani ya Kamati kuwa Chuo Kikuu cha Tiba cha Muhimbili kitaendelea kuitumia Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kuwa Hospitali yake ya kufundishia kama ilivyokuwa kwa kipindi chote tangu chuo hicho kuanzishwa.

k) Hospitali ya Benjamini Mkapa Dodoma

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Benjamini Mkapa ambayo ipo ndani ya Chuo Kikuu cha Dodoma, imejengwa kwa ubora mkubwa na kuwekwa vifaa vya kutosha na vya kisasa. Hospitali hii inakabiliwa na changamoto ya watumishi ambao wangeweza kutoa huduma kwa wananchi. Ni maoni ya Kamati kuwa Hospitali hii haitumiki ipasavyo (***Under-utilized***) ikililinganishwa na ubora wake kwa maana ya miundombinu, vifaa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali, ipeleke watumishi wa kutosha katika Hospitali ya Benjamin Mkapa ili iweze kuhudumia wakazi wa Dodoma na hata nje ya Dodoma ili iweze kupunguza msongamano mkubwa uliopo katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma ifahamikayo kama "General Hospital".

I) Idara ya Chakula na Lishe (TFNC)

Mheshimiwa Spika, Suala la lishe ni sehemu muhimu sana katika maisha ya mwanadamu. Afya ya binadamu huimarka kwa mambo mengi ikiwemo lishe bora. Wananchi wengi wanakula kwa kutimiza milo mitatu kama ilivyo mazoea lakini si kwa kuzingatia lishe bora. Ni Maoni ya Kamati kuwa, Elimu ya lishe bora inapaswa kutolewa na Taasisi ya Chakula na Lishe ambayo iliundwa kwa mpango maalumu kwa ajili ya kusaldia wananchi wa Tanzania kuboresha afya zao. Kwa mujibu wa taarifa zilizofika mbele ya Kamati imebainika kwamba, Taasisi hii haipewi kipaumbele, bajeti inayotengwa miaka yote ni ndogo sana ikilinganishwa na mahitaji halisi ya majukumu yao. **Kamati inaona ni wakati sasa Serikali itambue lishe ni kinga na tiba tosha kwa magonjwa mengi hasa yasiyo ya kuambukiza (*Non Communicable Diseases*) hivyo na kuipa bajeti ya kutosha ili kutoa elimu ya umuhimu wa lishe bora katika kukabiliana na magonjwa mbalimbali.**

3.1.4 **Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**
Mheshimiwa Spika, Wizara ya Habari na Taasisi zake zinakumbana na changamoto mbalimbali ambazo Kamati inapenda kuzitolea Maoni, Ushauri na Mapendekezo kama ifuatavyo:-

a) **Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC)**

Mheshimiwa Spika, Shirika la Utangazaji la Taifa ni shirika pekee la utangazaji linalomilikiwa na Serikali na linategemewa sana katika matukio ya jamii na Serikali pia. Lakini Shirika hili lina changamoto nyingi ikiwemo ya watumishi kuwa wachache kuliko majukumu yao, changamoto ya fedha na hata ya miundombinu ikiwemo majengo pamoja na mitambo au vifaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya mapinduzi ya mikakati ya namna ya kuweza kuliboresha shirika hili ili liweze kufanya kazi yenyе tija kwa shirika lenyewe na Taifa kwa ujumla katika kutoa habari zenyе uhakika. Ni wakati sasa Shirika hili kujifunza kutoka katika makampuni binafsi ya utangazaji kama vile AZAM TV na mengineyo kwa ajili ya kufanya uboreshaji wa Shirika hilo. Serikali ikiona inapendeza itangaze zabuni ili kampuni binafsi waweze kusaidia uboreshaji huo kwa manufaa ya nchi.

b) Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA)

Mheshimiwa Spika, Baraza la Sanaa ni Baraza lilioundwa kwa ajili ya kuboresha na kusimamia kazi za wasanii hapa nchini kwa kuwapa miongozo mbalimbali ya namna ya kuweza kufanikisha kazi zao. BASATA badala ya kuwa muelekezaji kwa wateja wake limegeuka kuwa mahakama ya kuhukumu wasanii pale wanapokesea tu lakini wanapofanya vizuri Baraza hili halisikiki kuwapa motisha au kuwapongeza wasanii hao.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mwenendo wa kuwafungia wasanii wanaokiuka yanayoitwa maadili ya mtanzania (**Kwa mujibu wa BASATA**) lakini hakuna katika matamko hayo kwamba tulikaa na msanii huyo kumuelekeza misingi na utaratibu wa kuwa msanii. Katika taarifa za Baraza hakuna mahali panapoonesha kuwa kuna vikao viliviyowahi kufanyika na wasanii chipukizi, wakongwe au wote kwa maana ya kuwaelekeza namna ya kuenenda kama msanii wa kitanzania. **Kamati inaona kuna changamoto ya mawasiliano kati ya Baraza na wasanii wa kitanzania ambao ni wateja wake, hivyo Serikali kuititia BASATA liweke mikakati maalumu ya kuhakikisha inakuwa na mahusiano mazuri kati ya wasanii na Baraza ili wasanii waone baraza ni sehemu ya kukimbilia na siyo kukimbia.** Kamati inaishauri Serikali kuliwezesha Baraza hili liweze kutimiza majukumu yake kiuweledi kwa kufanya kazi kimizania badala ya kugeuka kuwa Mahakama ya kuhukumu msanii aliyefanya vibaya pasipo na miongozo yao kwa msanii huyo kabla hajakosea.

c) Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA)

Mheshimiwa Spika, Lugha ya Kiswahili ni miuongoni mwa lugha kubwa duniani katika orodha ya lugha kumi (10) zinazotumika kimataifa. BAKITA ni chombo kinachosimamia lugha hiyo hapa nchini, lakini hakitekelezi majukumu yake kama ambavyo ilikuwa inatarajiwa. Lugha ya Kiswahili ikitumika vizuri inaweza kuwa ni sehemu ya kiteme uchumi kwa nchi kama ambavyo lugha nyingine zikitumika. Kwa kutengeneza rasilimali watu wakiwemo walimu ambapo wananchi wetu wanaweza kupata ajira nje ya nchi kwa kufundisha lugha ya Kiswahili. **Kamati inashauri Serikali kutengeneza mpango mkakati ambao utasaidia kukuza lugha yetu ya Kiswahili ndani na nje ya nchi kwa maendeleo ya Taifa.**

d) Uboreshaji wa Utamaduni na Sanaa

Mheshimiwa Spika, Nchi yoyote ile inatambulishwa na kazi ya Utamaduni na Sanaa yake na ni kazi kama kazi nyingine hapa nchini na duniani kote na inalipa kodi kubwa kwa Serikali husika. Na pia Utamaduni na Sanaa ukiendeshwa vizuri utakuwa ni sehemu ya utalii na kuweza kuzuia vizazi vyetu kuiga utamaduni wa nje ambao unakwenda kinyume na maadili ya Mtanzania. **Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha wasanii wote nchini wanasa jiliwa na kupewa utambulisho maalumu kwa ajili ya kusaidia kulipa kodi ya mapato lakini pia kuboresha maisha yao kama wasanii ikiwemo kuwaweka katika mfumo wa Bima ya afya na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ili kuendelea kulinda hadhi yao katika jamii badala ya kudhalilika wapatapo majanga kama vile ugonjwa.**

e) Uboreshaji wa Tasnia ya Filamu Tanzania

Mheshimiwa Spika, Tasnia ya Filamu Duniani kote imekuwa ni sehemu ya utangazaji wa vitu mbalimbali vya nchi husika ikiwemo mila, desturi na utamaduni wa nchi, vivutio vya kitalii, lugha husika na hata uwekezaji katika nchi hiyo ambayo inaongeza tija katika pato la taifa.

Mheshimiwa Spika, nchi ya Korea ya Kusini katika miaka 1990 iliweka mkakati wa kuwekeza katika kutangaza utamaduni

wa nchi hiyo kupitia Filamu, muziki na burudani ujulikanayo kama "**Korean Wave**" ambapo kwa kufanya hivyo mwaka 2004 ililingizia nchi hiyo pato la taifa kiasi cha **Bilioni 1.87** ambao ni sawa na **asilimia 0.2** kwa uchumi wa Korea Kusini na mwaka 2014 ililingizia tena pato la nchi hiyo kiasi cha **Bilioni 11.6**.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano huo wa Korea ya Kusini ni maoni ya Kamati kwa Serikali kupitia Wizara kuiboresha tasnia hiyo kwa kuiga mfano wa Korea Kusini ambayo imefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Aidha, uboreshaji huo unaweza kufanyika kwa njia mbalimbali ikiwemo kupunguza urasimu wa kupata vibali vyta kupata mandhari halisi kwa ajili ya kurekodi filamu hizo kama maeneo ya polisi, bandari, mbuga za wanyama, mlima Kilimanjaro na kwingineko. Hii itasaidia kutangaza utalii badala ya kuwa na filamu ambazo nusu saa nzima inaonesha mtu yupo kwa mganga wa kienyeji au kuonesha utapeli unavyofanyika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ni wakati sasa wa kufanya mageuzi makubwa ya ukuzaji wa tasnia hii ili kuendeleza uibuaji na ukuzaji wa viwanda ikiwemo viwanda vyta Filamu nchini na kuingiazia pato Taifa.

3.1.5 **Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

Mheshimiwa Spika, Wizara hii pamoja na Taasisi zake inakumbana na changamoto mbalimbali ambazo Kamati inapenda kuzitolea maoni, ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

a) **Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)**

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya ufundi stadi ni vyuo ambavyo ni muhimu sana kwa mustakabali wa maendeleo ya taifa leo hasa katikakaui mbiu ya Serikali ya awamu ya Tano ya nchi ya viwanda. Nchi nyingi duniani zimeendelea kwa kuimarisha vyuo vya VETA kwakuwa wahitimu hao ndiyo watendaji wakubwa katika miradi na viwanda mbalimbali

tofauti na wahandisi wakubwa kwani wao wanakuwa ni wasimamizi wa utekelezaji wa ufundi huo. Kamati imebaini kwamba bado Serikali hajafungamanisha Sera ya Uchumi wa Viwanda na uboreshaji wa vyuo hivyo vya ufundi stadi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa hakuna mkakati madhubuti wa kuboresha vyuo hivyo kwani hakuna nyongeza ya walimu, miundombinu ya kuonesha kuwa vyuo hivyo vina umuhimu wa kutoa mafundi mchundo wa kutosha katika jamii zetu iwe kwa kuajiriwa au kwa kujajiri. Aidha, vyuo vingi vya Ufundti stadi vimejikita katika kufundisha udereva na kuacha fani nyngine kama za ufundi uwashi, useremala na fani nyngine. **Kamati inasisitiza kuvifanyia tathmini vyuo vyote vya VETA nchini ili kubaini kama vinatekeleza malengo ya kuanzishwa kwake au la, na kama kuna haja ya kuhakikisha kila wilaya inakuwa na chuo cha Ufundti stadi kwa ajili ya kuzalisha taaluma mbalimbali kwa ajili ya kukuza uchumi wa nchi yetu.**

b) **Chuo Kikuu Huria (*Open University of Tanzania*)**

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Huria kilianzishwa kwa malengo ya kuwawezesha wale ambao hawakuweza kuendelea na utafutaji wa elimu kwa mfumo ambao umezoeleka na hasa kwa wale ambao wako makazini. Kwa msingi huo basi Chuo kiliwekewa utaratibu kwamba kwa mtu ambaye hakuwa na sifa za kuendelea na masono ya ngazi ya juu alitakiwa kuanza na kozi ya msingi (*Foundation course*) ili aweze kupata sifa za kuendelea na masomo ya elimu ya juu. Utaratibu huu ulianza kuigwa na vyuo vingine ambavyo havikuwa kwa malengo ya mfumo huu na kuonekana kupoka majukumu ya chuo kikuu Huria na hata kusababisha kufanya kozi ya msingi chini ya muda ule ambao ni utaratibu kwa mijibu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hiyo Serikali iliamua kufuta utaratibu wa Kozi ya msingi kwa vyuo vyote kikiwemo chuo kikuu Huria cha Tanzania ambao walikuwa wanafuata utaratibu ambao ulianzishwa chini ya Sera ya Elimu ya Masafa ya Mwaka 2014 kifungu cha 3.3.1. (*There is*

no escape for Foundation Course). Kwa kufanya hivyo kumepelekeea chuo hicho kukosa wanafunzi wa kuendelea kusoma katika chuo hicho na kakisababishia chuo kukosa kazi ya kufanya. Kamati inahoji je Chuo Kikuu Huria kinafutwa na kuwa katika utaratibu wa vyuo vingine au la? Na kama lengo la Serikali chuo hicho kiendelee, hivyo Kamati inaomba kulitaarifu Bunge ili liweze kuishauri Serikali kuhakikisha inarejesha majukumu ya Chuo hicho kama iivyokuwa hapo awali na kuweza kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

c) Hospitali ya Mloganzila

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya kisasa kabisa ilijojengwa kwa weledi mkubwa imekamilika na nchi nzima ilishuhudia uzinduzi wake. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kukamillisha mradi huo ullojengwa kwa viwango vikubwa na kwa wakati mfupi ikilinganishwa na miradi mingine. Kamati inaiomba Serikali kuendelea kusimamia viwango bora vya ujenzi wa majengo mengine yakiwemo nyumba za wafanyakazi, mabweni ya wanafunzi kama yaliyoanishwa katika ramani ya hospitali hiyo. Aidha, Serikali ihakikishe huduma katika hospitali hiyo ikiwemo elimu ya udaktari pamoja na matibabu iwe katika ubora wa juu ili kuweka ushindani katika nchi za Afrika ya Mashariki na Afrika nzima.

Mheshimiwa Spika, ni mapendekezo ya Kamati kwa Serikali kwamba ili kuendeleza ubora ule wa majengo, ihakikishe inapeleke watumishi wa kutosha wakiwemo wakufunzi na wafanyakazi wa kada nyingine mbalimbali wenye weledi na wapewe motisha kulingana na utendaji wao wa kazi ili waweze kufanya kazi vizuri zaidi. Iifikanyika hivyo hospitali ya Mloganzila inaweza ikawa ni Hospitali bingwa katika ufundishaji na utoaji wa huduma bora ya afya.

d) Taasisi ya Elimu ya Watu wazima

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya elimu ya watu wazima ilianzishwa kwa ajili ya kufuta ujinga kwa watu ambao waliikosa fursa ya elimu kwa sababu mbalimbali na

kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika. Kutokana na mabadiliko ya Sera na mikakati mbalimbali ya Sekta ya Elimu imefikia mahali elimu hiyo ya watu wazima haitolewi.

Aidha, ikumbukwe kwamba sasa kuna Sera ya Elimu bila malipo (**Waraka wa mwaka 2016**) ambayo inatoa fursa kwa kila mtoto kuingia darasani kwa ajili ya kufuta ujinga. Kwa msingi huo Taasisi ya Elimu ya watu wazima hakuna shughuli yoyote inayofanyika na hivyo kuiongezea mzigo wa uendeshaji kwa Serikali. **Kamati inashauri kwamba Taasisi hiyo ivunjwe kwani hakuna majukumu ya kutekeleza badala yake imegeuka kuwa kijiwe cha kupumzikia endapo mtumishi ataonekana hatoshi katika kitengo chake cha awali ndani ya Wizara ya Elimu. Na kwa kufanya hivyo basi kutakuwa kumeipunguzia mzigo Serikali na watumishi hao wapangiwe majukumu mengine**

e) **Madeni mbalimbali ya wahadhiri na walimu wa Elimu Msingi**

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati, ilibainika kuwa wahadhiri wa vyuo vikuu na walimu wakiwemo walimu wa shule za msingi na sekondari wana malimbikizo ya madeni yao kwa serikali ambayo inapunguza morali ya ufanyakaji kazi ya ufundishaji. Ikumbukwe kuwa kazi ya ufundishaji ni ngumu sana na inahitaji motisha.

Mheshimiwa Spika, Katika taarifa ya Kamati ya Mwaka 2016 iliyosomwa **tarehe 6 Februari, 2017** tulilieleza Bunge lako tukufu kuhusu madeni ya walimu wa shule za msingi kiasi cha shilingi **Trilioni 1.6** ni maoni ya Kamati kuwa deni hili litakuwa limeongezeka katika kipindi hiki cha mwaka mzima, ambayo kimsingi yanashusha morali ya walimu kutimiza wajibu wao wa kufundisha. Aliyewahi kuwa Rais wa Afrika ya Kusini Hayati Nelson Mandela aliwahi kusema, naomba kunukuu, "**No Country can really develop unless its citizens are educated**" kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba, hakuna nchi itnayoweza kuendelea isipokuwa wanachi wake wameelimika. Kwa kuwavunja moyo walimu hawa ni

kurudisha nyuma juhudzi za kuwaelimisha wananchi wa Tanzania ili kusukuma gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali kupitia TAMISEMI kwa kushirikiana na chama cha walimu kufanya uhakiki wa madeni haya ya walimu ili waweze kulipwa stahiki zao. Kwa masikitiko makubwa mpaka leo hii hakuna taarifa yoyote iliyo fika mbele ya Kamati au Bunge ya utekelezaji wa ushauri huu na kueleza ni kwa kiasi gani walimu wamelipwa au la.

Mheshimiwa Spika, naliomba Bunge lako, lichukue hoja hii na kuiagiza Serikali kutekeleza uhakiki huo na kuwalipa madeni walimu hao. Badala ya Serikali kukimbilia kuwaadhibu walimu amabo wanafundisha shule ambazo hazitoi matokeo mazuri kwa kumtaka mwalimu atimizi wajibu wake wakati kwa upande mwingine Serikali nayo haitimizi wajibu wake kwa mwalimu huyo.

f) **Vitabu vyenye makosa kuondolewa Shulenii**

Mheshimiwa Spika, wakati Bunge lako Tukufu likijadili Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2017/2018 iliibuka hoja ya suala la uchapisha na usambazaji wa vitabu vivilyo na makosa mengi ya kimaudhui pamoja na mantiki yake hali ili yopelekeea Kamishna wa Elimu na baadhi ya watendaji waliohusika katika jukumu hilo ndani ya Wizara ya Elimu kusimamishwa kazi na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, mpaka Kamati inapokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2017/2018, ilikuwa hajapata taarifa rasmi ya uondolewaji wa vitabu hivyo katika shule kwa mantiki hiyo ni maoni ya kamati kwamba vitabu vyenye makosa bado vinaendelea kutumika kuafundishia watoto shulenii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaviondoa vitabu hivyo mapema iwezekanavyo katika shule zote na kuviharibu. Aidha, Serikali isambaze vitabu vipyaa visivyo na makosa kwa ajili ya kuendeleza ufundishaji.

g) Mwenendo wa ufaulu katika Elimu ya Sekondari (Kidato cha nne)

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu imeweka utaratibu wa ufaulu katika elimu ya Sekondari kwa viwango vya madaraja kwa maana daraja la kwanza mpaka daraja la nne (*Division one to Division Four*). Kwa utaratibu huo, mwenendo wa ufaulu katika elimu ya sekondari haujawa wa kuridhisha kwani ufaulu huo kwa daraja la kwanza hadi la tatu (*Division 1 to 3*) haujawahi kuuvuka **asilimia 30** ya idadi ya watoto walifanya mtihani katika mwaka husika katika shule za serikali na shule za binafsi. Jedwali lifuatatalo linaonesha mwenendo wa ufaulu kwa miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2013 hadi 2017.

**Mwenendo wa ufaulu katika mtihani wa Kidato cha Nne
kuanzia Mwaka 2013-2017**

Mheshimiwa Spika, Kwa matokeo hayo kama ilivyooneshwa katika jedwali, ni dhahiri kuwa asilimia 70 ni watoto waliopata daraja la nne na daraja sifuri. Kamati inahoj ni taifa gani ambalo tunajaribu kulitengeneza na ikumbukwe kwamba elimu ndiyo msingi wa maisha.

Mheshimiwa Spika, kwakuwa Serikali hufanya tathmini ya ufaulu wa watoto kila mwaka, Kamati ina maoni kuwa taarifa hizo hazifanyiwi kazi kwa ajili ya kutatua changamoto

za zinazoikabili Wizara ya Elimu ili kuhakikisha inaboresha kiwango cha ufaulu wake ya mwaka uliopita ili kuweza kuboresha ufaulu na matokeo yake kila mwaka makosa hayo hujirudia.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali pamoja na uboreshaji wa masuala mengine ya msingi ikiwemo uongezaji wa walimu pamoja na uboreshaji wa miundo mbinu, Serikali ifanyie kazi maoni na mapendekezo ya taarifa ya tathmini inayofanywa kila mwaka ili iweze kuboresha ufaulu wa watoto katika ngazi ya Sekondari.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, napenda tena kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Mawaziri wote ambao Wizara zao zinasimamiwa na Kamati hii kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati kwa kipindi chote cha utendaji kazi wake akiwemo Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Ummy Mwalimu (Mb), Naibu Waziri wake Dkt. Faustine Ndugulile (Mb), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb) na Naibu Waziri wake Mhe. Juliana D. Shonza (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Joyce Ndalichako (Mb) na Naibu wake Mhe. William T. Olenasha (Mb). Aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu na Watendaji wa Wizara hizo kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati siku zote za utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Spika, kipekee zaidi namshukuru Makamu Mwenyekiti Mhe. Mussa A. Zungu kwa ushirikiano anaonipa. Aidha, nawashukuru mno Wajumbe wa Kamati hii kwa

umakini na ushirikiano mzuri ambao wamekuwa wakinipa katika utendaji kazi wangu. Napenda kulijulisha Bunge kuwa, Wajumbe hawa wamekuwa wakifanya kazi kwa weledi wa hali ya juu sana. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Peter J. Serukamba, Mb	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mussa A. Zungu, Mb	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Hussein M. Bashe, Mb	Mjumbe
4.	Mhe. Peter Ambrose Lijualikali	Mjumbe
5.	Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb	Mjumbe
6.	Mhe. Kasuku Samson Bilago, Mb	Mjumbe
7.	Mhe. Lucia Ursula Mlowe, Mb	Mjumbe
8.	Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa, Mb	Mjumbe
9.	Mhe. Ahmed Ally Salum, Mb	Mjumbe
10.	Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb	Mjumbe
11.	Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb	Mjumbe
12.	Mhe. Selemani Said Bungara, Mb	Mjumbe
13.	Mhe. Zitto Zuberi Kabwe, Mb	Mjumbe
14.	Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb	Mjumbe
15.	Mhe. Bernadetha K. Mushashu, Mb	Mjumbe
16.	Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb	Mjumbe
17.	Mhe. Sikudhani Yassin Chikambo, Mb	Mjumbe
18.	Mhe. Savelina Silvanus Mwijage, Mb	Mjumbe
19.	Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb	Mjumbe
20.	Mhe. Grace Victor Tendega, Mb	Mjumbe
21.	Mhe. Sonia Juma Magogo, Mb	Mjumbe
22.	Mhe. Nuru Awadh Bafadhili, Mb	Mjumbe
23.	Mhe. Rehema Juma Migira, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, kwa kipekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Stephen Kagaigai, pamoja na watendaji wake akiwemo Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati hii Ndg. Dickson M. Bisile na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Pamela E. Pallangyo na Ndg. Agnes Nkwera pamoja na Msaidizi wao Gaitana Chima na Ndg. Wazir Kizingiti kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuisaidia Kamati ikiwemo kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelawa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo mbele ya Bunge lako Tukufu, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Peter Joseph Serukamba, Mb

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA
MAENDELEO YA JAMII**

7 Februari, 2018

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, umeongelea suala la *EPforRna* umeonesha kama lipo ukurasa wa 68 lakini halimo, kwa hiyo, halitaingia kwenye *Hansard*.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Masuala ya UKIMWI, karibu. (*Makofii*)

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA – MAKAMU MWENYEKITI
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa Kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya shughuli zilizotekelawa na Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda naomba Taarifa ya Kamati iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo kwenye nakala mlizosambaziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo na majukumu ya Kamati. Muundo na Majukumu ya Kamati ni kama yalivyoolezwa kwenye Kanuni na Taarifa mlizogawiwa ambao unapatikana ukurasa wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliotumika kutekeleza majukumu ya kamati ilikuwa ni kwa njia ya ziara, vikao na semina. Taarifa hii inapatikana ukurasa wa pili wa nakala mlizosambaziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizotekelizwa na Kamati; Kamati tumepokea na kuchambua taarifa mbalimbali za Serikali na Miswada ya Sheria. Taarifa tulizopokea ni kama ifuatavyo:-

- (i) Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*);
- (ii) Mfuko wa Udhagini wa Kudhibiti UKIMWI Nchini (*AIDS Trust Fund*);
- (iii) Lishe na UKIMWI;
- (iv) Ukatili wa Kijinsia;
- (v) Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*);
- (vi) TAMISEMI katika Kutekeleza Mikakati ya Kudhibiti UKIMWI;
- (vii) Kitengo cha Kudhibiti UKIMWI Nchini (*National AIDS Control Program*);
- (viii) Wizara ya Mambo ya Ndani na Magereza;

(ix) Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevyta; na

(x) Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, Sura ya 95 wa mwaka 2017 (*The Drug Control and Enforcement Ammendment Act, 2017*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kwa kina kuhusu uchambuzi huu ipo kwenye nakala mlizosambaziwa ambazo zinapatikana ukurasa wa nne hadi ukurasa wa 22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kwenye maoni na mapendelekezo ya Kamati yanayopatikana kuanzia ukurasa wa 23 hadi ukurasa wa 32. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, Kamati ina maoni na mapendelekezo yafuatayo:-

(i) Ufinyu wa bajeti kwa Mamlaka; kwa kuwa Kamati imebaini kwamba ufinyu wa bajeti ya Serikali kwa Mamlaka unasababisha kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu ambayo mionganini mwake ni kufanya *operation* za kudhibiti kilimo na usafirishaji wa dawa za kulevyta kama bangi na mirungi nchi nzima pamoja na kudhibiti uingizwaji na usambawaji wa dawa nyingine za viwandani kama *cocaine* na *heroine*; Na kwa kuwa, kutotekelezwa kwa majukumu hayo ya Mamlaka kunaweza kuathiri juhudini za kupambana na kudhibiti dawa za kulevyta nchini jambo linaloweza kuwa na madhara makubwa kwa Taifa; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti kwa Mamlaka hii, ili iweze kupambana na kudhibiti kikamilifu biashara haramu ya dawa za kulevyta nchini.

(ii) Ukosefu wa Sera ya Taifa ya Dawa za Kulevyta; kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa hakuna Sera ya Taifa ya Dawa za Kulevyta ingawa kuna Sheria ya Udhibiti wa Dawa za kulevyta; Na kwa kuwa kukosekana kwa sera hiyo kunaifanya Taifa kukosa dira ya kupambana na kudhibiti tatizo la dawa za kulevyta; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali

kuhakikisha mchakato wa utungaji wa Sera ya Taifa ya Dawa za kulevyia ili kuweka dira ya namna Taifa litakavyopambana na janga la dawa za kulevyia.

(iii) Chombo cha kushughulikia dawa za kulevyia katika Halmashauri; kwa kuwa Kamati imebaini kutokuwepo kwa chombo cha kisheria cha kushughulikia udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevyia katika ngazi ya Halmashauri kama ilivyo kwa Kamati za UKIMWI; Na kwa kuwa kukosekana kwa chombo hicho kunachangia udhibiti hafifu wa wa dawa za kulevyia katika Halmashauri nchini; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kupertia Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kufanya maboresho ya Kamati za UKIMWI za Halmashauri ili ziruhusiwe kisheria kusimamia shughuli za udhibiti wa dawa za kulevyia katika ngazi ya Halmashauri.

(iv) Tiba kwa waathirika wa dawa za kulevyia. Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya upatikanaji wa tiba kwa waathirika wa dawa za kulevyia (*Medical Assisted Therapy*) nchini; na kwa kuwa huduma hizo zinapatikana katikana katika Mkoa wa Dar es Salaam, Mbeya na Zanzibar pekee, jambo ambalo linasababisha jamii kubwa ya Watanzania kutofikiwa na huduma hii; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali ifanye juhudhi za haraka ili Mikoa ya Mwanza na Dodoma ianze kutoa huduma hiyo kwani majengo kwa ajili ya huduma hiyo yapo tayari. Aidha, iendelee kuhuisha huduma hii katika Sera ya Afya kama ilivyofanyika katika masuala ya UKIMWI ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma hii kwa nchi nzima.

(v) Unyanyapaa kwa warahibu wa dawa za kulevyia. kwa kuwa Kamati imebaini uwepo wa unyanyapaa wa warahibu wa dawa za kulevyia kutengwa na jamii na kukosa ajira mara wanapoacha matumizi ya dawa za kulevyia; na kwa kuwa hali hiyo inawafanya warahibu hao kurudia tena matumizi ya dawa za kulevyia au kujingiza katika vitendo vya uhalifu na kuchangia kuenea kwa magonjwa kama vile kifua kikuu, UKIMWI pamoja na usugu wa tiba kwa magonjwa hayo; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuanzisha programu maalum za kuwasaidia warahibu

wa dawa za kulevya kuweza kujiinua na kujitegemea kiuchumi mara tu baada ya kuachana na matumizi ya dawa hizo.

(vi) Mwamko hafifu wa jamii katika kushiriki katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya; kwa kuwa Kamati imebaini kuwepo kwa muamko mdogo au ushiriki hafifu wa jamii katika mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya; na kwa kuwa, hali hiyo imesababisha ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevya, wagonjwa wa akili, homa ya ini na maambukizi ya virusi vya UKIMWI; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Mamlaka ya Dawa za Kulevya ishirikiane na vyombo vingine vya dola katika kuandaa kampeni endelevu kwa lengo la kuwajengea uelewa Watanzania kuhusu mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya.

(vii) Nyumba za upataji nafuu kwa warahibu wa dawa za kulevya (*sober houses*); kwa kuwa Kamati imebaini kwamba, nyumba za upataji nafuu (*sober houses*) zinamilikiwa na watu binafsi; na kwa kuwa nyumba hizo hazina miongozo ya namna ya kuwapokea na kuwahudumia waathirika wa dawa za kulevya na zinajiedhesha kibiashara kwa kutoza kiasi kikubwa cha fedha kuanzia shilingi 100,000 mpaka shilingi 200,000 kwa wathirika; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali ianzishe nyumba za kuwasaidia waathirika wa dawa za kulevya kila mkoa ili kuwahudumia Watanzania walioathirika na dawa hizo na ambao hawawezi kumudu gharama katika nyumba zinazomilikiwa na watu binafsi.

(viii) Dawa ya *methodone* kutolewa na wahisani; kwa kuwa Kamati imebaini kwamba asilimia 100 ya dawa aina ya *methodone* ambayo hutumika kuwasaidia waathirika wa dawa za kulevya nchini hutolewa na nchi wahisani kupitia Kituo chake cha Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza (*Centre for Disease Control and Prevention*); na kwa kuwa kuacha hali hiyo iendelee ni sawa na kuandaa bomu kwa siku za usoni kwani ufadhili huo unaweza kukoma muda wowote kutokana na sababu mbalimbali na hivyo kuathiri maisha ya Watanzania; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali

kutenga bajeti ya kutosha kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa dawa hizo, ikizingatiwa kwamba mahitaji ni mengi na wanaofikiwa na huduma ya dawa hizo ni wachache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*), Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

(i) Sera ya UKIMWI kupitwa na wakati; kwa kuwa Sera ya UKIMWI ya Tanzania ya mwaka 2001 ni ya muda mrefu; na kwa kuwa, mambo mengi yanayohusiana na masuala ya UKIMWI yamebadilika na hayaonekani kuakisiwa na Sera hiyo; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa mapitio ya Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001 ili iweze kuzingatia mabadiliko katika mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI kitaifa na kimataifa.

(ii) Masuala ya UKIMWI kutegemea Wafadhili; kwa kuwa, masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI yanategemea wafadhili kutoka nje ya nchi kwa asilimia 90; na kwa kuwa, Serikali imeanzisha Mpango wa *Test and Treat* ambapo mtu anapopatikana na maambukizi ya VVU humlazimu kuanza kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU mara moja, hivyo huongeza mahitaji na gharama za manunuzi ya ARVs; na kwa kuwa, wafadhili walio wengi wamepunguza kiwango cha ufadhilli kwa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Mfuko wa Udhaminini wa Kudhibiti UKIMWI ambao imeuanzisha ihakikishe unakuwa na vyanzo vya fedha vya uhakika kama ilivyo kwa mifuko mingine kama vile Mfuko wa Barabara (*Road Fund*), Mamlaka ya Umeme Vijijini (*Rural Energy Authority – REA*), ili uweze kukabiliana na janga hili la UKIMWI kikamilifu.

(iii) Kupungua kwa bajeti ya Tume Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*); kwa kuwa Kamati ilibaini kwamba bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imeshuka kwa asilimia 50; na kwa kuwa, hali hii inasababisha Tume kuendelea kutegemea fedha za

nje ambazo hazina uhakika katika kutekeleza afua za UKIMWI; kwa hiyo basi, Kamati inashauri Serikali ihakikisha Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania inatengewa fedha za kutosha na kuzitoa kwa wakati ili kuiwezesha Tume hiyo kutekeleza shughuli zake ipasavyo.

(iv) Upungufu wa Dawa ya Seprine; kwa kuwa kumekuwa na upungufu wa dawa aina ya Seprine ambayo ni muhimu sana kwa watu wanaoishi na VVU; na kwa kuwa dawa hizi ni muhimu sana kwa kupambana na magonjwa nyemelezi; kwa hiyo basi, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha dawa hiyo inapatikana kwa wingi nchini ili kusaidia waathirika wa UKIMWI. Aidha, Kamati inaona ni vema dawa hii ikaingizwa katika orodha ya dawa (*ARVs package*), ambazo wanapewa WAVIU ili kufubaza makali ya VVU na kuepusha magonjwa nyemelezi.

(v) Kufifia kwa Kampeni kuhusu VVU na UKIMWI; kwa kuwa, kampeni kuhusu masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI zimefifia; na kwa kuwa hali hiyo inawafanya watu kujingiza katika ngono zembe bila kuwa na hofu, jambo linaloweza kusababisha ongezeko la maambukizi mapya ya UKIMWI; kwa hiyo basi, Kamati inashauri Serikali kuwa na mikakati ya kuhakikisha Kamati za Udhhibit wa UKIMWI katika kila ngazi zinahuisha kampeni kuhusu VVU na UKIMWI, ili kuepusha uwezekano wa ongezeko la maambukizi mapya ya UKIMWI.

(vi) Ongezeko la Athari za UKIMWI maeneo ya kazi; kwa kuwa athari za UKIMWI zimebainika kuathiri nguvu kazi katika maeneo mengi ya kazi, iwe Serikalini au katika sekta binafsi; na kwa kuwa bila kuwa na mipango thabit ya kuwalinda watumishi katika maeneo yao kutaathiri ukuaji wa uchumi wa taifa na hivyo kuathiri maendeleo ya nchi; kwa hiyo basi, Kamati inashauri sekta zote mbili, yaani sekta ya umma na sekta binafsi, kuhakikisha zinatekeleza Mipango ya UKIMWI (*HIV/AIDS*) mahali pa kazi.

(vii) Umri wa maamuzi ya upimaji; kwa kuwa umri wa maamuzi Tanzania (*age of consent*) ni miaka 18; na kwa

kuwa, athari za UKIMWI kwa watoto chini ya miaka 18 ni kubwa; na kwa kuwa upimaji wa watoto hao hutegemea ridhaa ya wazazi kwa kuwa wao kisheria hawana mamuzi hayo; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali ipunguze umri wa maamuzi binafsi (*age of consent*) kutoka miaka 18 hadi miaka 15 ili hata Mkakati wa 90, 90, 90, uweze kufanikiwa na kufikia malengo ya tisini – tatu ifikapo mwaka 2020 na kuumaliza kabisa UKIMWI nchini ifikapo mwaka 2030. Aidha, Kamati inashauri suala la upimaji wa VVU lipewe mkazo zaidi ili kuweza kufikia malengo yaliyopo ambapo wigo mkubwa wa WAVIU waweze kujifahamu hali zao na kuanzishiwa dawa, ili virusi walivyonyavyo viweze kufubazwa na hatimaye kupunguza kasi ya maambukizi mapya ya VVU miongoni mwa jamii yetu.

(viii) Ukeketaji huchangia maambukizi ya VVU; kwa kuwa moja ya sababu zinazochangia maambukizi ya VVU kwa watoto wa kike ni ukeketaji kutokana na kuchangia vifaa wakati wa kukeketwa; na kwa kuwa jambo hili bado linafanyika kwa usiri mkubwa na hivyo kuendelea kusababisha maambukizi kwa watoto wa kike; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu katika kupiga vita vitendo vyta ukeketaji ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua kali za kisheria wanaotekeleza vitendo hivyo.

(ix) Usimamizi wa taasisi zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI; kwa kuwa, kuna taasisi nyngi za kitaifa na za kimataifa ambazo zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI nchini; na kwa kuwa hakuna ufuatiliaji Serikali kuhusiana na namna taasisi hizi zinavyopata na kutumia fedha za ufadhilli wa masuala ya UKIMWI; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuititia TACAIDS kuhakikisha kunakuwa na ufuatiliaji (*coordination*) kuhusu namna ya taasisi hizo zinavyopata fedha kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(x) Makundi maalum yanayoweza kuchangia maambukizi ya UKIMWI; kwa kuwa watumiaji wa dawa za kulevyta, watu wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja na watu wanaofanya biashara ya ngono ni makundi ambayo

yasipoangaliwa yanaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa maambukizi ya UKIMWI; na kwa kuwa vijana ndio wanajingiza katika makundi haya kwa kiwango kikubwa na hivyo kuhatarisha mustakabali wa maisha yao na nguvukazi ya Taifa kwa ujumla; kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali iandae programu maalum za makuzi na malezi kwa vijana kwenye shule na vyuo, ili kuwaepusha na kuijingiza katika makundi hayo na hivyo kuwa katika hatari ya kuambukizwa UKIMWI. Aidha, kuwe na uanzishwaji wa Huduma Rafiki kwa Vijana (*Youth Friendly Services*) katika mitaa na vijiji ambazo zitasimamia kwa karibu na Kamati za Kudhibiti UKIMWI za ngazi za mtaa na kijiji husika kwa lengo la kuwasaidia vijana kupata uelewa wa kupambana na maambukizi ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne inahusu hitimisho. Napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa namna ambavyo mnasimamia na kuendesha kwa umahiri shughuli za Bunge. Napenda kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu), Mheshimiwa Jenista Mhagama, Naibu Waziri Mheshimiwa Antony Mavunde na Mheshimiwa Stella Ikupa kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati ikitekeleza majukumu yake, ahsanteni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashukuru Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko, Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, Ndugu Rogers Siyan'ga na watendaji wote wa Tume na Mamlaka kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima, kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufanuzi mara zote ulipohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa uchapakazi wao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Wajumbe wamefanya kazi kubwa katika kuhakikisha Kamati inaisimamia na kuishauri vyema Serikali kwa mujibu wa Katiba, sheria za nchi na Kanuni za kudumu za Bunge.

Nawashukuru kwa ushirikiano walionipatia wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Aidha, kwa kutambua kwamba Kamati zinafikia ukomo wa uhai wake naomba niwatakie utumishi mwema katika Kamati watakazopangiwa. Napenda majina ya Wajumbe wote wa Kamati yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge yaani *Hansard*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wake kwa kwa Kamati. Namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athumani Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi, Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Asia Msangi, Ndugu Happiness Ndalu na pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Grace Mwenye, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza shughuli zilizotekelizwa, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mpaendelekezo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee kuikubali na kujadili taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI pamoja na maoni na nmapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA MASUALA YA UKIMWI KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2017
HADI JANUARI, 2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016; naomba kuwasilisha Taarifa ya Shughuli zilizotekelizwa na Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

1.1 Muundo na Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ya Kanuni chini ya 118 (10) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Taasisi mbili ambazo ni:

- (a) Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS);
- (b) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kanuni hiyo pia imeipa Kamati jukumu la kuratibu masuala yote yanayohusu UKIMWI katika sekta zote ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa Sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa dawa za kulevyta. Kamati hii imepewa jukumu la:-

- a) Kuratibu masuala yanayohusu UKIMWI katika sekta zote;
- b) Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Serikali kuhusu UKIMWI na udhibiti wa Madawa ya Kulevyta;
- c) Kujadili na kutoa mapendekozmo na ushauri kuhusu hatua za kudhibiti madawa ya kulevyta; na
- d) Kushughulikia Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta.

1.2 Utaratibu uliotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Kamati inateleleza Majukumu yake ipasavyo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitumia utaratibu ufuatao:-

(a) Kufanya vikao na Wizara na Taasisi kwa kuiomba kufika mbele ya Kamati ili kutoa Taarifa juu ya jambo au suala mahsusni ambalo Kamati ilipenda kupata taarifa zake kutoka kwa watendaji wa Wizara na Taasisi hizo;

(b) Kufanya ziara katika maeneo yenye maambukizi makubwa ya VVU na yenye mambukizo madogo;

(c) Semina na kongamano mbalimbali zilizohusu Masuala ya UKIMWI na Dawa za Kulevyaa; na

(d) Kufanya mikutano na Wadau kwa lengo la kupokea maoni yao juu ya Masuala mbalimbali ambayo Kamati ilikuwa inafanyaia kazi ikiwemo Muswada.

1.3 Shughuli zilizotekeliza na Kamati

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa na usimamizi wa kutosha wa majukumu yake kwa mujibu kwa Kanuni za kudumu za Bunge, katika kipindi cha Januari 2017, Kamati ili kutekeleza shughuli zifuarazo:-

i. Kupokea mafunzo;

ii. Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za utendaji wa Wizara mbalimbali, Taasisi, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa ;

iii. Ziara

iv. Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

v. Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa kwa Mwaka

wa Fedha 2016/2017 na mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

- vi. Uchambuzi wa Muswada wa Sheria ; na
- vii. Kupokea Semina mbalimbali.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, imefanya utekelezaji wa majukumu yake katika Mwaka 2017 kuititia mbinu mbalimbali, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kama ilivyoelelezwa hapo awali. Aidha, majukumu haya ni kama yalivyoelelezwa ambayo pia Kamati itaeleza katika uchambuzi wa utekelezaji wake katika Taarifa hii.

2.2 Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha mwaka 2017 shughuli zifuatazo zilitkelezwa;-

2.3 Mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa kuzingatia kuwa Wabunge (Wajumbe) wa kamati hii walikuwa wapya ilikuwa ni muhimu kabla ya kuanza utekelezaji wa majukumu ya Kamati kuwapatia mafunzo Wajumbe ambayo yaliandaliwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta. Mafunzo haya yalifanyika kuanzia tarehe 10 hadi 11 Januari, 2017 Ofisi ya Bunge Dodoma. Mafunzo haya yalikuwa na faida na

yaliwawezesha Wajumbe kufahamu muundo na majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyia. Elimu waliyoipata kuitia semina hizi iliwawezesha wajumbe kuelewa kwa undani taasisi watakazozisimamia na namna ambavyo wataweza kupambana na gongwa la UKIMWI na Udhibiti wa Dawa za Kulevyia.

2.4 Kupokea Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali

(a) Tume ya Kudhibiti UKIMWI, Tanzania (TACAIDS)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa ya Utendaji wa Tume hii ambayo ilionesa kuwa, takwimu za utafiti wa hali na viashiria vya UKIMWI Tanzania kwa mwaka 2016/17 zinaonesha kuwa idadi ya rala wa Tanzania inakisiwa kuwa ni **50.9** milioni. Ukubwa wa maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI (VVU) kitaifa mionganoni mwa jamii yenye umri wa miaka 15 – 49 ni wastani wa asilimia **4.7** kitaifa, wanawake wakiwa asilimia **6.2** na wanaume ni asilimia **3.1**. Inakadiriwa kuwa jumla ya watanzania **million 1.4** wanaishi na Virusi Vya UKIMWI. Na kwa vijana wa umri wa miaka kati ya 15 na 24 ni asilimia **1.4**. Wavulana asilimia **0.6** na wasichana ni asilimia **2.1**.

Mheshimiwa Spika, tafiti za awali zilizofanyika mionganoni mwa watu wenye umri wa miaka 15 – 49 zinaonyesha kuwa maambukizi mapya ya VVU yamekuwa yakipungua kutoka idadi ya watu **72,000** kwa mwaka 2013 hadi kufikia watu **48,000** kwa mwaka 2015. Hata hivyo, umri wa walengwa wa utafiti uliongezwa kutoka 15 – 64 katika tathmini ya mwaka 2016/17. Matokeo ya utafiti huo yamebainisha kiwango cha maambukizi mapya ya VVU kwa mwaka 2016/17 yamefikia watu **81,000**.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la idadi hii kwa mwaka 2017 ni ishara mbaya kwetu jambo ambalo linahitaji uwajibikaji wa pamoja kutoka ngazi ya mtu binafsi hadi ngazi ya kitaifa

kwa kushirikiana kimkakati ili kufikia malengo ya kuzuiya maambukizi mapya ya VVU hatimaye kufikia sifuri (**0**)

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa baadhi ya mikoa ina maambukizi ya VVU sawa au zaidi ya kiwango cha Taifa cha asilimia **4.7**. Mikoa hiyo ni: Njombe asilimia **11.4**, Iringa asilimia **11.3**, Mbeya asilimia **9.3**, Mwanza **7.2**, Kagera **6.5**, Shinyanga **5.9** na Katavi **5.9**; Songwe **5.8**, Rukwa asilimia **6.2**, Dar Es Salaam asilimia **4.7**, Ruvuma asilimia **5.6** na Pwani **5.5**. Mikoa miwili yenye maambukizi kidogo ni Lindi **0.3** na Arusha **1.9** kwa Tanzania Bara. Maambukizi ni madogo zaidi kwa upande wa Tanzania Visiwani ambapo Unguja ni asilimia **1.2** na Kusini Pemba ni asilimia **0.3**.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kwamba karibu kila mtu wa umri baina ya miaka kumi na tano hadi miaka arobaini na tisa (15 - 49) amesikia kuhusu UKIMWI. Kwa bahati mbaya, wenyе uelewa wa kina kuhusiana na maambukizi mapya ya VVU na njia za kujikinga bado ni chini ya nusu ya wale ambao wamesikia kuhusu UKIMWI. Aidha, kwa upande wa vijana wenyе umri wa miaka 15 hadi 24 kiwango cha uelewa halisi kwa wasichana ni asilimia **40** ambapo kwa wavulana ni asilimia **47**. Hii inaonyesha kuwa vijana wetu wana uelewa mdo go wa Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI na hivyo kuwa katika hatari zaidi ya kupata maambukizi mapya ya VVU.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya mwitikio kwa masuala ya VVU na UKIMWI nchini ambayo yamethibitishwa na takwimu, takwimu zinazoonyesha kuwa kiwango cha maambukizo mapya ya VVU kilishuka kwa zaidi ya 20% katи ya mwaka 2010 na 2015. Aidha, zaidi ya nusu ya WAVIU wanapata dawa ya kufubaza VVU (ARVs). Asilimia **86%** ya wanawake wajawazito wanaoishi na VVU wanapata dawa za kufubaza VVU (ARVs), hivyo dawa hizi zimesaidia kupunguza maambukizo mapya ya VVU kwa watoto (miaka 0 – 4) kwa takribani nusu (**50%**) katи ya mwaka 2010 na 2015.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio haya, kumekuwepo na changamoto nyingi ambazo zitahitajika

kufanyiwa maboresho ili kurekebisho mapungufu yaliyojitokeza katika mwitikio kwa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI:-

- a) Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001 imekuwa ya muda mrefu na mambo mengi yanayohusiana na masuala ya UKIMWI yamebadilika kwa maana hiyo, sera hii inahitaji kupitiwa upya ili kuiboresha.
- b) Maendeleo ya utafiti wa chanjo dhidi ya UKIMWI nchini bado ni kitendawili kwa maana hatujui tumefikia hatua gani kitaalamu.
- c) Ulinzi duni wa makundi ya watu kama wafungwa na watoto wanaoishi katika mazingira magumu ndiyo wako katika hatari zaidi;
- d) Msisitizo mdogo wa umuhimu wa kushiriki katika ngazi ya jamii na uwajibikaji kwa ajili ya utekelezaji wa mwitikio wa Taifa kwa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI;
- e) Ukosefu wa mikakati endelevu ya kushughulikia uwezo wa kaya kuboresha desturi za kulisha watoto lishe bora na huduma za lishe bora kwa WAVIU;

LISHE NA UKIMWI

Mheshimiwa Spika, Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI (WAVIU) na wanaotumia dawa wanakabiliwa na lishe duni hususani kwa watoto wanaoishi na virusi. Kamati inaipongeza serikali kwa kuanzisha program ya lishe ikiwa ni pamoja kuhamasisha viwanda kuweka virutubishi kwenye unga na mafuta ya kupikia. Kamati inashauri elimu zaidi bado inahitajika kuhusu lishe bora iendelee kutolewa katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na kuhamasisha viwanda vidogo vidogo kuongeza virutubishi.

UKATILI WA KIJINSIA

Mheshimiwa Spika, tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa, ukatili wa kijinsia (Gender Based Violence) ni chanzo cha

maambukizi mapya ya VVU. Ukatili wa kijinsia unajumuisha unyanyasaji wa kimwili, kiuchumi na kisaikolojia. Hata hivyo kuna baadhi ya mila zimekuwa hatarishi kwa kuchangia maambukizo mapya ya VVU zikiwemo ndoa za utotonii, kurithi wajane bila ya kujua afya ya anaerithiwa wala anaerithi na ngono zembe.

UKEKETAJI

Mheshimiwa Spika, suala la ukeketaji (Genital Mutilation) mbali na kuwa mionganii mwa masuala ya unyanyasaji wa Kijinsia, desturi zinazosababisha mwanamke kunyimwa haki yake kimsingi ya kibinaadamu, pamoja na kupata maambukizi mapya ya VVU kwa utumiaji wa vifaa visivyo salama. Aidha, imedhihirika kuwa kiafya ni kitendo ambacho humweka mwanamke katika hatari kubwa ya kutokwa na damu nydingi na hatimaye kupoteza maisha hususan wakati wa uzazi. Hivyo, hatuna budi kuhakikisha tunaunganisha nguvu zetu ili kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika Kamati inatoa wito kwa wananchi kuzingatia maudhui ya kampeni mbalimbali zinazofanywa na Serikali na wadau mbalimbali kwa ajili ya kubadili tabia, kuachana na mila hatarishi na kujikinga na maambukizo mapya ya VVU.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Jeshi la polisi kuanzisha dawati la jinsia kwenye vituo vyote vya polisi ambapo kazi yake kubwa ni kusikiliza malalamiko na kupokea taarifa kuhusiana na vitendo vya ukatili wa kijinsia bado kumekuwepo na kukithiri kwa vitendo vya ukatili.

Mheshimiwa Spika ili kupunguza maambukizi ya VVU na ukatili wa kijinsia, Kamati inaishauri serikali kuwa, Wizara ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Maendelao ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto na Wizara ya mambo ya ndani ya nchi kuliangalia suala hili ili kupata mikakati thabiti ya kupunguza ukatili wa huo ambao unachangia kwa kiasi kikubwa maambukizi ya UKIMWI.

MFUKO WA UDHAMINI WA KUDHIBITI UKIMWI (AIDS TRUST FUND -ATF)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya Utekelezaji wa shughuli za Mfuko huu ambapo ilionesa kuwa zaidi ya asilimia 90 ya gharama za UKIMWI kwa mwaka zinafadhiliwa na wadau wa maendeleo wa Serikali ya Marekani na Mfuko wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund).

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza utegemezi huo kutoka kwa wafadhili, Mfuko ulijiwekea malengo ambayo ni kuongeza rasilimali fedha za ndani kutoka asilimia **7** mwaka 2015 hadi kufikia asilimia **30** ifikapo mwaka 2018, pamoja na kuongeza mchango wa sekta binafsi katika udhibiti wa UKIMWI kutoka asilimia 8 hadi asilimia 15 kufikia 2018. Madhumuni ya Mfuko huu ni pamoja na:-

- a) Kuhakikisha kunakuwepo na vyanzo endelevu kwa ajili ya mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI Tanzania Bara.
- b) Kupunguza utegemezi katika kugharimia shughuli za mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI.
- c) Nchi kuweza kufanya maamuzi yake yenyeWE katika utekelezaji wa afua za UKIMWI.

Aidha, maeneo yaliyoanishwa kushughulikiwa na mfuko huu ni kama ifuatavyo;-

- (i) Asilimia 60 ya pesa za mfuko zitatumika kwa ajili ya upatikanaji wa vifaa tiba na dawa kama vile ARVs na condoms kwa ajili ya watu wazima, wanawake, wajawazito, watoto na vijana waliofikia umri wa kubalee .
- (ii) Asilimia 25 zitatumika kwa ajili ya kinga: ushauri nasihî na kupima, elimu ya uzazi na program zinazolenga kubadili tabia.

(iii) Asilimia 15 zitatumika kwa ajili ya mazingira wezeshi ikiwa ni tathimini ya ufuatiliaji, utafutaji wa rasilimali (resource mobilization) na madhara yatokanayo na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, pamoja na malengo na vipaumbele vilivyowekwa katika kutimiza majukumu ya Mfuko huo, Kamati ilielezwa changamoto mbalimbali, moja wapo ikiwa ni kukosekana kwa chanzo cha uhakika na endelevu cha fedha za Mfuko ambacho kingesaidia kupatikana fedha na kupunguza utegemezi kutoka kwa wafadhili kutoka nje ya nchi kwani kwa sasa nchi inategemea ufadhilli wa afua za UKIMWI kwa asilimia 90.

2.5 Kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zinazosimamiwa na Kamati Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa ya Utendaji wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia ufanisi wa utekelezaji wa Mwongozo wa utumiaji na ugawaji wa Fedha za UKIMWI kwenye Halmashauri na Manispaa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hilo, OR-TAMISEMI huangalia maeneo yenye mapungufu (gaps) hivyo kuweka vigezo vitakavyotumika katika kuihudumia Mikoa na Halmashauri katika program za ugawaji wa fedha za UKIMWI ambapo, ni pamoja na kuangalia hali ya maambukizi makubwa ya UKIMWI kutokana na tafiti zilizofanyika, kwa hiyo basi kipaumbele hutolewa kwenye maeneo yenye ukosefu au upungufu wa huduma za VVU na UKIMWI na kutokuwepo au kuwepo kwa wadau/ Asasi wachache wanaofanya shughuli za kuhudumia jamii katika mapmbano dhidi ya UKIMWI/VVU.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi juni, 2017 jumla shilingi bilioni **2.63** zilitolewa kwenye Mikoa na halmashauri. Aidha, Mikoa ilipata shilingi bilioni **2.31** sawa na asilimia **78.8** na halmashauri shilingi milioni **320** sawa na asilimia **21**. Aidha, Mikoa ilipata

fedha nyingi kwa ajili ya kuendeshea mafunzo kwa watoa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya ili waweze kutoa huduma stahiki kulingana na miongozo. Fedha zilizotolewa kwenye Halmashauri ni kwa ajili ya ufuutiliaji wa utoaji wa huduma katika vituo vya afya katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilielezwa changamoto za kuongezeka kwa idadi kubwa ya watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu, watu wanaoishi na VVU ukilinganisha na kiwango cha fedha kilichokuwa kinapatikana, uelewa mdogo kwa baadhi ya watu wanaoshi na VVU , kutozingatia matumizi sahihi ya dawa za kupunguza makali ya VVU pamoja na unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU. Hii husababisha watu kutojitokeza kupima VVU au kutosubiri majibu ya vipimo au kwenda mbali katika kituo cha kutolea huduma mahali ambapo hawafahamiki.

(i) **WIZARA YA MAMBO YA NDANI (JESHI LA MAGEREZA)**

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilipata fulsa ya kukutana na Wizara ya Mambo ya Ndani (Jeshi la Magereza) ili kupokea Taarifa kuhusu hali ya Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI Magerezani pamoja na upatikanaji wa kinga na tiba ya magonjwa nyemelezi. Katika mahojiano hayo Kamati ilielezwa kuwa Jeshi la Magereza lina jukumu la kuhakikisha kwamba, wafungwa na mahabusu wanapata huduma bora za afya kama ilivyo kwenye jamii nyingine ikiwa ni pamoja na kumwona daktari, uchunguzi wa afya, tiba, ushauri nasaha na upimaji wa VVU.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa kuwa, Jeshi la Magereza kwa mwaka 2015/2016 walipima jumla ya wafungwa na mahabusu **8,287**; kati yao waliokutwa na maambukizi ya UKIMWI walikuwa **376**, sawa na asilimia **4.5%**. Aidha, kwa mwaka 2016/2017 Jeshi la Magereza lilipima jumla ya wafungwa/mahabusu **34,793** (wanawake **1,451** na wanaume **33,342**) kati yao waliokutwa na maambukizi ni **953** (wanaume 818 na wanawake 135) sawa na asilimia **2.7**.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifahamishwa uwepo wa msongamano mkubwa wa wafungwa/mahabusu unaoathiri

utoaji wa huduma bora kwa wafungwa na kwamba, hivi sasa kuna wafungwa na mahabusu **39,312** wakati uwezo wa magereza ni kuhifadhi wafungwa na mahabusu **29,552**. Aidha, pamoja na msongamano mkubwa kuna ufinyu wa bajeti ambao umesababisha Miradi ya Afya kutotekelizwa, upungufu wa dawa, vifaa, vifaa tiba na chakula lishe kwa wafungwa, mahabusu na watumishi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

- (a) Ili kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu/magerezani, Serikali itumie adhabu mbadala kwa makosa madogo madogo. Kwa kufanya hivyo, kutapunguza msongamano, ghamama kwa Serikali na uwezekano wa kuambukizana magonjwa kama vile Homa ya Ini, UKIMWI na Kifua Kukuu.
- (b) Jeshi la Magereza lionezewe bajeti kwa ajili ya chakula pia libuni mkakati wa kuwatumia wafungwa hususan wanaotumikia vifungo vya muda mrefu kuongeza uzalishaji ili kujitosheleza kwa chakula pamoja na kuongeza maduhuli ya Serikali. Aidha, serikali itoe motisha kwa wataalam wa afya walioko Magereani ili waendelee kubaki na kutoa huduma stahili kwa wafungwa na mahabusu.
- (c) Elimu ya mara kwa mara itolewe kwa wafungwa na mahabusu ili wapate uelewa wa namna ya kupambana na janga la UKIMWI. Aidha, Kamati inashauri wafungwa wote wapatiwe chanjo ya kuzuia ugonjwa wa homa hatari ya Ini.
(d) Shughuli zozote zinazohusu madawa ya kulevyta na UKIMWI Magerezani, Uongozi wa Magereza uwahusishe Waratibu wa UKIMWI na dawa za kulevyta wa Mikoa na Wilaya husika ili kubadilishana uzoefu na elimu.

(ii) BOHARI KUU YA DAWA NCHINI (MSD)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utendaji wa MSD ilionesha kuwa dawa za UKIMWI hununuliwa na kupokelewa kutoka nje ya nchi. Manunuzi ya dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI (ARVs) yamegawanyika katika makundi mawili

ambayo kundi la kwanza ni dawa za ARVs ambazo hununuliwa na wafadhili wa Global Fund moja kwa moja kwa mfumo wa ((Pooled Procurement Mechanism), ambapo dawa hutolewa nchini na washitiri kulingana na mahitaji na maoteo ya Mpango wa Kudhibiti UKIMWI (NACP). Kundi la pili ni vitendanishi vya maabara (Laboratory Reagents) ambazo hununuliwa na MSD kulingana na mahitaji yanayoletwa na kitengo cha Taifa cha Kudhibiti UKIMWI-National AIDS Control Programme (NACP)

Mheshimiwa Spika, kamati ilijulishwa kuwa hali ya upatikaji wa dawa za kufubaza makali ya UKIMWI (ARVs) pamoja na vitendanishi zinapatikana kwa asilimia 100 na MSD ina dawa ghalani zenye uwezo wa kutosha kwa matumizi ya wastani miezi 6 hadi 15. Kamati inaipongeza serikali kwa juhudhi wanazofanya za kuhakikisha kuwa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara vinapatikana kwa wakati katika hospitali zote nchini bila upungufu wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa, idadi ya watoto wanaozaliwa na akina mama walio na maambukizi ya VVU/UKIMWI inaedndeala kupungua siku hadi siku kutokana na akina mama hao kuijunga na mpango wa kutokomeza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto Elimination of Mother to Child Transmission (eMTCT). Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhakikisha kuwa maambukizi ya VVU/UKIMWI yamepungua. Hata hivyo, Serikali longeze juhudhi katika usambazaji wa mashine ya viral load katika hospitali zote za mikoa na wilaya hasa ukizingatia kwamba kwa sasa mashine hizo zipo chache ukilinganisha na mahitaji. Aidha, Kamati inashauri pia dawa aina ya **Seprine** inayotibu magonjwa nyemelezi longezwe kwenye orodha ya dawa za ARVs ambazo hutolewa bure kwa WAVIU. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa shilingi Milioni **600** kwa ajili ya kununua dawa aina ya **Seprine**

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio mengi yaliyopatikana kutokana na upatikanaji wa dawa na vitendanishi. Kamati ilielezwa chagamoto mbalimbali kama ifuatavyo;

- (i) Upungufu na upatikanaji wa dawa za kuzuia magonjwa nyemelezi kutokana na ufinyu wa bajeti ya serikali baada ya wafadhili kujitoa kununua dawa hizo;
- (ii) Dawa na vitendanishi zinanunuliwa kwa pesa ya wafadhili ambapo bajeti yake ni zaidi ya shilingi bilioni 200;
- (iii) Mabadiliko katika matumizi ya dawa za ARVs (treatment regimen) hupelekea kubadilishwa kwa matumizi yake na hivyo kupelekea kuchina kwa dawa na vitendanishi;
- (iv) Bohari kuu ya dawa nchini kutoruhusiwa kununua dawa za ARVs kwa fedha za Mfuko wa Dunia (Global Fund) na hivyo kutegemea fedha za mgao wa kawaida wa dawa. na;
- (v) Bidhaa zote za UKIMWI hupatikana nje ya nchi na hivyo kuongezeka kwa gharama za utunzaji na upatikanaji.

(iv) KITENGO CHA KUDHIBITI UKIMWI NCHINI (NACP).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea Taarifa ya Utendaji wa Kitengo cha Kudhibiti UKIMWI ambapo ilionesa kuwa viwango vya mambukizi ya virusi vya UKIMWI mionganini mwa watu wenye umri wa miaka 15 – 49 vimeshuka kutoka asilimia **7** mwaka 2003/2004 na kufikia asilimia **5.7** mwaka 2007/2008 na kuendelea kushuka kutoka asilimia **5.7** hadi asilimia **5.1** mwaka 2011/2012. Kwa mujibu wa takwimu za Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI idadi ya watu waliopatiwa huduma za ushauri na kupima VVU kwa kwa hiari imeongezeka hadi kufikia watu **42,021,146** mwezi Juni 2017 pamoja na kuongezeka kwa vituo vya ushauri nasaha na kupima VVU kwa hiari kutoka vituo **59** mwaka 1997 hadi kufikia vituo **6259** mwezi Machi, 2017. Idadi hii inajumuisha vituo vyote vya serikali na visivyo vya serikali.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa hadi kufikia Juni 2017 watu wanaoishi na VVU na UKIMWI wapatao **951,595** sawa na asilimia **2.3** walipatiwa huduma za tiba na mafunzo. Kati yao walioanzishiwa dawa watoto na watu wazima ni **935,228**. Sawa na asilimia **2.2** mionganini mwao ni watoto chini

ya miaka 15 ni **59,704**, vijana waliobalehe wenye umri kati ya miaka 15 -19 ni **20,845**. (Taarifa ya kitengo cha Taifa cha Kudhibiti UKIMWI- National AIDS Control Programme - NACP, Juni 2017).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza serikali kwa juhudini wanazofanya kwani unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na VVU umepungua, utafiti wa viashiria vya UKIMWI na Malaria nchini wa mwaka 2011/2012 unaonyesha kwamba wanawake na wanaume zaidi ya asilimia **90** wako tayari kumhudumia mwanafamilia mwenye UKIMWI katika familia zao. Aidha, katika kuimarisha afya za wananchi wanaoishi na VVU kwa mwaka 2016/2017 mashine kubwa na za kisasa zenye uwezo wa kupima wingi wa VVU (HIV Viral Load Monitoring) kwa sampuli (192 kwa mkupuo) zimefungwa katika hospitali ya Taifa Muhimbili, hospitali ya Temeke, hospitali ya rufaa Mbeya, na hospitali za mikoa ya Iringa, Ruvuma, Lugalo, Bugando, Tabora, Mtwara, Morogoro, Arusha, Dodoma, Rukwa, na Rubya Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa pia kuhusu changamoto ya ufinyu wa rasilimali watu na fedha za kutekeleza afua mbalimbali za UKIMWI pamoja na baadhi ya watu wanaotumia dawa za ARVs kushindwa kuzingatia matumizi sahihi na endelevu ya ARVs. Pia, ushiriki mdogo wa wanaume na wenza katika kutumia huduma za VVU na UKIMWI.

(b) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI inalo jukumu la kufuatilia utekelezaji wa serikali kuhusu Sera na Mipango ya udhibiti wa Dawa za Kulevyta. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati iliweza kukutana na Mamlaka hiyo ili kupokea na kujadili taarifa juu ya masuala ya dawa za kulevyta.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imekuwa ikifanya kazi ya kubaini na kuharibu mashamba ya bangi, kuzuia uvunaji wa mirungi, kupeleleza na kuchunguza uchepushaji wa dawa za tiba zenye madhara ya kulevyta pamoja na kemikali

zilizosajiliwa kutoka kwenye vyanzo halali. Wakati huo huo kuhakikisha dawa hizo zinapatikana kwa matumizi ya tiba, biashara na mahitaji ya kisayansi pamoja na kuzuia biashara haramu ya dawa za kulevyta na kuteketeza dawa zilizokamatwa na kuzuia utengenezaji haramu wa dawa za Kulevyta.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudini zinazofanywa na serikali katika kupambana na dawa za kulevyta kwani kasi ya ukamataji wa dawa za kulevyta imeongezeka, kuteketezwa kwa kiasi kikubwa cha mshamba ya bangi na kutambua na kudhibiti njia mbalimbali za kuitisha na kusafirisha dawa hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudini zinazofanywa na Mamlaka pamoja na wadau wengine katika kufanikisha uanzishwaji kwa huduma ya tila za utengemao wa warahibu katika mkoa wa Mbeya. Hata hivyo, Kamati inasisisitiza kuwa juhudini za haraka zifanyike ili mikoa ya Mwanza na Dodoma ianze kutoa huduma hiyo kwa kuwa majengo kwa ajili ya kutumika ili kutoa huduma hiyo yapo. Pamoja na jitihada hizo, kuna haja ya Serikali kuendelea kuihuisha huduma hii katika Sera ya Afya kama ilivyofanyika katika Masuala ya UKIMWI ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma hii kwa nchi nzima. Aidha, dirisha la kutolea huduma kwa waathirika wa dawa za kulevyta lianzishwe katika hospitali zote za rufaa na za mikoa yote nchin ili kuweza kuwafikia waathirika wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kuwa huduma hii inakuwa endelevu. Vile vile Kamati inaishauri serikali kuanzisha huduma hii katika hospitali zote nchini pamoja na kuwajengea uwezo kwa kuwapa mafunzo na stadi mbalimbali pamoja na mitaji itakayowawezesha waathirika wa dawa za kulevyta kuweza kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokutana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta iliweza kubaini changamoto zifuatazo:-

- (i) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyahaina bajeti ya kutosha kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ukamilifu mfano kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Mamlaka imetengewa kiasi cha shilingi 3.4 Bilioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha hii haitoshelezi kutokana na ukweli kwamba inahitaji kufanya operesheni nyngi za kudhibiti ulimaji na usafirishaji wa dawa za kulevyahama bangi na mirungi nchi nzima. Pia Mamlaka inahitaji kufungua ofisi za kanda ili kupanua na kusogeza huduma yake mikoani , kwani kwa sasa inafanya kazi kutokea makao makuu tu;
- (ii) Kushamiri kwa kilimo cha bangi pamoja na kilimo hicho kufanyika katika maeneo ya milimani ambako hakufikiki kwa urahisi hivyo kufanya operesheni za ukamataji kuwa na changamoto nyngi;
- (iii) Kukosekana kwa vitendea kazi vya kisasa vinavyosababisha kupungua kwa ufanisi katika udhibiti wa dawa za kulevyahini;
- (iv) Mamlaka inashindwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevyahili kunusuru afya za Watanzania na nguvu kazi ya Taifa kutokana na ufinyu wa bajeti;
- (v) Upatikanaji wa tiba za utengemao wa warahibu wa dawa za kulevyahini haujitoshelezi. Kwa sasa huduma hizi zinapatikana katika mkoa wa Dar es Salaam na Zanzibar pekee; na
- (vi) Kukosekana kwa programu maalum zenyelengo la kuwainua kiuchumi warahibu wa dawa za kulevyahambao huchangia kukwamisha juhudzi zao katika kuachana moja kwa moja na matumizi ya dawa za kulevyah.

Mhesimiwa Spika, Kamati pia inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyah (Sura ya 95) wa Mwaka 2017 (The Drug Control and Enforcement Amendment) Act,

2017. Hivyo kuifanya Mamlaka Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta Kuwa na nguvu na uwezo mkubwa wa kukamata, kuzuia na kipeleleza makosa mengine yanayojitokeza wakati wa kushughulikiaji/uchunguzi wa makosa mengine yatokanayo na dawa za kulevyta. Aidha, kutokana na mabadiliko ya sheria hiyo Mamlaka sasa ina uwezo wa kumiliki na kutumia silaha pamoja na kuboresha na kupanua wigo wa taratibu za ukusanyaji ushahidi kwa kutumia vifaa vya kisasa na kieletroniki.

(b) Kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni ya mwaka wa Fedha wa 2016/2017 na mchakato wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti za Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Taasisi hizo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Taarifa hizo ziliwasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) Toleo la Januari, 2016, mnamo mwezi Machi, 2017.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa **Bajeti** imekuwa ni changamoto kubwa kwa kuwa Taasisi zote zimekuwa hzipewi fedha zilivyoidhinishwa na Bunge kama inavyoelezwa hapa chini:-

(a) Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na Utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Hata hivyo, mpaka Kamati inapokea Taarifa mwezi Machi, 2017, hata nusu ya Bajeti ilikuwa hajatolewa, kwa mfano, katika mwaka wa Fedha 2016/2017, kati ya shilingi **bilioni 10.1** zilizokuwa zimetengwa ni shilingi **2.7 bilioni** sawa na asilimia **27** ya bajeti ndizo zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2017. Hali hii huathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubaini changamoto hiyo, Kamati ilichambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya


Taasisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na kutoa maoni yake ambayo yaliwasilishwa Bungeni tarehe 6 April, 2017.

Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS)

Mheshimiwa Spika, katika kikao chake kilichofanyika tarehe 25 Machi, 2017, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Makadilio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambayo inaonesha kuwa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) kwa mwaka 2017/2018 imeshuka kutoka *shilingi 10,192,509,413/=* hadi shilingi **5,983,975,859** sawa asilimia **50**, pamoja na serikali kuanzisha Mpango wa Test and Treat kwa ajili ya kutoa dawa pale mtu atakapopatikana na maambukizi ya VVU kuanza kutumia dawa za kufubaza maambukizi ya UKIMWI bado bajeti hii imepungua. Kamati ilibaini changamoto mbalimbali za klutendaji ambazo kwa kiasi kikubwa zilisababishwa na ufinyu wa bajeti zilizotengwa na Serikali kwa Tume hii kama zinavyoonyeshwa katika majedwali na chati ifuatayo:

JEDWALI NAMBA 1

**MWENENDO WA BAJETI YA TUME YA KUDHIBITI UKIMWI
TANZANIA KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE MFULULIZO
KUANZIA 2013/2014 HADI 2017/2018**



Chanzo: Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania kwa miaka ya fedha 2013/2014, 2014/15, 2015/16, 2016/17 na 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania ilikuwa inatarajia kukusanya maduhuli ya shilingi **25,000,000/=**. Aidha, Bajeti ya Tume ilianza kupungua katika kipindi cha mwaka 2013/2014 na kuwa katika hali yakupanda na kushuka hadi mwaka 2015/2016 kutohana na kupungua kwa mtiririko wa fedha za wafadhili katika bajeti ya miradi ya maendeleo. Aidha, kupanda na kushuka kwa mtiririko wa fedha za matumizi ya kawaida kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania katika kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2017/2018, kumesababishwa na ukomo wa bajeti ya Serikali. Kwa kiasi kikubwa mwenendo huu wa bajeti umeathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania katika mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI nchini.

(b) Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy


Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ilikuwa ya kuridhisha. Utendaji wa Taasisi hii ulikuwa wa Kuridhisha kutokana na mwenendo wa utoaji wa fedha kwani katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 iliyokuwa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevy ambayo kwa sasa haipo na imeundwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy ilitengewa kiasi cha shilingi **2.3 bilioni**, kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, kiasi kilichopokelewa ni shilingi **milioni 851.** ambayo ni sawa na asilimia **37** ya fedha iliyotengwa. Kamati inaridhishwa na mwenendo huu wa utoaji wa fedha kwani ikumbukwe kuwa dawa za kulevy ni kama Janga la Taifa linaloathiri zaidi vijana ambao ndiyo nguvu kazi katika nchi yetu. Mwenendo huu wa utoaji wa fedha utasalidla kuungeza kasi ya mapambano dhidi ya dawa hizo, hivyo na kuendelea kuwabaini na kuwakamata watuhumiwa na kuokoa vizazi vyetu na kuwa na Taifa lenye afya njema.

Mheshimiwa Spika, katika vikao vya Kamati vilivyofanyika kuanzia tarehe 25 hadi 26 Machi, 2017 Mkoani Dodoma, pamoja na majukumu mengine, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama ifuatavyo:

JEDWALI NAMBA 2:

MWENENDO WA BAJETI YA ILIYOKUWA TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA NA BAADA YA KUUNDWA MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO MFULULULIZO KUANZIA 2013/2014 HADII 2017/2018

MWAKA	FEDHA ZA MAENDELEO	MATUMIZI YA KAWAIDA	JUMLA	MAONI
2017/2018	0	4,015,912,991	4,015,912,991	
2016/2017	0	2,340,236,000	2,340,236,000	
2015/2016	860,000,000	2,159,488,359	3,019,488,359	
2014/2015	3,430,000,000	3,601,549,718	7,031,549,718	Bajeti inajumlisha Fedha za Wafadhili
2013/2014	2,798,000,000	2,587,176,826	5,385,176,826	Bajeti inajumlisha Fedha za



Chanzo: Bajeti za Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa miaka ya fedha 2013/14, 2014/15, 2015/16 na 2016/17.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya iliyokuwa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevyta ambayo kwa sasa haipo na imeundwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta katika kipindi cha mwaka 2013/2014 ilikuwa chini ikilinganishwa na 2014/2015, ambapo kushamiri kwa biashara ya dawa za kulevyta uliongezeka na bajeti ya Tume hiyo iliongezeka kutokana na umakini wa Serikali na wafadhili katika kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevyta nchini. Hata hivyo, katika kipindi cha mwaka 2015/2016 na 2016/2017, bajeti za Tume zilishuka hadi kufikia shilingi **0** kwa miradi ya maendeleo ambako kulisababishwa na mabadiliko ya vipaumbele vya wafadhili husika katika mwaka 2016/2017. Kwa mwaka 2017/2018 Bajeti ya Mamlaka imeongezeka kwa shilingi **1,675,676,991/=** na kufikia Shilingi **4,015,912,991/=** ikilinganishwa na shilingi **2,340,236,000** zilizotengwa kwa mwaka 2016/2017, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia **72** na hivyo kuchangia katika kuongeza ufanisi wa utendaji wa Mamlaka katika kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevyta nchini.

2.6 Uchambuzi wa Miswada

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Novemba, 2017, Kamati ilijadili na kuchambua Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta (Sura ya 95) wa Mwaka 2017 (*The Drugs Control and Enforcement (Amendment) Act, 2017*). Marekebisho ya Muswada huu yaliwasilishwa Bungeni na kuitishwa kuwa Sheria.

2.7 Ziara

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya kufuatilia utekelezaji wa Sera za UKIMWI na Dawa za Kulevyta, Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara katika Mikoa ya Manyara, Arusha, Njombe na Iringa. Kutokana na ziara hizo, Kamati imebaini bado upo ukatili kwa wanawake na watoto unaosababishwa na mila na desturi pamoja na mfumo dume uliotawala katika jamii hizo, ambao unachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la maambukizi ya VVU licha ya jitihada zinazoendelea kufanywa na Serikali pamoja na wadau mbalimbali katika kupambana na janga hili.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuchukua jitihada katika kukomesha mila na desturi potofu zinazochangia kuongezeka kwa maambukizi ya VVU hata ikibidi kutumia vyombo vya dola. Aidha, Kamati inaupongeza Mkoa wa Manyara na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kwa juhudi wanazofanya kuhakikisha maambukizi yanashushwa na kuwa kiwango cha chini kitaifa.

2.8 Semina kwa Wajumbe wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipewa semina mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uwezo Wajumbe. Semina hizo ni pamoja na:

(a) Semina ya Uchambuzi wa Bajeti

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI walipatiwa mafunzo kwa njia ya semina ilioendeshwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (*UNDP*) chini ya Mradi unaojulikana kama *Legislative Support Program (LSP II)* ilio chini ya Ofisi ya Bunge. **Katika semina hiyo wajumbe walijengewa uwezo wa namna ya kuchambua Bajeti ya Serikali hususan upangaji wa vipaumbele vya Taifa**. Semina hiyo iliifanyika tarehe 25 Oktoba, 2017 katika Ukumbi wa African Dreams Dodoma.

(b) Semina ya Hali ya UKIMWI Tanzania

Semina hii iliendeshwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*). Semina ilieleza kuwa kiwango cha uambukizo kinashuka katika jamii pamoja na idadi ya maambukizi mapya yanapungua kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2013 ambapo maambukizi mapya yalikuwa **72,000**, mwaka 2014 maambukizi mpya **69,603** na mwaka 2015 maambukizi mapya yalikuwa **48,000**. Semina hii iliawezesha **Wajumbe kuelewa umuhimu wa kuongeza mwitikio dhidi ya UKIMWI na kuongeza utashi wa kisiasa katika ngazi za jamii na Taifa ili kupambana na kupunguza kasi ya kuenea kwa maambukizi mpya**. Semina hii iliifanyika tarehe 26 Novemba, 2017 katika Ukumbi wa Zahanati ya zamani Ofisi ya Bunge Dodoma.

(c) Semina ya Sera, Sheria na Mikakati ya Afya

Semina hii iliendeshwa na Shirika lisilo la Kiserikali la *Tanzania Council for Social Development (TACOSODE)*. Lengo lake lilikuwa ni pamoja na Shirika kujitambulisha kwa Wajumbe wa Kamati ili kuwaeleza kazi zinazofanywa na Shirika hilo, pia kuwapa uchambuzi kuhusu Sera, Sheria na Mikakati ya afya ya Tanzania na uhusiano wake na afua za VVU na UKIMWI miongoni mwa makundi maalum. **Semina ilisaidia kupanua uelewa wa Wajumbe wa Kamati kuhusu masuala ya UKIMWI katika makundi maalum ambayo ni makundi ya watu ambao wapo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa sababu ya tabia mbalimbali zinazofanywa na makundi hayo.** Semina hii ilifanyika tarehe 25 November, 2017 katika Ukumbi wa Zahanati ya zamani Ofisi ya Bunge Dodoma.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Mhesimiwa Spika, Kamati inapenda kutoa Maoni na Mpendekezo kama ifuatavyo:-

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Mhesimiwa Spika, ili kutekeleza vyema majukumu ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Kamati inashauri mambo manane (8) yafuatayo:-

1. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini kwamba ufinyu wa Bajeti ya Serikali kwa Mamlaka unasababisha kutotekeliza majukumu yake kwa ukamilifu, kwani kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mamlaka imetengewa kiasi cha shilingi billioni 4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **hakukuwa na fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo**.

Mhesimwa Spika, Fedha hii haitoshelezi na hivyo kukwamisha utendaji wa baadhi ya majukumu ya Mamlaka kama vile:-

- a) Kufanya operesheni nyingi za kudhibiti kilimo na usafirishaji wa dawa za kulevyta kama bangi na mirungi nchi nzima pamoja na kudhibiti uingizwaji na usambazaji wa dawa nyingine za viwandani kama cocaine na heroin.
- b) Mamlaka inahitaji kufungua Ofisi za Kanda ili kupanua na kusogea huduma zake mikoani kwa kuwa mpaka sasa Mamlaka inafanya kazi kutokea Makao Makuu tu.
- c) Kudhibiti uingizwaji wa dawa za kulevyta katika mipaka yote ya nchi ambayo ni mingi na ina vipenyo vingi vinavyofanya zoezi la udhibiti kuwa gumu;
- d) Mamlaka kushindwa kuteketeza mashamba ya bangi ambayo hulimwa sehemu zisizofikika kwa urahisi ambapo utekelezaji wa zoezi hilo huhitaji fedha nyingi.
- e) Mamlaka kushindwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevyta ili kunusuru afya za Watanzania na nguvu kazi ya taifa letu ; na
- f) Kushindwa kufuatilia udhibiti wa uingizwaji wa dawa za kulevyta ambapo wafanyabiashara wa dawa hizo wamebuni mbini mpya ya kutumia kemikali na dawa nyingine za matumizi ya binadamu kutengeneza dawa za kulevyta pamoja na kuibuka kwa maabara bubu zinazotumika kutengeneza dawa hizo hatari .

Na kwa kuwa, kutotekeliza kwa majukumu ya msingi ya Mamlaka hiyo kutokana na ufinyu wa bajeti kunaathiri juhudii za udhibiti wa dawa za kulevyta nchini jambo ambalo lina madhara makubwa kwa taifa;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uzito wa kipekee wa majukumu yanayotekeliza na Mamlaka hii katika kupambana na biashara haramu ya dawa za kulevyta nchini, kwa kuongeza bajeti yao ili kufanikisha mapambano na kuiongezea ufanisi Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta; na hivyo kwa pamoja tunaweza

kujenga jamii imara ya Watanzania kwa kuachana kabisa na matumizi, na biashara ya dawa hizo.

2. Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwa, hakuna Sera ya Taifa ya Dawa za Kulevyaa japo tayari kuna Sheria ya Udhhibitii wa Dawa za Kulevyaa;

Na kwa kuwa, Sera hii ni muhimu sana kwa taifa kwani hutoa dira ya jambo linalohusika na jinsi ya kulidhibiti;

Na kwa kuwa tayari Kamati imedokezwa na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyaa kwamba, mchakato wa utungaji wa sera hiyo umekwishaanza kwa kukusanya maoni kwa wadau wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri kuwa Serikali iharakishe mchakato wa utungwaji wa Sera hiyo ili kulinusuru taifa na janga hili la dawa za kulevyaa.

3. Kwa kuwa, Kamati imebaini kutokuwepo kwa chombo cha kisheria cha kushughulikia udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevyaa katika ngazi ya halmashauri kama ilivyo kwa Kamati za UKIMWI kwa ngazi ya Halmashauri;

Na kwa kuwa, kukosekana kwa chombo hicho kama ilivyo kwa Masuala ya UKIMWI kunachangia udhibiti hafifu wa dawa za kulevyaa katika halmashauri nchini;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kufanya maboresho ya Kamati za UKIMWI za Halmashauri ili kisheria ziwe na uwezo wa kusimamia shughuli za udhibiti wa dawa za kulevyaa katika ngazi ya halmashauri.

4. Kwa kuwa, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto za upatikanaji usiotosheleza wa tiba kwa waathirika wa dawa za kulevyaa (*Medically Assisted Therapy*)nchini;

Na kwa kuwa, huduma hizo zinapatikana katika Mkoa wa Dar es Salaam Mbeya na Zanzibar pekee, jambo ambalo linasababisha jamii kubwa ya Watanzania kutofikiwa na huduma hii;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali ifanye juhudzi za haraka ili Mikoa ya Mwanza na Dodoma ianze kutoa huduma kwa kuwa majengo kwa ajili ya kutumika kutoa huduma hiyo yapo tayari.

(b) Serikali iendelee na kuihuisha huduma hii katika Sera ya Afya kama ilivyofanyika katika Masuala ya UKIMWI ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma hii kwa nchi nzima.

5. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini uwepo wa unyanyapaa kwa waraibu wa dawa za kulevyia punde wanapoacha matumizi ya dawa hizo kama kutengwa na jamii na kukosa ajira;

Na kwa kuwa, hali hiyo huwapelekea kurudia tena matumizi ya dawa za kulevyia au kujingiza katika vitendo vya uhalifu na kuenea kwa magonjwa kama vile kifua kikuu na UKIMWI pamoja na usugu wa Tiba kwa magonjwa hayo unaochangiwa na matumizi ya dawa za kulevyia;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuanzisha programu maalum za kuwasaidia waraibu wa dawa za kulevyia kuweza kuijinua na kujitegemea kiuchumi mara tu baada ya kuachana na matumizi ya dawa hizo.

6. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini kuwepo kwa mwamko mdogo na ushiriki hafifu wa jamii katika mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevyia;

Na kwa kuwa, hali hiyo kwa kiasi kikubwa imesababisha ongezeko la watumiaji wa dawa za kulevyia, wagonjwa wa akili, homa ya ini na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri:-

- a) Mamlaka ishirikiane na vyombo nya dola katika kuandaan kampeni endeleku ambazo mbali na kuwajengenea uelewa Watanzania kuhusu umuhimu wa kushiriki katika mapambano haya, pia itawapa motisha ya kushiriki katika mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya;
- b) Viongozi Wakuu wa nchi kutoa kauli thabiti na kusimamia utekelezaji wa kauli hizo katika kukemea na kukomesha biashara na matumizi ya dawa za kulevya ili kuhamasisha ushiriki wa jamii nzima katika janga hili; na
- c) Mafunzo kuhusu athari ya matumizi ya dawa za kulevya yaingizwe kwenye mtaala wa shule za awali, msingi, sekondari na vymuo nya elimu ya juu haraka iwezekanavyo ili kuwapatia uelewa na hivyo kuihusuru Jamii ya Watanzania kutokana na athari hizo.

7. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini kwamba nyumba za upataji nafuu (*Sobber Houses*) zinamilikiwa na watu binafsi;

Na Kwa kuwa, nyumba hizo hazina miongozo ya namna ya kuwapokea na kuwahudumia waathirika wa madawa hayo japokuwa Kamati ilifahamishwa kwamba serikali imekwishaandaa rasimu ya mwongozo huo;

Na kwa kuwa, nyumba hizo kwa hivi sasa zinaendeshwa kibiashara kwa familia kuchangia kiasi cha Sh. 100,000 mpaka 200,000;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri kwamba, Serikali ianzishe nyumba zake za kuwasaidia waathirika wa dawa za kulevya (*Sobber Houses*) kila Mkao ili kuwahudumia Watanzania walioathirika na dawa hizo.

8. **Kwa kuwa**, Kamati imebaini kwamba asilimia 100 ya dawa aina ya Methadone ambayo hutumika kuwasaidia waathirika wa dawa za kulevya nchini hutolewa na nchi muhisani kuituo chake cha kudhibiti magonjwa ya

kuambukiza (*Centre for Disease Control and Prevention - CDC*) ;

Na kwa kuwa, kufanya hivyo ni kuandaa bomu kwa siku za usoni kwa maana ufadhili huo unaweza kukoma muda wowote kutokana na sababu mbalimbali na hivyo kuathiri maisha ya Watanzania;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuandaa Bajeti kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa dawa hizo ukizingatia kwamba mahitaji ni mengi na wanaofikiwa na huduma ya dawa hizo ni wachache.

TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA (*TACAIDS*);

Mheshimiwa Spika, ili Tume hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa, Kamati inashauri mambo kumi (11) yafuatayo:-

1. **Kwa kuwa**, Sera ya UKIMWI ya Tanzania ya Mwaka 2001 imepitwa na wakati;

Na kwa kuwa, yapo mambo mengi yanayohusiana na masuala ya UKIMWI yamebadilika;

Na kwa kuwa, bado sera yetu haijaakisi masuala hayo;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wamapitio ya Sera ya UKIMWI ya Mwaka 2001 ili iweze kuzingatia mabadiliko katika mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI kitaifa na kimataifa.

2. **Kwa kuwa**, mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI yanategemea wafadhili kutoka nje ya nchi kwa asilimia 90;

Na kwa kuwa, Serikali imeanzisha Mpango wa *Test and Treat* ambapo mtu anapopatikana na maambukizi ya VVU humlazimu kuanza kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU

mara moja, hivyo huongeza mahitaji na gharama za manunuzi ya ARVs;

Na kwa kuwa, katika nchi yetu wafadhili walio wengi wamepunguza kiwango cha ufadhili kwa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI;

Na kwa kuwa, kwa kulijua hilo serikali ilianzisha Mfuko wa Udharnini wa Kudhibiti UKIMWI (*ATF*) ili kukabiliana na janga hilo;

Na kwa kuwa, bado Mfuko huo hauna vyanzo mahususi vyatapato;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuangalia vyanzo hivi ili Mfuko upate fedha za kukabiliana na Janga hili la UKIMWI. Aldha, Serikali ianzishe kisheria chanzo mahususi cha kutunisha Mfuko huu kama ilivyo katika Mifuko mingine kama vile Mfuko wa Barabara (*Road Fund*), Mamlaka ya Umeme Vijijiini (*Rural Energy Authority – REA*) ili kusaidia kufanikisha mwitikio huu wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI.

Serikali ifikie mahali na kupata ufumbuzi wa upatikanaji wa fedha hizo. Kwa kufanya hivyo, tutapunguza utegemezi mkubwa kwa fedha za wafadhili ambapo kwa sasa fedha hizo zimeambatana na masharti magumu. Halikadhalika, kwa mtazamo huu wa Test and Treat inamanisha wigo la wahitaji wa ARVs unazidi kuongezeka wakati wafadhili wanapungua, hivyo hatuna budi kujipanga ili tusije fikia wakati ambapo mahitaji yanazidi uwezo.

3. **Kwa kuwa**, Kamati ilibaini Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (*TACAIDS*) kwa mwaka 2017/2018 imeshuka kwa asilimia **50**:

Na kwa kuwa, hali hii inasababisha:-

a) Tume kushindwa kuajiri watumishi wa kutosha kwa baadhi ya Idara na Vitengo na kupelekeea nafasi hizo kuendelea kutokujazwa kwa wakati;

- b) Tume kuendelea kuwa na utegemezi wa fedha za nje kwa kutekeleza afua za UKIMWI ambao si endelevu;
- c) Tume kushindwa kuwaendeleza kitaaluma watumishi wake hasa katika maeneo ya Ukaguzi wa Ndani, Tathminina Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inayokua kwa kasi duniani; na
- d) Tume kushindwa kumudu gharama za uendeshaji wa ofisi kwa ujumla.

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri kuwa, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania itengewe fedha za kutosha na zipatikane kwa wakati ili kuiwezesha Tume hiyo kutekeleza shughuli zake ipasavyo.

4. **Kwa kuwa**, kumekuwa na upungufu wa dawa aina ya *Seprine* na dawa hizo ni muhimu sana kwa Watu wanaoishi na VVU (WAVIU);

Na kwa kuwa, dawa hizi ni muhimu sana kwa kupambana na magonjwa nyemelezi;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri Serikali kwamba, dawa zipatikane kwa wingi nchini lakini pia dawa hizi ziingizwe katika orodha ya dawa (*ARVs package*) ambazo wanapewa WAVIU ili kufubaza makali ya VVU na kuepusha magonjwa nyemelezi.

5. **Kwa kuwa**, kampeni za mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI ni kama zimekuwa na hivyo watu sasa wanafanya ngono zembe bila kuwa na hofu;

Na kwa kuwa, ukimya huu husababisha watu kujisahau na hivyo kufanya ngono zembe, hali ambayo inaweza kuleta mfumuko mkubwa hapo baadaye wa maambukizi mapya ya UKIMWI;

Na kwa kuwa, tunazo Taasisi ambazo zinatakiwa kufanya kampeni na kuwaelimisha wananchi lakini zimekuwa haziwajibiki ipasavyo;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mikakati ya kuhakikisha Kamati za Udhhibit wa UKIMWI katika kila ngazi zinafanya kazi ipasavyo. Aidha, Kamati inasisitiza TAMISEMI kuhakikisha vikao vya Kamati za UKIMWI kuanzia ngazi ya Halmashauri, Kata na Mtaa/Vijiji zinawajibika ipasavyo katika mwitikio wa masuala yanayohusiana na VVU na UKIMWI.

6. **Kwa kuwa**, UKIMWI umeathiri sehemu nyingi za kazi iwe serikalini au katika sekta binafsi;

Na kwa kuwa, bila kuwa na mipango thabiti ya kuwalinda watumishi kwa sekta hizi mbili, ukuaji wa uchumi wa Tanzania utashuka na hivyo kuathiri maendeleo ya nchi;

Kwa hiyo basi, Kamati inashauri sekta zote mbili kwa maana ya Serikali na Taasisi zake na Sekta binafsi nchini, iwe ni lazima kutekeleza Mipango ya UKIMWI (*HIV/AIDS*) mahali pa kazi na taarifa ziwe zikitolewa kwa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuititia Tume ya kudhibiti UKIMWI, Tanzania (TACAIDS).

7. **Kwa kuwa**, umri wa maamuzi Tanzania (*Age of Consent*)ni miaka 18

Na kwa kuwa, kuna Mkakati wa UKIMWI wa Kimataifa ujulikanao kama 90, 90, 90; kwa maana ya asilimia 90 ya watu wote wanaokisiwa kuishi na Virusi Vya UKIMWI wanatambua hali zao za maambukizi, asilimia 90 kati yao wanatumia dawa za kufubaza makali ya Virusi Vya UKIMWI (*ARVs*) na asilimia 90 ya hao wanaotumia dawa uwezo wa virusi vyao kuambukiza uwe umefubazwa;

Na kwa kuwa, athari za UKIMWI kwa watoto chini ya miaka 18 ni kubwa;

Na kwa kuwa, upimaji wa watoto hao hutegemea ridhaa ya wazazi kwa kuwa wao kisheria hawana mamuzi hayo;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri serikali ipunguze umri wa maamuzi binafsi (*Age of Consent*) kutoka miaka 18 hadi miaka 15 au 16, illi hata Mkakati wa 90, 90, 90, uweze

kufanikiwa na kufikia malengo ya tisini – tatu (90 - 3) ifikapo mwaka 2020 na kuumaliza kabisa UKIMWI nchini ifikapo 2030. Aidha, Kamati inashauri suala la upimaji wa VVU lipewe mkazo zaidi ili kuweza kufikia malengo yaliyopo ambapo wigo mkubwa wa WAVIU waweze kujifahamu hali zao na kuanzishowi dawa ili virusi walivyonavyo viweze kufubazwa na hatimaye kupunguza kasi ya maambukizi mapya ya VVU mionganoni mwa jamii yetu.

8. **Kwa kuwa**, moja ya sababu zinazochangia mabinti wengi kuambukizwa VVU ni ukeketaji wa watoto wetu wa kike (*Female Genital Mutilation - FGM*) kwani wakati mwiningine hutumia kifaa kimoja kukeketa na kwa hivi sasa suala hili hufanyika kwa usiri mkubwa;

Na kwa kuwa, jambo hili pia ni kinyume cha haki za binadamu;

Na kwa kuwa, baadhi ya waathirika wa jambo hili wanashindwa kutimiza malengo yao kimaisha kutohana na madhara ya ukeketwaji;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri serikali kupiga marufuku ukeketaji na ikiwezekana kuwepo na sheria kuwa ukeketaji hauruhusiwi Tanzania.

9. **Kwa kuwa**, kuna taasisi za kitaifa na za kimataifa zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI nchini;

Nakwa kuwa, taasisi hizi hupokea fedha nydingi za UKIMWI;

Na kwa kuwa, bado hakuna ufuatiliaji wa kujua fedha hizi zinavyotumika;

Na kwa kuwa, Kamati pia ingependa kujua kazi zinazofanywa na taasisi hizo;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuititia *TACA/IDS* kufuatilia (*coordination*) taasisi hizo zinavyotekeleza kazi zao.

10. **Kwa kuwa**, kukaa bila kazi kunaruhusu makundi ya vijana kuijingga kwenye vishawishi mbalimbali ikwemo kufanya ngono zembe na hivyo kupata maambukizo ya magonjwa mbalimbali ikiwepo VVU;

Na Kwa kuwa, nchi yetu ina fursa ya kilimo kwa maana ya kuwa na ardhi ya kutosha na yenyе rutuba;

Na kwa kuwa, vijana wakipatiwa rasilimali fedha wanaweza kujikwamua kiuchumi kuitia kilimo na kuachana na tabia hatarishi;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mashamba na kuwakopesha vijana mikopo midogo midogo ili waweweze kulima mashamba hayo na ikiwezekana wapatiwe mbegu bure mfano za mikorosho ambayo ni kati ya mazao yanayohitajika sana katika soko la dunia hivi sasa.

11. **Kwa kuwa**, yapo makundi maalum ambayo yasipoangaliwa yataleta athari kubwa sana kwa siku za usoni;

Na kwa kuwa, makundi yanayofahamika ni watumia madawa ya kulevyia (*Injectable Drug Users – IDU*), watu wanaojihusisha na ngono za jinsia moja (*MSM & Lesbians*), watu wanaojiuza (*Sex Workers – SW*);

Na kwa kuwa, wanafunzi nao ni kundi hatarishi kutoekana na kujihusisha na mahusiano yasiyofaa ya kuwa na wapenzi wengi kwa wakati mmoja;

Na kwa kuwa, hali hiyo ni hatari sana kwa mustakabali wa maisha yao na uchumi wa Taifa;

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali iandae Programu Maalum kwa vijana walio ndani na nje ya shule. Ambapo waliopo shulenii waandaliwe klabu maalum zitazohusika na masuala ya VVU na UKIMWI kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu. Halikadhalika, uanzishwaji wa huduma rafiki kwa vijana (Youth Friendly Services) katika kila Mtaa na Kijiji ambazo zitasimamiwa kwa karibu na kamati za kudhibiti UKIMWI za ngazi ya Mtaa na Kijiji husika.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake hadi kufikia Januari, 2018. Tunaamini kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Ajira, Vijana na Walemavu, Mhe. Jenista Mhagama, Mb na Naibu Waziri Antony Mavunde na Stella Ikupa, Mb. Aidha, nampongeza pia Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, Dkt. Leonard Maboko na Kamishna wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevyta, Ndg. Rogers Siyan'ga na Watendaji wote wa Tume na Mamlaka kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kipindi cha mwaka mzima, kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufanuzi mara zote ulipohitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa uchapakazi wao wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa mwaka mzima. Wajumbe wamefanya kazi kubwa katika kuhakikisha Kamati inaisimamia na kuishauri vyema Serikali kwa mujibu wa Katiba ya Nchi na Kanuni za Kudumu za Bunge. Napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kwa majina kama ifuatavyo:-

- | | |
|---|--------------|
| 1. Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa Bunga, Mb | M/Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb | Mjumbe |
| 3. Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mb | Mjumbe |
| 4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb | Mjumbe |
| 5. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb | Mjumbe |

6. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Kemirembe Julius Lwota, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Lucia Ursula Michael Mlowe, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Mary Deo Muro, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Martha Mosses Mlata	Mjumbe
12. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Yussuf Kaiza Makame, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Zainab Matitu Vullu, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athumani Hussein, Wakurugenzi Wasaidizi, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Asia Msangi, Ndg. Happiness Ndalu na pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Mwenye, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelizwa, Uchambuzi wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo mbele ya Bunge lako Tukufu, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, kuikubali na kuijadili Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

.....

Dkt. Jasmin Tiisekwa Bunga, Mb

MAKAMU MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI

7 FEBRUARI, 2018

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jasmin kwa kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI. Sasa tunaanza mjadala wetu na tutaanza na Mheshimiwa George Lubeleje, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Mwalongo na Mheshimiwa Susan Lyimo ajiandae. (*Makofii*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Kamati hizi mbili. Kwanza niwapongeze sana Wenyevitit wa Kamati na Kamati kwa kazi nzuri sana wanayofanya kwa sababu kama Kamati ya Maendeleo ya Jamii majukumu yao ni mengi na sekta zao ni nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na suala la sekta ya afya. Sekta ya afya ina changamoto nyingi sana, sasa hivi wananchi wanajenga zahanati na vituo vya afya. Sasa unavyosema jengo la zahanati, kituo cha afya au hospitali ya Wilaya siyo jengo tu, ni dawa pamoja na watumishi. Hata hivyo, pamoja na kwamba katika bajeti hii tumetenga shilingi bilioni 251 kwa ajili ya kununua dawa, vifaa tiba pamoja na vitendanishi lakini bado kuna upungufu mkubwa sana wa dawa katika hospitali zetu za wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atembelee Hospitali za Mikoa, Wilaya na Vituo vya Afya hasa vijijini ndiyo kabisa maana linakwenda sanduku moja, idadi ya watu ni 2,000 mpaka 3,000, dawa hazitoshi. Naomba viongozi wetu wa Wizara ya Afya mnapotamka kwamba hakuna upungufu wa dawa kabisa, hospitali zetu zote zina dawa za kutosha, hapana, upo upungufu mkubwa sana wa dawa. Pamoja na hii bajeti kuongezwa, lakini tujitahidi kuongeza fedha za kutosha tununue dawa za kutosha ili wananchi wetu wapate huduma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo hii unakwenda katika hospitali, mganga anamwandikia mgonjwa dawa anakwenda kununua duka la mtu binafsi, bado wapo na

haipendezi kabisa. Tulishauri kwamba *MSD* wajenge maduka katika baadhi ya Hospitali za Wilaya ili dawa zinazokosekana kwenye *pharmacy* ya hospitali basi zipatikane pale. Kwa sababu bei ya dawa katika maduka ya watu binafsi ni kubwa zaidi kuliko haya maduka yetu ya *MSD*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni sekta ya elimu. Wizara ya Elimu imeanzisha kidato cha tano na cha sita katika baadhi ya shule kwenye wilaya zetu. Hata hivyo, kuna changamoto kubwa sana ya mabweni, mabwalo, na chakula. Hizi shule zimeanzishwa *form five* na *six* lakini wameachiwa wananchi ndiyo wanaojenga. Siyo vibaya wananchi wakajenga madarasa, mabwalo na hosteli lakini tunaomba Serikali isaidie vifaa vya kukamilisha majengo haya, ni shida sana, vijana wanasoma katika mazingira magumu. Maana *form five* na *six* vijana wale hawatoki mazingira ya pale pale bali Mikoa yote ya Tanzania. Kwa mfano, tuna Shule ya Sekondari ya Wasichana Mazae, mazingira yake ni magumu sana. Tumejenga hosteli na mimi Mbunge nilitoa mifuko 200 kwa ajili ya kujenga hosteli, lakini mazingira ni magumu. Kwa hiyo, naomba Serikali isaidie vifaa vya kukamilisha majengo yale. Wananchi tunawahamasisha, wako tayari wanajenga lakini vifaa vya kukamilisha majengo hayo hatuna. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya chakula ni kidogo sana. Mwanafunzi mmoja anapata hela ya chakula kwa siku shilingi 1,500 kwa asubuhi, mchana na jioni kwa hizi shule za bweni. Hivi kweli unaweza kula *breakfast, lunch* na *dinner* kwa shilingi 1,500? Haiwezekani. Kwa hiyo, naomba waongeze fedha za chakula kwa siku angalau iwe shilingi 2,500, hii inaweza kuwatoshha wanafunzi lakini siyo shilingi 1,500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri kwa kuwa Halmashauri zetu za Wilaya zina shule za msingi pamoja na sekondari kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne, naomba Wizara ya Elimu mngewapokea *form five* na *six* muwapunguzie majukumu Serikali za Mitaa maana wana majukumu kweli. Toka elimu ya msingi, darara la kwanza

mpaka darasa la kumi na mbili halafu mnaongezea tena kitado cha tano na kidato cha sita, yote Halmashauri ya Wilaya. Nashauri *form five* na *six* Wizara ya Elimu yenyewe ishughulikie hizi shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la lingine ni kuhusu suala la UKIMWI. Ushauri wangu ni kwamba Serikali inatenga fedha nyingi sana na wafadhili wanaleta fedha nyingi sana kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI na fedha hizi zinapelekwa katika Halmashauri zetu za Wilaya lakini zisimamiwe basi ziwahudumie waathirika wa UKIMWI wenyewe. Sasa hivi wananchi wanaelewa UKIMWI ni nini lakini fedha nyingi sana zinakwenda kwenye semina makongamano wale waathirika kabisa wa UKIMWI hawafaidiki. Kwa hiyo, nashauri wale waratibu wa UKIMWI kwa kila Halmashauri wakipata hizi fedha wahakikishe walengwa ndiyo wanafaidika na hizi fedha, siyo kuanzisha semina na mambo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini la pili nipongeze sana hizi Kamati mbili kwa kazi na taarifa nzuri sana. Naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje. Tunaendelea na Mheshimiwa Edward Mwalongo na Mheshimiwa Susan Lyimo ajiandae.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hizi taarifa za hizi Kamati mbili. Kwanza kabisa, niwapongeze Wenyeviti wa Kamati jinsi walivyowasilisha kwa umahiri lakini niwapongeze vilevile wanakamati wote walioshiriki kuchakata taarifa hizo mpaka hapo zilipofikia, tunawapongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la upungufu wa walimu kwenye shule hasa hasa za msingi. Tatizo hili ni kubwa sana na Serikali inachelewa sana kuajiri. Ukitaka kuona Taifa linajimudu ama linaenda vizuri kwa maana ya misingi

yake inajitetea vizuri na linaangalia mbele kwamba litafika wapi ni kusimamia elimu. Tunapokuwa hatupeleki walimu shulenii maana yake hili Taifa linaenda kuwa mfu kesho. Watoto hawa wanakosa walimu, wenyewe kama watoto hawawezi kulalamika, lakini matokeo yake tutayakuta huko mbele ya safari kwamba tutakuja kuwa na Taifa ambalo linajiwajibisha kabisa lenyewe kwa sababu watoto hawa watakuwa wamekosa elimu na maarifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi umetokea mgao wa walimu na tulivyojaribu kufuatilia tuliambiwa ni fidia ya walimu wenyewe vyeti batili. Mimi katika Halmashauri yangu Mji wa Njombe sikupata mwalimu hata mmoja wakati wenyewe vyeti batili walikuwa 12, hapa nifanyeje, si nione kama kuna upendeleo? Kama jibu ni vyeti batili, sijapata walimu na mimi wenyewe vyeti batili walikuwa 12. Kwa hiyo, tukienda kwa utaratibu huo kama ni kweli ni vyeti batili tunagawa tugawe kwa usawa. (*Makofii*)

Naomba niiambie Serikali kwamba Halmashauri ya Mji Njombe ni jina tu, lakini yenyewe ina kata 13 na kata moja tu ndiyo mji lakini kata nydingine ni vijijini, kwa hiyo, tuichukulie kwa kigezo hicho. Leo hii Halmashauri ya Mji Njombe ina upungufu wa walimu 454, hivi hapa tutaoa elimu kwa hawa watoto, si tunawapeleka tu wakacheze shulenii mwisho wa siku wanatoka hawajapata elimu yoyote. Naomba sana hili liangaliwe kwa sababu elimu ni suala muhimu sana, tukicheza na elimu maana yake ndiyo tunaliua Taifa taratibu. Sisi tunaweza tukawa hatuoni kwa sababu sisi tumepata elimu, lakini kipo kizazi ambacho tunakilea sasa ambacho kinahitaji kupata elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa watahamisha walimu kutoka sekondari, zoezi hilo linakwenda polepole mno utafikiri kwamba wanaofanya hilo zoezi sijui hawalijui au hawana uhakika au hawajiamini. Haioneshi kabisa kwamba hili zoezi ni la haraka kwa sababu kuna shida ya walimu mashulenii hasa ukizingatia sasa hivi limetolewa tamko la marufuku kuchangisha mashulenii. Madarasa ya awali na baadhi ya madarasa walikuwepo walimu

wanajitolea lakini wazazi walikuwa wanachangia sasa hiyo kitu tumeambiwa ni marufuku, hivi hatma ya hawa watoto itakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine matamko ya Serikali yanatia shaka kwa sababu unakuja kuona kwamba yalikuwepo madarasa ya awali katika maeneo mbalimbali ambayo yalikuwa yanakwenda vizuri kabisa na wananchi walikuwa wanalipa ada kwa ajili ya watoto wao, Serikali ikasema darasa lolote lile la awali lazima liwe chini ya shule ya msingi, ni marufuku kuwa na darasa la awali nje ya shule ya msingi. Watoto wale wamepelekwa kule shule ya msingi hakuna walimu, wameondoka mahali ambapo kuna walimu, hivi nia hasa ya Serikali ni nini, kwamba watoto wapate elimu au ni mtizamo ambao mimi nauona kwa upande fulani una kama vivu au chuki kwamba hawa wenye shule za watoto wananaufalka kwa hiyo tuwanyang'anye hawa watoto tuwapeleke shulenii. Mmewanyang'anya watoto mmewapeleka shulenii, shulenii kule wale watoto hawana walimu, matokeo yake mnawaathiri watoto hawa. Kwa sababu watoto hawawezi kulalamika hamuwezi kuona madhara yake, lakini tutambue sisi wote ni Watanzania leo sisi tunawawakilisha wananchi, lakini hawa Watanzania wa kesho wanakosa huduma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ziko ramani zinatoka Wizara ya Elimu zinaitwa MESS Makao Makuu kitu kama hicho zinapelekwa mashulenii kwa ajili ya ujenzi wa shule. Tumepiga kelele sana humu ndani juu ya suala la watoto wa kike kujisitiri. Maelezo yanasema kila shule iwe na mahali maalum pa watoto wa kike kujisitiri Serikali hiyo hiyo inaleta ramani haina chumba cha kujisitiri. Sasa hayo maelezo anapewa nani na anatekeleza nani? Hebu tuangalie tunapotoa maelezo tuhakikishe kwamba maelekezo haya yanakwenda kujibu ile kiu ambayo wananchi na wawakilishi wao wanahitaji wapewe huduma. Kama Serikali haiwezi kwa sasa kuwapa watoto hawa taulo za kujisitiri basi hata iwajee chumba maalum. Maelekezo yanasema hivyo, lakini utekelezaji unakwenda kinyume. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo jambo lingine, uko mkanganyiko kati ya taasisi mbili za Serikali, iko Idara ya Wakaguzi wa Elimu lakini iko Idara inashughulika na usalama mahali pa kazi. Wananchi wanajenga darasa ile idara inakuja kusema darasa hili halina mwanga wa kutosha wakati Wakaguzi wa Elimu wamekagua na wamepitisha hilo darasa, sasa hapo wananchi wafanye nini? Kwa hiyo, nafikiri Idara hizi za Serikali zijaribu kuona ni namna gani zinaweza kushirikiana ili kusudi wananchi wakifanya shughuli ikikamilika iwe imekamilika. Siyo Idara hii ya Serikali inaseme shughuli hii haina sifa, shughuli hii ina sifa. Kwa hiyo, naomba Idara za Serikali ziwasiliane katika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni elimu ya ufundi. Sasa hivi tunakwenda kwenye Tanzania ya Viwanda, ndugu zangu Wabunge humu ndani nawaambieni hivi viwanda tunavyohamasisha vijengwe tunakwenda kulfanya hili Taifa kuwa la watwana kwa sababu vijana wetu hawana ujuzi, sasa ni nani atakayefanya kazi kwenye hizo taasisi? Tunasema VETA wakati inakwenda mwendo wa konokono hakuna mfano wake, hawana vifaa wala walimu, VETA wana mitaala ya miaka 70 iliyopita wanafundisha sijui *calibrator*, wanafundisha vitu vya ajabu ajabu ambayo havipo kwenye ulimwengu wa sasa wa utendaji hasa hawa ndiyo wanatakiwa kwenda kufanya kazi kwenye viwanda vinavyojengwa na tunafahamu viwanda vinavyokuja ni vya teknolojia ya kisasa. Kwa hiyo, tunakwenda kuwapeleka Watanzania mahali ambapo watakuwa wafagia uwanja, wapakia mizigo, ndiyo kazi wanazokwenda kufanya. Kama kweli tunahamasisha viwanda sisi kama Watanzania tuwapange vizuri vijana wetu wapate elimu nzuri ya kuweza kuajirika huko kwenye viwanda vyenye teknolojia ya kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la UKIMWI. Tafiti za UKIMWI zinanitatanisha sana, mimi ni Mbunge wa Njombe Mjini na ukiangalia kwenye taarifa za Serikali Njombe ndiyo tunaambiwa sisi tunaongoza kwa UKIMWI katika nchi hii, lakini hizi *data* ni za lini kwa sababu mimi hapa nahisi kuna kuonewa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za miaka kumi mpaka leo ndiyo zinatumika kwamba Mkoa unaoongoza kwa UKIMWI Tanzania ni Njombe, siyo kweli tutendeane haki. Kama mnataka kutoa utafiti wa kisasa na wa kitaalam fanyeni utafiti kila mwaka.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU): Tumefanya mwaka jana.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Si kweli, si kweli. Kwa hiyo, mimi taarifa hizo za Serikali naanza kupambana nazo kwa sababu...

T A R I F A

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kumpa taarifa mzungumzaji anayezungumza hivi sasa. Ningependa tu nimwambie kwamba takwimu za maambukizi ya UKIMWI zilizotolewa na watafiti Mkoa wa Njombe ni za kweli kwa sababu moja, sisi watu wa Mkoa wa Njombe tunapima sana kuliko mikoa mingine na ndiyo maana tumeweza kupata nanihii.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwalongo, taarifa hiyo umeipokea?

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nina mashaka sana na takwimu hizi za Serikali juu ya suala la UKIMWI. Hata hivyo, kama kweli Serikali inatuona kweli sisi watu wa Njombe ndiyo tunaongoza kwa UKIMWI mbona haitusaidii kupunguza UKIMWI? Zana zile za kujikinga hatuletewi...

TAARIFA

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwalongo, subiri kidogo, Mheshimiwa Jenista.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka 2017 siku ya UKIMWI Duniani Serikali ndiyo imezindua taarifa ya utafiti ambayo ni *current*. Taarifa hiyo iliyozinduliwa tarehe 1 Desemba, 2017 ndiyo imeonesha hiyo hali halisi na hali ya Njombe ndivyo kama hivyo ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachoweza kusema hapa wakati tutakapokuwa tunajibu, tutamjibu vizuri. Cha msingi Mheshimiwa Mbunge atoe ushirikiano tu na Serikali kusudi tuweze kwa pamoja kwa sababu tumeweka nguvu ya pamoja kuhakikisha tunapambana na maambukizi ya mapya ya UKIMWI ili kupambana na UKIMWI katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, awe tu mtulivu, tutafanya kazi kama Serikali kwa pamoja na yeye.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwalongo.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi za Serikali sawa tunakubaliana nazo kimsingi, lakini ukitokea ukame hapa, wale wanaokuwa wamefiwa na ng'ombe huko, Serikali inawapa ng'ombe; ikitokea njaa watu wanapelekewa misaada ya chakula. Sisi tuna UKIMWI, kwa nini hatusaidiwi? Kama sisi tuna UKIMWI, tupeni hiyo misaada basi tuione. (*Kicheko/Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaichotaka Serikali ioneshe kweli kwamba Njombe wanateketea. Njombe ikiteketea, maana yake Watanzania watokosa *chips*, ndio wakulima wa viazi hao, watakosa maparachichi, mtakosa *ma-housegirl* mnaokuja kuwachukua Njombe na sisi tumepiga marufuku. Kwa sababu hawa watoto wetu mnawachukua kwa ajili ya kufanya kazi za ndani, nao ni sehemu ya kuchangia UKIMWI Njombe. Mnawaacha kwenye majumba

yenu, hawana ulinzi wala uangalizi, wanaambukizwa UKIMWI wanarudhishwa vijiji kule, wanaenda kupaka vijana vijiji. Kwa hiyo, nawaomba sana, msije tena Njombe kuchukua ma-housegirl, tumekataa. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu kwa leo ni hayo. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwalongo. Tunaendelea na Mheshimiwa Susan Lyimo na baadae Mheshimiwa Abdallaa Mtolea ajiandae.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Kipekee naipongeza sana Kamati yangu ambayo inaitwa Guantanamo kwa kuwa ina vichwa vikali sana. Pia napongeza kwa taarifa nzuri, lakini vilevile Taarifa ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza zaidi kwenye elimu kwa sababu mimi ni mwalimu, lakini vilevile nitagusia mambo ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi ye yeyote au jamii yoyote hapa duniani ambayo imeendelea bila kuwekeza kwenye elimu, lakini sekta ya elimu hapa nchini inakumbwa na changamoto nyingi sana. Changamoto ya kwanza hatuwezi kuwa na elimu bora kama walimu hawajapewa mahitaji yao. Kumekuwa na kilio kikubwa sana cha walimu na hapa Bungeni kila siku tumekuwa tukizungumza na hata leo maswali mengi huwa yanaelekezwa kutetea maslahi ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea, walimu walioajiriwa Januari hadi leo hawajapata mishahara wala fedha za kujimu. Hawa ni vijana wadogo wanaomaliza vyuo. Tunategemea vijana hao, hasa watoto wa kike waolewe na Wenye viti wa Mitaa au waolowe na Wenye viti wa Vitongoji? Kwa hiyo, hayo ni matatizo makubwa. Tunaomba Serikali ituambie, ni kwa nini wanaajiri watu halafu hawawapi mishahara wala posho za kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa walimu ni kuhusu masuala ya madaraja. Niliuliza swali kwa Waziri Mkuu hapa kwamba watumishi...

T A A R I F A

MHE. HAWA A. GHASIA: Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Susan, taarifa.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa anayezungumza anasema kwamba hao walimu wataolewa na Wenyeviti wa Mitaa au Wenyeviti wa Vitongoji, kwani Wenyeviti wa Mitaa na Vitongoji sio wanaume wa kuweza kuoa walimu au hata Wabunge na watu wengine?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo taarifa hiyo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wanaweza, lakini hiyo watakuwa wanaolewa bila ya ridhaa yao kutokana na matatizo hayo ambayo wanayapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu suala la madajara. Baada ya zoezi la kuhakiki, ndani ya mwaka mzima, baadhi ya watumishi pamoja na walimu hawakulipwa nyongeza hizo. Na sisi tunajua kabisa watumishi ni endelevu, kwa hiyo, hilo zoezi la uhakiki limewaathiri sana watumishi wa umma wakiwemo walimu. Tunaomba pia Serikali ituambie ni kwa nini katika zoezi hilo wamehakikisha kwamba mwaka mzima watu hawa hawajapata maslahi yao au nyongeza zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kwa sababu nimesema kwenye elimu bora, ni walimu, vitabu na mazingira bora ya kufundishia, utakumbuka kwamba wakati wa bajeti ya mwaka 2017 tulizungumza suala la vitabu vibovu, ikapelekea Kamishna wa Elimu pamoja na baadhi ya watumishi kusimamishwa kazi lakini mpaka leo tunavyozungumza na Waziri alisema itaundwa Tume, lakini

mpaka leo kama ambavyo imeandikwa kwenye Kamati yetu, bado hatujapata *report*, lakini kubwa ambalo nataka kuzungumza, mpaka leo wanafunzi hawana vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleweke kwamba *life span* ya vitabu ni miaka miwili mpaka mitatu kwa darasa la kwanza mpaka la nne kutokana na matumizi, lakini vitabu vya mwisho vimeduwa *published* mwaka 2013. Leo ni mwaka wa tano bado hatuna vitabu na tunategemea wanafunzi hawa wafaulu. Wanafaulu vipi kama walimu hawana *morale*, lakini na vitabu navyo havipo ambavyo ndio sehemu kubwa kabisa ambayo watoto wangeweza kusoma vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana kuwe na Tume kabisa au Kamati ya Bunge ambayo itapita kwenye shule kuona kweli tatizo hilli ni kubwa kiasi gani illi Wizara iwajibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna suala kubwa tulizungumza na limezungumzwa kidogo, suala la *re-entry policy*. Naomba nirudie, tulizungumza, nikategemea Kamati inapotoa ushauri, maana yake wameona mambo mengi, lakini Serikali ikalipiga chini. Leo limekuja kwa mlango mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme hivi, Serikali hii ilitoa *guidelines* kwa jinsi gani wanafunzi hawa wanaweza kurudi shulenii. Hata hivyo lilikuwa *diluted* ikaonekana kwamba watoto wanaopata ujauzito ni wachache sana. Sasa najuliza, kama ni wachache sana kwa nini wasirudi shulenii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mazingira mengi ambayo yanababisha matatizo hayo. Kuna mazingira magumu sana yanayosababisha matatizo hayo ambapo Serikali nayo inayajua. Mazingira hayo ni pamoja na kubakwa, vilevile tunajua kwamba shule ziko mbali, watoto wanakienda shule wanapita maeneo magumu, wazazi ni masikini, lakini hayo yote hayajazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba tunaomba sasa ni kwa nini kama Kamati imetoa maelekezo yake au ushauri, mtu mmoja tu anaweza kuja akabadilisha *the whole thing. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona mgongano mkubwa uliopo, pamoja na kwamba maombi ya *re-entry*, yaani warudishwe shulenii yamekataliwa, lakini hapo hapo, AG tayari Mahakama ilishatoa hukumu yake mwaka juzi (2016), kwamba ile Sheria ya Ndoa, kifungu namba 13 na 17 hukumu ikawa *in favour*, lakini AG hapa Bungeni akatuambia kwamba Serikali imekata rufaa na wakati kweli ilikuwa hajjakata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pamoja na kugundua kwamba AG amekata rufaa Septemba, 2017 yaani mwaka mmoja na mlezi miwili baada ya hukumu; tulikuwa tunaomba AG atasaidie, hivi ni muda gani au ni *time frame* gani baada ya hukumu mtu anaweza kukata rufaa? Kwa sababu hii ni mwaka mmoja na miezi miwili, ndiyo AG ameenda kukata rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtuambie, kwenye Katiba inaonesha kwamba kazi za AG ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye anaishauri Serikali. Sasa naomba mje mtueleze, hivi kweli AG anatoa ushauri kwamba mtoto wa chini ya miaka 18 anaweza akaolewa *at the same time* mnasema mtoto asipate ujauzito. Mtoto aliyepata ujauzito, asirudi shulenii! Kwa hiyo, hii *contradiction* na tutaomba hii *contradiction* mtusaidie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nataka kuzungumzia ni suala la mabweni yanayo julikana kama *Magufulli Hostel* kwa suala la *expansion joint*. Niliongea kwa muda mrefu, yale mabweni mltiuambia yamegharimu shillingi bilioni 10, lakini wengine wanasema shillingi bilioni 53, lakini madhara yake tumeyaona. Mnatuambia *expansion joint*; mimi navyojua *joint* ni pale kwenye maungano. Sasa kama zimepasuka mpaka maeneo mengine kwenye makabati na wapi, *joints* hapo ziko wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba kabisa *CAG* afanye utafiti na ukaguzi wa kina, aje atuletee ripoti, hayo mabweni yamegharimu shilingi ngapi? Kwa nini kumekuwa na huo mpasuko? Kwa nini aliyeripoti akapelekwa Polisi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni kuhusu matokeo ya mitihani ya kidato cha nne. Tumekuwa tukizungumza mara zote na kwa historia, nashukuru kwamba Kamati imeleta *summary* kwamba kwa miaka mitano na hata hiyo mingine, ufaulu haujawahi kuzidi asilimia thelathini kwa maana ya *division one* mpaka *division three*. Naamini ina maana *division four* na *zero*, hiyo ni sawa na *zero* tu.

MBUNGE FULANI: Kabisa.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Hawaendi popote. Kwa hiyo, ina maana asilimia 70 ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha nne kwa miaka yote, hawaendi popote. Halafu tunazungumzia ubora wa elimu. Ukiangalia, hiyo asilimia 30, asilimia zaidi ya 80 wanatoka shule binafsi. Halafu Serikali hii inawaambia watu wenyewe shule binafsi, ni marufuku watoto kukariri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishangaa hii Serikali, tumesema siku zote, haiwezekani Serikali ambayo ina shule zake, yenyewe iwe refa, iwe mchezaji, iwe kocha; haiwezekani. Tukasema ni lazima kuwe na chombo maalum kitakachosimamia hizi shule; na ndiyo sababu kumekuwa na ubaguzi mkubwa kwenye suala la ukaguzi katika shule za *private*. Wanalipa shilingi 5,000 kwa kila mwanafunzi, lakini kwenye shule za Serikali ni bure na ndiyo sababu hakuna ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni muhimu sana Serikali iangalie kwamba kuna umuhimu wa kuwa na chombo ili kudhibiti ubora wa elimu hapa nchini, na sio wao wenyewe wanasimamia, shule nyingine zinakuwa

hazina hata vyoo, hazifungwi, zinaendelea, zinasajiliwa, lakini za *private* hazifanyiwi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la afya. Kwenye suala la afya napongeza juhudzi zote, lakini niseme tuna tatizo kubwa la watumishi wa Wizara ya Afya na wamekiri wenye kwenye kitabu chao kwamba wana upungufu wa asilimia 48. Sasa hivi wana asilimia 52 tu. Kwa hiyo, jambo ambalo linanishangaza, nadhani linawashangaza Wabunge wote, kwamba tuna magraduate kibao wako mitaani, tunahamasishwa tufungue Vituo vya Afya na Hospitali, lakini Hospitali hizo na Vituo vya Afya vinafungwa kwa sababu hakuna watumishi. *What a contradiction? (Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa nadhani Serikali ituambie, tatizo ni kwamba hawana fedha za kuwalipa? Kwa sababu madaktari wapo, lakini hawaajiriwi, watu wanaendela kufa, akina mama wanajifungua wanakuifa, watoto wanakuifa na watu wazima wanakuifa. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani mtuondelee hiki kitendawili kwamba kama Serikali inakusanya kodi kama ambavyo mnatamba, kwa nini mkose fedha za kuwalipa wataalam ambao watakuja kusaidia maisha ya wananchi wetu kwa sababu naamini hakuna Taifa lolote linaloendelea kama wananchi wake wana afya mbovu. Kwa hiyo, niseme tu kwamba tuna kila sababu ya kuishawishi, kuiomba au kuishauri Serikali, ikahakikishe kwamba Watumishi wa Wizara ya Afya wanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la Mloganzila. Niseme tu kwamba ile hospitali ni ya kufundishia (*Training Hospital*). Tunaomba sana ibaki kwenye lengo lile lile, maana yake kulikuwa kuna maneno kwamba Hospitali ya Muhimbili ihamie kule na nini. Nadhani sisi kama Watanzania, ni lazima *tu-think globally but acting locally*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda vyuo vikuu vyote duniani vikubwa, vinakuwa na hospitali zake ambazo zina *specialty*. Hii yetu ya Mloganzila ina *specialty* yake ya moyo.

Hii ilikuwa ni kwa *East Africa* kwamba wagonjwa wa moyo wa kutoka Kenya, Rwanda na Uganda watibiwe hapa. Leo nasikia tayari kuna baadhi ya wagonjwa wa Mwaisela wameshahamishwa wamepelekwa kule, hali ambayo inafanya Madaktari wa Muhimbili watoke Muhimbili waende kutibu kule Mlonganzila, jambo ambalo haliwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani lengo lile la awali libaki pale pale ili ile Hospitali hii ya Chuo Kikuu cha Muhimbili ibaki na malengo yaliyokusudiwa. Maana yake tutaonekana watu wa ajabu kwamba Uganda wao wanaendelea, sisi Tanzania ibadilike iwe hospitali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Suzan Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kamati yangu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Mtolea na baadae Mheshimiwa Benardetha Mushashu ajiandae.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia katika Taarifa za Kamati hizi mbili, lakini nazipongeza sana Kamati hizi mbili, zimefanya kazi nzuri kwa kadri walivyoweza. Wamegusa maeneo mengi ambayo kimsingi yanaigusa jamii yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hali tu ya kuongezea, nami nina machache ya kuongezea ili tutakapoishauri Serikali, basi tuzidi kuboresha huduma za jamii kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hii ambayo kwenye Kamati ya UKIMWI umesema ni *gender based*

violence. Vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia vimekuwepo kwa muda mrefu. Mtakumbuka Bunge hili na Tanzania kwa ujumla ilionesa kukasirishwa sana na vitendo vile vya uuaji wa vikongwe, mnakumbuka Wanyamwezi walikuwa wanawaua vikongwe huko, sheria ikasimama kwamba watu hao waadhibiwe kiasi kwamba wengine hawatoiga. Pia matukio yale ya kuuawa kwa albino na kukatwa viungo, kama Taifa tuliungana pamoja kulaani vitendo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna jambo la ubakaji hasa kwa watoto wadogo. Matendo ambayo yametokea mwaka 2017 yametuvunja nguvu sana sisi wapigania haki za watoto na jinsia. Kwanza Serikali ilikataa watoto wa kike wanaopata ujauzito wasirudi mashulen. Kwetu lilikuwa pigo namba moja, lakini mwisho wa siku Serikali ikaamua hivyo. Kwetu imetunyong'onyeza sana kwa sababu tunaona watoto hawa ambao hawakupata hizo mimba kwa makusudi, zilikuwa bahati mbaya, wanakosa fursa ya kujiuliza tena na kurudi shuleni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi kwenye maadhimisho ya Uhuru wa Tanganyika, ukatoka msamaha kwa Babu Seya na wenzake, watu ambao pasipo na shaka mahakama zilithibitisha kwamba hawa watu ni wabakaji. Sasa tunapokuwa tunasamehe wabakaji, wapi ulinzi wa watoto katika Taifa hili? Tunawafundisha nini? Misingi yetu ya kukomesha vitendo hivi imepotelea wapi sasa? Tunakwenda mbali zaidi, tunawachukua, tunawapeleka lkulu, tunawapandisha kwenye majukwaa wafanye *show*, tunawaona kwamba ni kioo cha jamii, wanafundisha nini? Mnataka watoto wajifunze nini kutoka katika hilo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua mamlaka makubwa ambayo Mheshimiwa Rais anayo chini ya lbara ya 45 ya kuwafutia watu vifungo, lakini kufuta kifungo hakuondoi kuwa wewe ni mkosaji katika kosa fulani na mtatambua mwenye nguvu ya ku-*justify* kwamba huyu amekosa, huyu ana hatia ya jambo hili, ni mahakama peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Kisutu Jijini Dar es Salaam ilithibitisha hilo pasipo na shaka, lakini walikata Rufaa kwenda Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam na yenyewe pia ikajiridhisha kwamba hawa watu ni watuhumiwa katika kosa hilo. Wakaenda Mahakama ya Rufaa, Mahakama ya mwisho kabisa katika nchi hii; na yenyewe ikajiridhisha pasipo na shaka hawa ni wabakaji. Leo tunawachukua, tunatembea nao majukwaani. Je, mnataka siku ya mwisho tukiwaauliza watoto kwamba ukiwa mkubwa unataka kuwa nani, aseme nataka kuwa mbakaji? (*Makofî*)

T A A R I F A

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Mtolea subiri.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mwongeaji, anayeongea sasa hivi Mheshimiwa Abdallah Mtalea kuwa mwaka 2015 yeye alikuwa katika ile jumuiya waliyokuwa wanajiita UKAWA na mgombea wao wa Urais waliyekuwa wanampigania ndio alikuwa wa kwanza katika ilani yake, ahadi zake kubwa kuwa atamtoa huyu anayemwongelea sasa hivi. Sasa je, leo amemgeuka?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtalea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza siyo taarifa, lakini yawezekana humu ndani tukawa tunafana kiumri lakini tukatofautiana sana katika vichwa vyetu. Kwa hiyo, ni lazima haya pia tuyazingatie. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie tu mtoa taarifa, siyo nia yangu hata siku moja kuwa kituko ndani ya Bunge hili kama ambavyo wewe unataka niwe. Mimi nimeletwa hapa na wapigakura wa Jimbo la Temeke, moja kati ya Majimbo yaliyo mijini, moja kati ya majimbo ya watu waliokwenda shule, wanaojitambua na wanaojiheshimu.

Kwa hiyo, ninawakilisha *group* moja tofauti sana na *group* ambalo labda wewe unakuja kuliwakisha hapa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba ni lazima tuwe na jambo linalofanana, tuwe na nia moja. Tunapoamua kupabambana na mambo maovu, tupambane nayo kweli kweli. Mumshauri Mheshimiwa Rais afanye mambo ambayo wananchi ndio wanayataka. Mkipoteza naye anapotea, mnaipoteza Serikali, mnalipoteza Taifa na mnakipoteza chama chenu ambapo kimsingi kimeshapotea. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine...

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Mtulia subiri.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu nimpe taarifa Mheshimiwa anayezunguza kwamba siyo tu kwamba waliosamehewa walibaka, bali walilawiti na inasemekana kulingana na *rulling*, wale waliolawitiwa walipata na maambukizi ya UKIMWI. Kwa hiyo, apate tu hiyo taarifa kwamba ni kiasi gani Taifa limefedheheshwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hii. Naomba nisiendelee hapa, panaweza pakamliza mtu, ni kipande kizito sana hiki kukizungumzia hasa sisi ambao tunawajali watoto wa Taifa hili. Naomba niende kwenye mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezunguzwa pia suala la utoaji wa huduma hii ya *methadone* kwa wale warahibu

wa dawa za kulevya. Dawa hizi au huduma hii inatolewa kwa ufadhilli wa asilimia 100 na siyo kwamba huduma hii inatolewa kwa kiasi ambacho kinaridhasha, bado uhitaji wa huduma hii ni mkubwa kuliko ambavyo huduma yenyewe inatolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye vituo wanajaribu kuwachuja ili kupunguza wingi wa watu watakaowahudumia. Sasa hivi wanawapa dawa hizi wale tu ambao wanatumia madawa ya kulevya kwa njia ya kujidunga sindano. Zile njia nyingine, yaani kama mtu anatumia dawa za kulevya kwa njia nyingine kama zile za kunusa, kwa maana wanasema *sniff* au ile *cocktail* wao wanaambiwa ninyi bado hamjafia katika kiwango cha kupata huduma hiyo. Sasa kinachotokea ni nini? Kwa sababu vijana hao wana mwitikio mkubwa wa kujitoa katika matumizi ya dawa za kulevya, nao sasa wanaruka hizo hatua, wanatoka kwenye *cocktail*, wanatumia sindano ili wa-*qualify* kwenda kupata hiyo huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni hatari kwa sababu kwenye matumizi ya kutumia sindano ndiyo huko mnakutana na maambukizi ya magonjwa ya UKIMWI pamoja na magonjwa mengine. Sasa ni vizuri Serikali na yenyewe ikatia mkono ili kuifanya huduma hii ili ipatikane kwa kiwango cha kutosheleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikia Waziri Mkuu wakati anafungua Kituo cha *Methadone* pale Hospitali ya Rufaa Mbeya mwezi Juni, 2017 akizigiza hospitali zote za mkoa ziwe na Vituo vya *Methadone*; lakini kuviajiza peke yake bila Serikali kutenga fedha, hili agizo litatekelezwaje? Mwenyewe pale akasikia, wanasema kwamba Kituo cha *Methadone* cha Hospitali ya Rufaa ya Mbeya kitakuwa kinahudumia watu kutoka Njombe, Songwe, Iringa na Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mtu anatokaje Songwe, Njombe kwenda kula dawa Mbeya na kurudi kila siku? Kwa sababu hizi dawa hupewi ukale nyumbani, ni lazima ukazilie kituoni na za kila siku. Vituo vinapokuwa mbali, inakuwa ni

mzigo sana, hawa watu hawataweza kuzifuata. Ndiyo matokeo yake, wote hawa wanasaferi wanakuja kukaa Temeke sasa, tunaonekana Temeke ndio tuna warahibu wengi. Tusaidiane huu mzigo uweze kupungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni vitendo vya ushoga na usagaji. Hili tatizo linazidi kukua hapa nchini. Kwenye shule za msingi, sekondari za *dayna* za bweni vitendo hivi vinaendelea kinyemela. Watoto sijui wanajifunza wapi, sijui ni mitandao, lakini wanalaawitiana kiasi ambacho hawa wanakuja kujijenga kuja kuwa mashoga wa baadae. Vilevile kuna watu wanajitangaza kabisa mitandao na mitaani kwamba wao ni mashoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Serikali badala ya kwenda kupambana na watu ambaeo eti wanavaaa nguo fupi au *wana-post* picha za uchi mitandaoni, kwa nini tusipambane kwanza na mashoga na wasagaji? Tupambane na hawa ambao kwanza wanajitangaza kwa sababu ndio wanatengeneza, wanavutia watoto wengine wadogo waweze kujifunza hayo mambo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunawachukua watoto wa kike kwenda kuwapima mimba *randomly* kwa kuwashtukiza, tuanze na utaratibu wa kwenda kuwapima watoto wote kama wameshaingiliwa ili watutajie nani kawaingilia tuweze kuchukua hatua. Vinginevyo tatizo hili ninazidi kuwa kubwa nchini na itafika mahali tutaanza kukimbiana hapa. Hali ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni tatizo hili la kifua kikuu. Ugonjwa huu wa kifua kikuu sioni kama Serikali imeanza kuuchukua kwa nguvu inayostahili, lakini kuna tatizo kubwa la maambukizi ya ugonjwa huu wa kifua kikuu hasa sehemu hizi za mikusanyiko kwa maana ya huko migodini, sehemu za burudani, kwenye viwanja vya mipira ambako mikusanyiko ya watu inakuwa ni mikubwa. Ikiwa kuna watu wawili au watatu wana ugonjwa huu wa kifua kikuu ni rahisi kuusambaza kwa watu wengine. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali

ikawa na mpango mahususi katika maeneo yote ambayo yana mikusanyiko, tuone ni namna gani tunapambana na ugonjwa wa kifua kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni kule kuharibika haribika kwa *CT-Scan* katika Hospitali ya Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tatizo hili haliishi? Kila wakati lazima usikie *CT-Scan*imeharibika. Watu wanasaferi kutoka mikoa mbalimbali kupeleka mgonjwa Muhimbili, anafika pale mgonjwa ana hali mbaya, anaambia wiki hii yote *CT-Scan* imeharibika, kwa hiyo, usubiri. Watu wanapoteza maisha kila uchao. Kwa nini Serikali haiangalii jambo hili? Kama hiyo *CT-Scan* moja haitoshi, kwa nini tusiwe na nyine *standby*? Hebu tutambue kwamba hili tatizo ni kubwa sasa na ifike mahali tuone tuna mkakati mahususi kwa ajili ya kulingamiza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote hizi mbili. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mtulia. Tunaendelea na Mheshimiwa Benardetha Mushashu.

MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja hii. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii pamoja na Kamati nzima na Kamati ya UKIMWI kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuchambua taarifa za utekelezaji wa Wizara mbalimbali na kuweza kuyaleta mapendekezo mbalimbali. Nasema hongera sana, nami naunga mkono hoja mapendekezo yaliyoletwa mbele ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na afya, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa utendaji mzuri sana, wamefanya mambo makubwa sana kwenye upande wa afya. Wote tumeshuhudia *operations*kubwa sana zinazofanywa kwenye

Hospitali ya Mifupa ya *MOI*, wote tumeshuhudia *operation* za kileo zinazofanyika kwenye Hospitali ya Moyo ya Jakaya Kikwete, wote tumeshuhudia hata upandikizaji wa figo sasa hivi unaweza kufanyika Tanzania na watu wanatoka nchi za jirani kuja Tanzania kupatiwa huduma hizo. Kwa hiyo, nasema hongera sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na ugonjwa wa *cancer*. Ugonjwa wa *cancer* ni ugonjwa wa ambao umesambaa sana, sasa hivi watu wengi wanaugua ugonjwa wa huu. Kuna *cancerya* damu, ubongo, tezi dume, mlango wa kizazi, *cancermatiti*; kwa hiyo, *cancerziko* za aina nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mtu aweze kugundulika kabisa ana *cancer*, iwe *confirmed*, anapaswa afanyiwe vipimo vingi ikiwemo na *CT-Scan*. Unakuta gharama ya vipimo hivyo hasa kwenye Hospitali ya Bugando ambayo kwa Mkoa wa Kagera tunatumia hiyo, unakuta vipimo *vin-cost* kati ya shilingi 500,000 mpaka shilingi 600,000 kuweza kugundua kama huyu ana *cancer* kweli au hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda sasa kwenye matibabu labda amewekewa *chemo, dose* moja ni kati ya shilingi 600,000 mpaka shillingi 700,000. Je, hawa Watanzania tunaowajua na uwezo wao mdogo waliokuwa nao, ni wangapi wanaweza ku-*afford* kulipa hizo hela zote kusudi wagonjwa wao waweze kupata matibabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwa Serikali yangu siku na Mheshimiwa Waziri kwamba kwa ugonjwa huu wa *cancer* na kwa wingi na ukubwa wa tatizo lilivyojitokeza, Serikali ingeweka ruzuku kwenye dawa za ugonjwa wa *cancer* kusudi dawa hizi ziendelee kutolewa bure katika hospitali zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa Wizara imefanya kazi nzuri sana kwenye Hospitali za Rufaa kama Muhimbili na nyingine zote, nilikuwa naomba sasa *concentration* iende kwenye Hospitali za Mikoa, Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya pamoja na Zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia Mkoa wa Kagera; ukienda mkoa wa Kagera utakuta karibu Wilaya zote hazina Hospitali za Wilaya, sana sana tunadandia kwenye hospitali zile za *mission*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Wilaya ya Kyerwa. Wote tunajua kwamba Wilaya Kyerwa ni mpya, hawana kabisa Hospitali ya Wilaya, wanatumia pale Isingiro pamoja na Nkwenda ambapo sana sana zile ni sawasawa na zahanati. Nilikuwa naomba Serikali iwasaidie kwa kuwa ni Wilaya mpya hii, iweze kupata Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale Manispaa ya Bukoba, tangu mwaka 2013 wanajenga Hospitali ya Wilaya. Wameshindwa kwa sababu huu ni mradi mkubwa, kwa bajeti za Halmashauri hawawezi kuukamilisha. Nilikuwa naomba Serikali isaidie kukamilisha Hospitali ya Wilaya ya Manispaa ya Bukoba ikiwemo vilevile na Hospitali ya Wilaya ya Muleba. Hospitali ya Wilaya ya Muleba wananchi walijitahidi, wamejenga majengo mazuri, ila haijakamilika. Sasa hivi *MSD* wanapatumia pale, wakiondoka yataendelea kuwa magofu na zile juhudzi za wananchi zitaharibika bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itusaidie, kwa kuwa hii ni miradi mikubwa na najua siyo kwa Kagera peke yake, kuna maeneo mengine waendelee kutusaidia kuweza kukamilisha hii miradi kusudi huduma ziweze kutolewa kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua kwamba katika Mkoa wa Kagera tulipata tetemeko la ardhi. Tulipata athari nyangi, watu walifariki, taasisi mbalimbali ziliathiriwa na nyumba za watu zimeanguka na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia Kituo cha Afya ambacho kiko katika Wilaya ya Misenyi kinaitwa Kabyaile. Hiki kituo kimejengwa kwa nguvu ya Kamati ya Maafa ambayo ni michango ya wananchi na ya Serikali, ni kituo kizuri sana kimejengwa, hata Rais alishapelekwa kukikagua kile kituo. Pamoja na majengo mazuri, kuna

theatre lakini hakuna vifaa, kuna *mortuary* lakini hakuna mafriji na kuna *laundry* lakini hakuna vifaa vyta kusafishia. Naomba Serikali itusaidie kuweka hivyo vifaa kusudi Kituo cha Afya cha Kabyaile kilicho Ishozi, Misenyi kiweze kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Hospitali ya Mkoa wa Kagera ambayo inaitwa *Bukoba Government Regional Referral Hospital*. Hii ndiyo kimbilio la mkoa mzima. Wilaya zote tunategemea hii hospitali, lakini haina wataalamu, ina Madaktari Bingwa wanne tu amba ni wa meno, wa watoto pamoja na wa macho. Wanne kati ya Madaktari Bingwa kama 24 wanaotakiwa. Ukienda kwa wauguzi, hao ndio kabisa. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Serikali kwa hospitali hii ipatiwe wataalamu kusudi iweze kufanya kazi. Hatuna *surgeon*, hatuna daktari wa mifupa. Wote mnajua *accidents* za boda boda ni kila siku. Sasa bila kuwa na hawa Madaktari Bingwa inakuwa ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo hospitali, kuna wodi ya wazazi ambayo ni ndogo sana. Ina vitanda sita tu na hii ni *Referral Hospital* ya Mkoa, havitoshin na hakuna *theatre*. Mwanamke akitoka kule, ana uchungu, akaletwa pale kwenye *Regional Hospital*, akakuta ile *multipurpose theatre* ambayo na yenye ni ndogo, kuna mtu anafanyiwa *operation*, inabidi huyu mama amcheleweshe. Kwa hiyo, inabidi huyu mama afe kwa sababu amekuta ile *theatre* inatumika. Tulikuwa tunaomba basi, katika Hospitali ya Mkoa ijengwe *labour ward* kubwa ikiwa na *theatre* yake ili tuweze kupunguza vifo vyta mama na mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tukumbuke kwamba Mkoa wa Kagera hatuna mahali pa kukimbilia; ukienda huku ni Uganda, ukienda huku ni Rwanda; ukienda huku ni Burundi; sana sana umkimbize mgonjwa kumpeleka Bugando ambayo iko *something like* kilometra 500 kutoka Mkoa wa Kagera. Ukitaka kutembea kwa meli ni masaa kama manane mpaka 10 au ukizunguka lile ziwa. Tulikuwa tunaomba ile hospitali ipewe *ambulance*, kwanza na Mheshimiwa Waziri Mkuu alishakuja akaahidi pale kwamba

atatoa *ambulance*. Namuomba Mheshimiwa Waziri Ummy, hilo alichukue kwamba Hospitali ya *Government Regional Hospital* waweze kupata *ambulance* kwa sababu ni mbali sana na Bugando waweze kufanya hizo kazi zinazotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri mnayofanya. Nawapongeza kwa uamuzi wenu wa kuweza kukarabati zile shule kongwe. Wote hapa tumesoma zile shule za zamani, shule kongwe karibu 100. Pia naomba Mheshimiwa Waziri aikumbuke na shule yangu, mimi nilikuwa Mkuu wa Shule pale, lakini ni shule ambayo inasomesha wanafunzi wengi wasichana, Shule ya Rugambwa Sekondari na yenyeche imeanza tangu mwaka 1965 inahitaji ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumza juu ya matamko ya Waziri wa Elimu. Mheshimiwa Waziri hivi juzi ametamka kwamba watoto ambao watashindwa kufikia ile alama ya ushindi au *pass mark* wasikariri madarasa. Sasa hapa mimi nazungumza kama mwalimu. Huyu mwanafunzi asipokariri darasa au huyu mtoto aliyeshindwa kufikia alama ya ufaulu, kwa mfano akapata sifuri kati 100, akapata 10 kati 100, akapata 20 kati ya 100 tunamwambia apande tu darasa, tunakuwa tunamsaidia huyu mtoto au tunamlemaza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba watoto wengine hawataki kusoma. Tukumbuke kuna mahali ambapo walimu hawataki kufanya kazi. Sasa kwa nini huyu mtoto badala ya kumpitisha tu akafika *form four* akapata *division zero*, akikariri anakuwaje? Mbona hata humu ndani kuna wengi walikariri na wala hawakuathirika? Napendekeza kwamba watoto wawe wa *private* au wa *government*, yeyote ambaye atashindwa kufikia alama ya ufaulu akariri darasa tusije tena tukaanza kukimbizana kuangalia namna ya kufuta zero. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kuhusu shule za *private*. Kabla mzazi hajampeleka mtoto *private* anatafuta mwisho anapata shule moja, anaangalia ile shule ina vigezo

gani? Wanataka nini? *Discipline* ikoje? Ufaulu ukoje? Karo ikoje? Mzazi mwenyewe anachagua kwamba anataka kumpeleka kwenye shule fulani ambapo wengine wanatoza karo kubwa, lakini mzazi anaamua anamtafutia mtoto elimu bora, anampeleka kwenye ile shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Serikali kama inawezekana, hizi shule za *private* wangeziacha na alama zao za ufaulu kwa kuwa wazazi hawalazimishwi na wala wanafunzi hawalazimishwi kwenda kwenye hizo shule. Wazazi wanawapeleka kabisa kwa mapenzi yao, wawaache kusudi waweze kuwapeleka kwenye hizo shule na *pass mark* iendelee kuwa zile zile kama shule watakazokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu leo tunajivunia, naona Wizara tunatangaza kwamba baada ya mithani wa *form four*, kati ya shule kumi za kwanza au bora zilizofanya vizuri unakuta *most of them* ni za *private* ambaao walikuwa wameweka viwango vya ufaulu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba nishauri kama Mwalimu kwamba shule za *private* waziache ziweze kuweka ufaulu wao na hii itasaidia kuboresha elimu katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waitara, huyo mchangiaji ameshamaliza. Sasa taarifa itakuwaje?

MHE. PAULINE P. GEKUL: Alikuwa hajamaliza.

MWENYEKITI: Haya sema hiyo taarifa yako.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nilikuwa nampa taarifa mwalimu kwamba baada ya shule za *private* kufanya kazi nzuri sana hapa Tanzania, wanafunzi wengi walikuwa wanapelekwa Kenya

na Uganda, sasa hivi wanasomeshwa Tanzania hapa. Walipoanza kutengeneza kuweka viwango na kuto kariri madarasa, wanataka waanze kupeleka tena nje watoto wetu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Naona taarifa hiyo mwenyewe atakuwa ameisikia.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu kwa asubuhi hii umemalizika. Kabla sijamaliza, basi naomba niwataje wale ambao wataanza kuchangia jioni. Tutaanza na Mheshimiwa Devotha Ninja, tutaenda na Mheshimiwa Nuru Bafadhili baadaye Mheshimiwa Goodluck Mlinga na Mheshimiwa Gibson.

Baada ya kutangaza majina hayo ya wachangiaji wa jioni, tunasisitizwa hapa tuna sisitizo la tangazo tena, Waheshimiwa Wabunge Wakristo Wakatoliki, leo Jumatano tarehe 7 Februari, 2018 kutakuwa na Ibada ya Misa Takatifu itakayotanguliwa na Ibada Maalum ya Upatanisho katika kanisa lillopo ghorofa ya pili ukumbi wa Msekwa, mara baada ya kuahirishwa Bunge saa 7.00 mchana. Waheshimiwa Wabunge, wote Wakatoliki mnaombwa kushiriki.

Pia tunakumbwa semina ambayo tumetakiwa Wabunge wote saa 7.30 katika ukumbi wa Msekwa. Naomba kurudia tangazo hilo ili Waheshimiwa Wabunge wote tuweze kushiriki Semina hiyo.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.00 mchana Bunge lilitishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Bunge lilitrudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile wachangiaji ni wengi na mwisho tutakuwa na hoja binafsi, kwa hiyo, kila mchangiaji atatumia dakika saba na nusu ili wengine waweze kupata, tumalize.

Kwa hiyo, tutaanza na Mheshimiwa Devotha Minja, atagawana dakika na Mheshimiwa Upendo Peneza na baadae Mheshimiwa Nuru Bafadhili ataendelea.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. Kutokana na muda mfupi, naomba nianze kwa kupongeza taarifa za Kamati zote mbili, tumefatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwapongeze waandishi wa habari kwa kazi ambazo wanaendelea kuzifanya. Waandishi wa habari kwa sasa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, hilo lazima tuseme. Wanafanya kazi katika mazingira ya kutishwa, vitisho vikali, lakini sisi tunaendelea kuwaeleza waendelee kupambana kwa ajili ya Taifa hili. Zipo nchi nyingi zimepata uhuru kutokana na waandishi wa habari kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunawapa moyo na tunawaambia, ukweli utaendelea kuliweka huru Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia sana taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Maendeleo ya Jamii. Waandishi wakiwa katika kundi hili, kuna mambo ambayo nimeona hata Kamati haikuwatendea haki. Katika taarifa nilitegemea kuona taarifa ya hali halisi za waandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza leo Mwandishi Azory Gwanda wa Mwananchi, ana siku ya 79 hajaonekana, hajulikani alipo. Gazeti la Mwananchi limekuwa likiandika kila siku mtu huyu yuko wapi na hatuoni juhudzi zozote. Tulitegemea Kamati ingeelezea kuhusu wadau hawa muhimu kwenye tasnia hii, waandishi hawa ambao

wamepotea, ambao wametekwa, taarifa zao ikiwemo ile ya kina Roma Mkatoliki ambapo Mheshimiwa Waziri alituahidi hapa kwamba ataleta taarifa kamili kwamba tukio lile lilitokeaje? Tulyegemea kuyaona hayo ndani ya Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, naomba nizungumzie suala la *press card*. Nimesoma taarifa hii inaeleza kwamba waandishi 54 ndio wamepata *press card* na kati ya hao 14 ni waandishi wa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini waandishi? Sheria inawatambua waandishi, inatambua taaluma ya uandishi wa habari, wanashindwa kupata *press card*. *Press card* ni shilingi 50,000. Mwandishi wa habari shilingi 50,000 kwa mwaka; *driving licence* ni shilingi 40,000 kwa miaka mitatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali isione umuhimu wa kuhakikisha waandishi wa habari wanapata *press card* wa bei nafuu? *Passport* hizi ambazo tunatumia, ambazo zinakwenda kwisha muda wake, ni shilingi 50,000 ndani ya miaka 10, lakini mwandishi wa habari anakuwa na *press card* ambayo atalipa 50,000 ndani ya mwaka mmoja. Huu ni uonevu na tunasema, labda watuambie kama *TRA* imeahinisha *press card* ni moja ya vyanzo vya mapato, ndiyo tunaweza tukawaelewa. Vinginevyo kwa kuwa taaluma hii imeshafahamika, wapewe nafuu ili waweze kutambulika na wawe na vitambulisho vya kuelewka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu Habari Maelezo. Habari Maelezo imegeuka kuwa wahariri, wametoka kwenye majukumu yao ambayo yameelekezwa na sheria tuliyopitisha, hivi sasa ndio wanaofanya *editing* kwenye vyombo vya habari. Hivi karibuni Habari Maelezo imeiandikia Gazeti la Tanzania Daima barua lijieleze ni kwa nini lina-*cover story* za Kinondoni za upande wa upinzani peke yake? Hiyo siyo kazi ya msingi ya Habari Maelezo. Kwa nini Habari Maelezo isiiandikie Gazeti la Uhuru kwa nini linaandika habari za CCM? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, magazeti binafsi yanaangalia *story* zinazouza, yanaangalia yaandike nini ambacho kitauzwa ili wafanye biashara. Kuwalazimisha kwamba waweke *front page* habari za CCM na wasipouza, mbona gazeti la Uhuru haliuzi? Lina nakala ngapi hivi sasa na linatembea wapi? Kwa hiyo, watu wanaangalia, watu wanataka nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Habari Maelezo kwenda kusimamia kuhakikisha Tanzania Daima inaandika habari za uchaguzi siyo; kwa sababu kwa mujibu sheria, wakati wa uchaguzi vyombo vy ya habari vinakua chini ya Tume. Ilikuwa ni jukumu la Tume kusema kwa nini chama hiki kinakosa fursa kwenye gazeti? Siyo kazi ya Habari Maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Habari Maelezo wafanye kazi zao na siyo kuhakikisha wanafuatilia magazeti mengine kwa maana kwamba inatupelekea kuona kama kuna maelekezo fulani ambayo hatuyaelewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuyafungia magazeti. Magazeti yameendelea kufungiwa kila kukicha. Naomba kufahamu na Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha atueleze; anatoa wapi mamlaka hii ya kufungia magazeti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Vyombo vy ya Habari tulioipitisha hivi karibuni, haijampa mamlaka Waziri kufuta magazeti. Haijampa mamlaka hayo na atueleze ni kwa kutumia Kanuni zipo na Kipengele kipi? Kwa sababu tulisema mwamuzi wa mwisho atakuwa ni mahakama. Mahakama itakuwa na *room* ya kusikiliza upande huu na upande huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hapo sheria baada ya kusainiwa, kanuni zipo tayari, walitakiwa kuandaa yale mabaraza matatu ambayo kazi yake ilikuwa ni kushughulika endapo kuna mwandishi amepotosha, kuna mtu ambaye

amekwenda kinyume na maadili. Kwa nini Serikali inaona kigugumizi kuunda mabaraza haya ikiwemo Baraza la Ithibati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema unaadhibu gazeti kwa kulifungia, ni sawa na kusema kwamba eti unaifungia hospitali kutokana na daktari mmoja kuua mgonjwa. Huwezi kuifungia hospitali kwa sababu ya daktari mmoja; badala yake *uta-deal* na yule daktari. Ndivyo ilivyo kwa waandishi wa habari. Kama utalifungia gazeti, wapo wafagizi, wapo maafisa masoko, wapo watu ambao wao ni makarani na wahasibu; *chainzaidi* ya watu 300. Mtu mmoja kweli akoseshe watu 300 ajira? Haiingii akilini. (*Makof!*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Devotha muda wako umemalizika.

Tunaendelea na Mheshimiwa Upendo Peneza na baadae Mheshimiwa Nuru Bafadhili na Mheshimiwa Rehema Migilla wajiandae kwa dakika saba saba. (*Makof!*)

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote napenda kwanza kuipongeza Kamati hii ya Huduma na Maendeleo yaa Jamii kwa kuweka pendekezo la Serikali kutoa taulo za kujihifadhi watoto wa kike wakati wa hedhi na Serikali kutoa *pads* hizo bure mashuleni. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu wanafahamu na jamii pia inafahamu, kwamba niliandika hoja binafsi na kuiwakilisha ndani ya Bunge, kwa maana ya kwa Katibu wa Bunge ambayo kwa bahati mbaya haijapata nafasi kwa sababu Ofisi ya Katibu imenijibu kwamba hoja ya kugawa *pads* bure mashuleni inavunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 99(2) ya Ibara hiyo ya Katiba. Hayo ni majibu kutoka Ofisi ya Katibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, bado naipongeza Kamati kwamba wametoa mapendekezo ambayo mimi nimeambiwa navunja Katiba, kwamba sasa Serikali igharamie *pads* bure mashulen. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa hoja yangu ni moja, tuna watoto wa kike wengi mashulen ambao wanashindwa kukaa vizuri darasani, wanashindwa kuwa na ujasiri wa kujifunza kwa sababu wana hatari ya kujichafua wakiwa katika kipindi cha hedhi.

Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu, amewahi kuliambia Bunge hili kwamba watoto wetu wanatumia vitambaa, wanatumia majani, wanatumia mchanga mpaka wanatumia mavi ya ng'ombe. Hiyo ilikuwa ni kauli ambayo kipindi anatoa kauli hiyo, alikuwa akijibu swali la Mheshimiwa ambaye sasa ni Naibu Waziri wa kupitia Watu wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shida hiyo inayowakuta watoto wetu, bado kuna haja kubwa ya Serikali kuona umuhimu ya kuwapa watoto wetu *pads* bure mashulen. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ningependa kusema kwamba katika takwimu za Serikali, zilizotolewa na TAMISEMI kwamba wasichana wengi ndio wanaacha shule kuliko..

T A A R I F A

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Taarifa.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji anayechangia hivi sasa hivi. Nina imani kubwa kwamba sisi kama Wabunge wa Viti Maalum na Wabunge wa Majimbo ambao ni wanawake,

hili jambo tangu tumeapishwa tumelipa kipaumbele, tumeshalijadili sisi kama Wabunge Wanawake wa vyama vyote na tayari lilikuwa limeanza mchakato ambao ungeenda kumaliza hata hiyo Katiba Kifungu alichopewa tulikuwa tumeshayaona; hili jambo tuliliongelea na tayari *TWGP* iliunda Tume kwa ajili ya kufuatilia namna bora ya kuweza kuwahifadhi watoto wetu wakiwa mashulen. Kwa hiyo, nasema tu asipende kuharakia mambo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Upendo.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukaelewa mambo tunayoyajadili, tuache umbea kwenye mambo ya maana yanayogusa maisha ya watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya watoto wanaoacha shule katika kitando cha kwanza, kati ya wanafunzi 9,881 walioacha shule wasichana ni 9,337; kitando cha pili, ni 13,559 wasichana walioacha shule ni 12,617.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi kuanzia *form one* mpaka *form four* ni udhibitisho tosha kwamba watoto wetu wanaacha shule kwa sababu ya kukosa vifaa muhimu kama vifaa vya hedhi. Serikali kuititia takwimu za TAMISEMI, imesema wazi kwamba sababu kubwa inayowafanya watoto wa kike kuacha shule ni utoro. Utoro wakiwa kwenye hedhi, siku tano za hedhi wanashindwa kuhudhuria darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ifike wakati sasa Bunge ione umuhimu wa kuweza kuwapatia watoto wetu *pads* bire.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya mahesabu, kwa bei ya chini kabisa, kama Serikali ingeweza kununua *padya* kila mtoto kwa shilingi 2,500, kwa watoto wa shule wote ambao ni 1,870,889, wanafunzi wa shule ya msingi kuanzia nusu ya darasa la tano, darasa la sita na darasa la saba, Serikali ingegharimia shilingi 46,762,000,000 ndizo ambao Serikali ingegharimia kuwanunulia watoto wetu *pads*. Kwa

sababu ni Serikali, ingeweza kupata *pads* kwa bei chini kidogo, kwa hiyo, kama Serikali ingenunua *pad* kwa shilingi 1,500, basi Serikali ingetumia shilingi bilioni 28 tu kuwanunulia watoto wetu *pads* bure mashulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ikichagua kwamba tutumie *re-usable pads* suala ambalo mimi mwenyewe siliungi mkono sana kwa sababu vijiji ni asilimia 39 tu ya maji ndiyo yanayopatikana vijijini...

TAARIFA

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ingetumia shilingi 14,963,000,000 kugharimia watoto kama wangeweza kutumia *re-usable pads*.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kama mzazi mwanamme. Ninataka nimpe taarifa mzungumzaji, kwanza mimi kama baba niliye na watoto wa kike na kama Mbunge ambaye nina watoto wanafunzi kutoka *primary school* mpaka *secondary school*, naunga mkono hoja yake. Hiyo hoja asifikirie kwamba ni hoja ya Wabunge Wanawake wa Viti Maalum au wa Majimbo peke yake. Hii hoja ni hoja ya wazazi wote na Watanzania wote. (*Makofii*)

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, Bunge litakumbuka kwamba nilivyokuwa Mbunge mgeni kabisa kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017 ndiyo hoja iliylifanya Bunge hili lote mkapiga makofi kwa kuunga mkono hoja hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Maria Kangoye ni Mbunge ambaye amewahi kuchangia hoja hii ya watoto kupata *sanitary*bure mashulen. Mbunge ambaye sasa ni Naibu Waziri wa Walemau, ni binti ambaye amewahi kuiliza swali ndani ya Bunge hili na ndipo akapata majibu ya kuhusu *sanitary pads*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge tulilomaliza Novemba, niliuliza swali na Mheshimiwa Jafo akanijibu kwamba Serikali inajaribu kuweka mikakati ya namna ya kulifanya ili suala...

MWENYEKITI: Subiri.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo,...

MWENYEKITI: Subiri kidogo Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri.

T A R I F A

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji, kwamba tunakubali lipo tatizo la zana za kujisitiri kwa watoto wa kike, lakini sikusema kwamba wanatumia mavi ya ng'ombe na mchanga. Ni kweli watumia matambara na baadhi ya majani. Kwa hiyo, hiyo taarifa ya mchanga na mavi ya ng'ombe siyo sahihi. Naomba *Hansard* ifute.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *Hansard* ipo, unaweza ukani patia muda nikatafuta majibu ya Mheshimiwa Waziri nikakuletea hapa mbele. Nitakushukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukiangalia katika takwimu leo na ninatambua michango ya mpaka Waheshimiwa Wabunge wanaume ambao wameweza kuzungumzia hii *pads*, hata Wabunge wanaume ambao

wameunga kampeni ambazo tumezifanya mtaani. Ni ukweli kwamba kadri ya mtoto wa kike anavyopanda kimasomo, akitoka darasa la kwanza kwenda darasa la pili, kwenda darasa la tatu, kwenda darasa la nne, kwenda darasa la tano, ndivyo anavyoongeza uwezekano wa yeye kujipatia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika takwimu zilizopo, ni kwamba kadiri mtoto anavyosoma, anavyofika Sekondari na kwenda mbele, anaongeza asilimia 15 mpaka 25 ya uwezo wa yeye kuweza kujiingezea kipato. Kwa hiyo, ninaomba watoto wa kike, Serikali tuache kuangalia Upendo unatoka kwa nani, tuangalie suala la msingi linalogusa watoto wetu wa Kitanzania. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nuru Bafadhili na baadae Mheshimiwa Rehema Migilla ajiandae, dakika saba, saba.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuwa hapa kwa muda huu na kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Vilevile napenda kukishukuru chama changu, Chama cha Wananchi (*CUF*) kinachoongozwa na Profesa Ibrahim Haruna Lipumba kwa kuweza kunateua kuweza kuwakilisha wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mweyekiti, nitajikita kwanza kwenye masuala ya elimu. Kwa kweli elimu yetu ni nzuri, lakini kuna matatizo katika elimu. Matatizo yaliyopo ni kwamba mtoto mwenye njaa hafundishiki. Watoto wetu hawafanyi vizuri katika masomo kwa sababu ya njaa kutokana na hali duni ya uchumi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, ihakikishe inafanya utaratibu angalau wanafunzi wetu wa shule zetu waweze kupata angalau mlo mmoja kwa siku ili waweze kuhudhuria vizuri masomo. Kuna baadhi ya wanafunzi wanashindwa kwenda shulenii, wanakuwa watoro kutokana na ukosefu wa vyakula majumbani kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Serikali italitilia mkazo hilo, itawezekana na wanafunzi wetu wakaweza kufanya vizuri katika masomo yao. Kwani sisi tuliposoma pia, tulikuwa tunakwenda shule lakini tunapata milo miili. Saa 4.00 tunapata uji wa bulga na mchana tunapata chakula ambacho kilikuwa ni mlo uliokamilika. Basi hata kama Serikali itakuwa haina uwezo wa kufanya milo miili, basi angalau huo mlo mmoja ili mwanafunzi aweze kukaa darasani na kumsikila Mwalimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kuhusu suala zima la afya. Kwa kweli katika Wizara hii ya Afya kuna matatizo mengi sana. Kwa mfano katika hospitali yangu ya Rufaa ya Tanga, kuna matatizo ya Daktari Bingwa wa Wanawake, yaani Daktari Bingwa wa Akinamama, Daktari Bingwa wa Koo na Masikio. Kwa hiyo, wenye matatizo hayo ya koo, sikio wanashindwa kupata huduma nzuri kutokana na ukosefu wa daktari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna tatizo la watumishi katika kada zote. Kwa hiyo, Wizara iangalie katika mgawanyo huo wa Watumishi wa kada zote na Hospitali yetu ya Rufaa ya Tanga iangaliwe ili waweze kupata huduma nzuri na zilizo bora zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia vilevile kuhusu UKIMWI. Hili ni janga la kitaifa kwa kweli na vijana wetu ndio wanaoathirika zaidi na UKIMWI. Vijana wa umri kuanzia miaka 15 mpaka 24 ndio wanaoathirika zaidi na UKIMWI. Kuna vishawishi vingi kwa vijana hawa na wakati mwingine kuna wazee wengine wanawafuata wasichana wadogo wadogo eti wanadai kuwa wake zao majumbani wamechuja. Kwa hiyo, wanawafuata watoto wadogo na wengine tayari wanaume wale wazee au vijana wakubwa wameathirika, kwa hiyo, wanawaambukiza watoto wetu au vijana wetu wadogo maradhi ambayo hayana tiba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mila potofu ambazo zinachangia pia kuambukiza au kuenea gonjwa hili la

UKIMWI, mfano kuna mila nyingine mwanamke anapokuwa na mimba, mchumba anachumbiwa akiwa ndani ya tumbo, hajjulikani kama kutazaliwa mwanamke au mwanaume. Kwa hiyo, atakapozaliwa mwanaume siyo wake, lakini akizaliwa mwanamke ndio atakuwa ni wa kwake. Kwa hiyo, pia hizi ndoa za utotonii zinachangia katika kueneza gonywa hili la UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna mila za kurithi wajane. Utakuta mke akifiwa na mume wake anarithiwa au wakati mwingine na vile vile mume anarithiwa na mke mwingine. Kwa hiyo, hii inaleta matatizo kwa sababu hajjulikani mmojawapo kati ya hao waliokufa amekufa kwa ugonjwa gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunalomba Serikali hili lipigiwe kelele zaidi, lakini vilevile sisi kama wazazi, tuwafundishe watoto wetu maadili mazuri. Kwa kweli kuna wazazi ambao wanajifanya wao kila wakati wako *busy*, wako kazini tu, hawawaangallii watoto wao nyumbani. Kwa hiyo, maadili yanaporomoka na baada ya maadili kuporomoka, utakuta watoto wanaharibikiwa. (*Makofii*)

Kwa hiyo, sisi kama wazazi, tuhakikishe tunafuatilia nyendo zote za watoto wetu kwa sababu sisi kama Wabunge nadhani wazazi wetu walitufuatilia tukaenda shuleni tukasoma mpaka leo tumefikia kupata nafasi hii ya kuwawakilisha wananchi wetu. Kwa hiyo, sisi kama wazazi aidha wanaume au wanawake, tuhakikishe tunakwenda vizuri katika kutengeneza maadili katika nyumba zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo hilo kuhusu UKIMWI. Kuna mila nyingine wanatumia vifaa ambavyo havichemshwi. Kwa mfano, watu wanapotahiriwa, wanapokeketwa, wanaotogwa masikio sijui na pua na nini, unaona vitu vile havichemshwi wala haviko katika usalama, kwa hiyo, hivi pia vilevile vinachangia katika kueneza gonywa hili la UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaiomba Serikali ihakikishe inaongeza bajeti kwa ajili ya kununua dawa za waathirika wa ugonjwa wa UKIMWI...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzunguzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Rehema Migilla baadae Mheshimiwa Goodluck Mlinga na Mheshimiwa Jitu Soni ajiandae.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishukuru Kamati yangu ya Guantanamo ambayo imeshiriki kwa namna moja katika kuleta taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mwanakamati nitajikita zaidi katika suala la elimu. Ni wazi kuwa Serikali yetu ipo katika hatua za kuelekea katika Tanzania ya viwanda, lakini hatuwezi kufikia Tanzania ya viwanda bila kuwa na wataalam ambao wataenda kuvihudumia hivi viwanda. Wataalam hao ni wanafunzi na hawa wanafunzi hawawezi kupata yale yanayohitajiwa kama hawatakuwa na walimu wazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi walimu wamekuwa na changamoto nyingi sana zinazosababisha mpaka *morale* ya kufanya kazi ipotee. Sababu mojawapo kwanza ni kudhalilishwa kwa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi walimu wanadhalilishwa sana kana kwamba hawana taaluma, leo

hii na siku za nyuma baadhi ya ma-DC, ma-RC hata Wakurugenzi wamekuwa ni watu wa kuwadhalilisha walimu, wanawatandika fimbo, kuna walimu wameshadekishwa vyumba nya madarasa, kwa kweli hali hii inasababisha mpaka *morale* ya kazi ipungue. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine la kushusha vyeo walimu. Hili suala limekuwa sasa hivi ni *too much*. Mwalimu mwenye *professional* yake, leo kwa sababu ambazo ziko nje ya uwezo wake, anashushwa cheo na Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, eti tu kwa sababu shule imefelisha, je, anayefanya mtihani ni Mwalimu au mwanafunzi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya Serikali, kazi au majukumu ya kushusha vyeo au kutoa nidhamu na maadili kwa walimu yako chini ya Tume ya Utumishi wa Walimu, sasa nataka nijue, hili jukumu la kushusha vyeo walimu linachukuliwa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, je, mmeinyang'anya madaraka Tume ya Utumishi wa Walimu na kuwapa hawa viongozi wa Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine linalochangia hadi kuzorota kwa elimu yetu ni kuchanganywa kwa kauli mbalimbali zinazotolewa na viongozi wetu wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa juzi kulikuwa kuna kauli mbalimbali zinazotolewa na viongozi wa Serikali, mfano Mheshimiwa Rais alisema kwamba walimu wasihamishwe kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine mpaka pale atakapopewa mafao yake ya uhamisho. Ghafla kuna kauli imetolewa tena na Wizara ikisema kwamba kuna Walimu wanahamishwa kutoka sekondari kwenda *primary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa umma, hata kama ukimhamisha kutoka kituo 'A' kwenda 'B'....

T A A R I F A

MHE. ALLY K. MOHAMED: Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Keissy.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Hivi kwenye Bunge kuna Kamati inaitwa Guantanamo? Anasema mzungumzaji yuko kwenye Kamati ya Guantanamo, hivi kuna kamati ya Guantanamo hapa kwenye Bunge lako Tukufu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rehema.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ni Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ila hiyo ni *a.k.a. (alias known as). (Kicheko/Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine linalochanganya pia ni huku huku kuendelea kupotoshwa au kauli tatanishi. Leo hii Serikali ilisema kwamba hakuna kurudisha watoto shule za msingi mpaka sekondari, lakini leo hii hii Serikali inasema hakuna kukaririsha. Hivi tuelewe lipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tukirudi tena kwenye suala lingine la hizi hizi kauli, Waraka wa Elimu Namba Tatwa mwaka 2006 umetamka wazi majukumu ya kila mdau wa elimu kuanzia wazazi, Wakuu wa Mikoa hadi na walimu, lakini leo hii Mheshimiwa Rais anasema mzazi asihusishwe kwa mchangano wa aina yoyote. Sasa je, hii mchangano ambayo inapaswa itolewe na wazazi au Serikali inaposema elimu bure, hii ni elimu bure au elimu bila ada? Tunaomba majibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia *point* nyingine kwamba sababu nyingine zinazochangia kuwepo kwa uدوروري wa elimu ni kutolipwa kwa madai ya walimu

kutokana na vigezo mbalimbali mara uhakiki wa watumishi hewa, mara uhakiki wa wenye vyeti *fake*, sasa tunataka tujue huu uhakiki wa wenye vyeti *fake* na watumishi hewa utaisha lini ili hawa walimu waweze kulipwa madeni yao mbalimbali kama madeni ya uhamisho, madeni ya kupanda madaraja nauli na vitu mbalimbali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niendelee kuhusu uendeshaji wa shule za *private*. Shule hizi hazipo kwa kuwa tu eti zimejiamulia zenywewe. Shule hizi za *private* zimeanzishwa kwa kufuata kanuni na taratibu mbalimbali mojawapo ikiwa ni kupata usajili toka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Serikali imeanza kuziingilia hizi shule. Shule hizi zimewekeza, zinalipa ada na mzazi mwenyewe ameguswa, hakuangalia gharama, hakuangalia masharti mbalimbali akaamua kupeleka mtoto kwa matakwa yake ye ye mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii shule za *private* wanaambiwa wasikaririshe watoto. Wakati mwanzo walipewa masharti na wakakubali na Serikali ikawapa usajili, lakini leo hii haieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nijue, hii Serikali ina mpango wa kururudisha kule kwenye idadi ya kuongeza *division four* na tukose *division one* au *two*...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Rehema Migilla.

Tunaendelea na Mheshimiwa Goodluck Mlinga na baadae Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Felister Bura wajiandae dakika saba, saba.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze moja kwa moja kwenye mjadala, japokuwa wameni-*pre-empt* kwa kiasi kikubwa, nitaomba niyarudie yale lakini ni kwa msisitizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la kwanza ni ushukaji wa elimu kwa shule za Serikali za Tanzania. Kwa muda wa miaka miwili sasa Waziri wa Elimu amedumu katika Wizara hii lakini tumeshuhudia kwa uangukaji mkubwa wa shule za sekondari za Serikali. Mpaka sasa hivi anaweza akajipima ye ye mwenyewe ni kwa kiasi gani ni mzuri na kwa kiasi gani ni mbaya. Kwa hili naingiwa hofu, sielewi, sijui Maprofesa wa Tanzania wana tatizo gani? Ingekuwa ushauri wangu kwa Mheshimiwa Rais, angechaguliwa mtu kama Musukuma au Mheshimiwa Lusinde ambao wameishia darasa la saba kuwa Mawaziri wa Elimu kwa sababu wanajua matatizo gani yaliwafanya wasiweze kusoma. Maprofesa wa Tanzania wamekuwa wakiongoza kutoa miongozo, matokea yake elimu zinafeli. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu matokeo ya kidato cha nne shule za Sekondari katika kumi bora hamna na ndiyo tulizoeaga Mzumbe, sijui Kilakala sijui wapi, hazipo. Katika shule 100 bora za sekondari, shule za Serikali ziko nne. Jamani, hii si aibu!

Mheshimiwa Waziri wa Elimu una kitu gani cha kutuambia hapa? Hii ume-*prove failure*, haiwezekani. Halafu sasa ukija unawapiga vita watu wenyе shule za sekondari za *private*. Sasa kwa mfano hizi shule za sekondari za *private* tungeziondoa katika orodha ya zile shule 100, wewe si ungekuwa Waziri wa masifuri! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, angekuwa Waziri wa masifuri maana yake shule za Serikali zote zimefeli, shule za *private* ndiyo zinaongoza. Sasa ana nini cha kujivunia? Ukimwuliza tangu aingie madarakani ye ye vita yake na shule za sekondari za *private*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri wa Elimu amekuja na nyingine, bado anawakomalia, hakuna

kukaririshwa madarasa. Sasa unasema watu wasikaririshwe madarasa lakini unaruhusu watu *form four wa-re-sit*, ungeondo sasa, hamna watu kurudia mitihani ya kidato cha nne. Hapo tungekuelewa! Unasema wanafunzi wasikaririshwe madarasa, unataka wawahi wapi? Wanakuhusu nini? Tunasema elimu haina mwisho. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikupe kwa nini wanafunzi wa shule za sekondari za Serikali wanafeli? Mazingira mabovu ya walimu. Leo hii walimu wanadai malipo yao ya muda mrefu, mnasema mnahakiki, mnataka watoe risiti. Mbona sisi Wabunge tukileta madai yetu hamtuambii tulete risiti? Mnawaambia walimu walete risiti, mnawacheleweshea malipo. Walimu mnawapangia maeneo ya vijijini, hajui akaishi vipi, nyumba hakuna, ukienda walimu wanaishi kama makondoo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu hawana *break*. Wote mtakuwa mashahidi, ukienda kwenye shule mwalimu anaingia saa moja asubuhi mpaka saa kumi na moja jioni kama mfungwa. Wanafunzi wanaenda *break* saa nne, walimu hawana. Ule muda wa *break* ndio anatumia kusahihisha madaftari ya wanafunzi. Hamwangalii hilli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhalilishaji, leo hii mwalimu hana bosi. Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi, Afisa Utumishi, Waziri, wote mabosi zake. Huyo mfanyakazi wa namna gani? Hata sisi tungeweza? Sisi tungeweza kila mtu awe bosi wetu? Spika awe bosi wetu, Rais awe bosi wetu, sijui nani awe bosi wetu? Kwa hiyo, mnawachosha walimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine mwalimu akitaka kuhama ni msala (kazi), anaambiwa atafute mtu wa kubadilishana naye. Hebu niambie mimi nataka kwenda Dar es Salaam, naambiwa nitafute mtu wa kubadilishana Dar es Salaam. Hiyo kazi mimi nitaweza? Hiyo ni kazi ya mwajiri au mwalimu mwenyewe? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuchangishwa michango isiyo ya muhimu. Eti leo hii walimu wanaandikiwa barua na Mkuu wa Wilaya watoe michango ya Mwenge. Jamani! Mshahara wenyewe anaoupata mdogo, halafu mnawambia atoe mchango wa Mwenge, huu ni uonevu wa hali ya juu. Mbona Wabunge hatuambiwi tuchangie Mwenge? (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, hakuna malipo ya *overtime*. Mimi nimetoka kwenye semina; kila semina tunayoingia tunaulizia kwanza malipo, lakini walimu wanafanya kazi mpaka *weekend*, lakini hawapati malipo yoyote, jamani huu ni uonevu. Halafu elimu inashuka, Mheshimiwa Waziri anakazana na shule za *private* badala akazane na shule zake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihamie upande wa *NHIF*. Kamati imezungumzia suala la huduma za Bima za Afya kwa watu wote. Mheshimiwa Waziri wa Afya ukija naomba uniambie, *NHIF* haiwezi ikatoa huduma kwa watu wote, kama mashirika ya umma yenyewe ambayo yanatakiwa kisheria yajunge kule hayajajiunga, tunawang'ang'anaje watu wa mtaani ambao kwenye sheria haiwahusu? Tuanze kwanza na hilo. Kwa hiyo, akija Mheshimiwa Waziri wa Afya naomba aniambie, mpaka leo hii mashirika mangapi ya Serikali ambayo yameingia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina taarifa za kiintelijensia kuwa *BoT* baada ya mimi kuongea Bungeni kuwa mashirika yote yanatakiwa yahamie *NHIF* wamesaini mkataba wa siri na *Jubilee Insurance* wa miezi mitatu, ili tukiliamsa huku Bungeni waseme mkataba unaisha keshokutwa. Kwa hiyo, sasa hivi wanasaini mikataba ya miezi mitatu mitatu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri akija naomba aniambie. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala ambalo alizungumzia Mbunge mwenzangu kuhusu vitendo vya ushoga. Jamani vitendo vya ushoga vimeshamiri katika nchi yetu. Sasa basi ubaya unaokuja, watoto wadogo wa kiume wanavyokua wanajua ushoga ni *fashion* na hii inayoharibu

yote ni mitandao ya kijamii. Wanajitangaza sasa hivi kwenye mitandao ya kijamii, Mawaziri mnawaangalia. Sasa sijui mnataka wafanyakaje? Mbona wengine wanaotukana wanawakamata, lakini wanaojinadi katika mitandao ya kijamii mnawaachia? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Afya ukija naomba mtujibu, mmechukua hatua gani kuhakikisha ushoga hauendelei katika nchi yetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine nilikuwa sijalimalizia, Mheshimiwa Waziri hajatuambia, vile vitabu vibovu tulivyovizungumza vilivyokuwa vimeandikwa mbele nyuma na nyuma mbele, vimeishia wapi? Hatujapewa majibu na Serikali hii kuwa wale watu wamechukuliwa hatua gani? Vile vitabu vimetengenezwa vingine au vinaendelea kutumika vilevile? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba niishie hapo kwa leo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Mlinga. Tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Soni halafu Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi ajiandae dakika saba, saba.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza napongeza Kamati zote mbili kwa kazi nzuri na taarifa nzuri walijotuletea. Nawaunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kurudia kwamba Bunge lingeangalia mfumo wa namna ya kuboresha ili hizi Kamati tuweze kufanya kazi kwa pamoja, Kamati mbalimbali na Waheshimiwa Wabunge hawako kwenye Kamati hiyo wakitaka kuchangia pawe na namna ya kuweza kuchangia kwa sababu kwa hii siku moja Waheshimiwa Wabunge wachache, haya mawazo yetu bado hayatoshi kuboresha hizo taarifa za hizo Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la afya, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa na nzuri ambayo

inaendelea kufanywa hasa hii ya kujenga vituo vya Afya. Ombi langu ni kwamba kama kuna maeneo kwenye Kata, Wilaya au Vijiji wana ramani tofauti ambazo zinakidhi vigezo vyote na ubora wa majengo, basi hizo ramani waruhusiwe kama gharama za ujenzi zitapungua, tusiwe na mfumo ambao lazima zote zifanane nchi nzima. Watu wanaweza kuwa na *design* nzuri na wakaweza kujenga vituo vyao ambavyo vinapendeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye sekta ya afya suala la *non-communicable disease* (magonjwa yasiyoambukizwa) tulichukulie kwa uzito mkubwa sana. Juzi tulipofanya *high camp* kule Magugu kwenye watu 600 tumekuta watu zaidi 160 wana kisukari hawajijui, kuna watu zaidi ya 200 na kitu wana *pressure* hawajijui. Kumi kati yao ilibidi walazwe siku hiyo hiyo kwa sababu hawajui. Sasa ni jambo ambalo ni vizuri tulifanyile kazi kwa haraka na watu wapewe taarifa na wapewe elimu namna ya kujikinga na haya magonjwa na nini wafanye kama tayari wameshapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la lishe bora. Mimi naomba Serikali iangalie upya suala la lishe bora, tutilie mkazo elimu itolewe, lakini pia tukifika kwenye *Finance Bill*, mwaka 2017 tuliweka kodi kwenye virutubisho vya kuongeza kwenye unga, mafuta, vitaminini A. Vile virutubisho baada ya kuweka kodi, wale wote ambao walipewa misaada na *USAID* na wengine ambao wana viwanda vya kuongeza hivyo virutubisho, wamepunguza au wameacha kabisa kuweka. Kwa sababu huwezi kuuza unga au hayo mafuta kwa bei ya juu zaidi kuliko bei ya unga ya soko. Ina maana wenye hasara ni sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina kiwanda hata kimoja, kwa hiyo, tunaposema isipokuwa kwa Serikali; Serikali haina viwanda. Kwa hiyo, wangerudisha tu ile na waangalie namna ya kuratibu kwamba hivyo virutubisho watu waendelee kupewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuomba kwamba tuangalie namna ya kuboresha na kuongeza bajeti

ya *COSTECH* ili suala la tafiti mbalimbali liendelee kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara safari hii ikija ituwekee bajeti kwenye Kitengo cha Ngozi pale *KCMC* ambacho ndiyo kitengo pekee Tanzania kinachotengeneza madawa, *sunscreen yaani lotion* kwa ajili ya albino (watu wenyewe ulemavu wa ngozi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka yote kuna taasisi ambayo inafadhili, inatoa huduma pale, inatengeneza, wameweza kufikia maalbino 4,000 lakini ingependeza kama Serikali ingeweka bajeti kidogo ili badala ya 4,000 wafikie hata zaidi kwani wako zaidi ya 64,000. Kwa hiyo, bado tuna hatua ndefu na Serikali ingeunga mkono pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kwenye suala la elimu, Serikali iangalie namna ya kurudisha ile 2% katika ya nne ambazo zinazotakiwa kwenda *VETA* kwa ajili ya *Skills Development Levy (SDL)*. Leo hii 2% inaenda kwenye Bodi ya Mikopo. Tuangalie chanzo kingine cha kupata fedha kwa ajili ya Bodi ya Mikopo ili zile 4% zote ziende kwenye *skills development* kwa sababu nchi ambayo tunatarajia kuwa na viwanda, *VETA* ina kazi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunatakiwa kubadilisha mitaala kwa sababu leo hii mitaala mingi bado ni ile ya tindo na nyundo na sasa hivi tunatakiwa kubadilika kwenda kwenye *IT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii hata mashine ya kushona lazima ujue namna ya ku-*program*. Sasa ni vizuri hata hao mafundi umeme, mafundi gari wote hao wanafundishwa *VETA* kwa ule mfumo wa zamani, watakuja kukosa ajira na wazazi wao wamechangia fedha nyingi. Ni vizuri tubadilishi mfumo, vitu vyote sasa vinaenda na mfumo wa *IT* yaani wa *computer*. Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba kuanzia Juni safari hii suala la hiyo *VETA* na namna ya kubadilisha hiyo mitaala tuwe tumeshakamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni muhimu ni suala la vyuo vyetu. Mimi ningependekeza, Chuo kwa mfano cha Sokoine ambacho ni cha Kilimo na Mifugo Kingerudishwa Wizara ya Kilimo badala ya kubaki Wizara ya Elimu. Kwa sababu kwa Wizara ya Elimu inafanya kazi nzuri lakini inaona watoto wote wale ni sawa tu, bajeti inapelekewa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Wizara inayohusika ikisimamia chuo chake, kama Chuo cha Madini, kiko chini ya Wizara ya Madini, kile chuo kingekuwa kinapata msukumo mkubwa na Wizara ingeweza kukiangalia kwa ukaribu zaidi. Kwa hiyo, naomba suala hilo tuliangalie kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye suala la michezo, ningeomba pia Mheshimiwa Waziri angetoa tamko kwamba huko tunapokuwa na michezo katika ngazi ya Kata na ngazi ya Wilaya, hivi vyama vya mipira au vyama vya michezo vinadai sasa walipwe asilimia fulani ya fedha ambazo watu wamechangishana ili gharama za uendeshaji wakati hawajawahi kuchangia hata shilingi moja, wala kutoa elimu wala jambo lolote. Ukianzisha tu ligi, wao wanataka waingilie kati na wanataka walipwe hizo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashauri Mheshimiwa Waziri kwa hilo angetoa tamko ili kama wamewekeza, wana haki ya kudai, kama hawajawekeza, waachane kabisa na kudai watu wakichangishana kwa ajili ya kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine pia ningependa tuliangalie ni kwenye suala la elimu. Ni vizuri sasa tuangalie huko tunakoelekea tunahitaji kuwa na mafundi wengi kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo.

Pia tuondoe dhana nzima kwamba tukiwa na viwanda tutaajiri watu 4,000 au 5,000. Viwanda vya kisasa vyote vinaajiri watu wachache, *skilled labour* na vizuri sasa katika hizi taasisi zetu za kufundisha tubadilike na sisi tuwe tunaenda na mitaala hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba *TFDA* kwa suala hilo hilo la afya sasa, wawe na mashine za kupima. Leo hii mboga mboga nyingi ambazo zinaletwa sokoni, unakuta zimepigwa dawa leo, jana, ndani ya siku mbili, tatu zinapelekwa sokoni. Ndiyo maana magonjwa mengi haya ya *cancer* na nini yanatokea. Hizo mashine zingekuwa zimewekwa katika maeneo mbalimbali hasa katika masoko makubwa ya mboga mboga inaweza kusaidia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jitu, ahsante sana.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Vedatus Manyinyi na baadae Mheshimiwa Jesca Kishoa na Mheshimiwa Masoud wajiandae.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa ulinzi wake, lakini pia nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati, Kamati ya UKIMWI na Kamati ya Maendeleo ya Jamii na hasa nampongeza sana Mheshimiwa Serukamba kwa ripoti yake nzuri na hasa nimesoma katika ukurasa wa 41 kuhusu *pads* za watoto wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tuliliongea katika Kamati yetu ya Bunge Wanawake (*TWPG*) na tukaunda vikundi vidogo vidogo vinavyoshughulikia mambo ya jinsia, bajeti ya jinsia. Nakumbuka kikundi kinachoshughulikia taulo za wanawake ni kikundi cha ambacho Mwenyekiti ni

Mheshimiwa Zaynabu Vulu na Katibu wake ni Mheshimiwa Catherine Ruge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tumelishughulikia na Bunge la mwezi Novemba, 2017 tuliwaita Wakurugenzi kutoka Wizara mbalimbali tukakaa nao, tukajadili mambo mengi yaliyohusu jinsia na mambo yaliyohusu watoto wa kike na hasa tauzo za kike na tukaiomba Serikali kwamba isipoweza kupunguza bei, basi watoe bure tauzo hizo kwa sababu hata wanawake wa vijiji wanapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kabla ya Bunge la Bajeti kama tulivyowaagiza wale Wakurugenzi wapeleke taarifa ofisini kwa Mawaziri wao kwamba tukutane na Mawaziri, Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa Afya watuambie kwamba habari ya tauzo za kike kupunguzwa bei au kutolewa bure kwa wanafunzi limefikia wapi? Ninaamini Mawaziri watalishughulikia na kabla ya Bunge la Bajeti watatuletea taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la uhaba wa watumishi au uhaba wa wauguzi katika Mkoa wangu. Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri ya kuhamishia Makao Makuu Dodoma na sasa watumishi wengi wamekuja Dodoma na watumishi hawa wanahudumiwa na wauguzi wachache na watumishi wachache wa hospitali wa hapa Dodoma. Hatujaongezewa wauguzi, hatujaongezewa madaktari na kama Kamati ya Maendeleo ya Jamii walivyosema kwamba Hospitali ya Benjamin Mkapa haitumiki vizuri, ni kweli haitumiki vizuri kwa sababu ina vifaa vingi, ina wataalam wachache na ina wauguzi wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa kwamba Waziri utalichukua hilo na utaongeza watumishi pale Benjamin Mkapa na vifaa tiba najua viro vya kutosha, lakini hatuna wauguzi na watumishi wa kutosha wa kuweza kutumia vile vifaa ili kupunguza foleni kubwa iliyopo Hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia uhaba wa walimu katika Mkoa wangu. Siku moja tulikwenda na Waziri

wa TAMISEMI hapa lyumbu tu mjini na tukakuta wanafunzi wako 800 na walimu wako wanane. Hebu fikiria hao walimu wanavyofanya kazi ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule moja ya msingi Ntomoko, shule ya msingi Ntomoko, wanafunzi ni wengi lakini walimu wako watatu. Ninaamini Serikali itaona namna ya kuwaongeza walimu hasa katika shule zetu za msingi na hata shule zetu za sekondari pale ambapo kuna upungufu mkubwa wa walimu. Kwa sababu shule za vijivini, shule ambazo ni *remote areas* walimu ni wachache mno na hasa walimu wa sayansi, kiasi kwamba hawakidhi mahitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *capitation*. Zamani fedha za *capitation* zilikuwa zinapelekwa shulenii na Walimu Wakuu ndio waliokuwa wanahusika kununua vitabu. Tangu suala la elimu bure, Serikali au Wizara imeamua kununua vitabu kuanzia vitabu vya wanafunzi wa darasa la nne hadi wanafunzi wa darasa la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu mkubwa sana wa vitabu mashulenii. Siyo Dodoma tu, naamini hata mikoa mingine kuna upungufu mkubwa wa vitabu vya wanafunzi kuanzia darasa la tano hadi darasa la saba. Tunategemea kwamba hao wanafunzi wanapoanza darasa la tano, wanatarajia kufanya mitihani ya kuingia kidato cha kwanza. Kwa hiyo, kama hakuna vitabu, hawawezi kusoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Dodoma takriban kitabu kimoja wanatumia watoto sita hadi nane. Kwa hiyo, naomba tu Serikali yetu sikuvi ione umuhimu sasa wa kununua vitabu na kuvipeleka mashulenii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna upungufu mkubwa wa madarasa. Tangu Serikali itoe elimu bure mashulenii, sasa hivi kuna mfumuko mkubwa sana wa watoto wanaoanza darasa la kwanza. Kwa hiyo, madarasa hayatoshi na hakuna namna ya wananchi kuchangishwa au wazazi kuchangishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakuna namna ya kuongeza madarasa. Kwa hiyo, naomba Serikali sasa itoe tamko, namna gani tunaweza kuongeza madarasa bila kuchangisha wazazi? La sivyo, Serikali ichukue jukumu la kujenga madarasa ili wanafunzi wanaoingia darasa la Kwanza na wale wanaoanza *form one* wapate namna ya kusoma na namna ya kusoma kwa uzuri zaidi, wasisome chini ya miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napongeza sana, tumetoka kuwa na semina na Taasisi ya Moyo kule Dar es Salaam. Niwapongeze sana kwa kazi nzuri...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Fellister. Tunaendelea na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hili suala linalohusiana na Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulika na masuala ya UKIMWI pamoja na Kamati ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi lakini vilevile na watu wengi tumekuwa haturidhiki sana na maendeleo ya nchi hii kwa maana ya mafanikio yanayopatikana. Na mimi hili limekuwa likinisumbua sana kujua hivi shida ni nini, hasa ukiangalia kwenye hii Awamu ya Tano, ni awamu ambayo kila mmoja anakubali kwamba ukusanyaji wa mapato umeongezeka, lakini vilevile kumekuwa na nidhamu ya matumizi. Hata hivyo, bado kila ukiangalia kila upande, upungufu upo, kwenye upande wa elimu, upungufu upo; afya, upungufu upo; maji, upungufu upo; na kwenye huduma zote za jamii. Ukiija kuangalia upande mwengine wa bajeti, ukiangalia awamu iliopita na awamu hii, fedha zimeongezwa maeneo mengine zaidi ya asilimia 300, mfano kwenye afya, tulikuwa tunazungumzia

chini ya shilingi bilioni 50 kwa mwaka lakini leo tunazungumzia zaidi ya shilingi bilioni 200. Hizo ni fedha ambazo zimeenda kwenye afya, lakini bado kwenye elimu na kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utafiti wangu kuna jambo ambalo nimeona kama hatujalitambua wala hatuli-*address* ambalo nadhani kama tusipolizungumza basi tutaendelea kuathirika. Hayo maendeleo tutayategemea na bado hatutayaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu ninaona kama tunahitaji ku-*address* suala la uzazi wa mpango. Tunahitaji ku-*address* suala la uzazi wa mpango kwa nini? Nitoe tu mifano michache; nakumbuka mfano mwaka 2016 pale kwenye Jimbo langu kulikuwa na uhaba wa madawati, tukatengeneza madawati yasiyopungua dawati 3,000, lakini mwaka 2017 tu mwishoni tunaambiwa kulingana na wanafunzi ambao wameendelea kujiunga, bado hizo dawati tunaambiwa tena zinatakiwa karibu dawati 3,000 nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, kwenye shule yangu moja tu nakumbuka kule nakotoka, shule ya Nyakato, lile darasa la kwanza peke yake wamejiunga wanafunzi 800 kwenye darasa la kwanza. Kwa hiyo, ukiangalia kutokana na ongezeko la watu kila mwaka, kwa hiyo, ni kwamba chochote kile tunachokifanya lazima upungufu uendelee kuwepo. Kutokana na hali hiyo, ndio maana najiuliza, labda Mheshimiwa Waziri atatusaidia kwamba hivi ni kwa nini hili suala la uzazi wa mpango hatutaki kuli-*address*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukijaribu kuangalia katika nchi za wenzetu, ukitafuta nchi yoyote ile ambayo inaonekana imepiga hatua au inaendelea, unakuta watoto wadogo wanaozaliwa ni wachache kuliko watu wazima. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema kwamba nadhani tukiendelea na hali hii na kwa kutambua kwamba nchi ni ile ile, maeneo ni yale yale, kwa hiyo, kila siku itakuwa tuna

upungufu mkubwa, pamoja na juhudzi za Serikali ambazo itakuwa inafanya, lakini bado shida yetu itakuwa iko pale pale na bado changamoto zitaonekana kuwa bado ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilidhani Serikali inahitaji ilifanye ni suala la bima ya afya. Ukiangalia hasa katika nchi nyngine za kiafrika, mfano ukienda hata Rwanda hapo, suala la bima ya afya ni *compulsory*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali inajitahidi kupeleka vituo vya afya na zahanati, lakini kulingana na idadi kubwa ya watu tulionayo, kila leo zile huduma za afya unakuta ni mbovu, na kwa sababu ni mbovu ndiyo maana sisi kama Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa kawaida tunaendelea kuona tu kwamba hakuna ambacho hii Serikali ya Awamu ya Tano inafanya, kwa sababu bado upungufu ni mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nadhani watu wengi zaidi sasa tumejitahidi kuongeza kuzaa, kwa sababu leo una uhakika kwamba mama akipata ujauzito hata chandaria atapata bure kule kwenye zahanati. Akishajifungua mpaka miaka mitano mtoto atatibisha bure. Akitoka hapo, kule shule ataenda atasoma bure. Kwa hiyo, mzazi kama mzazi wala haoni shida yaani anaona jukumu lake yeche ni kuzaa tu, akishazaa, Serikali itaendelea.

Kwa hiyo, ndiyo maana nasema lazima tufike mahala tuamue na tuone kwamba ni kwa kiasi gani tunaweza kuendelea. Ahsante. (*Makofu*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Tunamalizia na wachangiaji watatu hawa kwa dakika tano tano. Naomba Mheshimiwa Jesca, Mheshimiwa Masoud na Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nianze kwa kusema jambo moja, hatuwezi kufanya mapinduzi ya viwanda kabla hatujafanya mapinduzi ya nguvukazi iliyo bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi sana ambayo ni muhimu kwenye mapinduzi ya viwanda. Ukiachana na habari ya umeme na *raw materials*, lakini jambo lingine ambalo ni la msingi na ni nguzo kwenye mapinduzi ya viwanda ni pamoja na nguvukazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata fursa ya kumsikia Mama Christina Lagade ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la Fedha la Kimataifa la *IMF* alipokuwa Ethiopia mwaka 2017 mwishoni, anasema nchi kama Tanzania, Kenya, Nigeria na Ethiopia yenye, pamoja na fursa zillizonazo za kupelekea uchumi wa viwanda, haziwezi kufikia huko kama hawatawekeza kwenye nguvukazi (*competitive labour force*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na nguvukazi kama mfumo wa elimu hau-*reflect* dira ya Taifa. Hivyo vitu vitatu vinategemeana; nguvukazi, mfumo wa elimu na dira ya Taifa ni vitu ambavyo vinategemeana kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu awamu ya pili ianze mpaka sasa hivi, kiwango cha elimu yetu kinashuka kwa *speed* iliyopindukia. Sizungumzii idadi ya wanafunzi mashulenii, nazungumzia kiwango cha ubora wa elimu inayotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia ripoti ya Shirika moja la viwanda la Kimataifa la *UNIDO* ambalo linaonesha kwamba asilimia 80 ya *labor force* katika Taifa letu ni *unskilled*. Mheshimiwa Waziri wa Elimu haya mambo unapaswa kuja na majibu, kwa sababu hatuwezi ku-*invest*, hatuwezi kuandaa kizazi kupeleka watu shulenii wakasoma halafu wakawa *unskilled*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ATE* (*Association of Tanzania Employers*), Shirikisho la Waajiri na wenyewe wamekuja na taarifa yao, wanasema *30% to 40%* ya ajira wanazozitangaza watu wanakosa vigezo/sifa. Tafsiri yake hapa kuna *mismatch*, *mismatch* kwa namna gani, kwa maana ya kwamba watu tunaowazalisha wanapishana na mahitaji ya soko la ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema suala hili likaangaliwa kwa umakini mkubwa kwa sababu tunaweza tukawa tunahubiri kwamba ajira hakuna na wakati sababu kubwa inaweza ikawa ni tunapishana na mazingira ya sasa na uhitaji wa elimu tunaotakiwa kuupata kutokana na ushindani uliopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi ni kwamba elimu hii inashuka kwa kasi kipindi ambacho tunaihitaji kutokana na ushindani ambao tunao. Wakati huo huo, nchi zote ambazo zimefanikiwa katika mapinduzi ya viwanda zime-*invest* sana kwenye nguvu kazi. Zime-*invest* kwenye nguvu kazi kwa namna gani? Zime-*invest* kupitia elimu ya kati. Tunachemka kweli kweli, tumeshindwa kutengeneza uwiano sahihi wa nguvu kazi kupitia elimu ya kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ambazo zimefanikiwa kwenye mapinduzi ya viwanda kupitia nguvu kazi ya elimu ya kati wanafanya hivi; uwiano wa elimu ya kati na elimu ya juu ni moja ya ishirini mpaka moja ya hamsini kwa maana ya kwamba, kama kwa elimu ya juu kuna mtu mmoja basi elimu ya kati kuna watu ishirini au kama elimu ya juu kuna mtu mmoja basi elimu ya kati kuna watu hamsini lakini sisi ni *vice versa*. Kama elimu ya juu kuna watu watatu eti nguvu kazi kuna mtu mmoja ambaye ni elimu ya kati. Tume-*invests* sana kutengeneza *managers* tunaacha kutengeneza watendaji ambao ni watu wa elimu ya kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka, nimepitia kitabu cha Ally Mafuruki ambacho amekizindua mwaka jana Mheshimiwa Rais mwenyewe, ningombaa au

ningependekeza kama Mheshimiwa Rais alikipeleka akakiweka kwenye *draw*, akifungue akisome kina majibu mengi sana ya matatizo yetu. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jesca. Tunaendelea na Mheshimiwa Masoud na baadaye Mheshimiwa Amina Mollel atamalizia dakika tano.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pia niwapongeze wawasilishaji wote wawili. Nianze na dawa tu tunazotumia binadamu ambapo ni matumaini kwamba kiwango cha ubora wa dawa za binadamu zinafanyiwa utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina masikitiko, baada ya dawa kutumia muda wa miaka mitano au miaka kumi tunaambiwa dawa hizo hasa hazifai zina madhara, hivi hamkufanya utafiti wa kutosha? Leo kuna baadhi ya dawa unaambiwa kabisa dawa hizi *chroloquine* usitumie tena, *metakelfin* zina madhara, hivi sisi ndio majoribio ya hizo dawa? Tumeshapata matatizo mengi, watu wameshaathirika na matatizo mbalimbali wanaambiwa sasa ninyi hizo dawa msitumie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, wafanye majoribio ya kutosha kwa viumbe vingine sio binadamu, sio Watanzania. Nafikiri Mheshimiwa Waziri atuambie sasa kwa nini tunatumia dawa hizi, tunapata madhara ndio wanasema baadhi ya dawa hizi hazifai. Kwa nini wasifanye majoribio kwenye viumbe vingine ambavyo sio binadamu, tatizo ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubora wa dawa zenyewe, unapokwenda maduka ya dawa (*pharmacy*) unaambiwa unataka ya India, Ujeruman, Kenya au ya Tanzania, dawa hiyo hiyo ya aina moja, imesemwa kwenye semina, tatizo ni

nini. Sasa kumbe ni kiwango cha ubora wa dawa zenyewe, nchi zinakotoka kuna ubora tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunataka tujue Mheshimiwa Waziri atuambie sasa baadhi ya madhara wanayoyapata Watanzania baada ya kutumia dawa katika nchi fulani, nchi ambazo inaonekana dawa zake ni hafifu hazina *standard* inayotakiwa. Hilo pia Mheshimiwa Waziri atuambie ana mkakati gani wa ziada kuelimisha jamii juu ya jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya kulelea watoto yatima wanaoishi na VVU/UKIMWI na mazingira magumu. Mbona vitu hivi hamvipi umuhimu unaostahili? Ukienda katika maeneo mbalimbali unaona huruma, watoto hawa hawana lishe, masomo ni shida, nguo ni shida, ni tabu, lakini ukija hapa Serikali ukiwaambia wana mkakati gani wa ziada juu ya watoto hawa kujua maisha, masomo na lishe zao wanasema tuna mkakati wa ziada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote nikwambie, Serikali haitaki kukubali lile Azimio la Abuja la kutenga fedha inayostahili halafu wamewaachia wafadhili zaidi, umeona wapi wewe wa mwenye shamba unasema msaidizi mwenye shamba ndio atamaliza hiyo kazi. Hili ni jambo moja kubwa ambalo linatia wasiwasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti hasa wa takwimu za hali ya maambukizi ya VVU na UKIMWI. Ukiangalia *TACAIDS*, *TACOSOA* na mashirika mengine unaambiwa kwamba Dodoma ni 2.9, ukienda *TACAIDS* 2.9 na *TACOSOA* 2.9 na wewe ni mjambe lakini ukikaa Dodoma zenyewe ukisoma mazingira ya Dodoma zenyewe, ukikaa na wataalam mbalimbali na ukifanya uchunguzi vizuri hospitali mbona mnadanganya watu Dodoma ni zaidi ya 2.9, tusidanganyane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu ambazo mnazitoa sio halisia, ni kwa nini ukienda *TACAIDS* 2.9, *TACOSOA* 2.9 Mheshimiwa Waziri mnapofanya sherehe mbalimbali hapa

Dodoma waambieni hali halisi ya ukweli ulivyo. Ukiangalia hali halisi hapa na pale mikusanyiko mikubwa ya watu, vyuo vya hapa zaidi ya wanafunzi 15,000. Ukiangalia hapa madereva wanaosafiri masafa marefu wanakaa hapa na mambo mengine mbalimbali yapo hapa. Sasa waambieni ukweli wananchi wa Dodoma kwamba hali sio shwari sana, lakini mnawapa moyo aah! Dodoma ipo vizuri sana ni 2.9 jamani mnataka muwamalize hata Dodoma, shauri yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka nizungumzie ni suala zima la swalilangu la asubuhi, suala la posho ya kufundishia kwa Walimu (*teaching allowance*). Huu ni mwaka wa sita tangu Serikali ikubali kwamba Walimu watapatiwa posho ya kufundishia, tangu Oktoba mwaka 2012 mpaka leo Walimu hawajapatiwa *teaching allowance*, wamepewa Wakuu wa Shule na Waratibu, wamepewa peke yao hao tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifika hapa, Serikali wanasema aaa tupo katika mkakati, Serikali ni sikivu, imepanga mikakati madhubuti, si muda mrefu Walimu watapata hizo fedha. Tunataka Mheshimiwa Waziri wa Elimu atuambie, simwoni sijui yuko wapo, yupo kule pembedi, atuambie sasa ni lini Walimu watapata *teaching allowance*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Masoud. Tunamalizia na Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kuhusiana na taarifa iliyowasilishwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Mendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumze mambo machache tu. Moja ni kuhusiana na ule Mfuko wa Maendeleo hasa kwa Wanawake ile asilimia kumi.

Nakumbuka mwaka jana katika bajeti tulipendekeza kwamba katika ile asilimia tano kwa wanawake na vijana pamoja na watu wenyewe ulemavu wakasema kwamba iende mbili. Naiomba Serikali iweze kuleta sheria kwa sababu wengine wanafanya kwa mapenzi tu, naomba kwamba iwe sheria. Vile vile lakini vilevile Watu wa Maendeleo ya Jamii wasaidie kutoa elimu ili hata wanapopewa hiyo mikopo waweze kuitumia katika malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie katika ukurasa wa hamsini ambao wamelizungumzia Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) na nakubaliana kabisa na maoni ya Kamati kwamba *TBC* ni shirika pekee la Serikali ambalo linategemewa kwa kazi nyingi na hata katika habari na matukio mbalimbali ya Serikali, *TBC* wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba jamii inapata taarifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na maoni yao kwamba *TBC* ikajifunze kwa *Azam TV* na kwa nini sikubaliani nao. Mionganoni mwa mshirika ambayo yana waandishi na wataalam wenyewe weledi ni *TBC*. Changamoto kubwa ya *TBC* wanayokutana nayo ni kwamba tangu mitambo imefungwa mwaka 1999 hatimaye *TBC* mwaka 2000 mpaka leo mitambo bado ni hiyo hiyo. *TBC* inakabiliwa na changamoto kubwa ya mitambo iliyochakaa na imechoka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Serikali itaamua kweli kuwekeza kwa shirika hili la *TBC* kufunga mitambo ya kisasa na vilevile hasa kwa kuzingatia wakati tulionao hivi sasa, naamini kabisa *TBC* itafanya kazi vizuri na ipasavyo. Naomba niseme tu nimekuwepo kwa miaka nane katika shirika hili na nimeshuhudia, inasikitisha baadhi ya mitambo ukienda *TBC* wafanyakazi wa *TBC* wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka mwaka 2008 ndipo ambapo mbali na ile *studio* ya awali kabisa ya mwaka 1999, baadaye wakaja wakafunga *studio* nyininge ndogo ambayo ndio wanayotumia kusomea habari na vipindi vyatya asubuhi vyatya jambo. Hakuna *studio* na mfano mzuri tu, kwa

bahati nzuri tunaona wakienda kuhojiwa na hasa kipindi cha tunatekeleza, wenyewe wanashuhudia ubovu na uchakavu wa mitambo iliyopo ya *TBC*. Hiyo *studio* iliyopo ni ya tangu mwaka 1999. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iweze kuhakikisha kwamba inazingatia umuhimu wa kuwekeza mitambo ya kisasa ili *TBC* iweze kutimiza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kabisa vituo vingine kwa mfano hata Azam ilivyokuwa inaanizhwa ni wataalam hao hao wa *TBC* ambao waliweza kwenda kusaidia katika uwekezaji wa mitambo ya kisasa. Hatuwezi kulinganisha na *TBC* kwa sasa kwa sababu wao wana mitambo ilio bora zaidi na vilevile *TBC* mitambo yao imechoka sana. Kwa hiyo, Serikali izingatie hilli, tusipende tu kumkamua ng'ombe maziwa pasipo kumlisha ipasavyo. Ikiama kuwekeza *TBC*ina wafanyakazi na watumishi wenyewe weledi na uzoefu mkubwa na itaweza kufanya kazi zake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusiana na Wizara ya Habari, mchangiaji mmoja alisema kwamba Wizara ya Habari hivi sasa na hasa Idara ya Habari (Maelezo) wamekuwa wakitumika sana kuhariri au kufungia vyombo vya habari. Utaratibu uliopo na kama inavyofahamika, endapo wanataaluma wakizingatia weledi na umakini zaidi...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ikupa.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Hayatoweza kutokea hayo.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ikupa, Waheshimiwa Wabunge labla sijaingia upande ...

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Amina Mollel.

MWENYEKITI: Ahsante.

Michango kwa Maandishi

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya UKIMWI imepitwa na wakati, sera hii ya UKIMWI imepitwa na wakati kwani sera ya mwaka 2001 naishauri Serikali ihuishe sera hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya masuala ya UKIMWI ni ndogo nasikitika kuona Serikali inatenga fedha kidogo wakati ugonjwa huu ni janga la kitaifa. Hii lnaonyesha kuwa Serikali haina mpango na kuona ugonjwa huu unatokomezwa. Naishauri Serikali kuhakikisha inatenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huu mbaya. Pia fedha zikitengwa zipelekwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya madawa ya kulevyaa; naishauri Serikali itenye pesa kwa ajili ya kujenga *sober house* ili kuwanusuru vijana wetu ambao wanashindwa kwenda kwenye *private sober houses* ambako wanatoza shilingi laki 400,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo dume unachangia sana katika ongezeko la ugonjwa wa UKIMWI. Hii inatokana na akinamama kutokuwa na uhuru na miili yao. Mfano, baba mlevi anatumia nguvu au analazimisha mama kufanya tendo la ndoa. Naomba Serikali iendelee kutoa elimu kwa jamii kuititia vyombo vyahabari, lakini pia kuititia taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iandae program maalum mashulenii kuanzia shule za misingi, sekondari ya vyuo zinazohusika na masuala ya UKIMWI. Fedha zinazopelekwa kwenye mkoaa kwa ajili ya semina au mafunzo

halmashauri moja ili zitumike kwa ajili ya kununua dawa za magonjwa nyemelezi na virutubisho.

MHE.RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudhi ambazo Serikali inafanya kuhakikisha inapunguza magonjwa yanayoambatana na Ugonjwa wa UKIMWI kama *TB* na Magonjwa ya Zinaa, pamoja na majukwaa maalum ya Elimu zinazofanyika, bado maambukizi katika jamii yapo hususani katika eneo la vijana linaloambatana na matumizi ya madawa ya kulevyia, je Serikali, haioni iko haja ya kuhakikisha vijana wanapata ajira ili kupunguza tatizo hili la chakula/lishe na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Serikali katika eneo hili pamoja na kuhakikisha jamii inapata aina ya vyakula vinakua na lishe, hivyo iko haja ya Serikali kuhakikisha mfumo wa viwanda hili tunavyovijenga sasa pia vizingatie suala la kutengeneza nafaka zenye lishe bora na pia kuna wagonjwa Watanzania maskini wanatumia dawa hizi wanashindwa kupata vyakula vyenye lishe bora ili kuwasaidia kupata afya wanapokua wanatumia dawa hizi za kupunguza makali ya UKIMWI. Je, Serikali haioni haja ya kuhakikisha inawapatia vyakula vyenye lishe bora waathirika hawa maskini pindi wanapofika katika dirisha la dawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukatili na Unyanyasaji wa Jinsia kwa Waathirika; kwa kuzingatia maoni ya Kamati, naomba Serikali iweke mkazo mkubwa kuitia madawati haya ya unyanyasaji wa kijinsia kutatua kero hii, kesi hizi zimekuwa zikichukua muda mrefu na hivyo kupelekea vitendo hivi kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira limekua kiini kikubwa cha tatizo la baadhi ya mikoa kuendelea kusambaa kwa magonjwa haya hususani Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Morogoro, mikoa ambayo kuna wimbi kubwa la starehe na biashara ya Madawa ya Kulevyia imeshamiri na pia wanawake wanaofanya biashara ya kuuza mili Yao inaendelea. Hili yote inatokana na ukosefu wa ajira

zisizoeleweka. Je, Serikali haioni kwamba ukosefu huu wa Ajira unapelekea maambukizi ya UKIMWI na matumizi ya Madawa ya Kulevyaa kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa dawa za kupunguza makali ya VVU; baadhi ya maeneo vijijini bado ni changamoto hususani waathirika wanaotoka vijijini na hii hupelekea mgonjwa kushindwa kufika hospitali kufuata dawa na hivyo Serikali ione haja ya kuongeza madirisha ya ugawaji dawa. Serikali kusimamia Halmashauri kupiditia fedha zinazotengwa kwa ajili ya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi Halmashauri hazitumii pesa hizi kwa mlengwa kuisaidia jamii hii, hivyo Serikali ione haja ya kusimamia katika Halmashauri hizi ili pesa zifike kwa walengwa, kupiditia elimu kuhusu masuala ya UKIMWI, Warsha, makongamano na misaada kwa walengwa isiishie tu kulipanalipana posho huku wahusika haziwafikii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya Magereza/Mahabusu, mfano wa Gereza la Kalila, Nkulunkulu na Mahabusu zilizopo katika Manispaa ya Mpanda hali ni mbaya. Hii sio Mkoa wa Katavi pekee bali ni katika Magereza mbali mbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mlundikano wa wafungwa unapelekea utoaji wa huduma za afya bora kushindwa na wanazidiwa uwezo kuna wafungwa na mahabusu 39,312 na uwezo wa magereza ni kuhifadhi mahabusu 29,552. Je, Serikali ina mkakati gani kutatua changamoto hii katika Taifa.

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kujikita kwenye pambano la kuufuta ugonjwa huu wa UKIMWI ifikapo mwaka 2030. Tunashauri kwa sasa tumekwisha toa elimu ya kutosha, ni vyema tujikite kuwashudumia waathirika kwa ukamilifu zaidi. Serikali kuongeza bajeti kwa fedha zetu bila kusubiri fedha za wafadhili, hatathamini ifanyike kila mwaka kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ni vyema ikafanye maamuzi magumu kwa kutoa ajira ya kukidhi mahitaji kwenvye upungufu wa watumishi vitendea kazi, rasilimali fedha, angalau kwa asilimia 75 ndani ya huduma ya afya, elimu – *VETA*, msingi na sekondari. Kwani hatua hii ngumu inawezekana ndani ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili gonjwa limekuwa na *NGO's* nyigi wakichukuliwa kuwa ni eneo la kupatia mapato, hivyo uwepo uchunguzi na kuweka vigezo vya kusababisha upunguzaji wa hizi *NGOs* kuelekea mwaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pawepo na utaratibu wa kuwadhibiti watu au familia zinazowanyanyapaa wenzao mionganini mwao, wanaobainika kuwa waathirika wa UKIMWI au madawa ya kulevy. Kutungwe Kanuni maalum ya kuwaweka hatiani na kupatiwa adhabu ya kutowajibika ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo ambao wanasantaza gonjwa hili na kufikia kuwasababishia vifo, nao kuendelea kutamba. Wahusika hawa wanaumiza moyo kwa baadhi ya wananchi na kuchukua sheria mkononi. Ni bora Serikali ikaona namna ya kuwajibisha watu hawa na walio ndani ya jamii yetu. Suala hili ni siri kubwa inahitajika katika kutolewa kwake taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono taarifa ya UKIMWI na nipongeze uwasilishaji mzuri. Nipende kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kuiwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Madawa ya Kulevy kupata vitendea kazi vya kisasa ili kuweza kuenda sambamba na vitendea kazi vinavyotumiwa na wahalifu. Serikali iwe *sober house* zake za binafsi ni ghali mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali kuipa meno Mamlaka ya Kudhibiti UKIMWI, kuwapa nguvu na mamlaka ya kufanya kulingana na uwezo wao. Serikali iwaongezee rasilimali watu ili kuwezesha utekelezaji wa kazi au majukumu yao kwa urahisi na kwa ufanisi. Nipende kuishauri Serikali kutoa waraka maalum ili kuwezesha halmashauri zote kuunganisha shughuli za UKIMWI kuunganishwa na madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, UKIMWI una vyanzo vingi vya kupata hasahaha wanaojidunga wamekuwa chanzo kikuu na hivyo suala hili linatakiwa kuangaliwa kwa makini ili kutoa elimu kwa vijana wetu jinsi ya kuishi maisha ambayo yatawaweka mbali na magonjwa hayo ambayo yana punguza nguvu kazi ya Taifa. Nishauri Serikali kuongeza bajeti ya UKIMWI na madawa ya kulevya. Niombi Serikali kuwezesha waathirika wa UKIMWI kupata lishe kwani waathirika wanashindwa kupata lishe ili waweze kumeza dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kuweka mpango maalum wa utoaji dawa za magonjwa nyemelezi yanayotibiwa na *septrin* na dawa hii haijaambatanishwa kwenye dawa za kufubaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo dume ni sababu mojawapo kwani mwanamke hana mamlaka juu ya mwili wao na pia wanawake wengi waume wao wengi hutumia dawa za UKIMWI kwa siri na huzihifadhi ofisini. Niishauri Serikali kuanzisha au kuendeleza taaluma, mitaala ya kujifunza jinsi gani UKIMWI unavyoenezwaa na pia kupunguza uwepo wa *night clubs* kwenye makazi ya watu.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kupongeza Kamati ya UKIMWI kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao. Ushauri, jitihada za kupambana na kudhibiti madawa ya kulevya haziridhishi, kwa kuwa bado vijana wengi mitaani wanaendelea kuathirika. Ushauri kwa kuwa madawa ya kulevya yamekuwa na athari kubwa kwa jamii na Taifa kwa ujumla ikiwa pamoja na kupunguza nguvu kazi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali iwe na mpango mahususi wa kufanya vipimo kwa vijana au watoto wetu mashulenii na mitaani wamekuwa na tabia ya kulawitiana . Kwa hiyo upimaji utasaidia kubaini na kudhibiti hiyo michezo hatarishi kwa watoto wetu. Aidha, nashauri upimaji huo uletwe pia hapa Bungeni ili kubaini waathirika wa ulawiti.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu; kwa sasa elimu yetu nchini imekuwa ni bure kuanzia ngazi ya msingi na sekondari. Suala hili limekuwa na mkanganyiko mkubwa kwani mapokeo ya wananchi wanajua kwa sasa hakuna mchango wowote ambao wanatakiwa kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Walimu kupandishwa, ni utaratibu tuliozoea katika nchi yetu Mwalimu anapojiendeleza anategemea kupandishwa daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vyuo, kuna baadhi ya mikoa haina chuo hata kimoja katika kozi mbalimbali kitu ambacho kinakuwa ni changamoto kubwa kwa wanafunzi wanaohitimu katika maeneo mbalimbali. Ushauri wangu kwa Serikali kuhakikisha vyuo vinajengwa kwenye mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Walimu, jambo hili limekuwa changamoto sana kwa Walimu wetu. Jambo hili ni hatari kwani sote tunatambua ualimu ni karama hivyo kutapelekea matokeo mabaya katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kukariri madarasa, jambo hili ni vizuri Serikali ikafanya tafiti za kutosha kabla haijazuia kwani suala hili lina athari kubwa sana kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Wauguzi; baada ya Serikali kuja na suala la vyeti feki kumebaki na

upungufu mkubwa wa nafasi mbalimbali katika hospitali nyingi nchini kwani jambo hili ni hatari sana kwa kitengo hiki muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uzazi wa mpango; suala hili limekuwa na changamoto kwani elimu kwa watu wa vijiji bado haijatolewa kikamilifu, lakini pia Serikali ifanye tafiti juu ya baadhi ya njia za uzazi kwani zinalalamikiwa sana kuwa zinaleta madhara.

MHE. MARIA N. KANGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa ya kuchangia hoja iliyopo Mezani. Nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati zilizowasilisha hoja leo kwa umakini walioonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia suala la utoaji wa taulo kwa watoto wa kike lilitumainishwa katika taarifa ya Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii katika ukurasa wa 41. Ni kweli, ipo haja ya kumkomboa mtoto wa kike kwa kuwagawia taulo safi, ili waweze kukamilisha malengo yao ya kimaisha hususani ya kielimu. Kwa sababu, nchi nyingine za Afrika zimejaribu na kufanikisha, hakika nasi tutaweza. Suala hili ni zito na uzuri Mheshimiwa Waziri wa Afya ni mwanamke na ni imani yangu kuwa atalisimamia vyema kama tunavyotarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu ya kuwa hofu kubwa inaweza kuwa katika kuweka uhakika wa watoto hawa kupata taulo hizi kwa wakati, lakini niihakikishie Serikali kwamba, nchi kama Uganda, Kenya, Ethiopia na nyingine ambazo tayari zimethubutu kufanya hivyo, zimefanikisha kwa kugawa taulo za kufua, maarufu kama *reusable sanitary pads* ambazo ni bora na zinagawiwa mara moja kwa mwaka hivyo, kuepusha gharama kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua mara nyingi taulo hizi zimehusishwa na ukosefu wa maji, ambako kiukweli ni tatizo tofauti kabisa. Tujiulize tunalalamika watoto kukosa taulo salama, je, wanatumia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni matambala yasiyo salama ambayo pia, yanatumia maji kuwekwa katika hali ya usafi. Hivyo, basi ni muhimu Serikali pia, kuangalia changamoto ya maji kwa afya ya hedhi salama kwa sababu, watoto wa kike na wanawake kwa ujumla ni lazima watumie maji bila kujali wanatumia nini wakiwa hedhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya mwanamke na uchumi; kwa kuzingatia maoni ya Kamati mazuri yakifanyiwa kazi katika nyanja mbalimbali nadhani kutamsaidia mwanamke ambaye kimsingi anabeба majukumu makubwa na magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekua ikitenga fedha kwa ajili ya mikopo kwa wanawake yenye riba nafuu kupitia Halmashauri na Taasisi za kifedha, je, Serikali haioni kupita mikopo hii kuwa haiwasaidii wanawake maskini na badala yake wanaonufaika ni wale wanaojiweza kiuchumi, Serikali inaondoaje ubaguzi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa watumishi wa afya nchini; Mkoa wa Katavi una upungufu mkubwa wa watumishi wa afya, Madaktari Bingwa hakuna, lakini pia Manesi hawatoshi katika Hospitali ya Wilaya ya Mpanda na hii inapelekea kuleta msongamano mkubwa wa wagonjwa katika zahanati na katika madirisha ya dawa na kuna kipindi msongamano mkubwa hupelekea wagonjwa kuzidiwa wakiwa katika foleni wakisubiri huduma na wengine kupoteza maisha wakisubiri huduma kwa madaktari. Je, ni kwa nini Serikali mpaka sasa haijaajiri watu wa kada ya afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali inapata changamoto hizi kila siku lakini, bado hazifanyiwi kazi? Je, Serikali hii haionti na haitaki kufanya kazi ni kwa nini inaacha walipa kodi wanateseka na huku pesa zinapelekwa katika mambo yasiyo vipaumbele kwa wananchi maskini, mfano, Ujenzi wa Uwanja wa Ndege Chato, *E-passport* mpya na

ununuzi wa ndege ambao kimsingi haujazingatia mchakato wa manunuzi? Ni kwa nini Serikali inazitelekeza huduma za jamii nchini na kujikita zaidi kwa wananchi wasio maskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 45, Kamati imeshauri Serikali kuja na mkakati wa kudhibiti tatizo la unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika jamii hii wanaoathirika ni watoto na wanawake zaidi na jamii imekuwa ikipeleka taarifa katika Madawati ya Jinsia, Polisi na Mahakama, je, ni kwa nini Serikali inashindwa kusimamia kesi hizi na malalamiko kwa jamii kuhusu suala la kesi kuchukua muda mrefu na hivyo jambo hili kuendelea kufanyika kwa sababu watuhumiwa wanaendelea kutoka wanaposhtumiwa? Je, Serikali haioni kuendelea kukaa kimya na hizi kesi inajenga mazingira ya watuhumiwa kuishi kwa hofu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Afya ya Akili, Mirembe Dodoma; hospitali hii ina changamoto ya nafasi na huku inachukua wagonjwa 317 Wodini kila siku na inahudumia wagonjwa wa akili 43 kwa siku na kuhudumia wagonjwa 119. Kwa uwiano huu hospitali hii ambayo ndiyo kubwa nchini bado hospitali hii haitoshi na majengo yake ni chakavu pamoja na upungufu wa watumishi wa afya. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha inaboresha huduma katika hospitali hii katika Mji wa Dodoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la wagonjwa wa akili bado lipo katika Mkoa wa Katavi na kwa kuwa Serikali haifanyi utafiti katika mikoa kuona ni kwa nini ongezeko hili linatokea na nini kifanyike kusaidia jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi Kashato, Shule ya Msingi Nyerere na Shule ya Azimio, Jimbo la Mpanda Mjini ina watoto wenye matatizo ya akili wengi tu, lakini wana tatizo la kupata madarasa, huduma za vyakula pamoja na Walimu.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa, kwanza naunga mkono hoja za Kamati mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule binafsi kukaririsha watoto; ni ukweli dhahiri kabisa wamiliki wa shule binafsi wa mtindo wa kufanya udahili wa watoto wanaojunga na pia katika mitihani yao wameweka kiwango cha ufaulu na wastani ni 75/100. Suala hili sio haki kwa watoto ambao huenda mazingira au uwezo wake wasiweze kufikia ufaulu huo, hivyo watoto wanakaririshwa darasa na umri wao unazidi kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, suala la Serikali kutoa mwongozo shule binafsi kutokaririsha watoto naunga mkono kwani hakuna mzazi asiyependa mtoto wake kufaulu. Kwa hiyo, Serikali iendelee na msimamo huo ili haki ya kikatiba itendeke kwa watoto wenye uwezo mdogo. Serikali imewe ka mtihani maalum ya kupima watoto kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni yallyorithiwa toka Wizara ya Afya yameenda Elimu; kuna baadhi ya vyuo vya mafunzo kwa jamii vimehamishiwa Wizara ya Elimu ambapo awali ilikuwa chini ya Wizara ya Afya, mfano Chuo cha Msaginya, Katavi; kuna kazi za ukarabati, mkandarasi hajamaliza miaka miwili imepita wala Serikali haijamlipa. Hivyo, Serikali iangalie madeni pia fedha za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji UKIMWI; Sheria ya UKIMWI inamtaka mama mjamzito kupima kwa lazima ambapo imetekelezwa kwa kiasi kikubwa lakini kwa wenza wa mama wajawazito sheria bado hajjawataka wao kwa lazima kupima VVU. Hivyo kuna hoja sheria iboreshwe ili wenza wao nao wapimwe kwa lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikundi cha jamii kingine ambacho ni muhimu sana sheria iwatambue kupima kwa lazima, Serikali iangalie wanafunzi wanaotaraji kujiunga na Elimu ya Vyuo Vikuu ili kulinda maambukizi mapya.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote mbili zilizowasilishwa na Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii pamoja na

Kamati ya Masuala ya UKIMWI. Napongeza kazi nzuri walizofanya Kamati zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia maoni yangu katika masuala matatu yaliyonigusa katika taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, katika ukurasa wa 49 hadi mwanzo wa ukurasa wa 50, Kamati imetoe maoni na kupendekeza Serikali ilipe kipaumbele suala la kutoa elimu ya lishe kwa jamii. Naafikiana na mapendekezo haya lakini pia naomba ligusiwe suala la watu au jamii ambayo inakabiliwa na janga la njaa. Pamoja na umuhimu wa kutoa elimu juu ya lishe, Serikali ipange mkakati wa kuwapa chakula jamii zinazokabiliwa na ukame wa muda mrefu katika Wilaya za Kaskazini, Mashariki ya nchi yetu hususan Wilaya za Longido Ngorongoro na Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili, linahusu maboresho yanayohitajika kwa Shirika la Utangazaji la Taifa (*TBC*), tazama ukurasa wa 50. *TBC Radio* ndicho chombo kinachotegemewa kupata habari, elimu na burudani na asilimia kubwa ya wananchi wanaishi vijiji mahali pasipo na *TV* wala magazeti au upatikanaji wa *Radio za FM*. Kwa jamii za pembezoni hasa wale waishio karibu na mipaka ya nchi jirani, wanaishilia kupata huduma muhimu ya habari, elimu na burudani kuititia radio za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maboresho yaliyopendekezwa na Kamati, naomba kipaumbele kitolewe katika kuboresha miundombinu ya kisasa na kuiwezesha Radio ya Taifa isikike katika kila kona ya nchi yetu kuititia *mid-wave(MW)* na *FM frequencies*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, ninalopenda kuchangia ni kuhusu Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kama ilivyoelezewa katika ukurasa wa 61 wa taarifa ya Kamati. Nakiri kwamba ni kweli Elimu ya Watu Wazima imedorora katika nchi yetu, lakini siafiki taasisi hii kufutwa bali ihuishwe

kwani bado kuna watu wengi katika nchi yetu na hasa katika jamii za wafugaji ambao hawajui kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, napendekeza Serikali ianzishe taasisi mahsusini ya Elimu ya Awali nchini. Hili ni kutokana na hali halisi kwamba Kiwango cha Elimu ya Awali ni duni mno katika jamii ya vijiji ambapo umbali wa shule kwa kaya nyingi ni kati ya kilomita kumi hadi kumi na tano hasa Umasaini. Kwa maoni yangu kazi ya Taasisi ya Elimu ya Awali itakapoundwa itakuwa ni pamoja na:-

(1) Kuhakikisha kila kitongoji kwa jamii za vijijini wanakuwa na shule ya awali yenye kukidhi haja ya kuwajengea watoto wetu wachanga msingi bora wa elimu.

(2) Kubeba jukumu la kusomesha na kuajiri Walimu stahiki wenyewe sifa kamili za kutoa Elimu ya Awali kwa watoto walio chini ya umri wa kuanza elimu ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ilivyo kwa sasa utakuta katika vitongoji vilivyo mbali na shule ya msingi kwa watoto wadogo kuweza kutembea, shule za awali zinafundishwa na *failures* wa darasa la saba ambao ni wanakijiji wa kawaida tu wasio na taaluma yoyote ya ualimu zaidi ya kujua kusoma na kuandika.

(3) Kuandaa na kusambaza mitaala ya Elimu ya Awali katika shule zote za awali nchini pamoja na kuzisimamia shule za awali hadi zile za ngazi ya kitongoji kwamba Wizara ya Elimu inavyosimamia shule za msingi na sekondari.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa Walimu; tatizo la upungufu wa Walimu hasa katika shule za msingi ni kubwa sana. Njombe Mjini inakosa Walimu 454. Nchi hii inaenda kuua elimu kwa sababu hatuwezi kuwa na elimu bora kama hatuna Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia walimu hawa walipandishwa madaraja wakawekewa pesa za kupandishwa madaraja haya, lakini baada ya mwezi mmoja wakasitishiwa pesa hizo. Naiomba Serikali ipeleke Walimu wa kutosha mashulen iakini pia Walimu wapandishwe madaraja yao na wapandishiwe pesa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo mabaya ya mitihani; matokeo ya mitihani ni mabaya sana hasa shule za Serikali. Shule zinazoongoza kuanzia ya kwanza hadi ya 10 ni shule za binafsi. Hata hivyo, shule za binafsi zinakandamizwa sana kana kwamba siyo Watanzania. Naomba Serikali itambue kuwa shule binafsi zinalipatia sifa na heshima Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itende haki kwa shule za *private* na za Serikali kwa sababu uendeshajili wa shule binafsi ni mgumu sana, kwa kweli ni huduma tu. Mbaya zaidi kwa wale wanaohudumia watoto yatima na wanaoishi mazingira hatarishi lakini wanasona katika shule hizo, lakini Serikali inawatoza michango mingi kama ya ukaguzi Sh.5,000 kila mtoto, Sh.15,000 ya Mitihani ya Taifa na Sh.1,000 kila mtoto kwa ajili ya michezo. Naiomba Serikali ione ni namna gani inawasaidia hasa shule za watoto yatima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya elimu ya juu ni kitendawili; vijana wengi wenye vigezo vyatupata mikopo wanaachwa. Naiomba Serikali kufanya tafiti kwa umakini namna ya kuwatambua vijana hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya; naomba watumishi wa afya waajiriwe wa kutosha na hasa kwenye vituo vya afya. Pia majengo ambayo yamejengwa na wananchi kama Vituo vya Afya na Zahanati, basi Serikali isaidie kumalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii nami nichangie kwa maandishi kuondolewa kwa vitabu vibovu mashulen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge liliopita wachangiaji walisisitiza juu ya ubovu au kutokuwa na usahihi wa vitabu vyta kufundishia mashulenii hivyo ili amuliwa viondolewe mashulenii, lakini cha kushangaza vitabu vile bado vipo mashulenii na kusababisha kufifia (kufifisha) kwa elimu yetu hapa nchini. Kwa hiyo, naishauri Serikali ihakikishe inaviondoa vitabu hivyo mashulenii haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Mloganzila; Chuo cha kujifunzia na kufundishia Madaktari Bingwa Mloganzila kimejengwa (kilijengwa) kwa madhumuni ya kufundishia Madaktari kwa mujibu wa kanuni za Madaktari ulimwenguni ya kwamba kila Hospitali Kuu ni lazima iwe na Chuo Kikuu cha kufundishia na kujifunzia Madaktari. Mimi naishauri Serikali kwamba chuo hiki kibaki kuwa chuo cha kufundishia na kujifunza na siyo kuwa Hospitali kama inavyotaka kufanya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubora wa elimu; kumekuwa na changamoto kubwa sana ya ubora wa elimu hasa kwa shule za Serikali na hii inatokana na Serikali yenye we kutotilia mkazo maslahi na motisha kwa Walimu na uhaba wa vifaa vyta kufundishia mashulenii pamoja na umbali wa makazi na umbali wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo shule binafsi zimeboresha na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi, lakini nashangaa na inasikitisha sana kwa Serikali kutoa matamko ya kuzuia kukaririsha wanafunzi na kusababisha mrundikano wa wanafunzi wanaofeli mashulenii. Ushauri wangu Serikali iachane na kuzuia kukaririsha kwa shule binafsi ili wawewe kuwajengea uwezo wale wanaoweza kufanya vizuri badala yake waboreshe shule za Serikali ili ziweze kutoa wanafunzi walio bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iache kutoa adhabu kwa Walimu ambao shule zao zimefelisha badala yake Serikali ifanye utafiti ili kujua kwa nini wanafunzi wanafeli ndio itoe adhabu na siyo kutoa adhabu bila kufanya utafiti.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii ya kuchangia mfano wa utoaji wa huduma ya afya nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la ukatili kwa watoto; kumekuwa na changamoto kubwa ya ukatili dhidi ya watoto hasa wa chini ya miaka mitano. Inapotokea mtoto huyu anapata jaribio la kutendewa ukatili au jaribio la kubakwa na anapotakiwa kutoa ushahidi Polisi inaonekana kuwa ushahidi hautoshelezi na hivyo watuhumiwa wengi kuachiwa huru, hali hii inaongeza sana matukio ya ubakaji

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma kwa wajawazito; pamoja na Serikali kuonesha msisitizo wa huduma ya bure kwa wajawazito bado kumekuwa na changamoto kubwa ya vifaa vyta kujifungulia hasa katika maeneo mengi ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati zetu zimechoka sana na maeneo mengine hata maji hakuna hii ni hatari sana wakati mama anakwenda kujifungua. Pia vitanda vyta kujifungulia ni changamoto kubwa kwenye zahanati zetu, vingi vimechakaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nizungumze suala la msongamano wa wagonjwa kwenye hospitali za Mikoa na Wilaya; hili limekuwa tatizo kubwa kwa kuwa zahanati zetu hazijaboreshwya kutosha, hivyo wagonjwa wengi kukimbilia hospitali za mikoa na kusababisha msongamano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upungufu wa Madaktari Bingwa bado ni tatizo kubwa hasa kwa upande wa akinamama na watoto. Naomba Waziri anapokuja kuhitimisha aniambie na hizi ajira mpya 2018/2019 wamejipangaje kuongeza idadi ya Madaktari katika hospitali zetu ili kusaidia tatizo hili la msongamano wa wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo la *MRI-Scan* kwenye hospitali zetu na hiyo kusababisha vifo visivyo na sababu kwa magonjwa yasiyoweza kugunduliwa kwa vipimo nya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lishe; kumekuwa na tatizo kubwa la lishe, hivyo kuendelea kupata magonjwa kama kisukari, shinikizo la damu, ongezeko la uzito kwa watoto wadogo na watu wazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri anapokuja kuhitimisha aniambie kama Wizara wana mkakati gani wa kutoa elimu ya afya ili kuokoa Taifa letu.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeza kwa kazi nzuri Kamati iliyofanya. Naomba nichangie kwanza kwa kuliomba Bunge liangalie namna ya kuratibu kazi za Kamati ili Wabunge wapate fursa ya kuchangia wanaotoka Kamati zingine ili taarifa na maazimio ya Kamati kuzishauri Serikali namna ya kutatua changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza katika shughuli za Kamati nichangie suala la afya. Niipongeze Serikali kwa kuboresha na kufanya vituo nya afya ambavyo vitakidhi haja ya huduma za afya katika ngazi ya kata. Nashauri Wilaya zisizo na hospitali kwa sasa wasikimbille kwenye hospitali bali waboreshe huduma za afya ya msingi katika kata mbalimbali itaharakisha huduma kuwa karibu na jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ikubali sehemu ambapo Kata, Wilaya au Kijiji wana ramani zao za majengo ambayo yanakidhi mahitaji bila kuondoa ubora wa majengo waruhusiwe kuwa na ramani zao (*different design in architecture*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie gharama za vifaa tiba na madawa yanayosambazwa na *MSD* kama tunafanya *bulk procurement* mbona bado kwa watu binafsi bei ni karibu sawa au wakati mwингine ni bei ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba suala la *non communicable diseases* (magonjwa yasiyoambukizwa) liliwe mkazo na kupewa umuhimu kama Kamati ilivyoshauri. Elimu juu ya magonjwa hayo itolewe kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la lishe bora, Serikali iondoe kodi kwenye virutubisho vyta kuchanganya kwenye unga na mafuta vyta kuitia. Leo hii ni kwa taasisi za Serikali tunazopata huo msamaha na Serikali haina hata kiwanda kimoja, suala la lishe bora hatutafikia kwa tamaa za kupata kodi. Wenye viwanda wameacha kuweka hivyo virutubisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri Serikali iangalie namna ya kuongeza bajeti ya *COSTECH*; bajeti ya utafiti na maendeleo. Tupange asilimia moja ya bajeti au bilioni 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie kwa bajeti hii kuchangia kituo cha kutengeneza mafuta ya wenye ulemavu wa albino pale *KCMC*. Kitengo cha ngozi tuwekeze katika dawa za asili (*homeopathy*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika elimu nashauri tuangalie namna ya kurudisha asilimia mbili ya *SDL* inayoenda Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwenda *VETA*. Bodi itafutiwe chanzo kingine. *VETA* ipate haki yake ya asilimia nne. Pia tubadilishe mitaala ya kuwa ya mfumo wa *IT*, kutumia kompyuta. Leo hii hawa vijana tunaowafundisha kwa teknolojia ya zamani watakosa ajira, leo mfano haya magari ya kisasa lazima ujue kutumia kompyuta, huwezi kurekebisha bila teknolojia, hata fundi umeme wa nyumba, taa na vifaa vingi vinatumia *sensors*, kama hawajui *IT* (masuala ya kompyuta) namna ya ku-programme elimu yao haitahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwekeze kwenye utafiti na maendeleo, *COSTECH* tupange angalau bilioni 120 kwa mwaka; asilimia moja ya bajeti nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Vyuo Vikuu Maalum kama *SUA*, virudishwe chini ya Wizara husika ili vipate huduma

za karibu zaidi. Chini ya Wizara ya Elimu haviwezi kupata kipaumbele na Wizara kwa haki inatenga bajeti sawa kwa wote. Chuo cha Nelson Mandela kingeenda Wizara ya TAMISEMI pamoja na VETA zote, vyuo vya afya viende Wizara ya Afya. Aidha, vyuo vikuu viwe *specialized* na hata suala la *field* katika masomo yao lingepata unafuu.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kupata nafasi ya kuchangia mfumo wa utoajia huduma wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti kuna haja ya kuimarisha mfumo wa rufaa kuanzia ngazi ya chini kutoka zahanati mpaka ufile hospitali aidha ya mkoa au za kanda. Unakuta wagomjwa wengi wanakimbilia kwenda hospitali za ngazi ya juu sababu zahanati hazina wauguzi wala madaktari, hakuna vitanda vya kupima wagonjwa, hakuna dawa na kadhalika. Wafanyakazi wengi kwenye zahanati ni *ward attendant*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kuleta ufanisi kwenye zahanati ni vizuri Serikali ukaangalia upya kule tulikotoka na kurudisha zile shule za kufundishia *nurses, assistant clinical officers, midwife, rural medical aid* na hawa walikuwa specifically trained kufanya kazi katika ngazi za chini, lakini sasa hawapo. Wangekuwepo na vifaa vikawepo kwa kiasi kikubwa tungepunguza sana vifo vya mama na mtoto ukizingatia wananchi zaidi ya 80% wapo vijijiini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali 80% ya bajeti yake ingeielekeza kuimarisha hizi zahanati, watu wengi wangeishia kutibiwa kule na kwa kiasi kikubwa tungepunguza msongamano kwenye Hospitali za Rufaa ambako kwa sasa hivi hata mtu akitaka kutumbuliwa jipu unakuta wanaenda hata Hospitali za Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri pia kuangalia hii sekta ya kada ya dawa za usingizi. Hawa wapo pungufu sana, kuna haja ya Serikali kuwezesha wengi zaidi waweze kufika mpaka ngazi za chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nguo za wagonjwa, limekuwa ni jambo la kawaida katika Hospitali za Serikali wagonjwa kutoka na nguo zao majumbani na kulala nazo hospitalini. Hii ni hatari sana kuambukizana magonjwa ya ngozi hata kuleta wadudu kama chawa na kunguni wodini, kila mgonjwa anaotoka mazingira tofauti, ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kununua nguo za wagonjwa wanaolazwa wodini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii huenda sambamba na kuimarisha kitengo cha mapokezi cha *emergency*. Watu wengi hufia *casualty* sababu unakuta kitengo hiki sehemu nyingine hazina sehemu ya *observation*, za kumpumzisha mgonjwa ili ajulikane je, atalazwa au ni mgonjwa wa kipeleka wodini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wagonjwa wengi wenye kuishi na VVU wanapopata magonjwa nyemelezi kama nimonia na kadhalika wanabidi wagonjwa hawa wajinunulie *antibiotics* wakati wengine hawana uwezo kabisa tu kujua kwamba ni rahisi wao kushambuliwa na magonjwa sababu *immune* yao ilikuwa imeshuka za *ARU*ni kwa hii wanapopata magonjwa mengi kuititia kitengo chao cha *CTC* wasipewe dawa hizo bure?

Mwisho, kwa kuwa kumekuwepo na ongezeko kubwa la magonjwa yasiyoambukiza (*NCD*) na magonjwa haya yanakumba rika zote ni bora elimu itolewe sasa mashulen i kwa nguvu zote. Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu waimarishe elimu ya afya mashulen i.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya afya vingi vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi Mkoani Ruvuma vingi vimefikia renta, havijaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali itengete fedha kwa ajili ya kumalizia hivyo vituo vya afya ili kuokoa nguvu za wananchi zilizotumika, lakini pia kuboresha huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na Sera ya Taifa ya Elimu Bure kumekuwa na changamoto ya upungufu wa madarasa. Ninashauri Serikali yangu kuweka mkakati madhubuti ambao utalenga kuongeza madarasa katika shule zote zenyehu upungufu wa madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa walimu mashulenii umekuwa ni kero kubwa sana. Shule nydingi hazina walimu wa kutosha. Kutohuwa na walimu wa kutosha ni sawa na kuandaa chakula kizuri ambacho hakina chumvi. Athari ambayo itajitokeza katika Taifa hili baada ya miaka mitano ni kuwa na kizazi ambacho hakitakuwa na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya, hospitali ya Wilaya ya Mbinga ina upungufu mkubwa wa wodi kwa ajili ya akina mama wanaosubiri kujifungua na wale ambao wameshajifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi, naomba Waziri wa Afya aje katika Hospitali ya Mbinga, Mkoani Ruvuma ajionee mwenyewe adha ambayo wanaipata wanawake hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti katika sekta ya afya hususani madawa na vifaa tiba, lakini bado madawa hayatoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanaa, nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupiga marufuku kwa wasanii wanawake kuvali nguo ambazo ni kinyume na maadili yetu sisi Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba hoja na maoni yangu mbalimbali yaingie kwenye *Hansard*.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niipongeze taarifa ya Kamati na kuunga hoja mkono kwa kazi nzuri iliyofanywa. Pili, niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano ya Chama cha Mapinduzi chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa

kupambana na kuziba mianya yote ya upotetu wa fedha na hatimaye kuboresha huduma za afya na elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli usiopingika kwa *MSD* inafanya kazi nzuri sana ya usambazaji wa madawa katika hospitali mbalimbali nchini kwa wakati. Niombe Serikali yangu sikivu iweze kuongeza fedha katika bajeti ili taasisi hii iweze kutekeleza majukumu yake vilivyo. Naomba niipongeze tena Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya ya kuhakikisha inapiga vita uingizwaji wa dawa za kulevyia nchini. Hali hiyo imesaidia sana nguvu kazi ya Taifa isiendelee kupotea na pia kwa mkakati mzuri wa uanzishwaji wa *sober houses* ili kuwasaidia vijana wote walioathirika na matumizi ya madawa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa mtoto wa kike hasa wa kijiji wanakosa siku tano mpaka saba kuhudhuria shule pindi anapokuwa kwenye siku zake. Ndiyo maana mimi na Wabunge wanawake wote waweze kupaza sauti ili pale Serikali yetu itakapopata uwezo uweze kutazama jambo hili kwa jicho la tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa Wizara ya Elimu imekuwa Wizara ya matamko na nyaraka hali inayopelekea kushuka kwa elimu. Takwimu zinaonesha mpaka sasa ufaulu unazidi kushuka hasa katika elimu ya sekondari. Ni asilimia 28 tu ndiyo wanaopata daraja la kwanza hadi la tatu na asilimia 72 wanapata daraja la nne na sifuri. Iko haja ya kutazama mifumo ya utolewaji elimu ndani ya Wizara hii kwani bila hivyo tutakuwa tikizalisha nguvu kazi duni na hafifu.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze na kuunga mkono hoja ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kuhusu wazee wa Tanzania walio wengi wako katika hali mbaya sana. Hawana chakula, hawana dawa na hawana kadi za bima, Serikali iliangularie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe mikopo ya wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu Serikali iangalie kwani inatolewa kwa upendeleo, wale wenye haki ya kupewa hawapewi na kupewa wasiostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba hospitali zina dawa za kutosha kwani ni mara nyingi nimefika Hospitali ya Tumbi kupeleka wagonjwa hakuna hata panadol; niiulize Serikali ni vipi dawa ziwepo na mgonjwa aambiwe hakuna?

Mheshimia Mwenyekiti, nipende kushauri kuhusu *TFDA*, tozo za *TFDA* ni kubwa mno tena kutozwa kwa dola tena hata kwa *product ambazo* ni ndogo. Hii imesababisha wajasiriamali kupata shida sana wanapokwenda kusajili *product zao*. Mfano *beer^{1H}* (20°C) \$ 10 kwa nini kwa dola na si kwa *Tanzanian shillings*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule nyingi hazina vyoo na madarasa ya kutosha. Walimu hawatoshelezi wakati mitaani walimu wamejaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali kuboresha Hospitali ya Milembe iongezewe mgao wa fedha na kuboreshwa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kabla sijaingia upande wa wachangiaji wa Serikali, naagiza neno Guantanamo liondolewe kwenye *hansard* kwa sababu sio neno rasmi la Bunge na linaondosha heshima ya Kanuni zetu, kwa ajili ya kuilenga Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. (*Makofii*)

Tunaendelea Waheshimiwa, sasa upande wa Mawaziri tutaanza na Mheshimiwa Stella Ikupa na baadaye Mheshimiwa Anthony Mavunde ajiandae kwa dakika tano tano.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WALEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote niseme nitajikita zaidi upande wa UKIMWI na

niseme kwamba UKIMWI bado upo kwa hiyo, ni jukumu la kila mtu binafsi kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI kwa kubadili tabia, lakini pia kuendelea kujilinda na zile njia nydingine ambazo zinasababisha maambukizi ya UKIMWI. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja za Kamati, Kamati imeshauri kwamba hii sera ya Taifa ya udhibiti wa maambukizi ya UKIMWI imepitwa na wakati. Niseme kwamba mchakato wa mapitio ya sera hii ulianza kufanyika toka mwaka 2010. Baada ya mapitio haya, iligundulika kwamba kuna upungufu na upungufu huu uliwasilishwa kwenye *Secretariat Cabinet* ambapo katika ile *Secretariat Cabinet* ilishauri kwamba ufanyike uthamini mpya wa utekelezaji wa sera hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi kinachofanyika ni kwamba *TACAIDS* wanaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali ili kuona kwamba sasa lile agizo ambalo lilitolewa la upitiaji upya wa hii sera unafanyika. Kwa kipindi hiki cha mpito, Serikali imeendelea kutekeleza vile vipengele ama ule upungufu ambao ulionekana katika mapitio ya hii sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niongelee suala la ushauri ambao umetolewa na Kamati kwa habari ya vile vyanzo vya Mfuko wa udhamini wa Mfuko wa UKIMWI. Kamati imependekeza kwamba kama ilivyo kwenye *Road Fund*, basi huu Mfuko kuwe kuna tozo ambayo itakuwa inasaidia kutunisha huu mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepokea ushauri huo na tayari utekelezaji umeshaanza kufanyika na naamini kwamba mapendekezo yatakapoletwa kwenye Bunge lako Tukufu basi Waheshimiwa Wabunge wataunga mkono utekelezaji wa hayo mapendekezo ambayo yatakuwa yameletwa kwa habari ya zile tozo ambazo zitakuwa zimependekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali pia imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha udhibiti wa masuala ya UKIMWI. Fedha hizi mpaka kufika mwaka jana Desemba, 2017, kiasi cha shilingi bilioni 1.3 zilikuwa zimekwishatolewa kwa ajili ya kuhakikisha masuala ya UKIMWI yanaenda vizuri. Fedha hizi zimekuwa zikitolewa kupitia Wizara ya Afya ambapo mwaka jana ilitolewa milioni 660 ambayo ilitumika kununulia dawa za *septrine* kwa ajili ya waathirika wa UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la *data* za maambukizi katika nchi yetu ya Tanzania imekuwa ni changamoto. Kuna Mbunge ambaye alichangia mchana akasema kwamba hizi *data* ni za miaka mingi. Niseme kwamba hizi *data* sio za miaka kumi iliyopita kama ambavyo Mbunge amesema, hizi *data* ni za mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maadhimisho ya Siku ya UKIMWI duniani mwaka jana tarehe 1 Desemba hizi ndio *data* ambazo zilitolewa na hiyo ni sambamba na hoja ya Mheshimiwa Mjumbe wa Kamati, Mheshimiwa Masoud kwamba Dodoma sio kweli kama ambavyo iko. Hizi ni *data* ambazo zimetolewa mwaka jana tu Desemba na Dodoma ina maambukizi ya 5.0, sasa hizo za kwako sijui ni za lini lakini kutokana na hizi *data* za mwaka jana Dodoma inaonesha kwamba kiasi cha maambukizi ni 5.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na Mjumbe alichangia kuhusiana na Njombe kwamba Njombe wanaonewa, hizi ni *data* halisi na Njombe inasemekana kwamba maambukizi ni kiasi cha asilimia 11.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ikupa. Tunaendelea na Mheshimiwa Anthony Mavunde na baadaye Mheshimiwa Ndlichako ajiandae.

NAIBU WAZIRI , OFISI YA WAZIRI MKUU (VIJANA, KAZI NA AJIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nitajielekeza katika kupambana na kudhibiti dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo napenda kulizungumza ni suala la bajeti kama ilivyoshauriwa na Kamati. Ni kweli ukiangalia bajeti ya mwaka 2017 na mwaka 2018, bajeti hii ililenga hasa katika muundo wa iliyokuwa Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya. Baada ya mabadiliko ya sheria na hivi sasa kuwa na mamlaka na kufahamu majukumu ya mamlaka, Serikali katika kipindi cha fedha cha mwaka 2018/2019, tutaangalia namna ya kuweza kuongeza bajeti ili iendane na kazi ambazo zinafanywa na mamlaka hasa kwa kuwa tumeshapata uzoefu wa kazi ya mwaka mmoja ambayo mamlaka imefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ya kuhusu Sera ya Taifa ya Dawa za Kulevya. Serikali inatambua umuhimu wa sera ya Taifa ya Dawa za Kulevya na utungwaji wa sera unapitia hasa katika kupata maoni ya wadau na mpaka ninapozungumza hivi sasa, tumeanza na Mikoa ya Kanda ya Ziwa ambapo tayari Mikoa ya Mwanza, Mara, Shinyanga, Kigoma na Geita wamekwishatoa maoni yao. Tunategemea kwamba katika bajeti ya mwaka 2018/2019 fedha zitaongezwa zaidi kuharakisha ukamilishaji utungwaji wa sera hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imekuwepo hoja ya kuwepo chombo cha kisheria kushughulikia udhibiti wa biashara na matumizi ya dawa za kulevya katika ngazi ya Halmashauri kama ilivyo kwa zile Kamati za UKIMWI katika ngazi ya Halmashauri. Kwa mujibu wa kifungu cha 66 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sheria Na. 5 ya mwaka 2015 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2017, sheria hii imeipa mamlaka Tume kufanya kazi na chombo chochote katika kushughulikia matatizo ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, tayari tumeanza mazungumzo chini ya uratibu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, sisi pamoja na TACAIDS kuona namna bora ya kufanya suala hili la uratibu ili Kamati zile zile za UKIMWI katika ngazi ya Halmashauri pia zifanye kazi ya Kamati ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ilikuwepo hoja hapa ya changamoto za upatikanaji wa tiba kwa waathirika wa dawa za kulevy, kwa hivi sasa tunavyo vituo vitano ambavyo vinatoa tiba kwa waraibu wa madawa ya kulevy lakini mpango wetu ni kuongeza vituo vingine vitano mwaka huu wa fedha pale fedha itakapopatikana ili kuwafikia waraibu wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hivi sasa tunakamilisha kituo cha Itega hapa Dodoma na Mwanza ambapo kwa Dodoma tayari tumeshapokea dola milioni 2.5 kutoka *Global Fund* ambayo lengo lake ni ukamilishaji wa kituo hiki ili tuweze kuwafikia vijana wengi zaidi ambao ni waathirika wa dawa za kulevy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali imeongeza ukomo wa uagizaji wa dawa ya *methadone* kutoka kilo 120 mpaka kilo 300 na hii inatokana na mikakati tuliyonayo kama Serikali, hasa katika eneo la *supply reduction*, hali inayosababisha kunakuwa na upungufu mkubwa sana wa dawa za kulevy mtaani na hivyo kuwalazimu waraibu hawa kukimbia katika vituo vya tiba. Hivyo, tumeongeza ukomo wa uagizaji wa dawa ya *methadone* na hivi sasa ninavyozungumza muda wowote dawa hii itaingia kwa ajili ya kuweza kuwashughulikia watu walioathirika na dawa za kulevy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, katika sehemu ya hoja ambazo zilisemwa hapa ni kuwepo kwa unyanyapaa kwa waraibu wa dawa za kulevy. Kwa kulitambua hili, ni kweli wako vijana na watu wazima ambao wameathirika na madawa ya kulevy ambao wakirudi mtaani wanapata

unyanyapaa mkubwa sana na vilevile hali hii inawasababisha pia kurudia kufanya matumizi ya dawa za kulevyaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tumeona hatua ya kwanza ni kuanzisha kituo ambacho tunakiita *occupational therapy* ambacho kitajengwa katika eneo la Itega Dodoma, lengo lake ni kuwapa elimu ya stadi za kazi ya fundi uashi, ufundi seremala, ili akiacha matumizi ya dawa za kulevyaa akirudi mtaani awe ana shughuli ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia limezungumzwa hapa jambo la nyumba za upataji nafuu (*sober houses*), Serikali inaendelea na ujenzi...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU WAZIRI , OFISI YA WAZIRI MKUU (VIJANA, KAZI NA AJIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nichangie katika hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza nianze kwa kuipongeza Kamati kwa taarifa nzuri ambayo wameilwasilisha, lakini pia nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Peter Serukamba, kwa uwasilishaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia fursa hii kuishukuru sana Kamati kwa namna ambavyo tumekuwa tunafanya kazi na kwa ushauri na maelekezo yao. Katika misingi hiyo, nianze tu kwa kusema kwamba Serikali imepokea ushauri ambao umetolewa na Kamati na itaufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza katika mambo machache ambayo yamezungumzwa na Kamati na mengine ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge ambao wamepata nafasi ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kuzungumzia suala la Hospitali ya Taaluma ya Kufundishia Mloganzila. Niseme kwamba Serikali imejenga Hospitali ya kufundishia ya Mloganzila kwa lengo la kuimarisha mafunzo ya fani za afya na tiba katika nchi yetu. Hii ilitokana na dira na malengo ya chuo hicho pamoja na malengo ya Serikali ya kuhakikisha kwamba inakuwa na wataalam wa kutosha, na utaratibu wa kuwa na hospitali ya kufundishia ni utaratibu ambao upo hata katika Mataifa na nchi nyingine za Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilihakikishie Bunge lako kwamba dhamira ya Serikali ya kuwa na Hospitali ya Taaluma ya Kufundishia ya Mloganzila bado iko palepale na Serikali kwa sasa haina mpango wowote kwa sababu ndiyo kwanza hospitali hiyo imekamilika, ni hospitali nzuri ya kisasa na ina uwezo wa kutoa mafunzo na tiba katika fani zote. Kwa hiyo, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kitaendelea na kusimamia hospitali hiyo kama ambavyo kimesimamia katika mchakato wote wa ujenzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia suala la vitabu ambalo limezungumziwa. Ni kweli kama ambavyo nilisema tarehe 15, Mei wakati nahitimisha hotuba, kulikuwa na changamoto ya vitabu na nikaahidi katika Bunge hili kwamba Serikali itaenda kuvifanyia kazi, kuvifanyia mapitio na kuchukua hatua kwa wale waliosababisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kazi ya kufanya mapitio ya vitabu imekamilika na baadhi ya vitabu vilivyorekebishwa viko hapa na viko katika hatua ya uchapaji ili viweze kusambazwa. Pia niwahakikishie Wabunge kwamba Serikali itaendelea kuimarisha Taasisi yetu ya Elimu Tanzania ili iweze kutekeleza vizuri majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba vitabu vyote shulenii vinapatikana vikiwa na ubora unaotakiwa na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na suala ambalo limezungumziwa la kuhusiana na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, kwamba hii taasisi ifutwe kwa sababu inaonekana

kwamba haina tija. Ningependa kusema kwamba Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ilianzishwa kwa Sheria Na. 139 ya Mwaka 1989 na lengo lake kubwa ilikuwa ni kutoa elimu kwa watu ambao hawakuweza kupata mafunzo katika mfumo ambao uko rasmi, lakini pia ina lengo la kutoa mafunzo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu kwamba bado madhumuni ya kuanzisha taasisi hiyo yapo na Serikali itaangalia namna ya kuimarisha na tupo tayari kupokea ushauri na mapendekezo kwa namna ambavyo taasisi hii inaweza ikaimarishwa zaidi ili iendane na mahitaji ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo mdogo wangu, Mheshimiwa Rehema alilizungumzia, kuhusiana na suala la Waraka wa Elimu Bila Malipo na kwamba Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo ambayo yanapingana na Waraka wa Elimu bila malipo. Ningependa tu kumwambia ndugu yangu, Mheshimiwa Rehema, Mwalimu mwenzangu Migila kwamba Serikali hii, kwanza niseme kwamba Waraka Namba Tatu wa Elimu Bila Malipo ni waraka wa Serikali na Kiongozi wa Serikali hii ya Awamu ya Tano ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na ni Rais ambaye ni mfuatiliaji, anajua kila kitu kinachoendelea katika Serikali yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo yote ambayo Mheshimiwa Rais aliyatoa kuhusiana na elimu bila malipo, tarehe 17, Januari, 2018, hakuna hata jambo moja ambalo Mheshimiwa Rais amelisema ambalo linakinzana na Waraka wa Elimu Bila Malipo ambao ni waraka wa Serikali ambayo Kiongozi wake mkubwa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ningependa kumshauri tu dada yangu atafute ile *clip* aisikilize kwa umakini kwa sababu hakuna jambo ambalo Mheshimiwa Rais alilosema ambalo ni kinyume na huo waraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia suala la Chuo Kikuu Huria. Chuo hiki kilianzishwa kwa Sura

344, Sheria Na. 346 na kupata hati idhini mwaka 2007 na madhumuni ya kuanzisha Chuo Kikuu Huria ilikuwa ni kutoa fursa kwa watu ambao hawawezি kwenda kukaa darasani kutokana na majukumu mbalimbali kwenda kusoma kwa kutumia huo mfumo wa masafa au *open and distance learning* bado kuna mahitaji hata sasa ya watu kupata mafunzo kwa kuititia mfumo huo huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Sheria ya Chuo Kikuu Huria iko hapa na majukumu ya Chuo Kikuu Huria yameainishwa vizuri na Serikali haina mpango wowote wa kufuta hicho Chuo Kikuu Huria kwa sababu inaona kwamba yale majukumu bado yanahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Serikali imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kuimarisha miundombinu katika Sekta ya Elimu. Tumeendelea kuboresha shule zetu kongwe, nafikiri Waheshimiwa Wabunge mnaona katika maeneo yenu shule mbalimbali tumezifanyia ukarabati. Ukienda Ifakara, ukienda *Musoma Technical*, ukienda Ifunda, ukienda Kondoa, Masasi, *Tabora Girls*, Ihungo huko watani wangu hawa akina Mheshimiwa Mwijage wananiambia Mheshimiwa hii sio sekondari, wananiambia hii ni *University of Ihungo* kwa sababu imejengwa kwa uimara ambao uko vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea pia kuimarisha miundombinu katika vyuo vya ualimu, tunafanya ukarabati katika Chuo cha Ualimu Tandala, Chuo cha Ualimu Nachingwea, Tarime, Kinampanda, Mandaka, Patandi na Ilonga. Vilevile...

MJUMBE FULANI: (*Hapa aliongea bila kutumia kipaza sauti*)

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Hata Tarime kwako tumefika tu, sisi hatuna ubaguzi, Serikali hii inawatumikia wananchi wote hata kama ni jimbo la Upinzani tunatumikia. Kwa hiyo tupo Tarime tunafanya hiyo kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme kwamba tunaendelea na ujenzi katika vyuo vyetu vya ualimu ambavyo ni pamoja na Chuo cha Ualimu cha Ndala, Chuo cha Ualimu cha Mpuguso pamoja na Chuo cha Ualimu cha Shinyanga ambapo majengo ya kisasa; madarasa, mabweni, maabara, kumbi za mihadhara, inaendelea kufanyiwa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika vyuo vikuu tunafahamu kwamba bweni namba mbili na namba tano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam lilikuwa limekuwa na uchakavu mkubwa mpaka lilikuwa haliwezi kutumika, Serikali hii ya Awamu ya Tano tayari imekwishaanza kulifanyia ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Chuo cha Elimu cha Mkwawa tunaendelea na ujenzi, tunakamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara ambao utaweza kuweka wanafunzi 1,200 kwa wakati mmoja, lakini pia tumewapatia shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kujenga maabara ya *chemistry*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaendelea na ujenzi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Maktaba ambayo ina uwezo wa kuweka wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, nataka kusema tu kwamba Serikali inaendelea na jitihada katika kuboresha miundombinu katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la shule binafsi, wachangiaji mbalimbali wamezungumza na kuna wengine wamesema kwamba Serikali inaziingilia hizi shule. Naomba niseme tu kwamba hizi shule zipo kwa mujibu wa sheria na Wizara ya Elimu ndiyo msimamizi wa sheria za elimu, kwa hiyo, niombe tu kwamba wamiliki wa shule binafsi wanafahamu sheria na walipewa nyaraka, walipewa miongozo wakati wanasajili shule zao wahakikishe kwamba wanaendesha shule kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitakuwa ni kitu cha ajabu kwamba Serikali iache tu, kwamba kwa sababu ni shule

binafsi wakati Serikali ndiyo imepewa dhamana ya kusimamia elimu ikiwa ni pamoja na shule binafsi. Kwa hiyo niseme kwenye suala la kukaririsha na suala la kufukuza wanafunzi kimsingi hivi vitu vinaongozwa na nyaraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka wa Elimu Na. 7 wa Mwaka 2004 ulikataza suala la kukaririsha wanafunzi au kuwafukuza wanafunzi kwa sababu hawajafikisha alama ambazo zimewekwa na shule na mitihani inayotungwa hakuna mtu ambaye anaikagua kuona kwamba ina kiwango gani lakini pia hata usahihishaji hakuna mtu ambaye anauangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Waraka Na. 12 wa Mwaka 2011 ukawa umeweka utaratibu kama kuna haja ya wanafunzi kukariri basi kuna utaratibu ambao unatakiwa kufuatwa. Kilicho jitokeza, wakati shule zimeanza mwaka huu, 2018, kulikuwepo na wimbi kubwa la wanafunzi ambao walikuwa wanafukuzwa shulenii kwa sababu shule zinadai kwamba hawajafikisha zile alama na hawa wanafunzi waliokuwa wanafukuzwa ni wanafunzi ambao wako katika miaka ya mitihani; wanafunzi wa *primary* wa dasara la saba na wanafunzi wa sekondari wa kidato cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo shule ambazo shule moja ilikuwa imediriki kufukuza wanafunzi 114, shule moja inafukuza wanafunzi 35, shule moja inafukuza wanafunzi 25, hawa wanafunzi wanapokuwa wanafukuzwa kwa wingi namna hiyo wanajua kwamba wana Serikali yao na wazazi wamekuwa wanakuja kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukianza kuangalia, hivi shule moja inafukuza wanafunzi 114 kwa mkupuo kwa kigezo kwamba hawajafikisha alama. Je, tatizo ni wanafunzi au Walimu? Kwa hiyo Serikali inaliangalia hilo jambo na tunashirikiana na shule binafsi, na wenyewe wameelewa na tutaendelea kuangalia kama kuna haja ya kupitia huu waraka wa kukariri basi tutafanya katika njia shirkishi, lakini suala la kuwafukuza wanafunzi nadhani ni suala ambalo halikubaliki. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ndalichako.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ummey Mwalimu baadaye Mheshimiwa Harrison Mwakyembe ajilandae.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa ushauri wao mzuri kuhusu utendaji kazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua hii niseme kwamba tumepokea ushauri na maoni ya Kamati yote yaliyotolewa na niahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba tutayazingatia kwa sababu lengo la ushauri ambao umetolewa ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, namba mbili, tumepokea pongezi za Kamati kuhusu kazi nzuri inayofanywa na taasisi zetu kama walivyoona; *TFDA, MSD, MOI, M NH na JKCI* na kupitia hatua hii niahidi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kuchukua jitihada hasa za kuimarisha upatikanaji wa huduma za matibabu ya kibingwa, matibabu bobezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Taasisi yetu ya Moyo ya Jakaya Kikwete wameendelea kufanya kazi nzuri ya kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi kutoka rufaa za wagonjwa 89 mwaka 2016 hadi wagonjwa wawili tu kwa mwaka 2017. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ya kazi hii nzuri ambayo wanafanya taasisi zetu sio kwamba tu Serikali

itapunguza gharama na kuokoa fedha, lakini maana yake Watanzania wote maskini au tajiri ana *accessibility* ya kupata huduma za matibabu bobezi, kwa hiyo ni suala la usawa kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge pia kwa kutambua kazi ya Muhimbili, bahati mbaya kwamba ile *CT Scan* ni siku mbili lakini inafanya kazi nzuri na tutambue kwamba Muhimbili wanafanya mabadiliko makubwa ya kutoa huduma za kibingwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimwambie Mheshimiwa Mt Olea tu kwamba tunafunga *CT Scan* kwenye Taasisi yetu ya Mifupa ya *MOI* kwa hiyo itakuwa ni *backup*, pale *CT Scan* ya Muhimbili itakapoharibika, basi ya *MOI* itafanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa nijikite katika maoni yaliyotolewa na Kamati, kama nilivyo sema ni mengi, lakini nizungumze mambo makubwa matano. Jambo la kwanza, ni kuhusu hali ya upatikanaji wa dawa. Tunashukuru Kamati kwa kuona jitihada ambazo zimefanyika ndani ya Serikali na tunakubali kwamba bado zipo changamoto chache katika upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme, changamoto kubwa ya upatikanaji wa dawa ilikuwa inachangiwa na upatikanaji wa fedha, hakukuwa na fedha za dawa. Sasa hivi fedha za dawa zipo katika halmashauri zetu, zipo katika zahanati zetu, zipo katika vituo vya afya na zipo katika hospitali zetu za rufaa za mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Lubeleje changamoto ambayo tunayo, ukiangalia *stock level* ya *MSD* na lingine ambalo nilitolee ufanuzi, hatuwezi kuangalia upatikanaji wa dawa zote, tunaangalia zile dawa muhimu (*essential medicine*) ambazo ziko 135, na kwa mujibu wa taarifa ya *MSD* dawa hizi zinapatikana zaidi ya asilimia 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyokuwepo ni suala la mfumo wa ugavi na usambazaji wa dawa. Nitoe mfano, katika maoteo ambayo tumeyapokea kutoka kwenye halmashauri inaonekana kwamba tunahitaji nchi nzima *paracetamol* kopo 7,000 lakini kiuhalisia tunauza *paracetamol* kopo moja yenyewe vidonge 1,000 kopo 16,000, kwa hiyo, huu ni mfumo ule ambaa wa maoteo kutoka halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa ya *amoxicillin*, kwa mujibu wa maoteo ambayo tumeyapata kutoka halmashauri, inaonekana kwamba tunahitaji kopo 6,500 lakini kiuhalisia tunauza kopo 19,000. Kwa hiyo, niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge na Kamati tutaendelea kuzihimiza halmashauri kuleta maoteo halisi ya dawa ambazo zinahitajika katika halmashauri zao na kuleta maoteo hayo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo tutalifanya, tumepata ufadhilli, tumenunua magari zaidi ya 180 ambayo yatatumika kusambaza dawa katika sehemu mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kubwa, tumezindua mfumo *Standard Treatment Guideline*, mwongozo wa matbabu na orodha ya dawa muhimu. Kwa sababu saa nyingine hali ya upatikanaji wa dawa unachangiwa pia na *prescription*, daktari anaandika dawa ambayo haipo kwenye mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swalii la kaka yangu anayesema kuna dawa za China, dawa za India, dawa za UK, Tanzania tunatumia *generic medicine*, tunatumia dawa ambazo ni *generic* na zimepitishwa na WHO. Kwa hiyo, saa nyingine mgonjwa anaenda pale anataka dawa ambayo anaitaka yeze haipo katika mwongozo. Kwa hiyo, tutaendelea kutoa mafunzo kwa watoa huduma za afya, hasa Waganga na Madaktari, kuhusu kuzingatia mwongozo wa matumizi ya dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *NHIF*, niseme kwamba tumepokea pia ushauri wa Kamati kwamba tuharakishe mchakato wa kuleta Bungeni sheria itakayomlazimisha kila Mtanzania kuwa na bima ya afya. Nakubaliana na Kamati kwamba ni kweli ni Watanzania wachache ambao wako katika bima ya afya, *NHIF* kuna Watanzania milioni 3.3 sawa na asilimia saba, *CHF* ni asilimia 11.7 na bima za afya binafsi ni asilimia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika Watanzania 100 ni Watanzania 32 tundio wanapata huduma za matibabu bila kutoa fedha *cash*, maana yake wanapata changamoto katika kupata huduma, lakini pia mtu anayetumia papo kwa papo analipa zaidi kuliko mtu mwenye kadi ya bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niithibitishie Kamati ya Bunge kwamba, Serikali tayari tumeshapata uzoefu wa nchi mbalimbali, *WHO* wametusaidia, *World Bank* wametusaidia, tunajua kipi kimefanya kazi Rwanda kipi hakijafanya kazi Ghana, lakini tunakubali kwamba tutaenda kutembelea, lakini kabla ya kwenda kutembelea nchi hizo tunapanga kuitisha semina ya wadau ili waone Ghana wamefanya vipi, Rwanda wamefanya vipi, *Philippines* wamefanya vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali ni kwamba bima ya afya ndiyo mwelekeo, ndiyo mhimili wa kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa Watanzania...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Hiyo sio ya kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuwa ya kwangu.

WABUNGE FULANI: Wewe ongea, ndiyo sio ya kwako.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la afya ya uzazi na mtoto ni suala la kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Nne na niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge suala la kutoa elimu ya uzazi hasa kwa wasichana tumelipa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana tulikuwa na kikao mimi na Waziri wa Elimu na Waziri wa TAMISEMI, tumeamua kwamba tutaangalia mitaala kuhusu masuala ya afya ya uzazi ili watoto wetu waweze kujua maumbo yao na waweze kujikinga na magonjwa. Vile vile tumeongelea suala la kuwa na Walimu walezi katika shule zetu na tayari pia mwongozo wa kuwafundisha Walimu unaangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo pia tunalfanya katika huduma ya afya ya uzazi ni kwamba Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za uzazi za dharura na nithibitishie Serikali ni moja, Wizara ya afya tutatafuta fedha lakini fedha hizi sisi tutazipeleka TAMISEMI na ndio maana tumepata fedha kwa ajili ya kuboresha vituo vya afya 100 katika Halmashauri mbalimbali. Tumepata fedha kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya vituo 100, Ubalozi wa Denimark wametupa fedha kwa ajili ya vituo vya afya 39 na *basket fund* tumepata fedha kwa ajili ya vituo 19. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme Wizara ya Afya haitajenga vituo vya Afya au Zahanati, kazi hiyo ni ya TAMISEMI sisi tunaingia katika suala la kuimarisha ubora wa huduma na hasa katika kuimarisha huduma ya afya ya mama na mtoto. Kwa hiyo, hela sisi tutazipeleka TAMISEMI lakini tunafanya vizuri na Mheshimiwa Jaffo, vituo vyote vya afya wanakaa wataalam wetu kwa pamoja na wanasesma fedha hizi tuzipeleke wapi na hizi tuzipeleke wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fedha za *WDF* ni kwamba Hazina tumeshafanya majadaliano lakini niwaimize Waheshimiwa kwamba suala la kuwawezesha wanawake kiuchumi ziko kwa kiasi kikubwa ni ile asilimia tano ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vitambulisho kwa wazee, niseme kwamba tumefanya kazi na tumewatambua wazee takribani milioni 1,600,000 na wazee takribani laki 462 tumeshawapa vitambulisho. Ufafanuzi vitambulisho hivi havitolewi na Wizara ya Afya. Vinatolewa na Halmashauri na kuna Halmashauri zinafanya vizuri; Kigamponi, Msalala, Ubungo, Ikwiriri nitumie fursa hii kuwataka Wakurugenzi wote kuhakikisha wanawapa wazee vitambulisho vyta matibabu bure. Pia niweke wazi hii ni hatua ya mpito lengo letu ni wazee wote kupata Bima za Afya pale ambapo tutaanza Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea malalamiko kuna baadhi ya Halmashauri zina waambia wazee wachangie hela ya picha Sh.1,000. Tukimgundua Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo anawachaji wazee kwa ajili ya kitambulisho cha matibabu bure tutapeleka jina lake kwa Mheshimiwa Rais iliaweze kuchukua hatua. Hatutakubali wazee wetu kudhalilishwa kunyanyaswa na sisi sote ni wazee watarajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni *human resource for health* watumishi katika Sekta ya Afya tunakubali kwamba changamoto ipo lakini tayari Serikali imeanza hatua tumeajiri mwaka huu watumishi takribani 3,152 na tumewasambaza katika vituo mbalimbali. Naamini kwamba na Waziri wa Utumishi ananisikia lengo letu ni kuhakikisha kwamba hakuna kituo au zahanati ambayo itaongozwa na mhudumu wa afya au mtu ambaye hana sifa. Tunataka Kama zahanati lazima awe ni *Clinical of Assistant* au *Clinical Officer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hili suala la watumishi dada yangu Benardetha Mushashu kuhusu hospitali za rufaa za mikoa na dada yangu Nuru Bafadhili kuhusu hospitali ya rufaa ya Bombo Mheshimiwa Rais ametukabidhi kuziendesha hospitali za rufaa za Mikoa tumesha-*identify*, tumeshachambua, tunafundisha Madaktari Bingwa katika fani saba za kipaumbele na Daktari Bingwa wa akinamama na magonjwa ya wanawake ya uzazi, Daktari Bingwa wa

watoto, Daktari Bingwa wa upasuaji, Daktari Bingwa wa usingizi na Wanadiolojia wa mionzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeshapata fedha kutoka *Global Fund* na tunaanza mwaka huu kucomesha zaidi ya madaktari 150, tunawachukua ndani ya Serikali kwa sababu ina kuwa rahisi baada ya kumaliza kurudi kufanya kazi katika mazingira haya, lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ummy, nimekuongezea muda mrefu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mwisho niseme kwenye watumishi tunategemea kuwa na *Community Health Workers* hawa wataweza pia kuimarisha masuala ya lishe na masuala ya uzazi wa mpango. Kwa hiyo, tunategemea kuwa nao wawili kila kijiji na tayari Mheshimiwa Mkuchika anakaribia kumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ummy. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Harison Mwakyembe na baadaye Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ajiandae.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA
MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nianze kwa kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Peter Serukamba na Makamu wake Mheshimiwa Mussa Zungu na Wajumbe wote kwa kweli kwa taarifa nzuri iliyokwenda shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie machache tu kwa uafanuzi. Suala la kwanza Kamati inasema sheria ya Baraza

Ia Michezo na *BMT* ina upungufu mwingu kwa kweli unaokwamisha utendaji wa baraza. Nakubaliana kabisa na Kamati kwa kweli sheria ni ya siku nyingi sana ya mwaka 1967 miaka 51 iliyopita, najua ilishafanyiwa marekebisho mwaka 71 lakini bado ni miaka 47 iliyopita na tumeshaanza hiyo kazi nzuri ya kuifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu yake ya wataalam kwa kukaa na wataalam wangu wa Wizara kuifanyia *first drafting* hii ya hii sheria na mtaiona baada ya muda si mrefu mbele yenu hapa Waheshimiwa wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la uboreshaji wa *TBC* limeongelewa na Kamati na vilevile Mheshimiwa Amina Moleli naye ameingolea na amezungumzia kuhusu vifaa kwamba vimechoka ye ye anaongelea *studio* mle ndani sawa. Hata hivyo, nataka tu kusema kwamba Serikali inalijua hilo na tumeanza kulifanyia kazi vizuri kabisa sisi hatujaanza kwa mwonekano wa ndani kwa sababu unaweza ukawa na makochi mazuri, lakini kwa kweli huko chumbani kuna matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi tumeanza na mitambo kuboresha usikivu na vile mwonekano wa *TBC*. Leo hii najua wote nyie mtakuwa mashahidi wangu kwamba mwonekano wa *TBC* wa picha umeongezeka tena kitaalam wanasema umeongezeka toka asilimia 52 hadi asilimia 88 na yote ni kwa ajili ya ukarabati wa mitambo ambayo inasaidia urushaji wa matangazo. Hata *radio* za *TBC FM* na *TBC Taifa* nazo usikivu wake umeongezeka toka asilimia 60 mpaka asilimia 90 na hiyo yote ni kwa ajili ya ukarabati tunaoufanya wa mitambo yake.

Ukifika pale Mikocheni kuna dude kubwa pale tunaita *Satellite uplink* ilikuwa wakati huo miaka miwili iliyopita ilikuwa na njia moja tu ambayo tulikuwa tunashindwa kuikarabati, lakini leo zote njia mbili zinafanya kazi na ndiyo maana mwonekano wa *TBC* umekuwa mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo hoja ya kwamba *BASATA* iko mbali na wasanii, kwa kweli hapana, si kweli. Nitatoa mifano michache, *BASATA* huwa inatoa ushauri *consultancy* kwa wasanii wetu na nitoe mfano mdogo tu wa mwaka jana kuanzia mwezi Julai hadi mwezi Desemba, wasanii 995 wamefika *BASATA* kupewa ushauri kuhusu kazi yao ya sanaa. Sasa kama hauna mawasiliano mazuri watu 995 katika miezi minne mitano wakafika isingetokea kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu tukumbuke kwamba pia vijana wetu wengi siku hizi wanaalikwa nje ya nchi kwa ajili ya muziki na ni *BASATA* inayohangaika kuwapeleka Balozini kuwatambulisha wapate *VISA*. Kwa kweli mnyonge mnyongeeni, haki yake tumpe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa tasnia ya filamu, nakubaliana kabisa na maoni ya Kamati lakin nataka kwamba kama tasnia kwenye sanaa imepiga hatua kubwa sana katika kipindi kifupi ni tasnia ya filamu ambapo leo hii, nadhani sisi ni wa pili kwa Nigeria hata kwa uzalishaji wa filamu kwa mwaka tunazalisha kwa wastani filamu 1,400 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa kuna suala la ubora wa filamu zetu kweli zipo zingine hazifurahishi kabisa, lakin katika hizo 1,400 bora zimejitokeza na ndiyo maana leo hii Tanzania tunajivunia tuzo za kimataifa zaidi ya 44 za waigizaji wetu waandaaji wa filamu na kadhalika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ndiyo maana leo hii hata wawekezaji wamejitokeza sasa kwa ajili ya filamu *industry*. Leo tunawapongeza sana *AZAM TV* kwa kuanzisha *a dedicated Channel* kwa ajili ya sinema zetu za Kiswahili inaitwa *Sinema Zetu* za Kiswahili. Si hao tu wenzetu *multichoice* na wameanzisha *a dedicated Channel* kwa ajili ya sinema za Kiswahili na sasa hivi tuna *TV* mpya imeanzhishwa *Jasson TV* ni kwa ajili ya sinema za Kiswahili. Yote haya ni mafanikio yalikuwa hayapo haya ndio yameanza kujitokeza na hii ni ushahidi mkubwa kwamba tasnia ya filamu nchini inaendelea kwa kasi kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka na muda naomba nigosie mambo mawili matatu ambayo Mheshimiwa Devotha Minja ameongelea kuhusu vyombo vyahabari. Ameongelea kuhusu maelezo wamemwandikia Tanzania daima barua kwa nini uchaguzi wa Kinondoni wanaandika upande mmoja. Anasema kama wana haki kwa nini hawajawaandikia Uhuru, nimecheka nimewambia Mheshimiwa Minja ilitaka nao Uhuru wakuletee hiyo barua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua huo ni ushahidi tosha kwamba hata waliokuletea barua hawana weledi, *there are not professionals* huwezi ukaandikiwa barua na Taasisi ya Serikali na Idara. Badala ya kuwasiliana nao wewe unapeleka kwa Mbunge ni kukosa weledi tu, Uhuru hawawezi kufanya hivyo au gazeti la maana kama Mtanzania na mengine wakakuletea wewe Mbunge hapa barua ambayo ilitakiwa wewe uwajibu, sijui hawajui kujibu wamekuomba wewe uwajibie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Minja anasema Waziri nina mamlaka gani chini ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 kuweza kuadhibu...

TAARIFA

MHE. ANTHONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa taarifa.

MHE. ANTHONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Dokta Mwakyembe rafiki yangu sana taarifa, kwamba katika Bunge hili sisi Wabunge tunawakilisha watu, tunawakilisha vyombo, wanakuja kwetu wanatueleza matatizo yao ndiyo tunayaeleza hapa kila siku. Sasa nitashanga sana kama mtu aliyebolea kwenye sheria kama Mheshimiwa Dokta Mwakyembe ataona ni vibaya mtu ambaye amepata kadha mahali, kuja kwa Mbunge na kueleza matatizo yake ili yasemwe hapa kwenye nyumba yao. Naomba nimpe hiyo taarifa (*Makof*).

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, inanishangaza, namheshimu sana Mheshimiwa Komu, lakini nashangaa leo anaongea utafikiri yeye haelewi, *etiquette* ya uandishi wa habari kutoka Serikali na kwako basi uwajibie, endelea kuwajibia tu, hongera na utafanikiwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la Waziri kufungia magazeti sio mimi tu, lakini sheria ya mwaka 2016 iko wazi kabisa, akisoma kifungu cha 59 naomba ukaisome, sijui kama umeisoma, kasome vizuri itaelewa. Ni kweli kabisa pengine nitumie dakika chache zilizobaki kwamba tulipotunga hii sheria lengo letu kubwa ni kuanzisha vyombo vy ya habari ambavyo ni *self regulatory*, vinaweza vikajidhidesha wenyewe, vikajidhibiti vyenyewe na vitajidhibiti kuititia vyombo vikuu vinne. Hili nimelisema mara nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo hivi ni:-

(i) Baraza Huru la Wanahabari, *Independent Media Council*;

(ii) Bodi ya Ithibati;

(iii) Kamati ya malalamiko ambayo tena chini ya sheria hiyo ina madaraka kabisa kama ya Mahakama *is a Quasi judicial Body*; na

(iv) Mfuko wa sanaa vyombo hivi havijaweza kuundwa kwa sababu ya kipengele ambacho nyie wenyewe Waheshimiwa Wabunge akiwemo la Mheshimiwa Minja kulalamika kwamba hatuwezi kumwadhibu Mwandishi wa Habari moja moja kwa sababu hata weledi bado hawana. Kwa hiyo tuwape kipindi cha miaka mitanowaweze sasa *meet requirements* za hii sheria za kuwa na Diploma au *Degree* kuweza kuwa Mwandishi wa Habari kuweza kutambuliwa kwamba hii ni taaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuko katika kipindi hicho cha mpito hatuwezi kufanya chochote. Ningetegemea Mheshimiwa Minja kama una uchungu kabisa wa hii tasinia, hebu njoo tuweze kuondoa hicho kipengele cha *transition* ili tuweze kuunda hivi vyombo, nitakuelewa vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Dkt Harrison Mwakyembe. Tunamalizia sasa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, karibu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea lakini kwa sababu ndio nafungua mdomo wangu kwa mara ya kwanza katika Bunge hili Tukufu, basi nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai. Nimshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kunitfea kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika Mwenyekiti na Wenyeviti wote. Naomba kuwashukuru na kuwapongeza Wabunge wote na hata Watanzania wote ambao wako nyuma yetu (*Makof*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuchangia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii yalizuka masuala kama mawili hivi matatu ya kisheria yaliyohitaji ufanuzi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Swali la kwanza lilitoka kwa Mheshimiwa Abdallah Mtale aliyependa kufahamu uhalali wa Mheshimiwa Rais kumpatia msamaha Nguza Viking maarufu kama Babu Seya pamoja na Johnson Nguza maarufu kama Papii Kocha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa msamaha kwa wafungwa upo kwa namna mbili kisheria; namna ya kwanza ni msamaha wa Rais ambao unatolewa chini ya Ibara ya 45 ya Katiba. Hata hivyo, nieleze hii inaitwa *prerogative of mercy*

ni kama Kiswahili chake nimeshindwa kukipata kwa haraka, lakini ni kama mamlaka ya kutoa msamaha au huruma. Sasa mamlaka haya yanaongozwa na sheria itwayo *Presidential Affairs Act* na kifungu husika ni kifungu cha tatu (3) (*Makof*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ya pili ya utoaji wa msamaha ni kupitia Bodi ya *Parole* huu unaitwa msamaha wa *Parole*. Aina hii inaongozwa na sheria itwayo *The Parole Boards Act* na kifungu husika ni kifungu cha nne (4) cha sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msamaha uliotolewa na Mheshimiwa Rais kwa Nguza Viking pamoja na Jonson Nguza...

TAARIFA

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

WABUNGE: Wewee!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtalea naomba ukae, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu malizia, subiri amalize, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu endelea.

MHE. MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, msamaha uliotolewa kwa wahusika hao ni ule wa aina ya kwanza na ambao unaongozwa na hiyo sheria niliyoitaja ya *Presidential Affairs Act*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, palikuwa pia na maswali kutoka kwa Mheshimiwa Suzan Lyimo ni maswali mawili. La kwanza, aliuliza kama ni halali na inakubaliwa kisheria kwa Serikali kukata rufaa dhidi ya uamuzi kuhusiana na Sheria ya Ndoa baada ya miaka miwili kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwamba kwa Serikali kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya kesi hiyo je,

inakubaliana na ndoa za utotoni. Kesi aliyokuwa anaizungumzia ni *miscellaneous civil cause No. 5 ya 2016*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza kama ni halali kukata rufaa baada ya miaka miwili kupita ni suala la *procedure* na kwa vyovyyote vile swali hili linaweza likajitokeza rufaa itakapokuwa inasikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ndiyo hilo kwamba kwa Serikali kukata rufaa dhidi ya kesi hiyo inakubaliana na ndoa za utotoni. Ni wazi Serikali ilivyokata rufaa imetoa sababu na sababu hizi zitakuwa ni sehemu ya vitu vinavyobishaniwa ile rufaa itakapoanza kusikilizwa. Kanuni ya 64(1)(c) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inakataza kuzungumzia jambo lolote linalosubiri uamuzi wa Mahakama na kwa hiyo hatuwezi kulizungumzia hapa. Ahsante sana (*Makofii*).

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu. Sasa tunamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ili aweze kuhitimisha hoja yake. Mheshimiwa Peter Serukamba karibu ili uweze kuhitimisha hoja yako.

MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nimesimama mbele ya Bunge lako Tukufu niweze kutoa baadhi ya maelezo na niweze kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, Wabunge waliochangia humu ndani kwa kuongea ni Wabunge 21 na Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Wabunge 15. Nawashukuru sana mmeefanya kazi kubwa ya kusaidia kuboresha *report* yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo makubwa yaliyoongeleva nitaomba nianze kwa sababu tuna Wizara tatu nitaanza na suala la Wizara ya Elimu:-

*Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ina Utatu Mtakatifu, elimu ina mambo makubwa matatu:- (**Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge**)*

- (1) Mitaala
- (2) Ubora wa Elimu (*quality assurance*)
- (3) Examiner (Mtahiniwa mwenyewe)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiwasikiliza Wabunge wote...

TAARIFA

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini, Mwenyekiti ana *windup* naomba umuache.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti taarifa fupi tu ya kiimani.

MWENYEKITI: Hapana Mheshimiwa Selasini naomba ukae muache Mheshimiwa Mwenyekiti aendelee.

MHE. PETER J. SERUKAMBA- MWENYEKITI KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu kila Wabunge waliochangia hapa ndani wameeleza matatizo tulionayo kwenye elimu na sisi kwenye Kamati tumeeleza baadhi ya mambo ambayo tunayaona yapo kwenye elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa mitaala maana yake huko utaongelea Walimu, majengo, vitabu, vifaa vya kufundishia, muda wa kusoma na wanafunzi wenyewe. Pia kwenye *quality assurance* ni suala la ukaguzi na baadaye tunakuja Baraza la mitihani ambalo kazi yake ni kutunga na kusahihisha mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeanza na hili? Nimeanza na hili kwa sababu kwenye ripoti yetu tumeonesha hali ya ufaulu nchini Tanzania. Ukiangalia hali ya ufaulu kwa Tanzania kuanzia mwaka 2013, *division one* ilikuwa ni asilimia 2.8; mwaka 2014, *division one* ilikuwa asilimia 4.2; mwaka 2015; asilimia 3.0; 2016, asilimia 3.7; na 2017, asilimia 3.5. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *division two* tulianza na asilimia 8.0; tukaja asilimia 14; tukaja 11 au 12 na sasa ni 14.9. Kwa hiyo, unachokiona kwa miaka hii yote, watoto wetu wanafaulu kwa *division one* mpaka *three* hawajawahi kuzidi asilimia 30.

Waheshimiwa Wabunge kwangu mimi hili ni kubwa sana, tunafanya nini sasa kama Taifa? Huko nyuma tulitoa maelezo sasa tuna shule za binafsi, tuna shule za Serikali. Kuna watu wamechangia hapa ukiangalia matokeo ya mwaka huu shule za Serikali katika shule 100 ni shule nne, naimi nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuleta elimu bure. Ameamua, ni uamuzi mkubwa kuleta elimu bure maana yake wazazi wa Tanzania wamepewa uchaguzi, wamepewa *choice*. Ukiwa mzazi una watoto wako, upande mmoja Serikali inasema zaa unavyoweza tutakusomeshea mpaka darasa la 12, upande mwingine una watoto wako unaweza ukasema mimi watoto wangu kwenye bure siendi nakwenda kuwasomesha kwa kuwalipia, ni *choice* Watanzania wamepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi Kamati tunataka tuiombe Wizara ya elimu, Wizara ya Elimu inaboresha shule zake ni jambo jema sana. Sasa kwa wale ambao wameamua wao wenyewe, kwa mapenzi yao kuwapeleka watoto wao kwenye shule za *private*, wakifika pale wanasantishwa mikataba kwamba bwana wewe umemleta mtoto wako hapa, masharti yetu sisi ni haya, mtoto wako asipofaulu kwa kiwango hiki hapandi darasa, lazima alipe *school fees* kiasi hiki. Sasa anakuja mtoto, wazazi watoto wake amefukuzwa tunakimbilia Wizara ya elimu kuomba msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani Wizara ya Elimu ingesema "Mzee mtoto wako amefukuzwa? Eeeh!, Lakini mbona tuna shule za bure kwa nini usimpeleke kwenye shule za bure?" *Why tunataka tuwa-punish* hawa wenyewe shule? Mtanisamehe kwa wale ambao walisoma *seminary* mimi nilisoma *seminary*. *Seminary* sisii tulianza 58, waliomaliza *form four* ni watu 23, maana yake ni nini? Ni *choice*, hujapata asilimia 50 hupandi darasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie upande mwingine wa shilingi, wale ambao wanawasimamia hawa watoto ili wasome kwa bidii ndiyo hizi *division one* tunazoziona za asilimia tatu. Naomba Serikali hili tulitafakari kwa kina, naamini shule hizi zinasaidia Taifa letu. Sasa Serikali ifanye nini? *I-set standard*, ifanye *monitoring*, na ifanye *followup*, lakini Serikali isianze ku-supervise process ya hizi shule. Serikali ijishughulishe zaidi kwenye shule za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi ambao wana umri wa miaka 40 kwenda juu, zamani ilikuwa usipofaulu kwenda shule ya sekondari unarudia ili uende ukasome shule ya Serikali kwa sababu shule za Serikali zilikuwa zinafanya vizuri. Zamani mtoto kwenda shule ya *private* ulikuwa unacheckwa kijijini kwamba wewe huna akili, lakini hali imebadilika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali ni muhimu sana kwenye suala la elimu mfanye *consultations* na hao wenyewe shule ili kutatua matatizo badala ya kutunishiana misuli ya kuandika waraka kama barua. Nataka niiombe sana Serikali kwenye jambo hili walisimamie vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tumelisema kwenye Kamati yetu, Baraza la Mitihani kila mwaka wakimaliza kusahihisha mitihani wanaandika ripoti ya watoto walivyofaulu na kila somo. Niiombe sana Wizara ya Elimu na Wizara ya TAMISEMI, ripoti hizi zikisambazwa kwenda kwenye Halmashauri zetu mhakikishe zinasimamiwa

zinakwenda kwa kila Mwalimu Mkuu ili aangalie hali kwa nini watoto ili mwaka ujao tuongeze idadi ya watoto waliofaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichopo ripoti zile kila mwaka zinaandikwa tuna-*shelf*kwa sababu ukienda mwaka ujao, matatizo yaliyosemwa mwaka huu, mwaka kesho yanasesemwa hayo hayo. Niiombe sana Serikali hasa Idara ya Ukaguzi, wanaosimamia *quality assurance report* hizi ni muhimu sana ili mwaka ujao tujue tunafanya *effort* wapi ili watoto wetu waweze kufaulu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tumelisema kwenye Wizara ya Elimu; narudia tena tulilisema mwaka jana na mwaka huu tumelisema, naombeni sabna Serikali mlitafakari. Umefika wakati watoto wetu wanaofanya vizuri sana darasani Mataifa yote yanatoa *scholarship*; Kenya kuna *President Kenyatta awards*, ukienda Uganda ipo, ukienda Rwanda ipo kwa nini Tanzania nchi kubwa na uwezo wetu wote huu hatuna *Presidential awards?* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya kuwa na *Presidential awards* unawafanya watoto wasome kwa bidii wakijua kwamba nikipata *point three, point nne, point tano* Serikali yangu itanisomesha na wenzetu wamekwenda mbali zaidi, ukienda hizo *Tiger countries*; China, Malaysia, Singapore watoto wote waliofanya vizuri sana wanapelekwa kwenye *Western countries*, kwenye *heavy league universities*, maana yake ni nini kule watakwendwa kupata *degree*, watakwendwa kujifunza na *culture*, wakirudi wanakuwa ni vijana, lakini hata wasiporudi hawa atafanya *remittance* nyumbani kwao. (*Makof*)

Mhesimiwa Mwenyekiti, mtoto aliymaliza *degree Harvard* akapata kazi *Wall-street* ni uhakika kama ni mtoto wa Kalinzi kijijini kwetu atajenga nyumba kijijini hata akiwa *Harvard*. Niwaombe sana Serikali mlitafakari angalau tuanze na watoto hata 100 huko nyuma ilikuwepo, kumetokea nini mwaka huu tumeamua kuiondoa? Baada ya kazi hii nzuri, Rais Magufuli anasomesha bure, nina hakika Serikali

mkimuambia hawesi kuacha kuweka *Presidential awards* kwa watoto walifanya vizuri sana *regardless* ni mtoto wa tajiri ama ni mtoto wa maskini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *MSD*; Waziri amesema kuhusu *MSD* wanafanya kazi nzuri sana, ningeomba suala la *MSD*, sasa kazi imekuwa kubwa. Kwenye zile hospitali ambazo hasa Muhimbili na hospitali hizi kubwa za rufaa waachiwe wanunue madawa wenyewe ili *MSD* wahangaike zaidi na hospitali za Mikoa, za Wilaya na zahanati mpaka kwenye vituo vya afya, nina uhakika wakifanya hivyo tutaweza kufanya vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo wachangiaji wengi wamesema ni kuhusu suala la *NHIF*. *NHIF* Serikali imesema wataleta Sheria, nampongeza sana Waziri lakini Sheria hii ni muhimu ije haraka sana. Dunia ya wenzetu kwa sababu matibabu ni gharama sana kinachosaidia ni kuwa na *insurance*. Nadhani umefika wakati tuweze kuwa na *insurance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kuimarisha huduma za Mama na Mtoto wanasema wao wanatafuta fedha tunawapongeza ni vizuri waendelee kufanya suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kupata wahudumu; Madaktari, Manesi na Walimu. Niombi sana Wizara ya ya Utumishi suala la kuajiri watu hawa ni muhimu sana kwa sababu hali vijiji kwetu kwenye hospitali zetu za vijiji, vituo vya afya na wilaya hali ni ngumu sana. Nadhani umefika wakati tuhakikishe watu wetu wanakwenda kufanya huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tutachangia na tumelieleza vizuri ni suala la vitabu. Waziri ametuonesha vitabu viliviotengenezwa, hoja yetu Kamati inasema; kuna vitabu vibovu vimeshasambazwa mashulenii, tunaomba vitabu hivyo vikaondolewe mashulenii, basi, halafu hivi vipyta vipelekwe kwa sababu kuendelea kufundishia watoto wetu kwa vitabu vya zamani nadhani siyo jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa suala la uboreshaji wa Chuo kikuu hasa kuanza ujenzi wa Bweni la tano na la pili ni kazi nzuri sana lakini nimpongeze Waziri kwa kusema amesema hapa hawana mpango wa kuifuta *Open University*, nadhani ni vizuri sana tuendelee kuinunga mkono ili iweze kusaidia maeneo ambayo tuna hakika yatasaidia kwenye elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *TBC*, niiombe sana Wizara iendelee kusaidia *TBC* ili iweze kufanya vizuri zaidi na *TBC* kinachotakiwa ni uwekezaji. Naombeni, hiki ni chombo chetu, Serikali iwekeze kwenye jambo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Sheria ya BMT ni muhimu sana Sheria ya BMT ije kwa sababu ni Sheria toka mwaka 1971, haiwezekani leo miaka 47 baadaye bado tunatumilia Sheria ya mwaka 1971 kwa sababu mambo ya michezo yanabadilika sana huko duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, michango ilikuwa ni mingi kwasbabu ya muda siwezi kuieleza yote, lakini kwa hakika niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho hasa ambalo liko tulilisema mwaka jana naomba tulirudie, naamini umefika wakati Serikali tukatafakari tulete, tuunde Tume ya Elimu. Nasema hili la elimu kwa sababu moja tu, elimu ndiyo uhai wa Taifa lolote. Tutajenga viwanda, tutajenga barabara, tutafanya kila kitu kama Taifa letu watoto hawajaelimika tutakuwa hatujafanya jambo lolote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini umefika wakati twende tukaangalie mfumo wetu wa elimu *in totality* hata haya tunaanza kubishana *private schools* ni kwa sababu tu, nadhani tukishaungalia mfumo wetu katika mapana yake tunaweza kujua tunakwenda wapi kwa sababu watu wamechangia hapa tuna watu wengi sana ni *unskilled labour*, tunafanyaje kupata *skilled labour* ili kufanya hiyo kazi kwenye viwanda ambayo mmeanza nayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kuanzisha Tume ya Elimu siyo la kwanza. Mwaka 1981 Rais Regan alianzisha Tume ya Elimu baada ya kuona Marekani inafanya vibaya sana kwenye elimu. Ukienda ku-google iko *report* tena jina lake inaitwa “*A Nation at Risk*” ilielezea hali ilivyokuwa mbaya inakwenda huko Marekani kwa suala la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao walifika *point* mpaka *ku-test output*, watoto waliomaliza *degree wanawa-test* wameelimika hawa? Wakakuta asilimia 60 ya watoto waliomaliza *degree hawakuelimika*. Kwa hiyo na sisi leo tukiamua *ku-test output* yetu, ndugu zangu tutashangaana watoto wetu wengi wanamaliza kweli lakini *output* siyo tulioitarajia. Nadhani umefika wakati kama nchi tuamue kuweka Tume ya Elimu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nitoe hoja kutaka Bunge liweze kuyakubali na kuyapitisha yale yote tuliyoyaleta kwenye Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii. Kabla sijalihoji Bunge, naagiza neno “Utatu Mtakatifu” ambalo Mheshimiwa Mwenyekiti amelishirikisha na elimu liondolewe kwenye *Hansard*, kwa sababu neno hili kwa wenzetu wanaoamini ni neno la juu kabisa katika imani, kwa hiyo isingependeza lichanganywe na elimu ya kidunia. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii Kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017 Iliridhiwa na Bunge)

MWENYEKITI: Sasa, maoni ya Mapendekezo ya Kamati ya Huduma, Maendeleo ya Jamii yamepitishwa na kuwa maazimio ya Bunge.

Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI ili aweze kuhitimisha hoja yake.

MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGAE YA MASUALA YA UKIMWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa tena nafasi ili niweze kuhitimisha hoja hii ya Kamati. Kwanza napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambaao wameweza kuchangia hoja yetu ya Kamati na tulikuwa na wachagaji jumla ya 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambaao wamechangia kwa maandishi walikuwa ni watano na waliochangia kwa kuzungumza walikuwa sita. Kwa sababu ya uchache wao napenda kuwatambua ambaao walikuwa ni Mheshimiwa Silafu Maufi, Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mheshimiwa Mary Muro, Mheshimiwa Rhoda Kunchela na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi hawa wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wapo sita ambaao wamechangia kwa kuzungumza ambaao ni Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Mwalongo, Mheshimiwa Mtalea, Mheshimiwa Mushashu amepongeza, Mheshimiwa Nuru Bafadhili na Mheshimiwa Bura naye amepongeza. Kwa hiyo, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ambayo kwa kweli michango hii ni mizuri sana na ina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru na Wabunge wote ambaao hamkuchangia kwa sababu inaonesha kwamba mmekubaliana na taarifa na mapendekezo na maoni ya Kamati na ninyi pia tunawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mawaziri wamechangia Waheshimiwa Naibu Mawaziri wawili, Mheshimiwa Naibu Waziri Stella Alex Ikupa pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Antony Peter Mavunde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wabunge hoja nyingi ambazo wamezichangia ni hoja ambazo kwa kweli Kamati iliziona na ilizitolea ushauri na mapendekezo. Kwa hiyo haja zote ambazo zimetolewa hakuna hoja ambayo imepingana na maoni na ushauri wa Kamati katika kuishauri Serikali ili iweze kuboresha huduma hii ya masuala ya UKIMWI na masuala ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issues* kubwa ambazo zilikuwa zimejitokeza wengi wamepongeza, lakini pia wamezungumzia upande wa ajira kwa vijana ambayo Kamati pia imeona ili kuweza kuwapatia *activities* ambazo zinaweza zikawapa kipato ili wasijingize kwenye masuala ya UKIMWI na masuala ya dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia masuala ya lishe ili iweze kupata virutubisho, fedha za UKIMWI kwamba ziwanufaishe wale waathirika siyo kwa ajili ya semina. *Issue* nyingine ilioonagelewa ni umbali wa vituo vya kutoa dawa za ARVs ambazo pia Kamati tumeiona, lakini kwa sasa hivi tunaipongeza Serikali kwamba vipo vituo zaidi ya 6,000 tukiangalia huku mwanzo ambapo tulianza na vituo 20 na baadaye tukazidi kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la ushoga na usagaji na lenyewe limezungumzwa kama vinaongeza matatizo ya maambukizo ya UKIMWI. Pia na madawa ya kulevya na Kamati pia imeliona hilo na tumeshauri Serikali katika kuweza kuwa-*empower* hawa vijana ili waweze kujitambua na kufanya shughuli halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawati la kijinsia imependekezwa kwamba zile kesi ziende haraka, pia Kamati iliona na tumeshauri Serikali kusimamia vizuri hili dawati, bajeti ndogo pia hata Kamati imezungumzia. Sera ya UKIMWI

kwamba imepitwa na wakati na yenyewe Kamati imezungumzia imetoa ushauri kwamba sasa irekebishwe na kuweka *program* mashulenii pamoja na ndoa za utotoni

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii ni michango ya jumla ambayo Waheshimiwa hawa Wajumbe 11 wameweza kuchangia kwa maandishi au kwa mazungumzo. Kwa hiyo hoja zao zote kwa kweli ukiangalia ni hoja za msingi kwa sababu hazitofautiani na ushauri na mapendekezo ya Kamati. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambaao mmeweza kusisitiza umuhimu wa kuweza kuboresha *areas* hizi ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za pekee sasa nizipeleke kwa upande wa Serikali ambapo Waheshimiwa Naibu Waziri Stella Ikupa pamoja na Naibu Waziri Mavunde wameweza kutoa michango yao. Kwa upande wa Mheshimiwa Naibu Waziri Ikupa ye ye alijikita kwa upande wa UKIMWI, kwa hiyo utakuta mambo aliyoazungumzia tunashukuru kwamba mmeweza kuchukua ushauri na mapendekezo ya Kamati, tunawashukuru sana, kwa sababu Kamati ilikuwa imesisitiza kwamba UKIMWI upo na kila mtu anatakiwa awe balozi kujilinda ye ye na kumlinda mwингine, tunashukuru kwa Serikali kuliona hili naamini kwa njia hii fedha zitatengwa ili kutoa elimu zaidi na watu waweze kujitambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Naibu Waziri Ikupa alizungumza kuhusu suala la sera kuitwa na wakati, amelitolea ufanuzi tunashukuru sana kwamba mchakato unaendelea. Vyano vy ya uhakika vy ya Mfuko wa AIDS Trust Fund Serikali imelipokea kwa sababu sasa hivi kwa upande wa UKIMWI tunategemea asilimia 90 fedha za wafadhili, wanatumia karibu bilioni 200 kwa mwaka kununua dawa za ARV.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku wakikata ule uzi, nafikiri mnajua shughuli itakavyokuwa. Kwa hiyo, ni vizuri sasa Serikali kuanza kuijandaa mapema kuwa na chanzo cha uhakika kama tulivyosema kule kwenye Mfuko wa REA au Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali inaendelea kuchangia kweli tumeona zaidi ya bilioni moja na zaidi zimetolewa, tunapongeza sana Serikali kwa upande huu wa Mfuko wa UKIMWI, kuna wakati kulikuwa na malalamishi mengi kwa ajili ya ukosefu wa dawa hizi za *septrine* kwa ajili ya magonjwa nyemelezi. Hata hiyo, tunashukuru sana tulimweleza Mheshimiwa Waziri Jenista akaipokea hoja yetu Serikali imetoa milioni 600 kuweza kununua hizi dawa, tunapongeza sana Serikali kwa kuweza kupokea ushauri wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la Njombe limezungumzwa Serikali imetoa ufanuzi kwamba kulingana na *survey* iliyo fanywa mwaka huu ilizinduliwa juzi tarehe Mosi Desemba kwamba ni kweli Njombe bado kuna tatizo. Kwa hiyo, tunapenda sana wenzetu wa Njombe kuweza kuendelea kutumia afua mbalimbali ili kuweza kupunguza UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri Antony Mavunde alijikita kwa upande wa madawa ya kulevyo. Naye amekiri kwamba bajeti ni ndogo, ambayo Kamati pia imeona kwamba bajeti ni ndogo. Pia amekiri kwamba Sera ya Taifa ya Dawa za Kulevyo inatakiwa haraka sana na ametuhaidi kwamba mchakato unaendelea. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuweza kuongea na Waziri wa TAMISEMI kwamba sasa zile Kamati za UKIMWI kwenye Halmashauri ziweze kuingiza dawa za kutibu waathirika wa dawa za kulevyo ni vizuri sana kwa sababu kule ndiko kwenye watu. Tunashukuru pia Serikali kusema itaendelea na mkakati wa kuongeza vituo vya *methadone* katika Mikoa hiyo mitano ya Arusha, Kilimanjaro, Pwani, Morogoro na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru na hii ya Dodoma kwa sababu tayari ipo tayari na Mwanza basi kama mtafanya haraka tutashukuru sana itasaidia kwa sababu waraibu wa dawa za kulevyo ni wengi mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia limezungumziwa suala la unyanyapaa kwa waraibu wa dawa za kulevyta. Tunashukuru Serikali kwamba sasa Dodoma kituo hiki kitamalizika ili kuweza kutoa elimu ya ufundi. Kwa sababu changamoto kubwa wale waraibu wakishapata ile tiba wakawa vizuri, wakiwa *idle* hawana kitu cha kufanya, watarudia tena kule walikotoka. Kwa hiyo, tunashukuru sana Serikali kwa kuweza kufikiria kutoa elimu hii, lakini pia kuhakikisha kwamba kila Mkoa kutakuwa na dirisha maalum kwa ajili ya kutolea dawa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza sana kwa kuongeza ile *ceiling* ya dawa kutoka kilo 120 hadi 300. Kwa kweli tunawashukuru sana sana kwa hii inaonesha kabisa nia ya dhati ya Serikali ya kutaka kuweza kupambana na majanga haya mawili UKIMWI pamoja na dawa za kulevyta, naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu wameniomba nimweleze Mheshimiwa Waziri Jenista kwamba wamefurahi sana kufanya kazi na yeye, kwa sababu akija pale jinsi anavyopokea ushauri, tunashauriana mwisho mambo mengi wameyatekeleza kama Serikali, tunashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwapongeze kwa sababu suala la UKIMWI na dawa za kulevyta ni masuala mtambuka siyo ya Wizara moja, lakini nawapongeza pia Waziri wa TAMISEMI kwa kukubali sasa kwamba Kamati zile za UKIMWI ziweze kuingiza na madawa ya kulevyta lakini pamoja na kutekeleza afua nyingine. Nampongeza sana pia Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa sababu kutokana na ripoti ya *MSD* ni kwamba dawa za UKIMWI zinapatikana asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Waziri wa Afya ni mchapakazi na mara nyingi tukimpa ushauri huwa anapokea tunakupongeza sana. Pia shukrani za pekee ziende kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, walikuja kwenye ripoti yao walikuja na Jeshi la Magereza kwa kweli hili Jeshi linatakiwa liigwe,

Kamati tumeanya ziara Arusha, Manyara, Njombe na Iringa, lakini ukienda kwenye vituo vya kazi unakuta kwenye Halmashauri unaoneshwa wale watu wa hali ya chini ambao wametoka tu huko kwenye mitaa kwenye vijiji na kadhalika, lakini utaambiwa tu kuna watumishi wanapata hiyo lishe nini lakini hatujawaona watumishi ambao wamejitokeza wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walivyokuja Jeshi la Magereza ile ripoti yao karibuvituo vingi vya Magereza kuna watumishi ambao wamejitokeza wengine zaidi ya 100, ile inaondoa unyanyapaa hata wale wafungwa mahabusu wanajiona kwamba siyo wao peke yao hili suala ni la watu wote. Tunashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati tunapenda kuwapongeza Wakuu wa Taasisi hizi mbili Tume ya Kudhibiti UKIMWI na Mamlaka ya Kudhibiti Madawa ya Kulevy, wanafanya kazi sana sana na wanapenda kuchukua ushauri, tunawashukuru sana. Kwa mfano, Mamlaka ya Dawa za Kulevy ni hivi karibuni tu kama sikosei Kamishna alianza kazi yake Februari, lakini ndani ya mwaka mmoja mambo yaliyofanyika katika kudhibiti dawa za kulevy ni makubwa mno utafikiri kama ni kipindi cha miaka mitano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tuchukue suala ambalo lilisumbua muda mrefu vijana wetu suala la viroba, sasa hivi vijana wako vizuri, ajali zimepungua watu huko wanasema *MB* zinasoma sasa! Anajitahidi sana lakini wengi wamekamatwa, wengine wamekimbia, kidogo mambo yanaenda vizuri. Tunammpongeza sana, isivyokuwa kama tulivyoshauri Serikali sasa taasisi hizi mbili mzipatie fedha za kutosha za matumizi ya kawaida na za maendeleo ili waweze kuboresha mikakati yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri, kwa kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa sababu hii Kamati haijaka muda mrefu, lakini sijui alitumia chujio gani kwa kweli Wajumbe walikuwa *committed*, walinipa ushirikiano mkubwa sana katika masuala mengi kuhakikisha tunaisaidia Serikali

kuboresha mbinu mbalimbali kuhusu kupambana na masuala haya ambayo ni majanga ya madawa ya kulevy ya pamoja na UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi ni kwamba dawa za kulevy ya pamoja na masuala ya UKIMWI kwa kweli ni majanga ya Kitaifa. Serikali inaweza ikatoa hata *trillions* za fedha lakini kama sisi wenyewe hatutabadili tabia hizi fedha hazitasaidia lolote. Kwa hiyo, lazima tuanze na mtu mmoja mmoja lakini baadaye jamii na Taifa kwa ujumla ili tuweze kupambana na hili janga kwa sababu lina madhara mengi; vifo, yatima wanazidi kudorora kwa uchumi na kadhalika gharama kwa Serikali inaongezeka kama hivi wanatoa *billions of money* kununua ARVs au kununua hizi *Methadone*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwa Serikali kuweza kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kupambana na janga hili la UKIMWI ingawa watu huko suala la unyanyapaa ni kubwa sana ndio maana inaweka usiri mkubwa kwa watu kutokupima afya zao. Kwa hiyo elimu ya kutosha inatakiwa kwa kweli itolewe ili watu waondoe ile dhana ya unyanyapaa, kujitambua na kuweza kupima na kutumia tiba ili itakapofika 2030, Tanzania iweze kufikia lile lengo la sifuri. Kwa hiyo, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho labda niseme tu kama *tip* watu wengi wanasema kwamba mtu akitumia dawa muda mrefu basi hawezi kuambukiza, mimi niwaambie kwa sababu tulikuwa kwenye Kamati ya UKIMWI siyo kweli, ila ni kweli vidudu vinafubaa vinakuwa sio vingi, kwa hiyo *chance* ya kuambukiza inakuwa ndogo. Mimi siyo mtaalam sana lakini bado ukichukua damu yake na kadhalika unaweza ukapata UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kitu cha msingi wengi kwa mfano, Wachungaji anaenda kupima *viral load* vile vidudu vikiwa chini sana haviwezi kuonekana, wanasema *not detected* anawapeleka watu anasema unaona hakuna, mimi sina UKIMWI kumbe ni vichache kwenye *viral load*,

akipima *CD4* itaonekana kwamba ziko kwenye *normal range*, atasema unaona *CD4* zangu mimi ni nyingi zinatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipimo kizuri cha kuhakikisha na kujua huyu mtu ni *positive* au ni *negative* ndiyo hicho uende ukapime *status* ya kujua kwamba huyu mtu kinga yake ina-react kama ni *positive* au ni *negative* tusi-rely kwenye *viral load* na *CD4* kwa sababu zile zitaonesha kwamba mtu hana lakini vile virusi anavyo ingawa ni vichache, kwa hiyo vikipata mazingira mazuri bado vitaendelea kusambaza UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naliomba Bunge lako Tukufu sasa liridhie taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Masuala ya UKIMWI, maoni na mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofii)

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI Mheshimiwa Jasmine Tisekwa na sasa nitalihoji Bunge.

*(Hoja illitolewa lamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi Kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017
Iliridhiwa na Bunge)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo maoni, mapendekezo na taarifa yote nzima ya Kamati ya Bunge yamepitishwa na Bunge hili kuwa Maazimio.

Nawashukuru wote kwa kazi kubwa waliyofanya wakiwemo Wabunge, Wajumbe wa Kamati pamoja na

Wenyeviti wao; Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Jasmine Tsekwa naamini Serikali imeyasikia na itayafanya kazi kadri iwezekanavyo.

Waheshimiwa Wabunge, naongeza nusu saa ili tuweze kumalizia kazi yetu. Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

HOJA BINAFSI ZA WABUNGE

Hoja Binafsi kuhusu Uzalishaji na Ununuzi wa Zao la Pamba Nchini

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suleiman Masoud Nchambi, karibu ili kuwasilisha hoja yako kuhusu uzalishaji na ununuzi wa zao la pamba nchini.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa tumekuwa na tatizo kubwa kwenye uzalishaji na uuzaaji wa zao la pamba nchini hususan kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni bei; kwa kipindi kirefu sasa bei ya zao la pamba iko chini na wakati wote mkulima wa pamba analima pamba bila kujua ataiuza bei gani, jambo ambalo limemkosesha mkulima wa pamba uhakika wa kipato katika zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili uzalishaji; idadi ya uzalishaji inashuka kila siku jambo linalosababisha wakulima wetu kukata tamaa. Naishukuru Serikali ya Awamu ya Tano imetoa kipaumbele katika kusimamia na hata kuhamasisha kilimo cha pamba. Serikali ya Awamu ya Tano imejitahidi kwa kiasi kikubwa sana kutoa miongozo na maelekezo katika mikoa yote inayolima pamba nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii bila uwoga naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, pia niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge na Wakuu wa Mikoa inayolima pamba pamoja na Wakuu wa Wilaya na Watendaji wote wa Serikali katika Halmashauri zetu kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha zao hili linapata uhai tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ubora; ubora wa zao la pamba unaosababishwa na ukosefu wa mbegu bora huiacha pamba pindi inapokuwa tayari kuvunwa na kukosa hifadhi kwa wananchi wetu, kwani wanapoivuna hawana mahali pa kuipeleka na kwa kuwa Serikali inaweka zuio la kuiiza pamba hiyo wakati msimu wetu wa pamba na hukaa nje katika mashamba hatimaye kuanza kuharibika pindi inapokaa muda mrefu katika mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni mionganini mwa majawabu ambayo nimeyafanya kazi kwa kina na kugundua ni sehemu gani tunakosea. Waheshimiwa Wabunge ni vema sana tukaangalia tunapoijikwaa na siyo tulipoangukia, kwani kuanguka kwetu kumesababishwa na kujikwaa. Sasa naomba niainishe maeneo hayo kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbuke zao la pamba halilimi nchini Tanzania pekee, zipo nchi luki duniani ambazo zinalima pamba kama vile India, China, Argentina, Brazil, Afrika Kusini, Sudan, Mali na Misri. Karibu nchi zote hizo msimu ya pamba na zao la pamba (*cotton season*) inafanana kwa kiasi kikubwa ambapo huvunwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Aprili na kuendelea. Tanzania tunavuna kuanzia Aprili na tunasubiri kuiiza Juni na Julai pindi Serikali inapofungua msimu wa zao la pamba.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba inayolimwa hapa nchini kwa kiwango kikubwa huuzwa nje ya nchi ikiwa bidhaa ghafi (*raw material*) badala ya kuitumia pamba hiyo katika viwanda na kuifanya kuwa zao la mwisho (*final product*). Kwa kushindwa kutumia fursa ya kutumia pamba tunayovuna katika viwanda vya ndani na kusababisha ukosefu wa mapato ya fedha za kigeni na kuzorotesha mzunguko wa fedha wa ndani kwa wananchi wetu.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Wanunuzi wa nje ya nchi tunakouza pamba yetu wanahitaji kufunga mikataba ya ununuzi wa marobota ya pamba yaani *cotton bales*, Wanunuzi hao wanashindwa kuingia mikataba ya kibiashara kwani tunakutana na kikwazo cha bei ya pamba kutotangazwa na Serikali kwani Bodi ya Pamba inakuwa hajakaa na kupanga bei.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja binafsi huwa haisomewi hapo mbele, inasomewa kwenye kiti anachokaa Mbunge anayetoa hoja binafsi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nchambi endelea tu midhali umeshaanza hapo.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, msimu wa ununuzi wa zao la pamba duniani (*World Market*) huanza tarehe Mosi Aprili kila Mwaka wa Fedha na huishia tarehe 31 Machi ya mwaka unaofuata. Wanunuzi wote duniani huanza kufunga mikataba kuanzia tarehe Mosi, Aprili katika nchi zinazolima pamba. Wakati huo Bodi ya Pamba Tanzania ambayo haimiliki hata kilo moja ya pamba inakuwa hajasaidia lolote kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote duniani hazina kitu kinachoitwa msimu wa pamba na msimu wa zao la pamba. Nchi kama China, India, Argentina na zingine nilizozitaja hununua pamba zao, wanunuzi wa Tanzania wanaanza kununua pamba zao wakati wanunuzi wa Tanzania huwa wanasubiri kwanza kufunga mikataba hiyo mpaka pale wanapopata bei elekezi kutoka Bodi ya Pamba ambayo iko chini ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwengine wanunuzi wa pamba kutoka nchi nydingine hulazimika kusubiri mpaka katikati ya mwezi Juni au Julai ili kupata bei hiyo elekezi na baadaye kuingia mikataba na wafanyabiashara wa ndani, yaani wanunuzi wa ndani kwa ajili ya kununua pamba hiyo.

Wakati huo nchi zinazohitaji pamba huenda nchi zilizo tayari kuza pamba yao. Watanzania tunakaa na pamba yetu kana kwamba wananchi wetu pamba hiyo siyo yao bali wao ni walinzi tu wa pamba hiyo. Dhambi hii itatuhukumu siku zote kwa kudhulumu haki ya mwenye nacho kwa hila tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo wafanyabiashara au wanunuzi wanaonunua na kuuza pamba yao nje ya nchi, wanakutana na changamoto ya wanunuzi wa nje ya nchi wakiwa tayari wameshanunua pamba kutoka nchi nyingine ambazo zimewauzia pamba mapema kwa ajili ya kulisha viwanda vyao na hivyo pamba yetu kununuliwa kama nyongeza tu. Hivyo, matokeo ya ucheleweshaji huu wa msimu yanawaathiri wakulima nchini kwa pamoja kwa sababu bei itakayouzwa pamba hiyo nje ya nchi inakuwa chini kwa kuwa wafanyabiashara wa ndani nao watanunua kwa bei chini zaidi ili waweze kutengeneza faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili ni kuharakisha msimu wa pamba mapema ili wafanyabiashara nchini wafunge mikataba hiyo mapema, ambapo mahitaji yanakuwa yako juu na wanunuzi wa nje watakuwa bado hawajanunua pamba nchi nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kilo moja ya pamba itauzwa katи ya Sh.1,500 na Sh.2000 kuanzia mwezi Mei badala ya katи ya Sh.600 na Sh.1,200 katи ya mwezi Julai na Oktoba faida zinazopatikana kwa kuharakisha msimu ni hizi zifuatazo:-

- (i) Mkulima atapata kipato kikubwa na kwa wakati kwa kuuza pamba yake kwa bei ya juu.
- (ii) Serikali itaongeza kipato kwa kukusanya kodi kwa kiwango kikubwa wakati bei iko juu.
- (iii) Ongezeko la bidhaa ya pamba kila mwaka kwa kuwa itashawishi wakulima wengi kujilingiza kwenye kilimo cha zao la pamba baada ya kuona manufaa ya zao

hilo. Pia ni vema Serikali ikasimamia ipasavyo Vyuo vyetu vya Kilimo kuanzisha na kuongeza uzalishaji wa mbegu bora ili kutoa fursa ya uhakika juu ya uzalishaji siku za usoni.

(iv) Ongezeko la ajira kutokana na watu kujajiri kupitia zao la pamba na hivyo kuweza kupunguza tatizo la ajira nchini.

(v) Serikali itaongeza kipato cha fedha za kigeni kwa kuuza zao la pamba nje ya nchi, ambako fedha hizo zitaongezeka kila mwaka na kuendelea kuimarisha uchumi wa Taifa letu.

(vi) Tufufue vyama vya Ushirika.

(vii) Tuweke nguvu katika viwanda vinavyotumia malighafi ya zao la pamba kwa kufufua, kuanzisha na kusimamia viwanda vidogo na vikubwa kama viwanda vya mafuta, nyuzi, nguo na chakula cha kuku.

(viii) Kuandaa mpango maalum wa kuwakopesha wakulima wa zao la pamba kwa riba ndogo na kuwapatia hati ya mashamba yao ili wakopesheke kwa urahisi.

(ix) Halmashauri zipewe maelekezo ya kujenga maghala ya kuhifadhi pamba wakati wa msimu ili wanunuzi watumie ghala zetu na tutadhibiti ubora na ukusanyaji wa kodi katika Halmashauri zetu.

(x) Vyuo vyetu vya Kilimo vianzishe na kuendeleza mpango wa kupima ardhi zifaazo kwa kilimo cha pamba kwa kufanya *soil test* lakini pia uzalishaji wa mbegu za kisasa zaidi.

(xi) Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Mazingira tuanze mchakato wa kutumia neema aliyotupa Mungu ya rasilimali ya maji ya maziwa, mito, visima na hata kutengeneza mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Ni aibu kama Taifa kwa neema tulizonazo kuendelea kusubiri mvua peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hayo, yapo matatizo mengine ambayo athari zake ni kubwa na zinamgusa mkulima wa pamba na Serikali moja kwa moja. Wakulima wa pamba nchini wengi wao ni wananchi wa kawaida tena wanaohangaika sana na zao hili ambapo wakulima wanalima kuanzia mwezi Novemba na Desemba, wanavuna pamba kati ya tarehe 1 Aprili na 15 Mei, wakati huo huo hawana sehemu ya kwenda kuihifadhi pamba yao kutokana na kuwa na makazi duni, ambayo huyatumia kwa ajili ya kujihifadhi na maisha yao ya kila siku pamoja na familia tu. Pia, wakulima hao hawana uwezo wa kujenga ghala ama hifadhi kwa ajili ya zao la pamba kutokana na uwezo duni walionao watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yafuatayo ni matokeo ya moja kwa moja pale mkulima wa pamba nchini anapochelewa kuuza pamba yake:-

(a) Anauza pamba hiyo kwa walanguzi katika Vijiji, Kata ama Wilaya anayoishi kwa bei kat i ya Sh.200 hadi Sh.400 kwa kilo moja.

(b) Kushuka kwa ubora wa bidhaa ya zao la pamba kutokana na kukosa sehemu ambayo pamba hiyo inaweza kuhifadhiwa kitaalam ambapo mara nyingi huhifadhiwa kwenye mazizi ya ng'ombe au juu ya ardhi mashambani na matokeo yake pamba hiyo hubadilika rangi yake ya asili kutoka kuwa nyeupe hadi nyekundu, kuchanganyikana na vumbi na mchanga, kupigwa jua na kupoteza kwango kinachostahili na kusababisha kupungua kwa ubora pindi inapotengenezwa kuwa nyuzi na mbegu kupungua ubora wake wakati wa kukamuliwa mafuta.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nchambi naomba usubiri.

T A R I F A

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ambayo Mheshimiwa Nchambi anaiwasilisha katika hizi *paper* ambazo tumegawiwa Wabunge

tunazisikiliza, *page* namba tano zinaenda vizuri katika mtiririko mpaka *point* namba tano zile faida, lakini kuanzia namba sita mpaka zile Kumi, karatasi hizo hatuna humu ndani Wajumbe wote. Kwa hiyo, nafikiri ofisi ambayo ilikuwa inashughulika na uchapaji nadhani hiyo *page* imekosekana. Naomba tupate hiyo *page* kwa ajili ya kuboresha taarifa yenyewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nchambi, naomba usome yale ambayo wamepewa Wabunge wote. Endelea.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa Nchambi.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa hoja hii, pale ambapo tutakuwa tumeteleza, nashauri tunge-note pembedi kwa sababu hoja hii ni ya msingi na ina maslahi takriban kwa asilimia 82 ya wananchi ambao wanalima pamba. (*Makofii*)

(c) Ipo mifano katika miaka ya nyuma ikiwemo mwaka 2013 ambapo bidhaa ya pamba kutoka nchini ilikataliwa nje ya nchi na kurudishwa nchini jambo ambalo limewaletea hasara kubwa sana wanunuzi wa pamba nchini na matokeo yake kama nchi jambo hili likatutia doa sana kwa kuza pamba isiyo na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, wakati mkulima anaandaa shamba, kulima shamba, kupanda shamba na kupalilia shamba na hata kuvuna shamba lake, anakuwa ye ye na familia yake tu na hakuna mshirika yeyote kutoka sehemu yoyote zaidi ya Serikali kumsimamia apande kwa mstari, asichanganye zao la pamba na mazao mengine. Cha ajabu pamba ikishakuwa tayari Bodi ya Pamba inawasili bila mwaliko wa mkulima, aliyehanganya ni ye ye na familia yake peke yake na kuanza kumpangia bei ya pamba, kumpangia tarehe ya kuza pamba yake aliyo hanganya nayo ye ye na familia yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge hususan tunaotoka mikoa inayolima pamba, tunaamini na tunaendelea kuamini pamba ni dhahabu nyeupe. Tuwafute machozi na kutowesha jasho na kilio cha muda mrefu juu ya adha na adhabu wanazopata wakulima wa pamba kote nchini. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tuanze leo na sasa kusaidia wakulima wa pamba. Tutakuwa tumefungua milango, mianya na fursa ya kuendeleza mijadala juu ya mazao mengine kama tumbaku, kahawa, mtama, alizeti, chai, michikichi, korosho, mihogo, ndizi na mengineyo na hata katika maeneo ya mifugo kama tulivyo simama pamoja wakati wa hoja ya Wizara ya Nishati na Madini kutetea rasilimali za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niipongeze sana Wizara ya Kilimo inayosimamiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba kwa ufuatiliaji na ushirikiano wanaouunesha kwa wakulima wetu. Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, kilimo kinahitaji pesa, tumbane ipasavyo Waziri wa Fedha kupitia Kamati zetu za Bunge na ndani ya Bunge ili atenye fedha za kutosha tusaidie wakulima wetu na kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuamue leo na sasa Bunge hili lichukue nafasi yake ya Kibunge, tuwasaidie Mawaziri pindi watakopapata fedha katika bajeti ijayo wasiwe na sababu ya kuwasaidia Watanzania wanyonge, wakulima wanaohangaika katika vijiji vyetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama Bunge tuchukue nafasi yetu ya Kibunge, kuishauri na kuielekeza Serikali namna bora ya kutatua kero za wananchi wetu, lakini kwa namna ya kipekee, naomba tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa namna anavyoendeleza mapambano ya kutetea maslahi ya wanyonge na wakulima wa pamba ni wanyonge, ni watu maskini wanaohangaika, wanahitaji kulima pamba yao ili waweze kujikimu na maisha yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu hizo na nyingine nyingi zilizonisukuma nikuombe kwa idhini yako kuwasilisha hoja binafsi kwa mujibu wa Kanuni ya 54(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, niwasilishe hoja binafsi mbele ya Bunge lako Tukufu kuhusu kuangalia upya msimu wa pamba nchini kama ifuatavyo:

KWA KUWA zao la pamba halilimwi nchini pekee, ziko nchi nyingi lukuki duniani ambazo zinalima pamba kama vile India, China, Argentina, Mali, Afrika Kusini na Brazil na takriban nchi zote hizo msimu wa kulima pamba unafanana kwa kiasi kikubwa ambako pamba huvunwa kwa kipindi cha miezi ya Aprili, Mei na kuendelea;

NA KWA KUWA; wakati huo wanunuzi hupenda kufanya mikataba mapema na nchi ambazo ziko tayari kuwauzia pamba;

NA KWA KUWA wakulima wa Tanzania husubiri kwanza kufunga mikataba hiyo mpaka baada ya kupata bei elekezi kutoka Bodi ya Pamba ambayo iko chini ya Wizara ya Kilimo;

NA KWA KUWA zao la pamba linalimwa nchini wakati nchi yetu hajawa tayari kuifanya pamba kama bidhaa, maana yake *final product* na badala yake kwa kiwango kikubwa huuzwa nje ya nchi ikiwa malighafi (*raw material*);

NA KWA KUWA, jawabu la moja kwa moja la kuondokana na changamoto hizo kwa wakulima wa pamba nchini ni kuharakisha msimu mapema ili wafanyabiashara wafunge mikataba na wanunuzi wa nje mapema ambako mahitaji yanakuwa yako juu na wanunuzi wa nje hawajanunua pamba katika nchi nyingine;

HIVYO BASI, mimi Suleiman Masoud Nchambi, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, naomba Bunge lako Tukufu liniunge mkono katika hoja yangu na kuazimia kuitaka Serikali ibadilishe msimu wa pamba kwa kuanza msimu tarehe Mosi mwezi Mei, badala ya kufungua msimu kuanzia katikati ya

mwezi Juni ili kuendana na hali halisi ya msimu wa uzalishaji na uuzaaji wa pamba nchini. Hali hii itasababisha kuendana na misimu ya pamba katika nchi nyingine zinazolima pamba duniani na hatimaye kuwa na uwezo wa kuuza pamba hiyo kwa bei nzuri kama wafanyakyo wafanyabiashara wa nchi nyingine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
(Makofî)

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Nchambi. Hoja imeungwa mkono na watu wachache siyo wengi sana.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Sawa, tunaendelea na mjadala sasa. Tutaanza na Mheshimiwa Mashimba Ndaki, baadae Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Joseph Selasini wajiandae, dakika tatu tatu.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la pamba ni muhimu sana kwenye nchi yetu hii na suala lilloetwa mbele yetu na Mheshimiwa Nchambi ni la muhimu sana. Nami niungane naye kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono suala hili kwa sababu litasaidia sana wakulima wetu wa pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba inalimwa Mikoa kama 16 kwenye nchi yetu sasa hivi na Wilaya kama 45 zinapata kipato chake kuititia zao la pamba. Kwa hiyo ni zao muhimu sana. *(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa mazao mengine, pamba hii hatuitumii ipasavyo hapa nchini, tunapoizalisha tunategemea soko kubwa nje ya nchi. Kama asilimia 70 hivi ya pamba yetu tunauza nje ya nchi, tunayotumia hapa nchini kwetu ni kama asilimia 30 hivi. Kwa hiyo, utakuta tunategemea kuuza zao hili kwa wenzetu ili tupate kipato kwa ajili ya wakulima wetu na sisi kama nchi fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilonalo kwa mazao haya kama nchi inayoendelea sisi ni wachukuaji wa bei. Hatupangi bei kwenye soko lile tunakouza pamba, tunachukua bei tunayoikuta sokoni ndiyo hiyo tunayouza pamba yetu. Kama alivyowasilisha Mheshimiwa mtoa hoja, kwa kufuata msimu ambao ulikuwepo nadhani kutoka ukoloni, bei ya pamba tunapopeleka huko tunakouza nchi za wenzetu tunakuta bei hiyo iko chini kwa sababu pamba yetu inakutana na pamba inayotoka kwenye nchi zingine ambazo wamezalisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukikuta bei iko chini hatuna namna, tunachukua bei hiyo kwa sababu hatupangi bei, hatuna uwezo wa kushawishi kama nchi ili bei ipandishwe kwenye soko hilo tunalouza pamba yetu. Kwa hiyo, tunachukua bei hiyo ndogo. Sasa kwa kuacha kuweka msimu kama ambavyo iko sasa hivi, maana msimu tulionao hapa unaanza mwezi Juni au mwezi Julai. Sasa wakati huo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ndaki. Tunaendelea na Mheshimiwa Ester Bulaya na baadaye Mheshimiwa Joseph Selasini aijandae.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami niunge hoja ya Mheshimiwa Nchambi kwa sababu Jimboni kwangu wananchi wangu wanalima pamba na wengine tumefika hapa kwa sababu ya zao la pamba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Nchambi kwa kubadilisha msimu kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza, msimu unapochelewa moja, hili Mheshimiwa Nchambi atakubaliana na sisi kama ambavyo tunasema pamba ni dhahabu nyeupe. Mosi, pamba inapungua uzito kwa sababu inakaa sana. Pamba hii pia inabadilika rangi kutoka nyeupe kwenda njano, hivyo inapunguza ubora. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokwenda kwenye soko, pamba yetu ya Tanzania inaonekana haina ubora na inashindwa kabisa kushindana kwenye soko. Kwa hiyo, hoja hii Mheshimiwa Waziri tena asikie siyo anaongea hapo, hoja hii ni ya msingi kweli kweli hatuwatendei haki wakulima wetu wanaolima pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hivyo, wakulima wanakuwa hawawezi kujipangia bei, imesemwa hapa na niwaambie kule vijijini pamba inashuka, wakulima wanlanguliwa kutoka Sh.200 mpaka Sh.300 siyo Sh.800 wala siyo Sh.600. Tukizunguka huko kwa wapiga kura wetu huwezi ukakutana na watu wasikuulize suala la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nchambi amezungumzia suala la mbegu bora. Kulikuwa kuna mbegu ambayo ilipigiwa upatu sana hapa ya *qoton*. Mbegu ile ililetatizo kubwa sana kwa wakulima wetu. Wakulima wale mbegu haikuota, wakulima hawakupata faida yoyote, mwisho wake Serikali ya Awamu ya Nne iliingia kwenye hasara ya kwenda kuwafidia wakulima wa pamba kutokana na hasara waliyoipata kwa sababu ya mbegu kuwa mbaya. Sasa ni lazima tuwe na mbegu yenye ubora, tukiwa na mbegu yenye ubora tunaongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni jambo la msingi sana na sasa hivi pamba imeingiliwa na wadudu...

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini, hayupo, Mheshimiwa Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza naunga mkono hoja ya Suleiman Nchambi. Vilevile nitumie fursa hii kumpongeza sana kwa dhati Mkuu wangu wa Mkoa wa Tabora Mheshimiwa Mwanri, kwa jitihada alizofanya kuhamasisha wananchi kulima pamba kwa wingi mwaka huu. Mwaka huu Mkoa wa Tabora tutakuwa tumelima hekari 187,000, Wilaya ya Igunga ndiyo inabeba asilimia 80 mpaka 85 ya zao hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote alizosema Mheshimiwa Nchambi na tutakapobadili msimu ni jambo moja. Tatizo letu la sekta nzima ya kilimo siyo tu pamba mazao yetu, ni pale ambapo Serikali inafanya *interference* ya kuharibu mizani ya soko kwa maana ya *demand and supply* wakati yenyewe haiwekezi. Hili ni tatizo kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeshauri Serikali pamoja na haya Bunge ku-*adopt* hili tuongeze *resolution* kama itawezekana, kuitaka Serikali inapokuja na mpango wa 2018/2019, ije na *chapter* maalum ambayo inaonesha namna gani mazao yetu makuu ya biashara, Serikali itawekeza kwa ajili ya uzalishaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lilioko kwenye pamba vilevile limekuwepo mwaka jana kwenye tumbaku. Mwaka huu tumbaku itaporomoka sana kwa sababu ya Serikali kutokuwa *proactive*. Vilevile Wizara ya Kilimo ni *punching box* tunampiga sana, wadudu kapata fedha yeye ndiyo dawa. Ni lazima Wizara ya Fedha ichukue *responsibility* yake ya kuwa yenyewe ina wajibu wa kuwekeza kwenye mazao yetu ya kilimo, bila ya hivyo hatuwezi kupeleka huu uchumi mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunataka watu waende wakanunue pamba, *what is our incentives scheme* kwa hawa wanunuzi? Tunawawekea *security measures* gani watakaponuna kama kutatokea kuna *fluctuation* yoyote kwenye soko la dunia? Mabenki tunayasaidiae ili yaweze kuwapatia hawa watu fedha za kununulia mazao yetu ya wakulima? Lazima tuwe na *broader thinking*, Mheshimiwa Waziri wa Fedha afahamu kwamba tunaponyooshea kidole Wizara ya Kilimo, yale ni matokeo ya maradhi yanayotoka Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwe na *long term plan*. Kwa mfano, leo tunasema tubadilishe msimu sawa; je, *quantity* ya uzalishaji wetu wa mazao ya pamba ni kiasi gani? Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya Nchambi lakini nadhani umewadia wakati kama nchi kutazama sekta ya Kilimo kwa mapana yake. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Bashe. Tunamalizia na Mheshimiwa Musukuma na baadaye Mheshimiwa Chenge.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nianze tu kwa kusema kwamba tunaotoka kwa wakulima wa pamba baada ya kuona jitihada za Waziri Mkuu kuhusiana na zao la korosho, tumelima pamba nyingi sana lakini tatizo liko moja. Dawa hazipatikani, ukiangalia kwenye *TV* Wizara inasema tuna madawa ya kutosha, yanapigwa picha sehemu kadogo, sasa tunapata shida sana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mdogo tu kwenye Jimbo langu jana wanakijiji 600 waliojiandikisha kupewa dawa, mpeleka dawa kaenda na chupa 20 tu, watu 600 toka asubuhi wanasubiri, amekwenda saa nane na chupa 20, anasema dawa hakuna. Kwa hiyo, nadhani Serikali wajipange. Kama Serikali ndio inatoa madawa ijipange kuliko kutuhamasisha wakulima wa pamba, tunalima pamba tunakuwa kama mbayuwayu, mwaka tusiolima pamba

mwaka unaofuata tunahamasishwa kwamba tunaambiwa pamba itanunuliwa, pamba itapandishwa bei, tukilima dawa tena hajji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono suala la kaka yangu Nchambi lakini na nina wazo la tofauti kidogo. Sipendi sana kusema tupeleke pamba yetu Ulaya tukashindanishe na nchi zingine. Nataka pamba yetu Serikali ije na mpango mzuri itumike hapa hapa. Hivi tunashindwa hata kuwa na viwanda vya kushona tu nguo za Askari na Magereza na *uniform* za wanafunzi, siyo pamba yetu itakuwa imepanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na viwanda vya nyuzi kwa nini tunawaza masoko ya nje na wakati Serikali Rais wetu anasema tupandishe na tutengeneze viwanda. Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mheshimiwa Mwijage ana viwanda karibu 6000, aje na mpango mzuri, avitoe kwenye begi hivyo viwanda sasa atupe huku ili tuweze kulima hii pamba, inunuliwe hapa hapa tusipeleke kwenye ushindani wa Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria kama tutashona *uniform* za watoto tu wa bure wa Magufuli hawa, tukashona tu *uniform* kwamba lazima *uniform* yake iandikwe pamba halisi ya Tanzania, tuna haja gani ya kupeleka pamba Ulaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni ombi langu. Nakushukuru. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Musukuma. Tunamalizia na Mheshimiwa Chenge.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nasimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Nchambi kwa zao hili la pamba hasa kwenye pendekezo lake la kuondokana na dhana ya msimu wa pamba. Ni hatua nzuri naomba tuiunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kote, nisiende mbali Kusini mwa Afrika ambapo pamba inalimwa na Mheshimiwa jirani yangu niliyekaa naye hapa Mheshimiwa Kishimba amefanya biashara na anafanya biashara Zimbabwe hakuna kitu kinachoitwa msimu wa pamba. Ukienda Misri ni hivyo hivyo. Kwa hiyo, tunaanza vizuri, naomba tuunge mkono mapendekezo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa tahadhari tu kwa wazo zuri la Serikali la kuua hizi Bodi hasa hii ya Pamba, kwa upande wa Halmashauri zetu ambayo tunasema ndiyo wasimamie, mimi natoka kwenye mkoa ambao unalima pamba nyingi sana nchi hii. Sasa tusipoweza kusaidia Halmashauri hizi tutapata tatizo lingine kwa upande wa bei. Ni vema tukalionna hili mapema kwamba, Halmashauri katika maeneo tunayolima pamba tuwasaidie kuweka Wataalam ambao wataweza kukokotoa vizuri bei ya zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho najua watakaopinga wazo hili ni wale wafanyabiashara ambao wanategemea mikopo ya benki, kwa sababu benki yeoyote haiwezi ikakupa mkopo mpaka imezunguka kuona pamba iliyopo, lakini wafanyabiashara wenye pesa zao au njia zao zingine ambao hawahitaji kwenda kuchukua mkopo katika msimu huo, nadhani watakuwa tayari kuukubali utaratibu huu tunaopendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kitu chochote kipyaa huwa kina changamoto zake, tutajifunza zaidi na kuboresha kadri tunavyokwenda mbele, tusiogope kuanza twende mbele. Mimi naunga mkono hoja hii na nishawishi twende pamoja katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Chenge upande wa Serikali, hakuna ambaye anazungumza Mheshimiwa Waziri Mwijage.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Nchambi, sioni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapa taarifa wengi waliochangia, tunao mkakati unaitwa pamba mpaka mavazi, hayo mapendekezo yote kama alivyosema Ndugu yangu Mheshimiwa Musukuma tunayo na mwezi huu itakaa sekta ya watu wanaonunua pamba mpaka kuitengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maandiko yanakwenda kwenye mamlaka ambayo tunalenga kuzalisha *uniform* kwa wanafunzi wote amba ni takribani milioni 15. Pia yako mapendekezo kwamba wazalendo mchague siku moja kama siku ya Ijumaa muweze kuva tisheti au nguo nzuri zilizoandikwa *Made in Tanzania*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna imani kwa kufanya hivyo kwa nguo tu za wanafunzi tunaweza kutumia robo ya pamba inayozalishwa nchini. Kwa hiyo, mawazo hayo tunayo na tijihada za ufufuaji wa viwanda zinaendelea lakini na wawekezaji wapya wa viwanda watakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu naunga mkono *flexibility* ya mahali pa kuuza tukiwa tunalenga soko likoje duniani, kama alivyosema Mjumbe mmoja mtaalam wa pamba, sisi ni wapokeaji, *we are price taker*, kwa hiyo ile *flexibility* ndio naiangalia. Kama kuwahi kwako kutakuweka kwenye shimo afadhali uchelewe, kama kuchelewa kwako kutakuwingiza kwenye faida chelewa, kama kuwahi kwako kunakuwingiza kwenye faida, ningependa nishauri kwamba tuwahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia hilo la viwanda tuko vizuri kwenye viwanda. Viwanda vilivyopo vilikuwa vinazalisha kidogo pamba haipatikani na walipotengeneza baadhi ya viwanda ambavyo vinazalisha hatutumii bidhaa yake, kwa hiyo tutaingia kwenye kampeni ya kuhimiza Tanzania yetu itumie viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Urafiki ambazo tulikuwa na ubia na Mchima tunambana Mchima sasa ili kusudi Serikali ichukue asilimia kubwa zaidi ya asilimia 75 kusudi sasa tuweze kuwekeza pale na Mji wa Dar es Salaam uweze kuwa *livable*, watu watoke *around* watembee waingie kwenye kiwanda kile kiweze kuajiri watu zaidi kutoka 800 wa sasa kirudi 3000 wa zamani na kwenda zaidi mpaka 10,000 kama walivyo Tooku na Mazava.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Nchambi Mbunge shapu wa Jimbo la Kishapu pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii ya msingi sana ya kubadilisha msimu wa pamba kuanza tarehe Mosi Mei badala ya katikati ya Mwezi wa Juni ili kuweza kuongeza dthamani ya bei iweze kuwa kubwa na pamba yetu iweze kuwa na uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wangu alifanya ziara Igunga na Kwigwa na alishatoa kabisa tamko kwenye Bodii ya Pamba kwamba msimu wa pamba uanze tarehe 25 Aprili, 2018. Vilevile kama Serikali tayari hilo tumejipanga na tunafanya utaratibu wa bei elekezi ili ukikamilika mpango huu wa bei elekezi, basi jambo hili liweze kufanya mpango mahsus wa zao hili la pamba ambalo ni zao la kimkakati Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa ni *champion* kabisa katika mfumo mzima wa kuhakikisha zao la pamba linakuwa ni zao ambalo linapata uhai ili Taifa letu pamoja na wakulima wote waweze kunufaika. Vilevile kama Serikali Wizara pia tumejipanga tumeanzisha kitengo cha *Marketing Intelligence* kuhakikisha

kwamba mazao yote hususani yale ya kimkakati ya kibishara, yanapata soko kwa wakati gani, mahali gani ili bei iweze kuwa nzuri kumnufaisha mkulima na kuweza kunufaisha pia Taifa la Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kama Serikali, kama Wizara tunaimarisha Vyama vya Ushirika. Juzi nilipokuwa najibu maswali hapa nilisema tunafanya *total transformation* kwa upande wa Vyama vya Ushirika kuhakikisha kwamba vinafanya bora na wakulima wasiweze kuonewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kama Waheshimiwa wengi Wabunge walivyosema ni vema kabisa tukawa na viwanda nchini ambavyo vitakuwa vinazalisha kutokana na malighafi ya wakulima wetu wenyewe Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme kabisa kwamba kama Serikali, Wizara ya Kilimo ambayo ni Wizara Mama, tunaunga mkono hoja hii ya muhimu kabisa kwa ajili ya wakulima wa zao la pamba pamoja na Taifa zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri wa Kilimo. Mheshimiwa Nchambi naomba uhitimishe hoja yako hapo ulipo.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana, niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja yangu kuhusu uzalishaji na uuzaji wa zao la pamba nchini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji wetu wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mwalimu wangu, namshukuru sana kwa kuunga mkono hoja hii na nimshukuru zaidi kwa kuliona hili kwa wakulima wetu katika Mikoa inayolima pamba zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndaki ameleeza umuhimu kwa namna ya kipekee ya Serikali isisitize zao hili kwa takribani zaidi ya asilimia 70 mpaka 80 litumike ndani. Nadhani Mheshimiwa Waziri Mwijage ndiyo uzuri wa kuchagua Mawaziri ambao kidogo wanakuwa na majibu yenyé utashi na matakwa ya wakati huo. Namshukuru sana Mheshimiwa Mwijage na umesisitiza namna ambavyo utatupeleka mbele kutoka katika pamba mpaka kwenda kwenye mavazi, Mungu akubariki na kwa kweli uzalendo ulioonesha ni hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Methali 27.10 katika maandiko matakatifu, Mheshimiwa Waziri Mwijage amejaribu kupita huko ambako mstari unasema: "Usimwache rafiki yako mwenyewe wala rafiki ya baba yako, wala usiende nyumbani kwa ndugu yako siku ya msiba wako. Afadhalii jirani aliye karibu kuliko ndugu aliye mbali". Kwa hiyo tunakushukuru sana Mheshimiwa Mwijage. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru sana Mheshimiwa Ester Bulaya ameondoa tofauti zetu na kuona kwamba jambo hili ni la msingi na kuwatetea wananchi wa Jimbo lake na peleka salamu kutoka kwa Mbunge shapu kuwa kwa kweli nimekupenda kwa namna ambavyo umechangia hoja hii na umeonesha utayari juu ya kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ester ameleeza juu ya tatizo kubwa lilitukumba miaka ya nyuma juu ya mbegu za *qoton* ambako kwa kweli tulathirika kufikia namna ya kipekee wakulima kuona kama vile mbegu zile sasa kwa sababu hatuzipeleki kwenye vibuyu vyetu pengine zinatoka kiwandani zinafungwa *sealed* zinasababisha kutoota na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Naibu Waziri ameleeza mpango mkakati pia amesisitiza lakini nimwombe sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na niwaombe Wabunge tatizo letu ni fedha, viko Vyuo vyetu vya Kilimo

ambavyo vinaweza vikazalisha mbegu bora, lakini hatuna pa kuanzia kwa sababu ya ukosefu wa fedha, nadhani Mawaziri wamelisikia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Hussein Bashe na nimpongeze kwa kweli rafiki yangu Katibu Mwenezi Mstaafu wa CCM Taifa, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, kwa kweli amefanya kazi nzuri. Mimi Igunga ni mwenyeji nina nyumba zangu pale, nina mashamba kwa hiyo nimeona jitihada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe ameeleza juu ya hoja mahsus, hapa kuna hoja ya msingi, tunapokwenda katika Bunge letu la Bajeti kama Wabunge tuchukue nafasi yetu ya Kibunge ya kuona namna ambavyo mazao makuu tunayawekea mpango mkakati ili kuwasaidia Watanzania zaidi ya asilimia 82 mpaka asilimia 88 vijijini na mijini ambako tunafanya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nimshukuru sana Mheshimiwa Musukuma, rafiki yangu kwa kuchangia hoja hii kwa weledi na kutoa ushauri wake kwa kifupi, lakini ameonesha namna ambavyo pia anafahamu kabisa tatizo la wapiga kura wake juu ya zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge kwa namna ya kipekee alivyoonesha msisitizo na dhamira ya dhati juu ya kuwasaidia wakulima wetu wa pamba. Hata hivyo, niende mbali zaidi kwa Mheshimiwa Chenge alieleza mambo na niombe Serikali tunayo benki yetu ya *TIB*, ni aibu sana kama Taifa, Serikali inahamasisha mazao makuu matano lakini Benki yetu ya *TIB* inashindwa kuwa ndiyo mtu wa kwanza kukopesha mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana lakini kwa sababu ya muda baada ya maelezo hayo niwatambue wapigakura wangu wawili, *Comrade Baraka Shemahonge* na Bakari Mfundu walioambatana na mimi kunitia moyo juu ya hoja hii wako hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu liniunge mkono katika hoja yangu na kuazimia kuitaka Serikali ibadilishe msimu wa pamba kwa kuanza msimu tarehe Mosi Mei badala ya kufungua msimu katikati ya Mwezi Juni ili kuendana na hali halisi ya msimu wa uzalishaji na uuzaji wa pamba nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana hoja imeungwa mkono sasa nawahoji Wabunge. Waheshimiwa Wabunge, ambao wanakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Nchambi sasa ili iweze kuwa Maazimio ya Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Hoja Binafsi ya Mheshimiwa Suleiman M. Nchambi
kuhusu Uzalishaji na Ununuzi wa Zao la Pamba
Nchini illridhiwa na Bunge)*

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKIT: Mheshimiwa Jenista

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mwongozo wa Spika.

MWENYEKIT: Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi katika mjadala wa leo asubuhi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametoa majibu mazuri sana akijibu hoja za Mheshimiwa Mt Olea. Kumeanza kujitokeza tabia ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanapochangia michango yao ndani ya Bunge ili kuhalalisha michango hiyo wakati mwingine wamekuwa wakitumia utendaji kazi wa Rais wetu kama ni kigezo cha kuhalalisha hoja zao ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapofanya hivyo wakati mwingine uhalalishaji huo hauna uhakika na wakati mwingine unapotosha jamii katika ile misingi tuliojiwekea ya kikanuni ndani ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara zote kwa kufanya hivyo Kanuni ya 64(1) na hasa (d) na (e) imekuwa ikivunjwa mara nyingi sana ndani ya Bunge, kwa tabia hiyo ya baadhi ya Wabunge kutumia utendaji kazi wa Rais wetu katika kuhalalisha michango yao na uhalalishaji huo wakati mwingine unapotosha maana halisi ya utendaji wa Rais katika nchi yetu na katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Mwongozo wako, kwa kuwa jambo hili sasa linaonekana kama linataka kuchukua mazoea ndani ya Bunge letu Tukufu, nini mwongozo wako kwa Wabunge wanapoondelea kuvunja Kanuni ya 64(1)(d) na (e) ili tuweze kwenda sambamba ndani ya Bunge na tuweze kutumia kanuni zetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jenista, Mwongozo huo nimeupokea na utafanyiwa kazi na utatolewa Mwongozo wake baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, natumia fursa hii sasa kumpongeza Mheshimiwa Nchambi kwa hoja yake ambayo naamini itaenda kuisukuma zaidi Serikali katika ule mpango wake iliyokuwa imeshajiwekea iweze kufanya vizuri zaidi. Pia

nawapongeza Wabunge wote ambao mmekuwa na uzalendo katika jambo hili na kuunga mkono Serikali yetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, niwatakie kila la kheri na wote mwende salama mwendako, ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho tarehe 8 Februari, saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.23 Usiku Bunge lilahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi
Tarehe 8 Februari, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*